# Mathayo

### *Kumbukumbu Za Ukoo Wa Yesu Kristo*
### *(Luka 3:23-38)*

1 Habari za ukoo wa Yesu Kristo mwana wa
Daudi, mwana wa Abrahamu:

2 Abrahamu akamzaa Isaki,
Isaki akamzaa Yakobo,
Yakobo akawazaa Yuda na ndugu zake,
3 Yuda akawazaa Peresi na Zera, ambao mama yao alikuwa Tamari,
Peresi akamzaa Hesroni,
Hesroni akamzaa Aramu,
4 Aramu akamzaa Aminadabu,
Aminadabu akamzaa Nashoni,
Nashoni akamzaa Salmoni,
5 Salmoni akamzaa Boazi, na mama yake Boazi alikuwa Rahabu,
Boazi akamzaa Obedi, ambaye mama yake alikuwa Ruthu,
Obedi akamzaa Yese,
6 Yese akamzaa Daudi ambaye alikuwa mfalme.

Daudi akamzaa Solomoni, ambaye mama yake ni yule aliyekuwa mke wa Uria.
7 Solomoni akamzaa Rehoboamu,
Rehoboamu akamzaa Abiya,
Abiya akamzaa Asa,
8 Asa akamzaa Yehoshafati,

Yehoshafati akamzaa Yoramu,*
Yoramu akamzaa Uzia,
9 Uzia akamzaa Yothamu,
Yothamu akamzaa Ahazi,
Ahazi akamzaa Hezekia,
10 Hezekia akamzaa Manase,
Manase akamzaa Amoni,
Amoni akamzaa Yosia,
11 wakati wa uhamisho wa Babeli, Yosia alimzaa Yekonia na ndugu zake.

12 Baada ya uhamisho wa Babeli:
Yekonia alimzaa Shealtieli,
Shealtieli akamzaa Zerubabeli,
13 Zerubabeli akamzaa Abiudi,
Abiudi akamzaa Eliakimu,
Eliakimu akamzaa Azori,
14 Azori akamzaa Sadoki,
Sadoki akamzaa Akimu,
Akimu akamzaa Eliudi,
15 Eliudi akamzaa Eleazari,
Eleazari akamzaa Matani,
Matani akamzaa Yakobo,
16 naye Yakobo akamzaa Yosefu ambaye alikuwa mumewe Maria, mama yake Yesu, aitwaye Kristo.†

17 Hivyo, kulikuwepo na jumla ya vizazi kumi na vinne tangu Abrahamu mpaka Daudi, vizazi kumi na vinne tangu Daudi hadi wakati wa uhamisho kwenda utumwani Babeli, na vizazi

---

* **1:8** Yoramu ndiye Yehoramu, maana yake ni Yehova yu juu.
† **1:16** Kristo maana yake ni Masiya, yaani Aliyetiwa mafuta.

kumi na vinne tangu wakati wa uhamisho
kwenda utumwani Babeli hadi Kristo.

### *Kuzaliwa Kwa Yesu Kristo*
### *(Luka 2:1-7)*

18 Basi Kuzaliwa kwake Yesu Kristo kulikuwa
hivi: Maria mama yake alikuwa ameposwa
na Yosefu, lakini kabla hawajakutana kimwili,
Maria alionekana kuwa na mimba kwa uweza
wa Roho Mtakatifu. 19 Kwa kuwa Yosefu,
mwanaume aliyekuwa amemposa alikuwa mtu
mwadilifu, hakutaka kumwaibisha Maria hadha-
rani, aliazimu kumwacha kwa siri.
20 Lakini mara alipoazimu kufanya jambo hili,
malaika wa Bwana akamtokea katika ndoto na
kusema, "Yosefu mwana wa Daudi, usiogope
kumchukua Maria awe mke wako, kwa maana
mimba aliyo nayo ni kwa uweza wa Roho
Mtakatifu. 21 Naye atamzaa mwana, nawe
utamwita Jina lake Yesu,‡ kwa maana yeye ndiye
atakayewaokoa watu wake kutoka dhambi zao."
22 Haya yote yalitukia ili litimie lile Bwana
alilokuwa amenena kupitia nabii, akisema:
23 "Tazama, bikira atachukua mimba, naye
atamzaa mwana, nao watamwita Jina lake
Imanueli": maana yake, "Mungu pamoja nasi."
24 Yosefu alipoamka kutoka usingizini,
akafanya kama vile alivyoagizwa na malaika
wa Bwana, akamchukua Maria kuwa mke
wake. 25 Lakini hawakukutana kimwili mpaka
Maria alipojifungua mwanawe kifungua mimba
akamwita Jina lake Yesu.

---

‡ **1:21** Yesu ni *Iesous* kwa Kiyunani, na kwa Kiebrania ni Yoshua au Yeshua. Maana yake ni Yehova ni wokovu.

# 2

## *Wataalamu Wa Nyota Wafika Kumwona Mtoto Yesu*

1 Baada ya Yesu kuzaliwa katika mji wa
Bethlehemu huko Uyahudi, wakati wa utawala
wa Mfalme Herode, wataalamu wa mambo ya
nyota kutoka mashariki walifika Yerusalemu
2 wakiuliza, "Yuko wapi huyo aliyezaliwa
mfalme wa Wayahudi? Kwa maana tumeona
nyota yake ikitokea mashariki, nasi tumekuja
kumwabudu."

3 Mfalme Herode aliposikia jambo hili ali-
ingiwa na hofu sana pamoja na watu wote
wa Yerusalemu. 4 Herode akawaita pamoja
viongozi wa makuhani na walimu wa she-
ria, akawauliza ni mahali gani ambapo Kristo*
angezaliwa. 5 Nao wakamwambia, "Katika Beth-
lehemu ya Uyahudi, kwa maana hivyo ndivyo
ilivyoandikwa na nabii:

6 " 'Nawe, Bethlehemu, katika nchi ya Yuda,
wewe si mdogo miongoni
mwa watawala wa Yuda;
kwa maana kutoka kwako atakuja mtawala
atakayekuwa mchungaji
wa watu wangu Israeli.' "

7 Ndipo Herode akawaita wale wataalamu wa
nyota kwa siri na kutaka kujua kutoka kwao
uhakika kamili wa wakati ile nyota ilionekana.
8 Kisha akawatuma waende Bethlehemu aki-
waambia, "Nendeni mkamtafute kwa bidii huyo

---

* **2:4** Kristo maana yake ni Masiya, yaani Aliyetiwa mafuta.

mtoto. Nanyi mara mtakapomwona, mniletee
habari ili na mimi niweze kwenda kumwabudu."
9 Baada ya kumsikia mfalme, wale wataalamu
wa nyota wakaenda zao, nayo ile nyota waliy-
oiona mashariki ikawatangulia, nao wakaifu-
ata mpaka iliposimama mahali pale alipokuwa
mtoto. 10 Walipoiona ile nyota wakajawa na
furaha kubwa mno. 11 Walipoingia ndani ya ile
nyumba, wakamwona mtoto pamoja na Maria
mama yake, wakamsujudu na kumwabudu yule
mtoto Yesu. Ndipo wakafungua hazina zao,
wakamtolea zawadi za dhahabu, uvumba na
manemane. 12 Nao wakiisha kuonywa katika
ndoto wasirudi kwa Herode, wakarudi kwenda
katika nchi yao kwa njia nyingine.

*Yosefu, Maria Na Mtoto Yesu Wakimbilia Misri*

13 Walipokwisha kwenda zao, malaika
wa Bwana akamtokea Yosefu katika ndoto
akamwambia, "Ondoka, mchukue mtoto na
mama yake mkimbilie Misri. Kaeni huko mpaka
nitakapowaambia, kwa maana Herode anataka
kumtafuta huyu mtoto ili amuue."
14 Kisha Yosefu akaondoka, akamchukua mtoto
pamoja na mama yake wakati wa usiku, nao
wakaenda Misri 15 ambako walikaa mpaka
Herode alipofariki. Hili lilifanyika ili litimie lile
lililonenwa na Bwana kwa kinywa cha nabii
kusema: "Nilimwita mwanangu kutoka Misri."
16 Herode alipong'amua kwamba wale
wataalamu wa nyota wamemshinda kwa akili,
alikasirika sana, naye akatoa amri ya kuwaua
watoto wote wa kiume wenye umri wa miaka
miwili kurudi chini katika mji wa Bethlehemu

na sehemu zote za jirani, kufuatana na ule
muda alioambiwa na wale wataalamu wa nyota.
17 Ndipo lilipotimia neno lililonenwa na nabii
Yeremia.
18 “Sauti ilisikika huko Rama,
maombolezo na kilio kikubwa,
Raheli akilia kwa ajili ya wanawe,
akikataa kufarijiwa,
kwa sababu hawako tena.”

*Kurudi Kutoka Misri*

19 Baada ya Herode kufa, malaika wa Bwana
akamtokea Yosefu katika ndoto huko Misri 20 na
kusema, “Ondoka, mchukue mtoto na mama
yake mwende, mrudi katika nchi ya Israeli kwa
sababu wale waliokuwa wanatafuta uhai wa
mtoto wamekufa.”
21 Basi Yosefu, akaondoka akamchukua mtoto
na mama yake wakaenda mpaka nchi ya Israeli.
22 Lakini aliposikia kwamba Arkelao alikuwa
anatawala huko Uyahudi mahali pa Herode baba
yake, aliogopa kwenda huko. Naye akiisha
kuonywa katika ndoto, akaenda zake sehemu za
Galilaya, 23 akaenda akaishi katika mji ulioitwa
Nazareti. Hivyo likawa limetimia neno lililo-
nenwa na manabii, “Ataitwa Mnazarayo.”

# 3

*Yohana Mbatizaji Atayarisha Njia*
*(Marko 1:1-8; Luka 3:1-18; Yohana 1:19-28)*

1 Siku hizo Yohana Mbatizaji alikuja akihubiri
katika nyika ya Uyahudi, akisema, 2 “Tubuni,
kwa maana Ufalme wa Mbinguni umekaribia.”

3 Huyu ndiye yule aliyenenwa habari zake na
nabii Isaya aliposema:
“Sauti ya mtu aliaye huko nyikani,
‘Tayarisheni njia kwa ajili ya Bwana,
yanyoosheni mapito yake.’ ”
4 Basi Yohana alivaa mavazi yaliyotengenezwa
kwa singa za ngamia, akiwa na mkanda wa
ngozi kiunoni mwake. Chakula chake kilikuwa
nzige na asali ya mwitu. 5 Watu walikuwa
wakimwendea kutoka Yerusalemu, Uyahudi yote
na nchi zote za kandokando ya Mto Yordani.
6 Nao wakaziungama dhambi zao, akawabatiza
katika Mto Yordani.
7 Lakini alipowaona Mafarisayo na
Masadukayo wengi wakija ili kubatizwa,
aliwaambia: “Ninyi watoto wa nyoka! Ni nani
aliyewaonya kuikimbia ghadhabu inayokuja?
8 Basi zaeni matunda yastahiliyo toba. 9 Wala
msidhani mnaweza kusema mioyoni mwenu
kuwa, ‘Sisi tunaye Abrahamu, baba yetu.’
Nawaambia kuwa Mungu anaweza kumwinulia
Abrahamu watoto kutoka kwa mawe haya.
10 Hata sasa shoka limeshawekwa tayari kwenye
shina la kila mti, basi kila mti usiozaa matunda
mazuri, hukatwa na kutupwa motoni.
11 “Mimi nawabatiza kwa maji kwa ajili ya
toba. Lakini nyuma yangu anakuja yeye aliye
na uwezo kuliko mimi, ambaye sistahili hata
kuvichukua viatu vyake. Yeye atawabatiza kwa
Roho Mtakatifu* na kwa moto. 12 Pepeto lake liko
mkononi mwake, naye atasafisha sakafu yake

* **3:11** …kwa Roho Mtakatifu hapa ina maana ya katika Roho Mtakatifu.

ya kupuria, na kuikusanya ngano ghalani na kuyateketeza makapi kwa moto usiozimika."

### *Yesu Abatizwa*
### *(Marko 1:9-11; Luka 3:21-22)*

13 Kisha Yesu akaja kutoka Galilaya mpaka Mto
Yordani ili Yohana ambatize. 14 Lakini Yohana
akajitahidi kumzuia, akimwambia, "Mimi ninahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu nikubatize?"

15 Lakini Yesu akamjibu, "Kubali hivi sasa, kwa maana ndivyo itupasavyo kwa njia hii kuitimiza haki yote." Hivyo Yohana akakubali.

16 Naye Yesu alipokwisha kubatizwa, mara
alipotoka ndani ya maji, ghafula mbingu zikafunguka, akamwona Roho wa Mungu akishuka
kama hua na kutulia juu yake. 17 Nayo sauti
kutoka mbinguni ikasema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa, ambaye ninapendezwa sana naye."

# 4

### *Kujaribiwa Kwa Yesu*
### *(Marko 1:12-13; Luka 4:1-13)*

1 Kisha Yesu akaongozwa na Roho Mtakatifu
kwenda nyikani ili akajaribiwe na ibilisi. 2 Baada
ya kufunga siku arobaini usiku na mchana,
hatimaye akaona njaa. 3 Mjaribu akamjia na
kumwambia, "Ikiwa wewe ndiye Mwana wa Mungu, amuru mawe haya yawe mikate."

4 Lakini Yesu akajibu, "Imeandikwa: 'Mtu haishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu.' "

5 Ndipo ibilisi akamchukua Yesu mpaka mji
mtakatifu na kumweka juu ya mnara mrefu
wa Hekalu, 6 akamwambia, “Kama wewe ndiwe
Mwana wa Mungu jitupe chini. Kwa kuwa
imeandikwa:

“ ‘Atakuagizia malaika zake,
nao watakuchukua mikononi mwao
ili usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe.’ ”

7 Yesu akamjibu, “Pia imeandikwa: ‘Usim-
jaribu Bwana Mungu wako.’ ”
8 Kwa mara nyingine, ibilisi akamchukua Yesu
mpaka kwenye kilele cha mlima mrefu na kum-
wonyesha falme zote za dunia na fahari zake,
9 kisha akamwambia, “Nitakupa hivi vyote kama
ukinisujudia na kuniabudu.”
10 Yesu akamwambia, “Ondoka mbele yangu,
Shetani! Kwa maana imeandikwa, ‘Mwabudu
Bwana Mungu wako, na umtumikie yeye peke
yake.’ ”
11 Ndipo ibilisi akamwacha, nao malaika
wakaja na kumhudumia.

### *Yesu Aanza Kuhubiri*
### *(Marko 1:14-15; Luka 4:14-15)*

12 Yesu aliposikia kwamba Yohana Mbati-
zaji alikuwa ametiwa gerezani, alirudi Galilaya.
13 Akaondoka Nazareti akaenda kuishi Kaper-
naumu, mji ulioko karibu na bahari, katika
mipaka ya nchi ya Zabuloni na Naftali, 14 ili ku-
timiza unabii wa nabii Isaya, kama alivyosema:
15 “Nchi ya Zabuloni na nchi ya Naftali,
kwenye njia ya kuelekea baharini,
ng’ambo ya Yordani,
Galilaya ya watu wa Mataifa:

16 watu wale waliokaa gizani
wameona nuru kuu;
nao wale walioishi katika nchi ya uvuli wa
mauti,
nuru imewazukia."
17 Tangu wakati huo, Yesu alianza kuhubiri
akisema: "Tubuni, kwa maana Ufalme wa Mbin-
guni umekaribia."

### *Yesu Awaita Wanafunzi Wake Wa Kwanza (Marko 1:16-20; Luka 5:1-11)*

18 Yesu alipokuwa anatembea kando ya Bahari
ya Galilaya, aliwaona ndugu wawili, Simoni
aitwaye Petro, na Andrea ndugu yake. Walikuwa
wakizitupa nyavu zao baharini kwa kuwa wao
walikuwa wavuvi. 19 Yesu akawaambia, "Njooni,
nifuateni nami nitawafanya mwe wavuvi wa
watu." 20 Mara wakaziacha nyavu zao, wakam-
fuata.
21 Alipoendelea mbele kutoka pale, akawaona
ndugu wengine wawili, Yakobo mwana wa Zebe-
dayo na Yohana nduguye, wakiwa wamekaa
kwenye mashua pamoja na baba yao Zebedayo,
wakizitengeneza nyavu zao. Yesu akawaita.
22 Nao mara wakaiacha mashua yao, pamoja na
baba yao, wakamfuata.

### *Yesu Ahubiri Na Kuponya Wagonjwa (Luka 6:17-19)*

23 Yesu akapita katika Galilaya yote, ak-
ifundisha katika masinagogi yao, akihubiri
habari njema za Ufalme, na akiponya kila
ugonjwa na kila aina ya maradhi miongoni
mwa watu. 24 Kwa hiyo sifa zake zikaenea

sehemu zote za Shamu, nao watu wakam-
letea wote waliokuwa na magonjwa mbal-
imbali na maumivu, waliopagawa na pepo
wachafu, wenye kifafa na waliopooza, naye
akawaponya. 25 Makutano makubwa ya watu
yakawa yanamjia kutoka Galilaya, Dekapoli,*
Yerusalemu, Uyahudi na kutoka ng'ambo ya Mto
Yordani.

# Mahubiri Ya Yesu Kwenye Mlima

# 5

*(Mathayo 5–7)*

*Sifa Za Aliyebarikiwa*
*(Luka 6:20-23)*

1 Basi Yesu alipoona makutano, alipanda
mlimani akaketi chini, nao wanafunzi wake
wakamjia. 2 Ndipo akaanza kuwafundisha,
akisema:

3 "Heri walio maskini wa roho,
maana Ufalme wa Mbinguni ni wao.
4 Heri wale wanaohuzunika,
maana hao watafarijiwa.
5 Heri walio wapole,
maana hao watairithi nchi.
6 Heri wenye njaa na kiu ya haki,
maana hao watatoshelezwa.
7 Heri wenye huruma,
maana hao watapata rehema.
8 Heri walio na moyo safi,
maana hao watamwona Mungu.
9 Heri walio wapatanishi,
maana hao wataitwa wana wa Mungu.

---

* **4:25** Yaani Miji Kumi.

10 Heri wanaoteswa kwa sababu ya haki,
maana Ufalme wa Mbinguni ni wao.
11 “Heri ninyi watu watakapowashutumu, na
kuwatesa na kunena dhidi yenu mabaya ya aina
zote kwa uongo kwa ajili yangu. 12 Furahini na
kushangilia kwa maana thawabu yenu ni kubwa
mbinguni, kwa kuwa hivyo ndivyo walivyowa-
tesa manabii waliokuwa kabla yenu.

### *Chumvi Na Nuru*
### *(Marko 9:50; Luka 14:34-35)*

13 “Ninyi ni chumvi ya ulimwengu. Lakini
chumvi ikipoteza ladha yake, yawezaje kurud-
ishiwa ladha yake tena? Haifai tena kwa kitu
chochote, ila kutupwa nje ikanyagwe na watu.
14 “Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji ulio-
jengwa kilimani hauwezi kufichika. 15 Wala
watu hawawashi taa na kuifunika kwa bakuli.
Badala yake, huiweka kwenye kinara chake,
nayo hutoa mwanga kwa kila mtu aliyemo ndani
ya ile nyumba. 16 Vivyo hivyo, nuru yenu
iangaze mbele ya watu, ili wapate kuona ma-
tendo yenu mema wamtukuze Baba yenu aliye
mbinguni.

### *Kutimiza Sheria*

17 “Msidhani kwamba nimekuja kufuta She-
ria au Manabii; sikuja kuondoa bali kutimiza.
18 Kwa maana, amin nawaambia, mpaka mbingu
na dunia zitakapopita, hakuna hata herufi moja
ndogo wala nukta itakayopotea kwa namna
yoyote kutoka kwenye Sheria, mpaka kila kitu
kiwe kimetimia. 19 Kwa hiyo, yeyote atakaye-
vunja mojawapo ya amri ndogo kuliko zote ya

amri hizi, naye akawafundisha wengine kufanya
hivyo, ataitwa mdogo kabisa katika Ufalme wa
Mbinguni, lakini yeyote azitendaye na kuzi-
fundisha hizi amri ataitwa mkuu katika Ufalme
wa Mbinguni. 20 Kwa maana nawaambia, haki
yenu isipozidi haki ya Mafarisayo na walimu
wa sheria, kamwe hamtaingia katika Ufalme wa
Mbinguni.

### *Kuhusu Hasira*
### *(Luka 12:57-59)*

21 "Mmesikia walivyoambiwa watu wa zamani
kwamba, 'Usiue. Yeyote atakayeua atapaswa
hukumu.' 22 Lakini mimi nawaambia kwamba,
yeyote atakayemkasirikia ndugu yake, atapaswa
hukumu. Tena, yeyote atakayemwambia ndugu
yake, 'Raka,'*atapaswa kujibu kwa Baraza la
Wayahudi.†Lakini yeyote atakayesema 'Wewe
mpumbavu!' atapaswa hukumu ya moto wa
jehanamu.
23 "Kwa hiyo, kama unatoa sadaka yako mad-
habahuni, ukakumbuka kuwa ndugu yako ana
kitu dhidi yako, 24 iache sadaka yako hapo mbele
ya madhabahu. Enda kwanza ukapatane na
ndugu yako; kisha urudi na ukatoe sadaka yako.
25 "Patana na mshtaki wako upesi wakati
uwapo njiani pamoja naye kwenda mahaka-
mani, ili mshtaki wako asije akakutia mikononi
mwa hakimu, naye hakimu akakutia mikononi

---

* **5:22** Raka ni neno la Kiaramu ambalo maana yake ni dharau au dhihaka ya hali ya juu. † **5:22** Baraza la Wayahudi lilikuwa kundi kuu kabisa la utawala wa Wayahudi lililoundwa na wazee 70 pamoja na kuhani mkuu.

mwa askari, nawe ukatupwa gerezani. 26 Amin,
nakuambia, hautatoka humo hadi uwe umelipa
senti ya mwisho.

*Kuhusu Uzinzi*

27 “Mmesikia kwamba ilinenwa, ‘Usizini.’
28 Lakini mimi nawaambia kwamba, yeyote am-
tazamaye mwanamke kwa kumtamani, amek-
wisha kuzini naye moyoni mwake. 29 Jicho
lako la kuume likikusababisha kutenda dhambi,
ling’oe ulitupe mbali. Ni afadhali kwako
kupoteza kiungo kimoja cha mwili wako ku-
liko mwili wako mzima ukatupwa jehanamu.
30 Kama mkono wako wa kuume ukikusababisha
kutenda dhambi, ukate, uutupe mbali. Ni
afadhali kwako kupoteza kiungo kimoja cha
mwili wako kuliko mwili wako mzima utupwe
jehanamu.

*Kuhusu Talaka*

*(Mathayo 19:9; Marko 10:11-12; Luka 16:18)*

31 “Pia ilinenwa kwamba, ‘Mtu yeyote
amwachaye mkewe sharti ampe hati ya talaka.’
32 Lakini mimi nawaambia, yeyote amwachaye
mkewe isipokuwa kwa kosa la uasherati,
amfanya mkewe kuwa mzinzi. Na yeyote
amwoaye yule mwanamke aliyeachwa, anazini.

*Kuhusu Kuapa*

33 “Tena mmesikia walivyoambiwa watu wa
zamani kwamba, ‘Usiape kwa uongo, bali timiza
kiapo kile ulichofanya kwa Bwana.’ 34 Lakini
mimi nawaambia, msiape kabisa: iwe kwa
mbingu, kwa kuwa ni kiti cha enzi cha Mungu;
35 au kwa dunia, kwa kuwa ndipo mahali pake pa

kuwekea miguu; au kwa Yerusalemu, kwa kuwa
ndio mji wa Mfalme Mkuu. 36 Nanyi msiape kwa
vichwa vyenu, kwa kuwa hamwezi kuufanya
hata unywele mmoja kuwa mweupe au mweusi.
37 'Ndiyo' yenu iwe 'Ndiyo,' na 'Hapana' yenu
iwe 'Hapana.' Lolote zaidi ya hili latoka kwa yule
mwovu.

*Kuhusu Kulipiza Kisasi*
*(Luka 6:29-30)*

38 "Mmesikia kwamba ilinenwa, 'Jicho kwa
jicho na jino kwa jino.' 39 Lakini mimi nawaam-
bia, msishindane na mtu mwovu. Lakini kama
mtu akikupiga kwenye shavu la kuume, mgeuzie
na la pili pia. 40 Kama mtu akitaka kukushtaki
na kuchukua joho lako, mwachie achukue na
koti pia. 41 Kama mtu akikulazimisha kwenda
maili moja, nenda naye maili mbili. 42 Mpe
yeye akuombaye, wala usimgeuzie kisogo yeye
atakaye kukukopa.

*Upendo Kwa Adui*
*(Luka 6:27-28, 32-36)*

43 "Mmesikia kwamba ilinenwa, 'Mpende
jirani yako na umchukie adui yako.' 44 Lakini
ninawaambia: Wapendeni adui zenu na
waombeeni wanaowatesa ninyi, 45 ili mpate
kuwa watoto wa Baba yenu aliye mbinguni.
Kwa maana yeye huwaangazia jua lake watu
waovu na watu wema, naye huwanyeshea mvua
wenye haki na wasio haki. 46 Kama mkiwapenda
tu wale wanaowapenda, mtapata thawabu
gani? Je, hata watoza ushuru hawafanyi hivyo?
47 Nanyi kama mkiwasalimu ndugu zenu tu, je,

mnafanya nini zaidi ya wengine? Je, hata watu
wasiomjua Mungu, hawafanyi hivyo? 48 Kwa
hiyo kuweni wakamilifu kama Baba yenu wa
mbinguni alivyo mkamilifu.

# 6

*Kuwapa Wahitaji*

1 “Angalieni msitende wema wenu mbele ya
watu ili wawaone. Kwa maana mkifanya hivyo,
hamna thawabu kutoka kwa Baba yenu aliye
mbinguni.

2 “Hivyo mnapowapa wahitaji, msipige panda
mbele yenu kama wafanyavyo wanafiki katika
masinagogi na mitaani, ili wasifiwe na watu.
Amin nawaambia wao wamekwisha kupokea
thawabu yao. 3 Lakini ninyi mtoapo sadaka,
fanyeni kwa siri, hata mkono wako wa kushoto
usijue mkono wako wa kuume unachofanya, 4 ili
sadaka yako iwe ni siri. Ndipo Baba yako wa
mbinguni, yeye aonaye sirini atakupa thawabu
kwa wazi.

*Kuhusu Maombi*
*(Luka 11:2-4)*

5 “Nanyi msalipo, msiwe kama wanafiki,
maana wao hupenda kusali wakiwa wamesi-
mama katika masinagogi na kando ya barabara
ili waonekane na watu. Amin nawaambia, wao
wamekwisha kupata thawabu yao. 6 Lakini
wewe unaposali, ingia chumbani mwako, funga
mlango na umwombe Baba yako aliye sirini.
Naye Baba yako aonaye sirini atakupa thawabu
yako. 7 Nanyi mnaposali msiseme maneno

kama wafanyavyo watu wasiomjua Mungu. Kwa
maana wao hudhani kwamba watasikiwa kwa
sababu ya wingi wa maneno yao. 8 Msiwe
kama wao, kwa sababu Baba yenu anajua kile
mnachohitaji kabla hamjamwomba.

9 “Hivi basi, ndivyo iwapasavyo kuomba:

“ ‘Baba yetu uliye mbinguni,
Jina lako litukuzwe.
10 Ufalme wako uje.
Mapenzi yako yafanyike
hapa duniani kama huko mbinguni.
11 Utupatie riziki yetu
ya kila siku.
12 Utusamehe deni zetu,
kama sisi nasi tulivyokwisha
kuwasamehe wadeni wetu.
13 Usitutie majaribuni,
bali utuokoe kutoka kwa yule mwovu
[kwa kuwa Ufalme ni wako, na nguvu,
na utukufu, hata milele. Amen].’

14 Kwa kuwa kama mkiwasamehe watu
wengine wanapowakosea, Baba yenu wa
mbinguni atawasamehe ninyi pia. 15 Lakini
msipowasamehe watu wengine makosa yao,
naye Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa
yenu.

*Kuhusu Kufunga*

16 “Mnapofunga, msiwe wenye huzuni kama
wafanyavyo wanafiki. Maana wao hukunja
nyuso zao ili kuwaonyesha wengine kwamba
wamefunga. Amin, amin nawaambia wao
wamekwisha kupata thawabu yao kamilifu.
17 Lakini mnapofunga, jipakeni mafuta kichwani

na kunawa nyuso zenu
18 ili kufunga kwenu kusionekane na watu wengine ila Baba yenu aketiye mahali pa siri; naye Baba yenu aonaye sirini atawapa thawabu yenu kwa wazi.

*Akiba Ya Mbinguni*
*(Luka 12:33-34)*

19 “Msijiwekee hazina duniani, mahali ambapo nondo na kutu huharibu, nao wevi huvunja na kuiba.
20 Lakini jiwekeeni hazina mbinguni, mahali ambapo nondo na kutu haviharibu, wala wevi hawavunji na kuiba.
21 Kwa sababu mahali hazina yako ilipo, hapo ndipo pia moyo wako utakapokuwa.

*Jicho Ni Taa Ya Mwili*
*(Luka 11:34-36)*

22 “Jicho ni taa ya mwili. Kama jicho lako ni nyofu, mwili wako wote utajaa nuru.
23 Lakini kama jicho lako ni ovu, mwili wako wote utajawa na giza. Kwa hiyo basi, kama nuru iliyomo ndani yako ni giza, hilo ni giza kuu namna gani!

*Mungu Na Mali*
*(Luka 16:13; 12:22-31)*

24 “Hakuna mtu awezaye kuwatumikia mabwana wawili. Kwa kuwa atamchukia huyu na kumpenda yule mwingine, au atashikamana sana na huyu na kumdharau yule mwingine. Hamwezi kumtumikia Mungu pamoja na Mali.*

*Msiwe Na Wasiwasi*

---

* **6:24** Mali (au Utajiri) hapa inatoka neno Mamoni kwa Kiaramu au Mamona kwa Kiyunani.

25 “Kwa hiyo nawaambia, msisumbukie
maisha yenu kwamba mtakula nini au
mtakunywa nini; au msumbukie miili yenu
kwamba mtavaa nini. Je, maisha si zaidi
ya chakula, na mwili zaidi ya mavazi?
26 Waangalieni ndege wa angani; wao
hawapandi wala hawavuni au kuweka ghalani,
lakini Baba yenu wa mbinguni huwalisha. Je,
ninyi si wa thamani zaidi kuliko hao ndege? 27 Ni
nani miongoni mwenu ambaye kwa kujitaabisha
kwake anaweza kujiongezea hata saa moja zaidi
katika maisha yake?

28 “Nanyi kwa nini mnajitaabisha kwa ajili ya
mavazi? Fikirini maua ya shambani yameavyo.
Hayafanyi kazi wala hayafumi. 29 Lakini
nawaambia, hata Solomoni katika fahari yake
yote hakuvikwa vizuri kama mojawapo ya hayo
maua. 30 Basi ikiwa Mungu huyavika hivi
majani ya shambani, ambayo leo yapo na kesho
yanatupwa motoni, je, hatawavika ninyi vizuri
zaidi, enyi wa imani haba? 31 Kwa hiyo msiwe
na wasiwasi, mkisema, ‘Tutakula nini?’ au
‘Tutakunywa nini?’ au ‘Tutavaa nini?’ 32 Watu
wasiomjua Mungu ndio wanaoshindania hayo,
lakini Baba yenu wa mbinguni anafahamu kuwa
mnahitaji haya yote. 33 Lakini utafuteni kwanza
Ufalme wa Mungu na haki yake, na haya yote
atawapa pia. 34 Kwa hiyo msiwe na wasiwasi
kuhusu kesho, kwa sababu kesho itajitaabikia
yenyewe. Yatosha kwa siku masumbufu yake.

# 7

*Kuwahukumu Wengine*
*(Luka 6:37-38, 41-42)*

1 “Usihukumu ili usije ukahukumiwa. 2 Kwa
maana jinsi unavyowahukumu wengine, ndivyo
utakavyohukumiwa, na kwa kipimo kile upimi-
acho, ndicho utakachopimiwa.
3 “Mbona unatazama kibanzi kilicho ndani ya
jicho la ndugu yako, na wala huoni boriti iliyo
ndani ya jicho lako mwenyewe? 4 Au unawezaje
kumwambia ndugu yako, ‘Acha nitoe kibanzi
kwenye jicho lako,’ wakati kuna boriti kwenye
jicho lako mwenyewe? 5 Ewe mnafiki, ondoa
boriti ndani ya jicho lako kwanza, ndipo utaweza
kuona dhahiri jinsi ya kuondoa kibanzi kilicho
ndani ya jicho la ndugu yako.
6 “Msiwape mbwa vitu vilivyo vitakatifu;
wala msitupie nguruwe lulu zenu. Kama mk-
ifanya hivyo, watazikanyagakanyaga na kisha
watawageukia na kuwararua vipande vipande.

*Omba, Tafuta, Bisha*
*(Luka 11:9-13)*

7 “Ombeni nanyi mtapewa; tafuteni nanyi
mtapata; bisheni nanyi mtafunguliwa mlango.
8 Kwa kuwa kila aombaye hupewa; naye kila
atafutaye hupata; na kila abishaye hufunguliwa
mlango.
9 “Au ni nani miongoni mwenu ambaye
mwanawe akimwomba mkate atampa jiwe?
10 Au mwanawe akimwomba samaki atampa
nyoka? 11 Ikiwa ninyi basi mlio waovu mna-
jua kuwapa watoto wenu vitu vizuri, si zaidi
sana Baba yenu aliye mbinguni atawapa vitu

vizuri wale wamwombao? 12 Kwa hiyo chochote
mnachotaka mtendewe na watu, ninyi nanyi
watendeeni vivyo hivyo. Kwa kuwa hii ndiyo
Sheria na Manabii.

### *Njia Nyembamba Na Njia Pana*

13 “Ingieni kupitia mlango mwembamba, kwa
maana lango ni pana na njia ni pana ielekeayo
upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa kupitia
lango hilo. 14 Lakini mlango ni mwembamba
na njia ni finyu ielekeayo kwenye uzima, nao ni
wachache tu waionao.

### *Mti Na Tunda Lake*
### *(Luka 6:43-44)*

15 “Jihadharini na manabii wa uongo,
wanaowajia wakiwa wamevaa mavazi ya
kondoo, lakini ndani ni mbwa mwitu wakali.
16 Mtawatambua kwa matunda yao. Je, watu
huchuma zabibu kwenye miiba, au tini kwenye
michongoma? 17 Vivyo hivyo, mti mwema
huzaa matunda mazuri, na mti mbaya huzaa
matunda mabaya. 18 Mti mwema hauwezi kuzaa
matunda mabaya, wala mti mbaya hauwezi
kuzaa matunda mazuri. 19 Kila mti usiozaa
matunda mazuri hukatwa na kutupwa motoni.
20 Hivyo, mtawatambua kwa matunda yao.

### *Mwanafunzi Wa Kweli*
### *(Luka 13:25-27)*

21 “Si kila mtu aniambiaye, ‘Bwana, Bwana,’
atakayeingia katika Ufalme wa Mbinguni, bali
ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye
mbinguni. 22 Wengi wataniambia siku ile,
‘Bwana, Bwana, hatukutoa unabii kwa jina lako,

na kwa jina lako kutoa pepo wachafu na kufanya
miujiza mingi?’ 23 Ndipo nitakapowaambia wazi,
‘Sikuwajua kamwe. Ondokeni kwangu, ninyi
watenda maovu!’

### *Msikiaji Na Mtendaji*
### *(Luka 6:47-49)*

24 “Kwa hiyo kila mtu ayasikiaye haya maneno yangu na kuyatenda, ni kama mtu mwenye busara aliyejenga nyumba yake kwenye
mwamba. 25 Mvua ikanyesha, mafuriko yakaja,
na upepo ukavuma ukaipiga hiyo nyumba.
Lakini haikuanguka; kwa sababu msingi wake
ulikuwa kwenye mwamba. 26 Naye kila
anayesikia haya maneno yangu wala asiyatende,
ni kama mtu mjinga aliyejenga nyumba yake
kwenye mchanga. 27 Mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, nao upepo ukavuma ukaipiga
hiyo nyumba, nayo ikaanguka kwa kishindo
kikubwa.”

28 Yesu alipomaliza kusema maneno haya,
makutano ya watu wakashangazwa sana na
mafundisho yake, 29 kwa sababu alifundisha
kama yeye aliye na mamlaka, wala si kama
walimu wao wa sheria.

# 8

### *Yesu Amtakasa Mwenye Ukoma*
### *(Marko 1:40-45; Luka 5:12-16)*

1 Yesu aliposhuka kutoka mlimani, makutano
makubwa ya watu yakamfuata. 2 Mtu mmoja
mwenye ukoma akaja na kupiga magoti mbele

yake, akasema, “Bwana, kama ukitaka, unaweza
kunitakasa.”
3 Yesu akanyoosha mkono wake akamgusa
yule mtu, akamwambia, “Nataka. Takasika!”
Mara yule mtu akatakasika ukoma wake. 4 Kisha
Yesu akamwambia, “Hakikisha humwambii mtu
yeyote. Lakini nenda ukajionyeshe kwa kuhani,
na utoe sadaka aliyoamuru Mose, ili kuwa
ushuhuda kwao.”

### *Yesu Amponya Mtumishi Wa Jemadari (Luka 7:1-10)*

5 Yesu alipoingia Kapernaumu, jemadari
mmoja alimjia, kumwomba msaada, 6 akisema,
“Bwana, mtumishi wangu amelala nyumbani
na amepooza, tena ana maumivu makali ya
kutisha.”
7 Yesu akamwambia, “Nitakuja na kumponya.”
8 Lakini yule jemadari akamwambia, “Bwana,
mimi sistahili wewe kuingia chini ya dari yangu.
Lakini sema neno tu, naye mtumishi wangu
atapona. 9 Kwa kuwa mimi mwenyewe ni mtu
niliyewekwa chini ya mamlaka, nikiwa na askari
chini yangu. Nikimwambia huyu, ‘Nenda,’ yeye
huenda; na mwingine nikimwambia, ‘Njoo,’
yeye huja. Nikimwambia mtumishi wangu,
‘Fanya hivi,’ yeye hufanya.”
10 Yesu aliposikia maneno haya, alishangaa,
akawaambia wale waliomfuata, “Amin,
nawaambia, hata katika Israeli sijapata kuona
yeyote mwenye imani kubwa namna hii.
11 Ninawaambia kwamba wengi watatoka
mashariki na magharibi, nao wataketi karamuni
pamoja na Abrahamu, Isaki na Yakobo katika

Ufalme wa Mbinguni. 12 Lakini warithi wa
Ufalme watatupwa katika giza la nje, ambako
kutakuwako kilio na kusaga meno."
13 Kisha Yesu akamwambia yule jemadari,
"Nenda na iwe kwako sawasawa na imani yako."
Naye yule mtumishi akapona saa ile ile.

### *Yesu Aponya Wengi*
### *(Marko 1:29-34; Luka 4:38-41)*

14 Yesu alipoingia nyumbani kwa Petro, al-
imkuta mama mkwe wa Petro amelala kitandani,
akiwa ana homa. 15 Akamgusa mkono wake
na homa ikamwacha, naye akainuka na kuanza
kumhudumia.
16 Jioni ile, wakamletea watu wengi waliopa-
gawa na pepo wachafu, naye akawatoa wale
pepo wachafu kwa neno lake, na kuwaponya
wagonjwa wote. 17 Haya yalifanyika ili litimie
lile lililonenwa kwa kinywa cha nabii Isaya
kwamba:

"Mwenyewe alitwaa udhaifu wetu
na alichukua magonjwa yetu."

### *Gharama Ya Kumfuata Yesu*
### *(Luka 9:57-62)*

18 Yesu alipoona makutano mengi wamemzun-
guka, aliwaamuru wanafunzi wake wavuke
mpaka ng'ambo ya ziwa. 19 Kisha mwalimu
mmoja wa sheria akamjia Yesu na kumwambia,
"Mwalimu, nitakufuata kokote uendako."
20 Naye Yesu akamjibu, "Mbweha wana ma-
pango, nao ndege wa angani wana viota, lakini
Mwana wa Adamu hana mahali pa kulaza
kichwa chake."

21 Mwanafunzi mwingine akamwambia, “Bwana, niruhusu kwanza nikamzike baba yangu.”
22 Lakini Yesu akamwambia, “Nifuate, uwaache wafu wawazike wafu wao.”

### *Yesu Atuliza Dhoruba*
### *(Marko 4:35-41; Luka 8:22-25)*

23 Naye alipoingia kwenye mashua, wanafunzi
wake wakamfuata. 24 Ghafula, kukainuka dhoruba kali baharini hata mashua ikaanza kufunikwa na mawimbi, lakini Yesu alikuwa amelala
usingizi. 25 Wanafunzi wake wakamwendea na kumwamsha, wakisema, “Bwana, tuokoe! Tunazama!”
26 Naye Yesu akawaambia, “Kwa nini mnaogopa, enyi wa imani haba?” Kisha akaamka na kukemea dhoruba na mawimbi, nako kukawa shwari kabisa.
27 Wale watu wakashangaa, wakisema, “Ni mtu wa namna gani huyu? Hata upepo na mawimbi vinamtii!”

### *Wawili Wenye Pepo Waponywa*
### *(Marko 5:1-20; Luka 8:26-39)*

28 Walipofika ng’ambo katika nchi ya Wagerasi, watu wawili waliopagawa na pepo wachafu walitoka makaburini nao wakakutana naye. Watu hawa walikuwa wakali mno kiasi kwamba hakuna mtu aliyeweza kupita njia ile.
29 Wakapiga kelele, “Una nini nasi, Mwana wa Mungu? Umekuja hapa kututesa kabla ya wakati ulioamriwa?”
30 Mbali kidogo kutoka pale walipokuwa, kulikuwa na kundi kubwa la nguruwe wakilisha.
31 Wale pepo wachafu wakamsihi Yesu, “Ukitutoa

humu, turuhusu twende kwenye lile kundi la
nguruwe."
32 Akawaambia, "Nendeni!" Hivyo waka-
toka na kuwaingia wale nguruwe, nalo kundi
lote likateremka gengeni kwa kasi, likaingia
katika ziwa na kufa ndani ya maji. 33 Wale
watu waliokuwa wakiwachunga hao nguruwe
wakakimbia wakaingia mjini, wakaeleza yote
kuhusu yale yaliyowatokea wale waliokuwa
wamepagawa na pepo wachafu. 34 Kisha watu
wote wa mji huo wakatoka kwenda kukutana
na Yesu. Nao walipomwona wakamsihi aondoke
kwenye nchi yao.

# 9

### *Yesu Amponya Mtu Aliyepooza (Marko 2:1-12; Luka 5:17-26)*

1 Yesu akaingia kwenye chombo, akavuka na
kufika katika mji wa kwao. 2 Wakati huo huo
wakamletea mtu aliyepooza, akiwa amelazwa
kwenye mkeka. Yesu alipoiona imani yao,
alimwambia yule mtu aliyepooza, "Mwanangu,
jipe moyo mkuu. Dhambi zako zimesamehewa."
3 Kwa ajili ya jambo hili, baadhi ya walimu
wa sheria wakasema mioyoni mwao, "Huyu mtu
anakufuru!"
4 Lakini Yesu akiyafahamu mawazo yao,
akawaambia, "Kwa nini mnawaza maovu
mioyoni mwenu? 5 Je, ni lipi lililo rahisi zaidi:
kusema, 'Umesamehewa dhambi zako,' au
kusema, 'Inuka, uende'? 6 Lakini, ili mpate
kujua kwamba Mwana wa Adamu anayo
mamlaka duniani kusamehe dhambi…" Ndipo

akamwambia yule aliyepooza, "Inuka, chukua
mkeka wako, uende nyumbani kwako." 7 Yule
mtu akasimama, akaenda nyumbani kwake.
8 Makutano walipoyaona haya, wakajawa na
hofu ya Mungu, wakamtukuza Mungu ambaye
alikuwa ametoa mamlaka kama haya kwa
wanadamu.

### *Kuitwa Kwa Mathayo*
*(Marko 2:13-17; Luka 5:27-32)*

9 Yesu alipokuwa akienda kutoka huko, alimwona mtu mmoja jina lake Mathayo akiwa ameketi forodhani mahali pa kutoza ushuru. Yesu akamwambia, "Nifuate." Mathayo akaondoka, akamfuata.

10 Yesu alipokuwa akila chakula ndani ya
nyumba ya Mathayo, watoza ushuru wengi
na "wenye dhambi" wakaja kula pamoja naye
na wanafunzi wake. 11 Mafarisayo walipoona
mambo haya, wakawauliza wanafunzi wake,
"Kwa nini Mwalimu wenu anakula pamoja na
watoza ushuru na 'wenye dhambi'?"

12 Lakini Yesu aliposikia hayo, akawaambia,
"Watu wenye afya hawahitaji tabibu, lakini
wale walio wagonjwa ndio wanaohitaji tabibu.
13 Nendeni mkajifunze maana ya maneno haya:
'Nataka rehema, wala si dhabihu.' Kwa maana
sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi."

### *Yesu Aulizwa Kuhusu Kufunga*
*(Marko 2:18-22; Luka 5:33-39)*

14 Wanafunzi wa Yohana Mbatizaji wakaja na kumuuliza Yesu, "Imekuwaje kwamba sisi na

Mafarisayo tunafunga, lakini wanafunzi wako hawafungi?”
15 Yesu akawajibu, “Wageni wa bwana arusi
wawezaje kuomboleza wakati angali pamoja
nao? Wakati utafika ambapo bwana arusi
ataondolewa kwao. Hapo ndipo watakapofunga.
16 “Hakuna mtu anayeshonea kiraka kipya
kwenye nguo iliyochakaa, kwa maana kile ki-
raka kitachanika kutoka kwenye hiyo nguo,
nayo hiyo nguo itachanika zaidi. 17 Wala watu
hawaweki divai mpya kwenye viriba vikuukuu.
Kama wakifanya hivyo, viriba vitapasuka nayo
divai itamwagika, navyo viriba vitaharibika.
Lakini divai mpya huwekwa kwenye viriba
vipya, na hivyo divai na viriba huwa salama.”

### *Mwanamke Aponywa*
### *(Marko 5:21-43; Luka 8:40-56)*

18 Yesu alipokuwa akiwaambia mambo haya,
mara akaingia kiongozi wa sinagogi akapiga
magoti mbele yake, akamwambia, “Binti yangu
amekufa sasa hivi. Lakini njoo uweke mkono
wako juu yake, naye atakuwa hai.” 19 Yesu
akaondoka akafuatana naye, nao wanafunzi
wake pia wakaandamana naye.
20 Wakati huo huo, mwanamke mmoja, am-
baye alikuwa na ugonjwa wa kutokwa damu
kwa muda wa miaka kumi na miwili, akaja
nyuma ya Yesu, akagusa upindo wa vazi lake,
21 kwa maana alisema moyoni mwake, “Kama
nikigusa tu vazi lake, nitaponywa.”
22 Yesu akageuka, naye alipomwona
akamwambia, “Binti, jipe moyo mkuu, imani

yako imekuponya." Naye yule mwanamke
akapona kuanzia saa ile ile.

### *Yesu Amfufua Binti Wa Kiongozi Wa Sinagogi*

23 Yesu alipofika nyumbani kwa yule kiongozi
wa sinagogi na kuwaona waombolezaji wakipiga
filimbi za maombolezo na watu wengi wakipiga
kelele, 24 akawaambia, "Ondokeni! Kwa maana
binti huyu hakufa, bali amelala." Wakamcheka
kwa dhihaka. 25 Lakini watu walipokwisha
kutolewa nje, akaingia mle ndani na kumshika
yule binti mkono, naye akaamka. 26 Habari hizi
zikaenea katika maeneo yale yote.

### *Yesu Awaponya Vipofu*

27 Yesu alipokuwa akiondoka mahali pale,
vipofu wawili wakamfuata wakipiga kelele kwa
nguvu na kusema, "Mwana wa Daudi, tuhuru-
mie!"
28 Alipoingia mle nyumbani wale vipofu
wakamjia. Naye Yesu akawauliza, "Mnaamini
kwamba ninaweza kufanya jambo hili?"

Wakamjibu, "Ndiyo, Bwana."

29 Ndipo Yesu akagusa macho yao na kusema,
"Iwe kwenu sawasawa na imani yenu." 30 Macho
yao yakafunguka. Yesu akawaonya vikali,
akisema, "Angalieni mtu yeyote asijue kuhusu
jambo hili." 31 Lakini wao wakaenda na kueneza
habari zake katika eneo lile lote.

### *Yesu Amponya Mtu Bubu*

32 Walipokuwa wanatoka, mtu mmoja
aliyekuwa amepagawa na pepo mchafu na
ambaye hakuweza kuongea aliletwa kwa Yesu.

33 Yule pepo mchafu alipotolewa, yule mtu aliyekuwa bubu akaongea. Ule umati wa watu ukastaajabu na kusema, "Jambo kama hili kamwe halijapata kuonekana katika Israeli."

34 Lakini Mafarisayo wakasema, "Huyo anatoa pepo wachafu kwa uwezo wa mkuu wa pepo wachafu."

### *Watendakazi Ni Wachache*

35 Yesu akazunguka katika miji yote na vijiji
vyote, akifundisha katika masinagogi yao, akihu-
biri habari njema za Ufalme, na akiponya kila
ugonjwa na kila aina ya maradhi. 36 Alipoona
makutano, aliwahurumia kwa sababu walikuwa
wanasumbuka bila msaada, kama kondoo wa-
siokuwa na mchungaji. 37 Ndipo akawaambia
wanafunzi wake, "Mavuno ni mengi lakini wa-
tendakazi ni wachache. 38 Kwa hiyo mwombeni
Bwana wa mavuno, ili apeleke watendakazi
katika shamba lake la mavuno."

# 10

### *Yesu Awatuma Wale Kumi Na Wawili (Marko 3:13-19; 6:7-13; Luka 6:12-16; 9:1-6)*

1 Ndipo Yesu akawaita wanafunzi wake kumi na wawili, naye akawapa mamlaka juu ya pepo wachafu, ili waweze kuwatoa na kuponya kila ugonjwa na maradhi ya kila aina.

2 Haya ndiyo majina ya hao mitume kumi
na wawili: wa kwanza, Simoni aitwaye Petro,
na Andrea nduguye; Yakobo mwana wa Zebe-
dayo, na Yohana nduguye; 3 Filipo, na Bartholo-
mayo; Tomaso, na Mathayo mtoza ushuru;

Yakobo mwana wa Alfayo, na Thadayo; 4 Simoni
Mkananayo, na Yuda Iskariote aliyemsaliti Yesu.

5 Hawa kumi na wawili, Yesu aliwatuma
akawaagiza: “Msiende miongoni mwa watu
wa Mataifa, wala msiingie mji wowote wa
Wasamaria. 6 Lakini afadhali mshike njia
kuwaendea kondoo wa nyumba ya Israeli
waliopotea. 7 Wakati mnapokwenda, hubirini
mkisema, ‘Ufalme wa Mbinguni umekaribia.’
8 Ponyeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni
wenye ukoma, toeni pepo wachafu. Mmepata
bure, toeni bure. 9 Msichukue dhahabu,
wala fedha, wala shaba kwenye vifuko vyenu.
10 Msichukue mkoba wa safari, wala kanzu mbili,
wala jozi ya pili ya viatu, wala fimbo, kwa maana
mtendakazi anastahili posho yake.

11 “Mji wowote au kijiji chochote
mtakapoingia, tafuteni humo mtu anayestahili,
nanyi kaeni kwake mpaka mtakapoondoka.
12 Mkiingia kwenye nyumba, itakieni amani.
13 Kama nyumba hiyo inastahili, amani yenu
na iwe juu yake. La sivyo, amani yenu
na iwarudie ninyi. 14 Kama mtu yeyote
hatawakaribisha ninyi, wala kusikiliza maneno
yenu, kung’uteni mavumbi kutoka kwenye
miguu yenu mtakapokuwa mnatoka kwenye
nyumba hiyo au mji huo. 15 Amin, nawaambia,
itakuwa rahisi zaidi kwa miji ya Sodoma na
Gomora kustahimili katika hukumu kuliko mji
huo.

### *Mateso Yanayokuja*
*(Marko 13:9-13; Luka 21:12-17)*

16 “Tazama, ninawatuma kama kondoo
katikati ya mbwa mwitu. Kwa hiyo mwe werevu
kama nyoka na wapole kama hua.
17 “Jihadharini na wanadamu; kwa maana
watawapeleka katika mabaraza yao na
kuwapiga kwenye masinagogi yao. 18 Nanyi
mtaburutwa mbele ya watawala na wafalme
kwa ajili yangu, ili kuwa ushuhuda kwao na kwa
watu wa Mataifa. 19 Lakini watakapowapeleka
humo, msisumbuke kufikiria mtakalosema, kwa
maana mtapewa la kusema wakati huo. 20 Kwa
sababu si ninyi mtakaokuwa mkinena, bali
ni Roho wa Baba yenu atakayekuwa akinena
kupitia kwenu.
21 “Ndugu atamsaliti ndugu yake ili auawe,
naye baba atamsaliti mtoto wake. Watoto nao
wataasi dhidi ya wazazi wao na kusababisha
wauawe. 22 Watu wote watawachukia kwa ajili
ya Jina langu. Lakini yule atakayevumilia hadi
mwisho ataokolewa. 23 Wakiwatesa katika mji
mmoja, kimbilieni mji mwingine. Amin, amin
nawaambia, hamtamaliza miji yote ya Israeli
kabla Mwana wa Adamu kuja.
24 “Mwanafunzi hawezi kumzidi mwalimu
wake, wala mtumishi hamzidi bwana wake.
25 Yatosha mwanafunzi kuwa kama mwalimu
wake, na mtumishi kuwa kama bwana wake.
Ikiwa mkuu wa nyumba ameitwa Beelzebuli,*je,
si watawaita zaidi wale wa nyumbani mwake!

*Anayestahili Kuogopwa*
*(Luka 12:2-9)*

---

* **10:25** Beelzebuli kwa Kiyunani ni Beelzebubu, yaani mkuu wa pepo wachafu.

26 “Kwa hiyo msiwaogope hao, kwa maana
hakuna kilichofichika ambacho hakitafunuliwa,
wala hakuna siri ambayo haitajulikana.
27 Ninalowaambia gizani, ninyi lisemeni mchana
peupe. Na lile mnalosikia likinong’onwa
masikioni mwenu, lihubirini juu ya nyumba.
28 Msiwaogope wale wauao mwili lakini
hawawezi kuua roho. Afadhali mwogopeni yeye
awezaye kuiangamiza roho na mwili katika
jehanamu.† 29 Je, shomoro wawili hawauzwi
kwa senti moja tu? Lakini hakuna hata mmoja
wao atakayeanguka chini pasipo Baba yenu
kujua. 30 Hata nywele za vichwa vyenu zote
zimehesabiwa. 31 Hivyo msiogope; kwa maana
ninyi ni wa thamani kubwa kuliko shomoro
wengi.
32 “Kila mtu atakayenikiri mbele ya watu,
mimi nami nitamkiri yeye mbele za Baba yangu
aliye mbinguni. 33 Lakini yeyote atakayenikana
mimi mbele ya watu, mimi nami nitamkana
mbele za Baba yangu aliye mbinguni.”

### *Sikuleta Amani, Bali Upanga*
### *(Luka 12:51-53; 14:26-27)*

34 “Msidhani kwamba nimekuja kuleta amani
duniani. Sikuja kuleta amani bali upanga.
35 Kwa maana nimekuja kumfitini
“ ‘mtu na babaye,
binti na mamaye,
mkwe na mama mkwe wake;
36 nao adui za mtu watakuwa

† **10:28** Jehanamu kwa Kiyunani ni Gehena, maana yake ni Kuzimu, yaani motoni.

ni wale watu wa nyumbani kwake.’
37 “Yeyote ampendaye baba yake au mama
yake kuliko anavyonipenda mimi, hastahili
kuwa wangu. Yeyote ampendaye mwanawe au
binti yake kuliko anavyonipenda mimi, hastahili
kuwa wangu. 38 Tena yeyote asiyeuchukua
msalaba wake na kunifuata, hastahili kuwa
wangu. 39 Kwa maana yeyote anayetaka
kuyaokoa maisha yake atayapoteza, lakini yey-
ote atakayeyapoteza maisha yake kwa ajili yangu
atayapata.

*Watakaopokea Thawabu*
*(Marko 9:41)*

40 “Mtu yeyote atakayewapokea ninyi atakuwa
amenipokea mimi, na yeyote atakayenipokea
mimi atakuwa amempokea yeye aliyenituma.
41 Mtu yeyote anayempokea nabii kwa kuwa
ni nabii atapokea thawabu ya nabii, naye
mtu anayempokea mwenye haki kwa kuwa ni
mwenye haki atapokea thawabu ya mwenye
haki. 42 Kama yeyote akimpa hata kikombe
cha maji baridi mmoja wa hawa wadogo kwa
kuwa ni mwanafunzi wangu, amin, nawaambia,
hataikosa thawabu yake.”

# 11

*Yesu Na Yohana Mbatizaji*
*(Luka 7:18-35)*

1 Baada ya Yesu kumaliza kutoa maagizo kwa
wanafunzi wake kumi na wawili, aliondoka
hapo akaenda kufundisha na kuhubiri katika
miji yao.

2 Yohana aliposikia akiwa gerezani mambo
ambayo Kristo* alikuwa akiyafanya, aliwatuma
wanafunzi wake 3 ili wakamuulize, “Wewe ndiye
yule aliyekuwa aje, au tumngojee mwingine?”
4 Yesu akajibu, “Rudini mkamwambie Yohana
yale mnayosikia na kuyaona: 5 Vipofu wanap-
ata kuona, viwete wanatembea, wenye ukoma
wanatakaswa, viziwi wanasikia, wafu wanafu-
fuliwa, na maskini wanahubiriwa habari njema.
6 Amebarikiwa mtu yule asiyechukizwa na
mimi.”
7 Wale wanafunzi wa Yohana walipokuwa
wanaondoka, Yesu akaanza kusema na maku-
tano kuhusu Yohana Mbatizaji. Akawauliza,
“Mlipokwenda kule nyikani, mlikwenda kuona
nini? Je, ni unyasi ukipeperushwa na upepo?
8 Kama sivyo, mlikwenda kuona nini basi? Mtu
aliyevaa mavazi ya kifahari? La hasha, watu
wanaovaa mavazi ya kifahari wako katika ma-
jumba ya wafalme. 9 Basi mlikwenda kuona
nini? Mlikwenda kumwona nabii? Naam,
nawaambia, yeye ni zaidi ya nabii. 10 Huyu ndiye
ambaye habari zake zimeandikwa:

“ ‘Tazama nitamtuma mjumbe wangu mbele yako,
atakayetengeneza njia mbele yako.’

11 Amin, nawaambia, miongoni mwa wale
waliozaliwa na wanawake, hajatokea mtu aliye
mkuu kuliko Yohana Mbatizaji. Lakini aliye
mdogo kabisa katika Ufalme wa Mbinguni ni
mkuu kuliko Yohana. 12 Tangu siku za Yohana

* **11:2** Kristo maana yake ni Masiya, yaani Aliyetiwa mafuta.

Mbatizaji hadi sasa, Ufalme wa Mbinguni hupatikana kwa nguvu, nao wenye nguvu wanauteka.
13 Kwa maana manabii wote na Sheria walitabiri mpaka wakati wa Yohana.
14 Ikiwa mko tayari kukubali hilo, yeye ndiye yule Eliya ambaye manabii walikuwa wamesema angekuja.
15 Yeye aliye na masikio, na asikie.

16 "Lakini kizazi hiki nikifananishe na nini? Kinafanana na watoto waliokaa sokoni wakiwaita wenzao na kuwaambia,

17 " 'Tuliwapigia filimbi,
lakini hamkucheza;
tuliwaimbia nyimbo za maombolezo,
lakini hamkuomboleza.'
18 Kwa maana Yohana Mbatizaji alikuja, alikuwa hali wala hanywi, nao wanasema, 'Yeye ana pepo mchafu.'
19 Mwana wa Adamu alikuja akila na kunywa, nao wanasema, 'Tazameni huyu mlafi na mlevi, rafiki wa watoza ushuru na "wenye dhambi." ' Lakini hekima huthibitishwa kuwa kweli kwa matendo yake."

### *Onyo Kwa Miji Isiyotubu*
### *(Luka 10:13-15)*

20 Ndipo Yesu akaanza kushutumu miji ambamo alifanya miujiza yake mingi kuliko kwingine, kwa maana watu wake hawakutubu.
21 "Ole wako, Korazini! Ole wako Bethsaida! Kwa maana kama miujiza iliyofanyika kwenu, ingefanyika Tiro na Sidoni, miji hiyo ingekuwa imetubu zamani kwa kuvaa magunia na kujipaka majivu.
22 Lakini nawaambia, itakuwa rahisi zaidi kwa Tiro na Sidoni kustahimili

katika siku ya hukumu, kuliko ninyi. 23 Nawe
Kapernaumu, je, utainuliwa hadi mbinguni?
La hasha, utashushwa mpaka kuzimu.†Miujiza
iliyofanyika kwako ingefanyika huko Sodoma,
mji huo ungalikuwepo hadi leo. 24 Lakini
nakuambia kwamba, itakuwa rahisi zaidi kwa
Sodoma kustahimili katika siku ya hukumu
kuliko wewe."

### *Hakuna Amjuaye Baba Ila Mwana (Luka 10:21-22)*

25 Wakati huo Yesu alisema, "Nakuhimidi
Baba, Bwana wa mbingu na nchi, kwa kuwa
umewaficha mambo haya wenye hekima na
wenye elimu, nawe ukawafunulia watoto
wadogo. 26 Naam, Baba, kwa kuwa hivyo ndivyo
ilivyokupendeza.

27 "Nimekabidhiwa vitu vyote na Baba yangu:
Hakuna mtu amjuaye Mwana ila Baba, wala
hakuna amjuaye Baba ila Mwana na yeyote
ambaye Mwana anapenda kumfunulia.

### *Yesu Awaita Waliolemewa Na Mizigo*

28 "Njooni kwangu, ninyi nyote mnaotaabika
na kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha.
29 Jifungeni nira yangu, mjifunze kutoka
kwangu, kwa maana mimi ni mpole na
mnyenyekevu wa moyo, nanyi mtapata raha
nafsini mwenu. 30 Kwa maana nira yangu ni
laini na mzigo wangu ni mwepesi."

† **11:23** Kuzimu ni Mahali pa wafu.

# 12

*Bwana Wa Sabato*
*(Marko 2:23-28; Luka 6:1-5)*

1 Wakati huo Yesu alipitia kwenye mashamba
ya nafaka siku ya Sabato. Wanafunzi wake
walikuwa na njaa, nao wakaanza kuvunja ma-
suke ya nafaka na kuyala. 2 Lakini Mafarisayo
walipoona jambo hili, wakamwambia, “Tazama!
Wanafunzi wako wanafanya jambo lisilo halali
kufanywa siku ya Sabato.”

3 Yesu akawajibu, “Je, hamjasoma alichofanya
Daudi na wenzake walipokuwa na njaa?
4 Aliingia katika nyumba ya Mungu, akala
mikate iliyowekwa wakfu, yeye na wenzake,
jambo ambalo halikuwa halali kwao kufanya,
isipokuwa makuhani peke yao. 5 Au hamjasoma
katika Sheria kwamba siku ya Sabato makuhani
huvunja sheria ya Sabato Hekaluni lakini
hawahesabiwi kuwa na hatia? 6 Nawaambia
wazi kwamba, yeye aliye mkuu kuliko Hekalu
yupo hapa. 7 Kama mngekuwa mmejua maana
ya maneno haya, ‘Nataka rehema, wala si
dhabihu,’ msingewalaumu watu wasio na hatia,
8 kwa maana Mwana wa Adamu ndiye Bwana
wa Sabato.”

*Yesu Anamponya Mtu Aliyepooza Mkono*
*(Marko 3:1-6; Luka 6:6-11)*

9 Yesu akaondoka mahali hapo, akaingia ndani
ya sinagogi lao, 10 na huko alikuwepo mtu aliye-
pooza mkono. Wakitafuta sababu ya kumshtaki
Yesu, wakamuuliza, “Je, ni halali kuponya siku
ya Sabato?”

11 Yesu akawaambia, “Ni nani miongoni
mwenu, mwenye kondoo wake ambaye huyo
kondoo akitumbukia shimoni siku ya Sabato
hatamtoa? 12 Mtu ana thamani kubwa kuliko
kondoo. Kwa hiyo ni halali kutenda mema siku
ya Sabato.”
13 Ndipo akamwambia yule mtu, “Nyoosha
mkono wako.” Akaunyoosha, nao ukaponywa
ukawa mzima kama ule mwingine. 14 Lakini Ma-
farisayo wakatoka nje, wakafanya shauri baya
juu ya Yesu jinsi watakavyoweza kumuua.

*Mtumishi Aliyechaguliwa Na Mungu*

15 Lakini Yesu alipoyatambua mawazo yao,
akaondoka mahali hapo. Watu wengi wakam-
fuata, naye akawaponya wagonjwa wao wote,
16 akiwakataza wasiseme yeye ni nani. 17 Hii
ilikuwa ili litimie lile neno lililonenwa kwa
kinywa cha nabii Isaya kusema:

18 “Tazama mtumishi wangu niliyemchagua,
mpendwa wangu, ninayependezwa naye.
Nitaweka Roho wangu juu yake,
naye atatangaza haki kwa mataifa.
19 Hatagombana wala hatapiga kelele,
wala hakuna atakayesikia sauti yake njiani.
20 Mwanzi uliopondeka hatauvunja,
na utambi unaofuka moshi hatauzima,
mpaka atakapoifanya haki ishinde.
21 Katika Jina lake mataifa
wataweka tumaini lao.”

*Yesu Na Beelzebuli*
*(Marko 3:20-30; Luka 11:14-23)*

22 Kisha wakamletea mtu aliyekuwa amepa-
gawa na pepo mchafu, na alikuwa kipofu na bubu. Yesu akamponya, hata akaweza kusema
na kuona. 23 Watu wote wakashangaa na
kusema, “Je, yawezekana huyu ndiye Mwana wa Daudi?”

24 Lakini Mafarisayo waliposikia jambo hili wakasema, “Mtu huyu anatoa pepo wachafu kwa uwezo wa Beelzebuli,* mkuu wa pepo wachafu.”

25 Yesu alijua walichokuwa wakiwaza, hivyo akawaambia, “Kila ufalme ukigawanyika dhidi yake wenyewe huangamia. Hali kadhalika kila mji au watu wa nyumba moja waliogawanyika dhidi yao wenyewe hawawezi kusi-
mama. 26 Kama Shetani akimtoa Shetani, atakuwa amegawanyika yeye mwenyewe. Basi
ufalme wake utawezaje kusimama? 27 Nami
kama natoa pepo wachafu kwa nguvu za Beelzebuli, watu wenu je, wao hutoa pepo wachafu kwa uwezo wa nani? Hivyo basi, wao ndio
watatakaowahukumu. 28 Lakini kama mimi ni-
natoa pepo wachafu kwa Roho wa Mungu, basi Ufalme wa Mungu umekuja juu yenu.

29 “Au tena, mtu awezaje kuingia katika nyumba ya mtu mwenye nguvu na kuteka nyara mali zake asipomfunga kwanza yule mwenye nguvu? Akishamfunga, ndipo hakika anaweza kuteka nyara mali zake.

30 “Mtu asiyekuwa pamoja nami yu kinyume nami, na mtu ambaye hakusanyi pamoja nami,

* **12:24** Beelzebuli au Beelzebubu; pia 12:27.

hutawanya. 31 Kwa hiyo nawaambia, kila
dhambi na kufuru watu watasamehewa, lakini
mtu atakayemkufuru Roho Mtakatifu hatasame-
hewa. 32 Mtu yeyote atakayesema neno dhidi
ya Mwana wa Adamu atasamehewa, lakini
yeyote anenaye neno dhidi ya Roho Mtakatifu
hatasamehewa, iwe katika ulimwengu huu au
katika ulimwengu ujao.

### *Mti Na Matunda Yake*
### *(Luka 6:43-45)*

33 “Ufanye mti kuwa mzuri, nayo matunda
yake yatakuwa mazuri. Au ufanye mti kuwa
mbaya, na matunda yake yatakuwa mabaya.
Kwa maana mti hutambulika kwa matunda
yake. 34 Enyi uzao wa nyoka! Mnawezaje
kunena mambo mema, wakati ninyi ni waovu?
Kwa maana kinywa cha mtu huyanena yale
yaliyoujaza moyo wake. 35 Mtu mwema hutoa
yaliyo mema kutoka hazina ya mambo mema
yaliyohifadhiwa ndani yake, naye mtu mwovu
hutoa yaliyo maovu kutoka hazina ya mambo
maovu yaliyohifadhiwa ndani yake. 36 Lakini
nawaambia, katika siku ya hukumu watu wata-
toa hesabu kuhusu kila neno lisilo maana walilo-
nena. 37 Kwa maana kwa maneno yako utah-
esabiwa haki, na kwa maneno yako utahuku-
miwa.”

### *Ishara Ya Yona*
### *(Marko 8:11-12; Luka 11:29-32)*

38 Kisha baadhi ya Mafarisayo na walimu
wa sheria wakamwambia, “Mwalimu, tunataka
kuona ishara kutoka kwako.”

39 Lakini yeye akawajibu, “Kizazi kiovu na
cha uzinzi kinaomba ishara! Lakini hakitapewa
ishara yoyote isipokuwa ile ishara ya nabii Yona.
40 Kwa maana kama vile Yona alivyokuwa ndani
ya tumbo la nyangumi† kwa siku tatu, usiku
na mchana, vivyo hivyo Mwana wa Adamu
atakuwa katika moyo wa nchi siku tatu, usiku
na mchana. 41 Siku ya hukumu watu wa
Ninawi watasimama pamoja na kizazi hiki na
kukihukumu; kwa maana wao walitubu wali-
posikia mahubiri ya Yona. Na tazama, hapa
yupo yeye aliye mkuu kuliko Yona. 42 Malkia
wa Kusini atasimama wakati wa hukumu na
kukihukumu kizazi hiki. Kwa kuwa yeye alikuja
kutoka miisho ya dunia ili kuisikiliza hekima
ya Solomoni. Na hapa yupo aliye mkuu kuliko
Solomoni.”

*Mafundisho Kuhusu Pepo Mchafu*
*(Luka 11:24-26)*

43 “Pepo mchafu amtokapo mtu, hutangatanga
katika sehemu zisizo na maji akitafuta mahali pa
kupumzika, lakini hapati. 44 Ndipo husema, ‘Ni-
tarudi kwenye nyumba yangu nilikotoka.’ Naye
arudipo huikuta ile nyumba ikiwa tupu, imefag-
iliwa na kupangwa vizuri. 45 Kisha huenda na
kuwaleta pepo wachafu wengine saba wabaya
kuliko yeye mwenyewe, nao huingia na kukaa
humo. Nayo hali ya mwisho ya yule mtu
huwa ni mbaya kuliko ile ya kwanza. Ndivyo
itakavyokuwa kwa kizazi hiki kiovu.”

---

† **12:40** Nyangumi ni samaki mkubwa sana.

### *Mama Na Ndugu Zake Yesu*
*(Marko 3:31-35; Luka 8:19-21)*

46 Wakati alikuwa angali anazungumza na
makutano, mama yake na ndugu zake wakasi-
mama nje wakitaka kuongea naye. 47 Ndipo
mtu mmoja akamwambia, “Tazama, mama yako
na ndugu zako wamesimama nje, wanataka
kuongea na wewe.”
48 Lakini yeye akamjibu na kumwambia yule
mtu, “Mama yangu ni nani, nao ndugu zangu
ni nani?” 49 Akawanyooshea mkono wanafunzi
wake, akasema, “Hawa hapa ndio mama yangu
na ndugu zangu! 50 Kwa maana yeyote afanyaye
mapenzi ya Baba yangu wa mbinguni, huyo
ndiye ndugu yangu, na dada yangu na mama
yangu.”

# 13

### *Mfano Wa Mpanzi*
*(Marko 4:1-9; Luka 8:4-8)*

1 Siku iyo hiyo Yesu akatoka nje ya nyumba,
akaketi kando ya bahari. 2 Umati mkubwa mno
wa watu ukakusanyika kumzunguka, hata ik-
abidi aingie katika chombo na kuketi humo, nao
watu wote wakawa wamesimama ukingoni mwa
bahari. 3 Ndipo akawaambia mambo mengi
kwa mifano, akisema: “Mpanzi alitoka kwenda
kupanda mbegu zake. 4 Alipokuwa akitawanya
mbegu, nyingine zilianguka kando ya njia, nao
ndege wakaja na kuzila. 5 Nyingine zilianguka
kwenye ardhi yenye mwamba isiyo na udongo
wa kutosha. Zikaota haraka, kwa kuwa udongo

ulikuwa haba. 6 Lakini jua lilipozidi, mimea
ikanyauka na kukauka kwa kuwa mizizi yake
haikuwa na kina. 7 Mbegu nyingine zilian-
guka kwenye miiba, nayo miiba hiyo ikakua,
ikaisonga hiyo mimea. 8 Mbegu nyingine zil-
ianguka kwenye udongo mzuri ambapo zilitoa
mazao, nyingine mara mia moja, nyingine mara
sitini, na nyingine mara thelathini. 9 Mwenye
masikio ya kusikia, na asikie."

### *Sababu Ya Kufundisha Kwa Mifano*
### *(Marko 4:10-12; Luka 8:9-10)*

10 Wanafunzi wake wakamwendea, waka-
muuliza, "Kwa nini unasema na watu kwa
mifano?"

11 Akawajibu, "Ninyi mmepewa kuzifahamu
siri za Ufalme wa Mbinguni, lakini wao hawa-
japewa. 12 Kwa maana yule aliye na kitu atapewa
zaidi, naye atakuwa navyo tele. Lakini yule asiye
na kitu, hata kile alicho nacho atanyang'anywa.
13 Hii ndiyo sababu nasema nao kwa mifano:

"Ingawa wanatazama, hawaoni;
wanasikiliza, lakini hawasikii, wala hawaelewi.
14 Kwao unatimia ule unabii wa Isaya aliposema:
" 'Hakika mtasikiliza lakini hamtaelewa;
na pia mtatazama lakini hamtaona.
15 Kwa kuwa mioyo ya watu hawa imekuwa migumu;
hawasikii kwa masikio yao,
na wamefumba macho yao.
Wasije wakaona kwa macho yao,
na wakasikiliza kwa masikio yao,
wakaelewa kwa mioyo yao,

na kugeuka nami nikawaponya.’
16 Lakini heri macho yenu kwa sababu yanaona,
na heri masikio yenu kwa sababu yanasikia.
17 Amin, nawaambia, manabii wengi na wenye
haki walitamani kuona yale mnayoyaona lakini
hawakuyaona, na walitamani kusikia yale mnay-
oyasikia lakini hawakuyasikia.

### *Maelezo Ya Mfano Wa Mbegu*
### *(Marko 4:13-20; Luka 8:11-15)*

18 “Sikilizeni basi maana ya ule mfano wa
mpanzi: 19 Mtu yeyote anaposikia neno la
Ufalme naye asilielewe, yule mwovu huja na
kunyakua kile kilichopandwa moyoni mwake.
Hii ndiyo ile mbegu iliyopandwa kando ya njia.
20 Ile mbegu iliyopandwa kwenye sehemu yenye
mawe ni mtu yule ambaye hulisikia neno na
mara hulipokea kwa furaha. 21 Lakini kwa kuwa
hana mizizi yenye kina ndani yake, lile neno
hudumu kwa muda mfupi tu. Kisha dhiki au
mateso yanapoinuka kwa ajili ya lile neno, yeye
mara huchukizwa. 22 Ile mbegu iliyopandwa
katika miiba ni yule mtu alisikiaye neno, lakini
masumbufu ya maisha haya na udanganyifu wa
mali hulisonga lile neno na kulifanya lisizae
matunda. 23 Lakini ile mbegu iliyopandwa
kwenye udongo mzuri ni yule mtu ambaye
hulisikia neno na kulielewa. Naye hakika huzaa
matunda, akizaa mara mia, au mara sitini, au
mara thelathini ya mbegu iliyopandwa.”

### *Mfano Wa Magugu*

24 Yesu akawaambia mfano mwingine,
akasema: “Ufalme wa Mbinguni unaweza

kufananishwa na mtu aliyepanda mbegu nzuri
katika shamba lake. 25 Lakini wakati kila mtu
alipokuwa amelala, adui yake akaja na kupanda
magugu katikati ya ngano, akaenda zake.
26 Ngano ilipoota na kutoa masuke, magugu
nayo yakatokea.
27 "Watumishi wa yule mwenye shamba
wakamjia na kumwambia, 'Bwana, si tulipanda
mbegu nzuri shambani mwako? Basi, magugu
yametoka wapi?'
28 "Akawajibu, 'Adui ndiye alifanya jambo
hili.'
"Wale watumishi wakamuuliza, 'Je, unataka
twende tukayang'oe?'
29 "Lakini akasema, 'Hapana, msiyang'oe,
kwa maana wakati mking'oa magugu mnaweza
mkang'oa na ngano pamoja nayo. 30 Acheni
ngano na magugu vikue vyote pamoja mpaka
wakati wa mavuno. Wakati huo nitawaambia
wavunaji wayakusanye magugu kwanza, waya-
funge matita matita ili yachomwe moto; kisha
wakusanye ngano na kuileta ghalani mwangu.' "

### *Mfano Wa Mbegu Ya Haradali*
*(Marko 4:30-32; Luka 13:18-19)*

31 Akawaambia mfano mwingine, akasema,
"Ufalme wa Mbinguni ni kama punje ya
haradali, ambayo mtu aliichukua, akaipanda
shambani mwake. 32 Ingawa mbegu hiyo ni
ndogo kuliko mbegu zote, lakini inapokua ni
mmea mkubwa kuliko yote ya bustanini, nao
huwa mti mkubwa, hadi ndege wa angani
wanakuja na kutengeneza viota katika matawi
yake."

### *Mfano Wa Chachu*
### *(Luka 13:20-21)*

33 Akawaambia mfano mwingine, “Ufalme
wa Mbinguni unafanana na chachu ambayo
mwanamke aliichukua akaichanganya katika ki-
asi kikubwa cha unga mpaka wote ukaumuka.”

### *Sababu Ya Yesu Kutumia Mifano*
### *(Marko 4:33-34)*

34 Yesu alinena mambo haya yote kwa maku-
tano kwa mifano. Wala hakuwaambia lolote
pasipo mfano. 35 Hii ilikuwa ili kutimiza lile
lililonenwa kwa kinywa cha nabii aliposema:

“Nitafungua kinywa changu niseme nao kwa
mifano;
nitahubiri mambo yaliyofichika
tangu kuumbwa kwa misingi ya
ulimwengu.”

### *Ufafanuzi Wa Mfano Wa Magugu*

36 Kisha Yesu akaagana na makutano, akain-
gia nyumbani. Wanafunzi wake wakamjia
wakamwambia, “Tueleze maana ya ule mfano
wa magugu shambani.”

37 Akawaambia, “Aliyepanda mbegu nzuri ni
Mwana wa Adamu. 38 Shamba ni ulimwengu na
mbegu nzuri ni wana wa Ufalme. Magugu ni
wana wa yule mwovu. 39 Yule adui aliyepanda
magugu ni ibilisi. Mavuno ni mwisho wa dunia,
nao wavunaji ni malaika.

40 “Kama vile magugu yang’olewavyo na ku-
chomwa motoni, ndivyo itakavyokuwa wakati
wa mwisho wa dunia. 41 Mwana wa Adamu

atawatuma malaika zake, nao watakusanya ku-
toka Ufalme wake kila kitu kinachosababisha
dhambi na watenda maovu wote. 42 Nao
watawatupa katika tanuru la moto ambako ku-
takuwa na kilio na kusaga meno. 43 Ndipo wenye
haki watang'aa kama jua katika Ufalme wa Baba
yao. Yeye aliye na masikio, na asikie.

### *Mfano Wa Hazina Iliyofichwa Na Lulu*

44 "Ufalme wa Mbinguni unafanana na haz-
ina iliyofichwa shambani, ambayo mtu mmoja
alipoiona akaificha tena. Kisha katika furaha
yake, akaenda akauza vyote alivyokuwa navyo,
akalinunua lile shamba."
45 "Tena, Ufalme wa Mbinguni unafanana na
mfanyabiashara aliyekuwa akitafuta lulu safi.
46 Alipoipata lulu moja ya thamani kubwa, alik-
wenda akauza vyote alivyokuwa navyo akain-
unua."

### *Mfano Wa Wavu*

47 "Tena, Ufalme wa Mbinguni ni kama wavu
wa kuvua samaki uliotupwa baharini ukavua
samaki wa kila aina. 48 Ulipojaa, wavuvi
wakavuta pwani, wakaketi na kukusanya samaki
wazuri kuwaweka kwenye vyombo safi, lakini
wale samaki wabaya wakawatupa. 49 Hivi
ndivyo itakavyokuwa wakati wa mwisho wa
dunia. Malaika watakuja na kuwatenganisha
watu waovu na watu wenye haki. 50 Nao
watawatupa hao waovu katika tanuru la moto
ambako kutakuwa na kilio na kusaga meno."
51 Yesu akauliza, "Je, mmeyaelewa haya yote?"
Wakamjibu, "Ndiyo."

52 Akawaambia, “Basi kila mwalimu wa sheria
aliyefundishwa elimu ya Ufalme wa Mbinguni ni
kama mwenye nyumba anayetoa kutoka ghala
yake mali mpya na mali ya zamani.”

### *Yesu Akataliwa Nazareti (Marko 6:1-6; Luka 4:16-30)*

53 Yesu alipomaliza kutoa mifano hii, akaon-
doka. 54 Alipofika mji wa kwao, akawafundisha
watu katika sinagogi lao. Nao wakastaajabu,
wakauliza, “Mtu huyu amepata wapi hekima hii
na uwezo huu wa kufanya miujiza?” 55 “Huyu
si yule mwana wa seremala? Mama yake si
yeye aitwaye Maria, nao ndugu zake si Yakobo,
Yosefu, Simoni na Yuda? 56 Nao dada zake wote,
hawako hapa pamoja nasi? Mtu huyu amepata
wapi basi mambo haya yote?” 57 Wakachukizwa
naye.

Lakini Yesu akawaambia, “Nabii hakosi heshima, isipokuwa katika nchi yake na nyumbani kwake.”

58 Naye hakufanya miujiza mingi huko kwa
sababu ya kutokuamini kwao.

# 14

### *Yohana Mbatizaji Akatwa Kichwa (Marko 6:14-29; Luka 9:7-9)*

1 Wakati huo, Mfalme Herode, mtawala wa
Galilaya, alisikia habari za Yesu, 2 akawaambia
watumishi wake, “Huyu ni Yohana Mbatizaji;
amefufuka kutoka kwa wafu! Hii ndiyo sababu
nguvu za kutenda miujiza zinafanya kazi ndani
yake.”

3 Herode alikuwa amemkamata Yohana, akam-
funga na kumweka gerezani kwa sababu ya
Herodia, mke wa Filipo, ndugu yake, 4 kwa
kuwa Yohana alikuwa amemwambia Herode:
“Si halali kwako kuwa na huyo mwanamke.”
5 Herode alitaka sana kumuua Yohana, lakini
akaogopa watu, kwa maana walimtambua kuwa
ni nabii.

6 Katika siku ya kuadhimisha sikukuu ya kuza-
liwa kwa Herode, binti wa Herodia alicheza
mbele ya watu waliohudhuria, akamfurahisha
sana Herode, 7 kiasi kwamba aliahidi kwa kiapo
kumpa huyo binti chochote angeomba. 8 Huyo
binti, akiwa amechochewa na mama yake,
akasema, “Nipe kichwa cha Yohana Mbatizaji
kwenye sinia.” 9 Mfalme akasikitika, lakini kwa
sababu ya viapo alivyoapa mbele ya wageni,
akaamuru kwamba apatiwe ombi lake. 10 Hivyo
akaagiza Yohana Mbatizaji akatwe kichwa mle
gerezani. 11 Kichwa chake kikaletwa kwenye
sinia, akapewa yule binti, naye akampelekea
mama yake. 12 Wanafunzi wa Yohana wakaja na
kuuchukua mwili wake kwenda kuuzika. Kisha
wakaenda wakamwambia Yesu.

### *Yesu Alisha Wanaume 5,000*
### *(Marko 6:30-44; Luka 9:10-17; Yohana 6:1-14)*

13 Yesu aliposikia yaliyokuwa yametukia,
aliondoka kwa chombo akaenda mahali pasipo
na watu ili awe peke yake. Lakini watu
walipopata habari, wakamfuata kwa miguu
kupitia nchi kavu kutoka miji. 14 Yesu alipofika
kando ya bahari, aliona makutano makubwa ya

watu, akawahurumia na akawaponya wagonjwa wao.
15 Ilipofika jioni, wanafunzi wake walienda kwake, wakamwambia, “Mahali hapa ni nyikani, na muda sasa umekwisha. Waage makutano ili waende zao vijijini wakajinunulie chakula.”
16 Yesu akawaambia, “Hakuna sababu ya wao kuondoka. Ninyi wapeni chakula.”
17 Wakamjibu, “Tuna mikate mitano na samaki wawili tu.”
18 Akawaambia, “Nileteeni hivyo vitu hapa.”
19 Yesu akaagiza makutano wakae chini kwenye nyasi. Akaichukua ile mikate mitano na wale samaki wawili, akainua macho yake akatazama mbinguni, akavibariki na kuimega ile mikate. Kisha akawapa wanafunzi, nao
wanafunzi wakawagawia makutano. 20 Wote
wakala, wakashiba. Nao wanafunzi wakakusanya vipande vilivyosalia, wakajaza vikapu
kumi na viwili. 21 Idadi ya watu waliokula walikuwa wanaume wapatao 5,000, bila kuhesabu wanawake na watoto.

### *Yesu Atembea Juu Ya Maji (Marko 6:45-52; Yohana 6:15-21)*

22 Mara Yesu akawaambia wanafunzi wake waingie kwenye mashua watangulie kwenda ng’ambo ya bahari, wakati yeye alikuwa akiwaaga wale makutano.
23 Baada ya kuwaaga,
akaenda zake mlimani peke yake kuomba. Jioni
ilipofika, Yesu alikuwa huko peke yake. 24 Wakati
huo ile mashua ilikuwa mbali kutoka nchi kavu ikisukwasukwa na mawimbi, kwa sababu upepo ulikuwa wa mbisho.

25 Wakati wa zamu ya nne ya usiku,* Yesu
akawaendea wanafunzi wake akiwa anatembea
juu ya maji. 26 Wanafunzi wake walipomwona
akitembea juu ya maji, waliingiwa na hofu kuu,
wakasema, "Ni mzimu." Wakapiga yowe kwa
kuogopa.

27 Lakini mara Yesu akasema nao, akawaambia, "Jipeni moyo! Ni mimi. Msiogope."

28 Petro akamjibu, "Bwana, ikiwa ni wewe, niambie nije kwako nikitembea juu ya maji."

29 Yesu akamwambia, "Njoo."

Basi Petro akatoka kwenye chombo, akatem-
bea juu ya maji kumwelekea Yesu. 30 Lakini
alipoona upepo mkali aliingiwa na hofu, naye
akaanza kuzama, huku akipiga kelele, "Bwana,
niokoe!"

31 Mara Yesu akaunyoosha mkono wake na kumshika, akamwambia, "Wewe mwenye imani haba, kwa nini uliona shaka?"

32 Nao walipoingia ndani ya mashua, upepo
ukakoma. 33 Ndipo wote waliokuwa ndani
ya ile mashua wakamwabudu Yesu, wakisema,
"Hakika, wewe ndiwe Mwana wa Mungu."

### *Yesu Awaponya Wagonjwa Genesareti (Marko 6:53-56)*

34 Walipokwisha kuvuka, wakafika nchi ya
Genesareti. 35 Watu wa eneo lile walipom-
tambua Yesu, walipeleka habari sehemu zote
za jirani. Watu wakamletea wagonjwa wao

* **14:25** Zamu ya nne ya usiku ni kati ya saa tisa na saa kumi na mbili asubuhi.

wote, 36 wakamsihi awaruhusu wagonjwa wa-
guse tu pindo la vazi lake, nao wote waliomgusa,
wakaponywa.

# 15

*Mapokeo Ya Wazee*
*(Marko 7:1-13)*

1 Ndipo baadhi ya Mafarisayo na walimu wa
sheria wakamjia Yesu kutoka Yerusalemu na ku-
muuliza, 2 "Mbona wanafunzi wako wanakiuka
mapokeo ya wazee? Kwa maana wao hawanawi
mikono yao kabla ya kula!"

3 Yesu akawajibu, "Mbona ninyi mnavunja
amri ya Mungu kwa ajili ya mapokeo yenu?
4 Kwa maana Mungu alisema, 'Waheshimu baba
yako na mama yako,' na, 'Yeyote amtukanaye
baba yake au mama yake, na auawe.' 5 Lakini
ninyi mwafundisha kwamba mtu akimwambia
baba yake au mama yake, 'Kile ambacho
ningeweza kukusaidia kimewekwa wakfu kwa
Mungu,' 6 basi hana tena sababu ya kumheshimu
baba yake nacho. Basi kwa ajili ya mafundisho
yenu mnavunja amri ya Mungu. 7 Ninyi
wanafiki! Isaya alikuwa sawa alipotabiri juu
yenu kwamba:

8 " 'Watu hawa huniheshimu kwa midomo yao,
lakini mioyo yao iko mbali nami.
9 Huniabudu bure;
nayo mafundisho yao
ni maagizo ya wanadamu tu.' "

*Vitu Vitiavyo Unajisi*
*(Marko 7:14-23)*

10 Yesu akaita ule umati wa watu, akawaambia,
“Sikilizeni na mwelewe: 11 kinachomfanya mtu
kuwa najisi mbele za Mungu si kile kiingiacho
kinywani mwake, bali ni kile kitokacho kinywani
mwake.”
12 Kisha wanafunzi wake wakamjia na
kumuuliza, “Je, unajua kwamba Mafarisayo
walichukizwa sana waliposikia yale uliyosema?”
13 Akawajibu, “Kila pando ambalo Baba
yangu wa mbinguni hakulipanda, litang’olewa.
14 Waacheni; wao ni viongozi vipofu, wanaoon-
goza vipofu. Kama kipofu akimwongoza kipofu
mwenzake, wote wawili watatumbukia shi-
moni.”
15 Petro akasema, “Tueleze maana ya huu
mfano.”
16 Yesu akawauliza, “Je, bado ninyi hamfa-
hamu? 17 Je, hamwelewi kwamba chochote
kiingiacho kinywani huenda tumboni, na hati-
maye hutolewa nje kikiwa uchafu? 18 Lakini
kitokacho kinywani hutoka moyoni, na hiki
ndicho kimtiacho mtu unajisi. 19 Kwa maana
ndani ya moyo hutoka mawazo mabaya, uuaji,
uzinzi, uasherati, wizi, ushahidi wa uongo na
masingizio. 20 Haya ndiyo yamtiayo mtu unajisi;
lakini kula bila kunawa mikono hakumtii mtu
unajisi.”

### *Imani Ya Mwanamke Mkanaani (Marko 7:24-30)*

21 Yesu aliondoka mahali pale, akaenda se-
hemu za Tiro na Sidoni. 22 Mwanamke mmoja
Mkanaani aliyeishi sehemu jirani na hizo akaja
kwake akilia, akasema, “Nihurumie, Ee Bwana,

Mwana wa Daudi! Binti yangu amepagawa na pepo mchafu, na anateseka sana."

23 Lakini Yesu hakumjibu neno. Hivyo wanafunzi wake wakamwendea na kumsihi sana, wakisema, "Mwambie aende zake, kwa maana anaendelea kutupigia kelele."

24 Yesu akajibu, "Nimetumwa tu kwa ajili ya kondoo wa Israeli waliopotea."

25 Lakini yule mwanamke akaja, akapiga magoti mbele ya Yesu, akasema, "Bwana, nisaidie!"

26 Yesu akajibu, "Si haki kuchukua chakula cha watoto na kuwatupia mbwa."

27 Yule mwanamke akajibu, "Ndiyo, Bwana, lakini hata mbwa hula makombo yanayoanguka kutoka kwenye meza za bwana zao."

28 Ndipo Yesu akamwambia, "Mwanamke, imani yako ni kubwa! Iwe kwako kama unavyotaka." Naye binti yake akapona tangu saa ile.

### *Yesu Aponya Watu Wengi*

29 Yesu akaondoka na kwenda kando ya Bahari ya Galilaya. Kisha akapanda mlimani, akaketi
huko. 30 Umati mkubwa wa watu ukamjia, wakiwaleta vilema, vipofu, viwete, bubu na wengine wengi, wakawaweka miguuni pake;
naye akawaponya. 31 Hao watu wakashangaa walipoona bubu wakisema, vilema wakipona, viwete wakitembea na vipofu wakiona, wakamtukuza Mungu wa Israeli.

### *Yesu Alisha Watu Elfu Nne*
### *(Marko 8:1-10)*

32 Kisha Yesu akawaita wanafunzi wake,
akawaambia, “Ninauhurumia huu umati wa
watu, kwa sababu sasa wamekuwa pamoja nami
kwa muda wa siku tatu, na hawana chakula
chochote. Nami sipendi kuwaaga wakiwa na
njaa, wasije wakazimia njiani.”

33 Wanafunzi wake wakasema, “Tutapata wapi
mikate ya kutosha kuwalisha umati huu wa watu
mkubwa namna hii, nasi tuko nyikani?”

34 Yesu akawauliza, “Mnayo mikate mingapi?”

Wakamjibu, “Tunayo mikate saba na visamaki
vichache.”

35 Yesu akawaambia ule umati wa watu waketi
chini. 36 Kisha akachukua ile mikate saba na
wale samaki, naye akiisha kumshukuru Mungu,
akavimega na kuwapa wanafunzi wake, nao
wakawapa ule umati wa watu. 37 Wote wakala
na kushiba. Baadaye wanafunzi wakakusanya
vipande vilivyosalia, wakajaza vikapu saba.
38 Idadi ya watu walikuwa wanaume 4,000, bila
kuhesabu wanawake na watoto. 39 Baada ya
kuaga ule umati wa watu, Yesu aliingia katika
mashua, akaenda sehemu za Magadani.*

# 16

### *Mafarisayo Wadai Ishara (Marko 8:11-13; Luka 12:54-56)*

1 Mafarisayo na Masadukayo wakamjia Yesu
na kumjaribu kwa kumwomba awaonyeshe
ishara kutoka mbinguni.

---

* **15:39** Magadani ni Magdala, mji wa Galilaya, kama kilomita 16 kusini mwa Kapernaumu.

[2] Yesu akawajibu, “Ifikapo jioni, mnasema,
‘Hali ya hewa itakuwa nzuri, kwa kuwa anga
ni nyekundu.’ [3] Nanyi wakati wa asub-
uhi mnasema, ‘Leo kutakuwa na dhoruba,
kwa sababu anga ni nyekundu na mawingu
yametanda.’ Mnajua jinsi ya kupambanua kule
kuonekana kwa anga, lakini hamwezi kupam-
banua dalili za nyakati. [4] Kizazi kiovu na
cha uzinzi kinatafuta ishara, lakini hakitapewa
ishara yoyote isipokuwa ishara ya Yona.” Yesu
akawaacha, akaenda zake.

### *Chachu Ya Mafarisayo Na Masadukayo (Marko 8:14-21)*

[5] Wanafunzi wake walipofika ng’ambo ya ba-
hari, walikuwa wamesahau kuchukua mikate.
[6] Yesu akawaambia, “Jihadharini. Jilindeni na
chachu ya Mafarisayo na ya Masadukayo.”

[7] Wakajadiliana wao kwa wao, wakisema, “Ni
kwa sababu hatukuleta mikate.”

[8] Yesu, akifahamu majadiliano yao, akauliza,
“Enyi wa imani haba! Mbona mnajadiliana
miongoni mwenu kuhusu kutokuwa na mikate?
[9] Je, bado hamwelewi? Je, hamkumbuki
ile mikate mitano iliyolisha watu 5,000 na
idadi ya vikapu vingapi vya mabaki mlivyoku-
sanya? [10] Au ile mikate saba iliyolisha watu
4,000 na idadi ya vikapu vingapi vya mabaki
mlivyokusanya? [11] Inakuwaje mnashindwa
kuelewa kwamba nilikuwa sisemi nanyi habari
za mikate? Jilindeni na chachu ya Mafarisayo
na Masadukayo.” [12] Ndipo wakaelewa kwamba
alikuwa hasemi juu ya chachu ya kutengeneza

mikate, bali juu ya mafundisho ya Mafarisayo na Masadukayo.

### *Petro Amkiri Yesu Kuwa Ni Mwana Wa Mungu*
### *(Marko 8:27-30; Luka 9:18-21)*

13 Basi Yesu alipofika katika eneo la Kaisaria-Filipi, akawauliza wanafunzi wake, “Watu husema kwamba mimi Mwana wa Adamu ni nani?”

14 Wakamjibu, “Baadhi husema ni Yohana Mbatizaji; wengine husema ni Eliya; na bado wengine husema ni Yeremia au mmojawapo wa manabii.”

15 Akawauliza, “Je, ninyi mnasema mimi ni nani?”

16 Simoni Petro akamjibu, “Wewe ndiwe Kristo,* Mwana wa Mungu aliye hai.”

17 Naye Yesu akamwambia, “Heri wewe, Si-
moni Bar-Yona,†kwa maana hili halikufunuliwa
kwako na mwanadamu, bali na Baba yangu aliye
mbinguni. 18 Nami nakuambia, wewe ndiwe
Petro na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa
langu, hata malango ya Kuzimu hayataweza
kulishinda. 19 Nitakupa funguo za Ufalme
wa mbinguni, na lolote utakalolifunga duni-
ani litakuwa limefungwa Mbinguni, nalo lolote
utakalofungua duniani litakuwa limefunguliwa
mbinguni.” 20 Kisha akawakataza wanafunzi
wake wasimwambie mtu yeyote kwamba yeye
ndiye Kristo.

---

* **16:16** Kristo maana yake ni Masiya, yaani Aliyetiwa mafuta.

† **16:17** Bar-Yona ni neno la Kiaramu, maana yake ni Mwana wa Yona.

### *Yesu Anatabiri Juu Ya Kifo Chake (Marko 8:31–9:1; Luka 9:22-27)*

21 Tangu wakati huo, Yesu alianza kuwaeleza wanafunzi wake kwamba hana budi kwenda Yerusalemu na kupata mateso mengi mikononi mwa wazee, viongozi wa makuhani, na walimu wa sheria, na kwamba itampasa auawe lakini siku ya tatu kufufuliwa.

22 Petro akamchukua kando, akaanza kumkemea akisema, "Haiwezekani, Bwana! Jambo hili kamwe halitakupata!"

23 Lakini Yesu akageuka na kumwambia Petro, "Rudi nyuma yangu, Shetani! Wewe ni kikwazo kwangu. Moyo wako hauwazi yaliyo ya Mungu, bali ya wanadamu."

24 Ndipo Yesu akawaambia wanafunzi wake,
"Mtu yeyote akitaka kunifuata, ni lazima
ajikane mwenyewe, auchukue msalaba wake,
anifuate. 25 Kwa maana yeyote anayetaka
kuyaokoa maisha yake atayapoteza, lakini yey-
ote atakayeyapoteza maisha yake kwa ajili yangu
atayapata. 26 Kwa maana, je, itamfaidi nini mtu
kuupata ulimwengu wote, lakini akayapoteza
maisha yake? Au mtu atatoa nini badala ya
nafsi yake? 27 Kwa maana Mwana wa Adamu
atakuja katika utukufu wa Baba yake pamoja
na malaika zake, naye ndipo atakapomlipa kila
mtu kwa kadiri ya matendo yake. 28 Nawaambia
kweli, baadhi yenu hapa hawataonja mauti
kabla ya kumwona Mwana wa Adamu akija
katika Ufalme wake."

# 17

### *Yesu Abadilika Sura Mlimani*
### *(Marko 9:2-13; Luka 9:28-36)*

1 Siku sita baada ya jambo hili, Yesu
akawachukua Petro, Yakobo na Yohana ndugu
yake Yakobo, akawapeleka juu ya mlima mrefu
peke yao. 2 Wakiwa huko, Yesu alibadilika
sura mbele yao. Uso wake ukang'aa kama jua
na nguo zake zikawa na weupe wa kuumiza
macho. 3 Ghafula wakawatokea mbele yao Mose
na Eliya, wakizungumza na Yesu.

4 Ndipo Petro akamwambia Yesu, "Bwana,
ni vyema sisi tukae hapa. Ukitaka, nitafanya
vibanda vitatu: kimoja chako, kingine cha Mose
na kingine cha Eliya."

5 Petro alipokuwa angali ananena, ghafula
wingu lililong'aa likawafunika, na sauti ika-
toka kwenye hilo wingu ikisema, "Huyu ni
Mwanangu mpendwa. Ninapendezwa naye
sana. Msikieni yeye."

6 Wanafunzi waliposikia haya, wakaanguka
chini kifudifudi, wakajawa na hofu. 7 Lakini
Yesu akaja na kuwagusa, akawaambia, "Inukeni
na wala msiogope." 8 Walipoinua macho yao,
hawakumwona mtu mwingine yeyote isipokuwa
Yesu.

9 Walipokuwa wakishuka kutoka mlimani,
Yesu akawaagiza, "Msimwambie mtu yeyote
mambo mliyoyaona hapa, mpaka Mwana wa
Adamu atakapofufuliwa kutoka kwa wafu."

10 Wale wanafunzi wakamuuliza, "Kwa nini
basi walimu wa sheria husema kwamba ni
lazima Eliya aje kwanza?"

[11] Yesu akawajibu, “Ni kweli, Eliya lazima
aje kwanza, naye atatengeneza mambo yote.
[12] Lakini nawaambia, Eliya amekwisha kuja, nao
hawakumtambua, bali walimtendea kila kitu
walichotaka. Vivyo hivyo Mwana wa Adamu pia
atateswa mikononi mwao.” [13] Ndipo wale wana-
funzi wakaelewa kuwa alikuwa anazungumza
nao habari za Yohana Mbatizaji.

### *Yesu Amponya Kijana Mwenye Pepo (Marko 9:14-29; Luka 9:37-43)*

[14] Walipofika penye umati wa watu, mtu
mmoja akamjia Yesu na kupiga magoti
mbele yake, akasema, [15] “Bwana, mhurumie
mwanangu. Yeye ana kifafa na anateseka sana.
Mara kwa mara huanguka kwenye moto au
kwenye maji. [16] Nilimleta kwa wanafunzi wako,
lakini hawakuweza kumponya.”

[17] Yesu akajibu, “Enyi kizazi kisichoamini
na kilichopotoka! Nitakaa nanyi mpaka lini?
Nitawavumilia mpaka lini? Mleteni mvulana
hapa kwangu.” [18] Yesu akamkemea yule pepo
mchafu, akamtoka yule kijana, naye akapona saa
ile ile.

[19] Kisha wanafunzi wakamwendea Yesu
wakiwa peke yao, wakamuuliza, “Kwa nini
sisi hatukuweza kumtoa?”

[20] Akawajibu, “Kwa sababu ya imani yenu
ndogo. Ninawaambia kweli, mkiwa na imani
ndogo kama punje ya haradali, mtauambia
mlima huu, ‘Ondoka hapa uende pale,’ nao
utaondoka. Wala hakutakuwa na jambo
lisilowezekana kwenu. [ [21] Lakini hali kama hii
haitoki ila kwa kuomba na kufunga.]”

22 Siku moja walipokuwa pamoja huko
Galilaya, Yesu akawaambia, “Mwana wa
Adamu atasalitiwa na kutiwa mikononi mwa
watu. 23 Nao watamuua, lakini siku ya tatu
atafufuliwa.” Wanafunzi wakahuzunika sana.

### *Yesu Na Petro Watoa Kodi Ya Hekalu*

24 Baada ya Yesu na wanafunzi wake kufika Kapernaumu, wakusanya kodi ya Hekalu* wakamjia Petro na kumuuliza, “Je, Mwalimu wenu halipi kodi ya Hekalu?”
25 Petro akajibu, “Ndiyo, yeye hulipa.” Petro aliporudi nyumbani, Yesu akawa wa kwanza kulizungumzia, akamuuliza, “Unaonaje Simoni? Wafalme wa dunia hupokea ushuru na kodi kutoka kwa nani? Je, ni kutoka kwa watoto wao au kutoka kwa watu wengine?”
26 Petro akamjibu, “Kutoka kwa watu
wengine.” Yesu akamwambia, “Kwa hiyo
watoto wao wamesamehewa. 27 Lakini ili tusije
tukawaudhi, nenda baharini ukatupe ndoana. Mchukue samaki wa kwanza utakayemvua. Fungua kinywa chake nawe utakuta humo fedha, ichukue ukalipe kodi yako na yangu.”

# 18

### *Aliye Mkuu Katika Ufalme Wa Mbinguni (Marko 9:33-37; Luka 9:46-48)*

1 Wakati huo, wanafunzi wakamjia Yesu na kumuuliza, “Je, nani aliye mkuu kuliko wote katika Ufalme wa Mbinguni?”

---

* **17:24** Kodi ya Hekalu ilikuwa didrachmas, yaani drakma mbili, ambazo ni sawa na nusu shekeli.

2 Yesu akamwita mtoto mdogo na kumsi-
mamisha katikati yao. 3 Naye akasema: "Amin,
nawaambia, msipookoka na kuwa kama watoto
wadogo, kamwe hamtaingia katika Ufalme wa
Mbinguni. 4 Kwa hiyo mtu yeyote anyenyekeaye
kama huyu mtoto, ndiye aliye mkuu kuliko wote
katika Ufalme wa Mbinguni.
5 "Yeyote amkaribishaye mtoto mdogo kama
huyu kwa Jina langu, anikaribisha mimi.
6 Lakini kama mtu yeyote akimsababisha mmo-
jawapo wa hawa wadogo wanaoniamini kutenda
dhambi, ingekuwa bora kwake afungiwe jiwe
kubwa la kusagia shingoni mwake, na kutoswa
katika kilindi cha bahari.

### *Kujaribiwa Ili Kutenda Dhambi*
### *(Marko 9:42-48; Luka 17:1-2)*

7 "Ole kwa ulimwengu kwa sababu ya yale
mambo yanayosababisha watu kutenda dhambi!
Mambo hayo lazima yawepo, lakini ole wake
mtu yule ambaye huyasababisha. 8 Ikiwa mkono
wako au mguu wako unakusababisha utende
dhambi, ukate na uutupe mbali. Ni afadhali
kwako kuingia katika uzima ukiwa huna mkono
mmoja au mguu mmoja, kuliko kuwa na mikono
miwili au miguu miwili, na kutupwa katika moto
wa milele. 9 Nalo jicho lako likikusababisha
kutenda dhambi, ling'oe, ulitupe mbali. Ni
afadhali kwako kuingia katika uzima ukiwa na
jicho moja, kuliko kuwa na macho mawili lakini
ukatupwa katika moto wa jehanamu.

### *Mfano Wa Kondoo Aliyepotea*
### *(Luka 15:3-7)*

10 “Angalia ili usimdharau mmojawapo wa
hawa wadogo, kwa maana nawaambia, malaika
wao mbinguni daima wanauona uso wa Baba
yangu aliye mbinguni. [ 11 Kwa maana Mwana
wa Adamu alikuja kuokoa kile kilichopotea.]
12 “Mwaonaje? Ikiwa mtu ana kondoo mia
moja, na mmoja wao akapotea, je, hatawaacha
wale tisini na tisa vilimani na kwenda kumtafuta
huyo mmoja aliyepotea? 13 Naye akishampata,
amin, nawaambia, hufurahi zaidi kwa ajili ya
huyo kondoo mmoja kuliko wale tisini na tisa
ambao hawakupotea. 14 Vivyo hivyo, Baba
yenu wa mbinguni hapendi hata mmojawapo wa
hawa wadogo apotee.

*Ndugu Yako Akikukosea*

15 “Kama ndugu yako akikukosea, nenda
ukamwonyeshe kosa lake, kati yenu ninyi wawili
peke yenu. Kama akikusikiliza, utakuwa umem-
pata tena ndugu yako. 16 Lakini kama hatakusik-
iliza, nenda na mtu mwingine mmoja au waw-
ili ili kila neno lithibitishwe kwa ushahidi
wa mashahidi wawili au watatu. 17 Kama
akikataa kuwasikiliza hao, liambie kanisa. Naye
kama akikataa hata kulisikiliza kanisa, basi awe
kwenu kama mtu asiyeamini au mtoza ushuru.
18 “Amin, nawaambia, lolote mtakalolifunga
duniani litakuwa limefungwa mbinguni, na
lolote mtakalolifungua duniani litakuwa lime-
funguliwa mbinguni.
19 “Tena nawaambia, ikiwa wawili wenu
watakubaliana duniani kuhusu jambo lolote
watakaloomba, watafanyiwa na Baba yangu
aliye mbinguni. 20 Kwa kuwa wanapokusanyika

pamoja watu wawili au watatu kwa Jina langu, mimi niko papo hapo pamoja nao."

### *Kusamehe*

21 Ndipo Petro akamjia Yesu na kumuuliza, "Bwana, ndugu yangu anikosee mara ngapi nami nimsamehe? Je, hata mara saba?"

22 Yesu akamjibu, "Sikuambii hata mara saba, bali hata saba mara sabini.

### *Mfano Wa Mtumishi Asiyesamehe*

23 "Kwa hiyo Ufalme wa Mbinguni unaweza kufananishwa na mfalme aliyetaka kufanya hesabu zake za fedha na watumishi wake.
24 Alipoanza kufanya hesabu zake, mtu mmoja aliyekuwa anadaiwa talanta*10,000, aliletwa
kwake. 25 Kwa kuwa alikuwa hawezi kulipa deni hilo, bwana wake akaamuru kwamba auzwe, yeye, mkewe, watoto wake na vyote alivyokuwa navyo, ili lile deni lipate kulipwa.

26 "Yule mtumishi akampigia magoti, akamsihi yule bwana akisema, 'Naomba univumilie, nami
nitakulipa deni lako lote.' 27 Yule bwana wa huyo mtumishi akamwonea huruma, akafuta deni lake lote, akamwacha aende zake.

28 "Lakini yule mtumishi alipokuwa anatoka nje, akakutana na mtumishi mwenzake aliyekuwa amemkopesha dinari†mia moja. Akamkamata, akamkaba koo akimwambia, 'Nilipe kile ninachokudai!'

---

* **18:24** Talanta moja ni sawa na mshahara wa kibarua wa miaka 15. † **18:28** Dinari moja ilikuwa kama mshahara wa kibarua wa siku moja.

29 “Yule mtumishi mwenzake akapiga magoti
akamsihi akisema, ‘Naomba univumilie, nami
nitakulipa deni lako lote.’
30 “Lakini akakataa. Badala yake, alienda
akamtupa gerezani hata atakapolipa hilo deni.
31 Watumishi wenzake walipoona haya yaliy-
otukia wakaudhika sana, nao wakaenda na
kumwambia bwana wao kila kitu kilichokuwa
kimetukia.
32 “Yule bwana akamwita yule mtumishi
akamwambia, ‘Wewe mtumishi mwovu! Mimi
nilikusamehe deni lako lote uliponisihi. 33 Je,
haikukupasa kumhurumia mtumishi mwenzako
kama mimi nilivyokuhurumia wewe?’ 34 Kwa
hasira, yule bwana wake akamtia yule mtumishi
mikononi mwa askari wa gereza ili ateswe
mpaka atakapolipa yote aliyokuwa anadaiwa.
35 “Hivi ndivyo Baba yangu wa mbinguni
atakavyomfanyia kila mmoja wenu ikiwa hatam-
samehe ndugu yake kutoka moyoni mwake.”

# 19

### *Yesu Afundisha Kuhusu Talaka*
### *(Marko 10:1-12)*

1 Yesu alipomaliza kusema maneno haya,
aliondoka Galilaya, akaenda sehemu za Uyahudi,
ng’ambo ya Mto Yordani. 2 Umati mkubwa wa
watu ukamfuata, naye akawaponya huko.
3 Baadhi ya Mafarisayo wakamjia ili kum-
jaribu, wakamuuliza, “Ni halali mtu kumwacha
mke wake kwa sababu yoyote?”
4 Akawajibu, “Je, hamkusoma kwamba hapo
mwanzo Muumba aliwaumba mwanaume na

mwanamke, 5 naye akasema, 'Kwa sababu hii
mwanaume atamwacha baba yake na mama
yake, naye ataambatana na mkewe, na hao waw-
ili watakuwa mwili mmoja'? 6 Hivyo si wawili
tena, bali mwili mmoja. Kwa hiyo alichokiun-
ganisha Mungu, mwanadamu asikitenganishe."
7 Wakamuuliza, "Kwa nini basi Mose alia-
giza mtu kumpa mkewe hati ya talaka na
kumwacha?"
8 Yesu akawajibu, "Mose aliwaruhusu
kuwaacha wake zenu kwa sababu ya ugumu
wa mioyo yenu. Lakini tangu mwanzo haikuwa
hivyo. 9 Mimi nawaambia, yeyote amwachaye
mkewe isipokuwa kwa sababu ya uasherati naye
akaoa mke mwingine, anazini. Naye amwoaye
yule mwanamke aliyeachwa pia anazini."
10 Wanafunzi wake wakamwambia, "Kama
hali ndiyo hii kati ya mume na mke, ni afadhali
mtu asioe!"
11 Yesu akawaambia, "Si watu wote
wanaoweza kupokea neno hili, isipokuwa
wale tu waliojaliwa na Mungu. 12 Kwa maana
wengine ni matowashi kwa sababu wamezaliwa
hivyo; wengine wamefanywa matowashi
na wanadamu; na wengine wamejifanya
matowashi kwa ajili ya Ufalme wa Mbinguni.
Yeye awezaye kulipokea neno hili na alipokee."

### *Yesu Awabariki Watoto Wadogo*
### *(Marko 10:13-16; Luka 18:15-17)*

13 Kisha watoto wadogo wakaletwa kwa Yesu
ili aweke mikono yake juu yao na awaombee.
Lakini wanafunzi wake wakawakemea wale
waliowaleta.

14 Yesu akasema, “Waacheni watoto wadogo
waje kwangu, wala msiwazuie, kwa maana
Ufalme wa Mbinguni ni wa wale walio kama
hawa.” 15 Naye akaweka mikono yake juu yao,
na akaondoka huko.

### *Kijana Tajiri*
### *(Marko 10:17-31; Luka 18:18-30)*

16 Mtu mmoja akamjia Yesu na kumuuliza,
“Mwalimu mwema, nifanye jambo gani jema ili
nipate uzima wa milele?”
17 Yesu akamjibu, “Mbona unaniuliza habari
ya mema? Aliye mwema ni Mmoja tu. Lakini
ukitaka kuingia uzimani, zitii amri.”
18 Yule mtu akamuuliza, “Amri zipi?”

Yesu akamjibu, “Usiue, usizini, usiibe,
usishuhudie uongo, 19 waheshimu baba yako
na mama yako, na umpende jirani yako kama
nafsi yako.”
20 Yule kijana akasema, “Hizi zote nimezishika.
Je, bado nimepungukiwa na nini?”
21 Yesu akamwambia, “Kama ukitaka kuwa
mkamilifu, nenda, ukauze vitu vyote ulivyo
navyo, na hizo fedha uwape maskini, nawe
utakuwa na hazina mbinguni. Kisha njoo,
unifuate.”
22 Yule kijana aliposikia hayo, akaenda zake
kwa huzuni, kwa sababu alikuwa na mali nyingi.

### *Hatari Za Utajiri*

23 Ndipo Yesu akawaambia wanafunzi wake,
“Amin, nawaambia, itakuwa vigumu kwa mtu
tajiri kuingia katika Ufalme wa Mbinguni.
24 Tena nawaambia, ni rahisi zaidi kwa ngamia

kupita kwenye tundu la sindano kuliko mtu tajiri kuingia katika Ufalme wa Mungu.”

25 Wanafunzi wake waliposikia haya, walishangaa sana na kuuliza, “Ni nani basi awezaye kuokoka?”

26 Lakini Yesu akawatazama, akawaambia, “Kwa mwanadamu jambo hili haliwezekani, lakini mambo yote yanawezekana kwa Mungu.”

27 Ndipo Petro akamjibu, “Tazama, sisi tumeacha kila kitu na kukufuata! Tutapata nini basi?”

28 Yesu akawaambia, “Amin, nawaambia,
wakati wa kufanywa upya vitu vyote, Mwana wa
Adamu atakapoketi kwenye kiti chake kitukufu
cha enzi, ninyi mlionifuata pia mtaketi katika viti
vya enzi kumi na viwili, mkiyahukumu makabila
kumi na mawili ya Israeli. 29 Kila mtu aliyeacha
nyumba, au ndugu zake wa kiume au wa kike,
baba au mama, watoto au mashamba kwa ajili
yangu, atapokea mara mia zaidi ya hayo, na
aturithi uzima wa milele. 30 Lakini wengi walio
wa kwanza watakuwa wa mwisho, na walio wa
mwisho watakuwa wa kwanza.

# 20

*Mfano Wa Wafanyakazi Katika Shamba La Mizabibu*

1 “Kwa maana Ufalme wa Mbinguni unafanana na mtu mwenye shamba aliyetoka alfajiri ili kwenda kuajiri vibarua kufanya kazi
katika shamba lake la mizabibu. 2 Baada ya
kukubaliana na hao vibarua kuwalipa ujira

wa dinari*moja kwa siku, akawapeleka kwenye
shamba lake la mizabibu.
3 “Mnamo saa tatu akatoka tena, akawakuta
wengine wamesimama sokoni bila kazi.
4 Akawaambia, ‘Ninyi nanyi nendeni mkafanye
kazi katika shamba langu la mizabibu, nami
nitawalipa chochote kilicho haki yenu.’ 5 Kwa
hiyo wakaenda.

“Akatoka tena mnamo saa sita na pia saa
tisa akafanya vivyo hivyo. 6 Mnamo saa kumi
na moja akatoka tena akawakuta wengine bado
wamesimama bila kazi. Akawauliza, ‘Kwa nini
mmesimama hapa kutwa nzima pasipo kufanya
kazi?’
7 “Wakamjibu, ‘Ni kwa sababu hakuna yeyote
aliyetuajiri.’

“Akawaambia, ‘Ninyi nanyi nendeni mkafanye
kazi katika shamba langu la mizabibu.’
8 “Ilipofika jioni, yule mwenye shamba la
mizabibu akamwambia msimamizi, ‘Waite hao
vibarua na uwalipe ujira wao, ukianzia na
wale walioajiriwa mwisho na kuishia na wale
walioajiriwa kwanza.’
9 “Wale vibarua walioajiriwa mnamo saa kumi
na moja, wakaja na kila mmoja wao akapokea
dinari moja. 10 Hivyo wale walioajiriwa kwanza
walipofika, walidhani watalipwa zaidi. Lakini
kila mmoja wao pia alipokea dinari moja.
11 Walipoipokea, wakaanza kulalamika dhidi ya
yule mwenye shamba, 12 wakisema, ‘Hawa watu
walioajiriwa mwisho wamefanya kazi kwa muda

---

* **20:2** Dinari moja ilikuwa kama mshahara wa kibarua wa siku moja.

wa saa moja tu, nawe umewafanya sawa na
sisi ambao tumestahimili taabu na joto lote la
mchana kutwa?'
13 "Yule mwenye shamba akamjibu mmoja
wao, 'Rafiki, sijakudhulumu. Je, hukukubaliana
nami kwa ujira wa kawaida wa dinari moja?
14 Chukua ujira wako na uende. Mimi nimea-
mua kumlipa huyu mtu aliyeajiriwa mwisho
kama nilivyokupa wewe. 15 Je, sina haki
yangu kufanya kile nitakacho na mali yangu
mwenyewe? Au unaona wivu kwa kuwa
nimekuwa mkarimu?'
16 "Vivyo hivyo, wa mwisho watakuwa wa
kwanza, na wa kwanza watakuwa wa mwisho."

### *Yesu Atabiri Tena Kuhusu Kifo Chake (Marko 10:32-34; Luka 18:31-34)*

17 Basi Yesu alipokuwa anapanda kwenda
Yerusalemu, aliwachukua kando wale wana-
funzi wake kumi na wawili na kuwaambia,
18 "Tunapanda kwenda Yerusalemu, na Mwana
wa Adamu atatiwa mikononi mwa viongozi
wa makuhani na walimu wa sheria. Nao
watamhukumu kifo 19 na kumtia mikononi mwa
watu wa Mataifa ili wamdhihaki na kumpiga
mijeledi na kumsulubisha msalabani. Naye
atafufuliwa siku ya tatu!"

### *Ombi La Mama Yake Yakobo Na Yohana (Marko 10:35-45)*

20 Kisha mama yao wana wa Zebedayo akamjia
Yesu pamoja na wanawe, naye akapiga magoti
mbele yake, akamwomba Yesu amfanyie jambo
fulani.

21 Yesu akamuuliza, “Unataka nini?” Akajibu,
“Tafadhali, wajalie wanangu hawa ili mmoja
aketi upande wako wa kuume, na mwingine
upande wako wa kushoto katika Ufalme wako.”
22 Yesu akawaambia, “Ninyi hamjui mnalo-
liomba. Je, mnaweza kukinywea kikombe ni-
takachonywea mimi?”

Wakajibu, “Tunaweza.”

23 Yesu akawaambia, “Kwa kweli kikombe
changu mtakinywea, lakini kuketi upande
wangu wa kuume au wa kushoto si langu
mimi kuwapa. Nafasi hizo ni za wale ambao
wameandaliwa na Baba yangu.”
24 Wale wanafunzi wengine kumi waliposikia
haya, waliwakasirikia hao ndugu wawili.
25 Lakini Yesu akawaita wote pamoja na
kuwaambia, “Mnafahamu kuwa watawala wa
watu wa Mataifa huwatawala kwa nguvu, nao
wenye vyeo huonyesha mamlaka yao. 26 Isiwe
hivyo kwenu. Badala yake, yeyote anayetaka
kuwa mkuu miongoni mwenu hana budi kuwa
mtumishi wenu, 27 naye anayetaka kuwa wa
kwanza miongoni mwenu hana budi kuwa
mtumwa wenu: 28 kama vile ambavyo Mwana
wa Adamu hakuja ili kutumikiwa, bali kutumika
na kuutoa uhai wake uwe fidia kwa ajili ya
wengi.”

### *Yesu Awaponya Vipofu Wawili (Marko 10:46-52; Luka 18:35-43)*

29 Yesu na wanafunzi wake walipokuwa
wakiondoka Yeriko, umati mkubwa wa watu
ulimfuata. 30 Vipofu wawili walikuwa wameketi

kando ya barabara. Waliposikia kwamba Yesu
alikuwa anapita, wakapiga kelele wakisema,
“Bwana, Mwana wa Daudi, tuhurumie!”
31 Ule umati wa watu ukawakemea na
kuwaambia wanyamaze, lakini wao wakazidi
kupaza sauti, wakisema, “Bwana, Mwana wa
Daudi, tuhurumie.”
32 Yesu akasimama na kuwaita, akawauliza,
“Mnataka niwafanyie nini?”
33 Wakamjibu, “Bwana, tunataka kuona.”
34 Yesu akawahurumia na kuwagusa macho
yao. Mara macho yao yakapata kuona, nao
wakamfuata.

# 21

*Yesu Anaingia Yerusalemu Kwa Shangwe*
*(Marko 11:1-11; Luka 19:28-40; Yohana 12:12-19)*

1 Walipokaribia Yerusalemu, wakafika
Bethfage katika Mlima wa Mizeituni. Ndipo
Yesu akawatuma wanafunzi wake wawili,
2 akawaambia, “Nendeni katika kijiji kilichoko
mbele yenu, nanyi mtamkuta punda amefungwa
hapo, na mwana-punda pamoja naye.
Wafungueni na mniletee. 3 Kama mtu yeyote
akiwasemesha lolote, mwambieni kwamba
Bwana ana haja nao, naye atawaruhusu mwalete
mara.”
4 Haya yalitukia ili litimie lile lililonenwa na
nabii, akisema:
5 “Mwambieni Binti Sayuni,
‘Tazama, mfalme wako anakuja kwako,
ni mnyenyekevu, naye amepanda punda,

juu ya mwana-punda, mtoto wa punda.' "
6 Wale wanafunzi wakaenda, wakafanya kama
Yesu alivyokuwa amewaagiza. 7 Wakamleta
yule punda na mwana-punda, nao wakatandika
mavazi yao juu ya hao punda, naye Yesu akaketi
juu yake. 8 Umati mkubwa wa watu ukatandaza
mavazi yao barabarani, na wengine wakakata
matawi kutoka kwenye miti, wakayatandaza
barabarani. 9 Ule umati wa watu uliomtangulia
na ule uliomfuata ukapiga kelele ukisema,

"Hosana,* Mwana wa Daudi!"

"Amebarikiwa yeye ajaye kwa Jina la Bwana!"

"Hosana juu mbinguni!"

10 Yesu alipoingia Yerusalemu, mji wote ukata-
haruki, watu wakauliza, "Huyu ni nani?"
11 Ule umati wa watu ukajibu, "Huyu ni Yesu,
yule nabii kutoka Nazareti katika Galilaya."

### *Yesu Atakasa Hekalu*

*(Marko 11:15-19; Luka 19:45-48; Yohana 2:13-22)*

12 Yesu akaingia katika eneo la Hekalu na
kuwafukuza wote waliokuwa wakinunua na ku-
uza vitu Hekaluni. Akazipindua meza za wale
waliokuwa wakibadilisha fedha, na pia viti vya
wale waliokuwa wakiuza njiwa. 13 Akawaambia,
"Imeandikwa, 'Nyumba yangu itaitwa nyumba
ya sala,' lakini ninyi mmeifanya kuwa pango la
wanyang'anyi."

---

* **21:9** Kiebrania kusema Okoa, basi likawa neno la shangwe.

14 Vipofu na vilema wakamwendea kule
Hekaluni, naye akawaponya. 15 Lakini viongozi
wa makuhani na walimu wa sheria walipoona mambo ya ajabu aliyofanya na kuwasikia watoto wakishangilia katika eneo la Hekalu wakisema, "Hosana Mwana wa Daudi," walikasirika.

16 Wakamuuliza Yesu, "Je, unasikia hayo hawa wanayosema?"

Akawajibu, "Naam; kwani hamkusoma,

" 'Midomoni mwa watoto wachanga na wanyonyao
umeamuru sifa'?"

17 Akawaacha, akatoka nje ya mji, akaenda hadi Bethania, akalala huko.

### *Mtini Wanyauka (Marko 11:12-14, 20-24)*

18 Asubuhi na mapema, Yesu alipokuwa
akirudi mjini, alikuwa na njaa. 19 Akauona
mtini kando ya barabara, naye akaukaribia, lakini hakupata tunda lolote ila majani. Ndipo akauambia, "Wewe usizae matunda tena kamwe!" Papo hapo ule mtini ukanyauka.

20 Wanafunzi wake walipoona jambo hili, wakashangaa, wakamuuliza, "Imekuwaje mtini huu kunyauka ghafula?"

21 Yesu akawajibu, "Amin, nawaambia, kama mkiwa na imani wala msiwe na shaka, si kwamba mtaweza kufanya tu yale yaliyofanyika kwa huu mtini, bali hata mkiuambia huu mlima, 'Ng'oka, ukatupwe baharini,' litafanyika.
22 Yoyote mtakayoyaomba mkisali na mkiamini, mtayapokea."

### *Wahoji Kuhusu Mamlaka Ya Yesu (Marko 11:27-33; Luka 20:1-8)*

23 Yesu alipoingia Hekaluni, viongozi wa makuhani na wazee wa watu wakamjia alipokuwa anafundisha na kusema, "Unafanya mambo haya kwa mamlaka gani? Na ni nani aliyekupa mamlaka hayo?"

24 Yesu akawajibu, "Nami nitawauliza swali moja. Kama mkinijibu, nami nitawaambia ni kwa mamlaka gani ninafanya mambo haya.
25 Ubatizo wa Yohana, ulitoka wapi? Je, ulitoka mbinguni au kwa wanadamu?"

Wakahojiana wao kwa wao na kusema, "Tukisema ulitoka mbinguni atatuuliza, 'Mbona basi hamkumwamini?' 26 Lakini tukisema, 'Ulitoka kwa wanadamu,' tunawaogopa hawa watu, maana wote wanamtambua Yohana kuwa ni nabii."

27 Kwa hiyo wakamjibu Yesu, "Sisi hatujui."

Naye akawaambia, "Wala mimi sitawaambia ni kwa mamlaka gani ninatenda mambo haya."

### *Mfano Wa Wana Wawili*

28 "Lakini mwaonaje? Mtu mmoja alikuwa na wana wawili. Akamwendea yule wa kwanza akamwambia, 'Mwanangu, nenda ukafanye kazi kwenye shamba la mizabibu leo.'

29 "Yule mwanawe akamjibu 'Mimi sitakwenda.' Baadaye akabadili mawazo yake akaenda.

30 "Kisha yule baba akamwendea yule mwanawe mwingine akamwambia vilevile. Yeye akajibu, 'Nitakwenda, bwana,' lakini hakwenda.

31 “Ni yupi kati yao hao wawili aliyetimiza kile
alichotaka baba yake?”

Wakamjibu, “Ni yule wa kwanza.”

Yesu akawaambia, “Amin, amin nawaambia,
watoza ushuru na makahaba wanawatangulia
kuingia katika Ufalme wa Mungu. 32 Kwa
maana Yohana alikuja kwenu kuwaonyesha njia
ya haki, lakini hamkumsadiki, lakini watoza
ushuru na makahaba wakamsadiki. Nanyi hata
mlipoona hayo, baadaye hamkutubu na kumsadiki.

### *Mfano Wa Wapangaji Waovu*
*(Marko 12:1-12; Luka 20:9-19)*

33 “Sikilizeni mfano mwingine: Kulikuwa na
mtu mmoja mwenye shamba ambaye alipanda
shamba la mizabibu. Akajenga ukuta kulizunguka, akatengeneza shinikizo ndani yake na
akajenga mnara wa ulinzi. Kisha akalikodisha
hilo shamba la mizabibu kwa wakulima fulani, naye akaondoka, akasafiri kwenda nchi
nyingine. 34 Wakati wa mavuno ulipokaribia,
akawatuma watumishi wake kwa hao wapangaji
ili kukusanya matunda yake.

35 “Wale wapangaji wakawakamata wale
watumishi, wakampiga mmoja, wakamuua
mwingine, na yule wa tatu wakampiga mawe.
36 Kisha akawatuma kwao watumishi wengine,
wengi kuliko wale wa kwanza, nao wale
wapangaji wakawatendea vilevile. 37 Mwisho
wa yote, akamtuma mwanawe kwao, akisema,
‘Watamheshimu mwanangu.’

38 “Lakini wale wapangaji walipomwona
mwanawe, wakasemezana wao kwa wao, ‘Huyu

ndiye mrithi. Njooni tumuue, ili tuchukue urithi
wake.’ 39 Hivyo wakamchukua, wakamtupa nje
ya shamba la mizabibu, wakamuua.

40 “Kwa hiyo, huyo mwenye shamba la mizabibu atakapokuja, atawafanyia nini hao wakulima?”

41 Wakamjibu, “Kwa huzuni kuu atawaangamiza kabisa hao wadhalimu na kulipangisha shamba lake la mizabibu kwa wakulima wengine ambao watampatia fungu lake la matunda wakati wa mavuno.”

42 Yesu akawaambia, “Je, hamjasoma katika Maandiko kwamba:

“ ‘Jiwe walilolikataa waashi
limekuwa jiwe kuu la pembeni.
Bwana ndiye alitenda jambo hili,
nalo ni la ajabu machoni petu’?

43 “Kwa hiyo ninawaambia, Ufalme wa
Mungu utaondolewa kwenu na kupewa watu
wengine wawezao kuzaa matunda yake.
44 Yeye aangukaye juu ya jiwe hili atavunjika
vipande vipande, lakini yule litakayemwangukia
atasagwa kabisa.”

45 Viongozi wa Makuhani na Mafarisayo wali-
posikia mifano ya Yesu, walitambua kuwa
alikuwa akiwasema wao. 46 Wakatafuta njia ya
kumkamata, lakini wakaogopa umati wa watu,
kwa kuwa watu walimwona Yesu kuwa ni nabii.

# 22

*Mfano Wa Karamu Ya Arusi*
*(Luka 14:15-24)*

1 Yesu akasema nao tena kwa mifano,
akawaambia, 2 “Ufalme wa Mbinguni
unaweza kufananishwa na mfalme mmoja
aliyemwandalia mwanawe karamu ya arusi.
3 Akawatuma watumishi wake kuwaita wale
waliokuwa wamealikwa karamuni, lakini
wakakataa kuja.

4 “Kisha akawatuma watumishi wengine
akisema, ‘Waambieni wale walioalikwa kwamba
nimeandaa chakula. Nimekwisha kuchinja
mafahali wangu na vinono, karamu iko tayari.
Karibuni kwa karamu ya arusi.’

5 “Lakini hawakuzingatia, wakaenda zao:
huyu shambani mwake na mwingine kwenye
biashara zake. 6 Wengine wao wakawakamata
wale watumishi wake, wakawatesa na kuwaua.
7 Yule mfalme akakasirika sana, akapeleka
jeshi lake likawaangamiza wale wauaji na ku-
uteketeza mji wao kwa moto.

8 “Kisha akawaambia watumishi wake,
‘Karamu ya arusi imeshakuwa tayari,
lakini wale niliowaalika hawakustahili kuja.
9 Kwa hiyo nendeni katika njia panda
mkamwalike karamuni yeyote mtakayemwona.’
10 Wale watumishi wakaenda barabarani,
wakawakusanya watu wote waliowaona, wema
na wabaya. Ukumbi wa arusi ukajaa wageni.

11 “Lakini mfalme alipoingia ndani ili kuwaona
wageni, akamwona mle mtu mmoja ambaye
hakuwa amevaa vazi la arusi. 12 Mfalme aka-
muuliza, ‘Rafiki, uliingiaje humu bila vazi la
arusi?’ Yule mtu hakuwa na la kusema.

13 “Ndipo mfalme akawaambia watumishi
wake, ‘Mfungeni mikono na miguu mkamtupe
nje, kwenye giza. Huko kutakuwa na kilio na
kusaga meno.’
14 “Kwa maana walioitwa ni wengi, lakini
walioteuliwa ni wachache.”

*Kulipa Kodi Kwa Kaisari*
*(Marko 12:13-17; Luka 20:20-26)*

15 Ndipo Mafarisayo wakatoka nje wakaandaa
mpango wa kumtega Yesu katika maneno yake.
16 Wakatuma wanafunzi wao kwake pamoja
na Maherode. Nao wakasema, “Mwalimu,
tunajua kwamba wewe ni mtu mwadilifu na
unafundisha njia ya Mungu katika kweli bila
kuyumbishwa na mtu wala kuonyesha upen-
deleo. 17 Tuambie basi, wewe unaonaje? Je, ni
halali kulipa kodi kwa Kaisari, au la?”
18 Lakini Yesu, akijua makusudi yao mabaya,
akawaambia, “Enyi wanafiki, kwa nini mna-
jaribu kunitega? 19 Nionyesheni hiyo sarafu
inayotumika kwa kulipia kodi.” Wakamletea
dinari. 20 Naye akawauliza, “Sura hii ni ya nani?
Na maandishi haya ni ya nani?”
21 Wakamjibu, “Ni vya Kaisari.”

Basi Yesu akawaambia, “Mpeni Kaisari kilicho cha Kaisari, naye Mungu mpeni kilicho cha Mungu.”

22 Waliposikia hili, wakashangaa. Hivyo
wakamwacha, wakaenda zao.

*Ndoa Na Ufufuo*
*(Marko 12:18-27; Luka 20:27-40)*

23 Siku hiyo hiyo Masadukayo, wale
wasemao kwamba hakuna ufufuo wa wafu,
wakamjia Yesu na kumuuliza swali, wakisema,
24 “Mwalimu, Mose alisema, ‘Kama mtu akifa
bila kuwa na watoto, ndugu yake inampasa
amwoe huyo mjane ili ampatie watoto huyo
nduguye aliyekufa.’ 25 Basi palikuwa na ndugu
saba miongoni mwetu. Yule wa kwanza akaoa
mke, naye akafa, na kwa kuwa hakuwa na
watoto, akamwachia nduguye yule mjane.
26 Ikatokea vivyo hivyo kwa yule ndugu wa
pili, na wa tatu, hadi wote saba. 27 Hatimaye,
yule mwanamke naye akafa. 28 Sasa basi,
siku ya ufufuo, yeye atakuwa mke wa nani
miongoni mwa wale ndugu saba, kwa kuwa
wote walikuwa wamemwoa huyo mwanamke?”

29 Yesu akawajibu, “Mwapotoka kwa sababu
hamjui Maandiko wala uweza wa Mungu.
30 Wakati wa ufufuo, watu hawataoa wala
kuolewa, bali watakuwa kama malaika wa mbin-
guni. 31 Lakini kuhusu ufufuo wa wafu, ham-
jasoma kile Mungu alichowaambia, kwamba,
32 ‘Mimi ni Mungu wa Abrahamu, Mungu wa
Isaki, na Mungu wa Yakobo’? Yeye si Mungu wa
wafu, bali ni Mungu wa walio hai.”

33 Ule umati wa watu uliposikia hayo, ulis-
hangaa sana kwa mafundisho yake.

### *Amri Kuu Kuliko Zote*
*(Marko 12:28-34; Luka 10:25-28)*

34 Mafarisayo waliposikia kwamba Yesu
alikuwa amewanyamazisha Masadukayo,
Mafarisayo wakakusanyika pamoja. 35 Mmoja

wao, mtaalamu wa sheria, akamuuliza swali ili
kumjaribu, akisema, 36 “Mwalimu, ni amri ipi
katika Sheria iliyo kuu kuliko zote?”

37 Yesu akamjibu, “ ‘Mpende Bwana Mungu
wako kwa moyo wako wote na kwa roho yako
yote na kwa akili zako zote.’ 38 Hii ndiyo amri
iliyo kuu, tena ni ya kwanza. 39 Nayo ya pili
ni kama hiyo, nayo ni hii: ‘Mpende jirani yako
kama nafsi yako.’ 40 Amri hizi mbili ndizo msingi
wa Sheria na Manabii.”

### *Swali Kuhusu Mwana Wa Daudi*
### *(Marko 12:35-37; Luka 20:41-44)*

41 Wakati Mafarisayo walikuwa wameku-
sanyika pamoja, Yesu akawauliza, 42 “Mnaonaje
kuhusu Kristo?*Yeye ni mwana wa nani?”

Wakamjibu, “Yeye ni mwana wa Daudi.”

43 Akawaambia, “Inakuwaje basi kwamba
Daudi, akinena kwa kuongozwa na Roho,
anamwita Kristo ‘Bwana’? Kwa maana asema,
44 “ ‘BWANA alimwambia Bwana wangu:
“Keti mkono wangu wa kuume,
hadi nitakapowaweka adui zako
chini ya miguu yako.” ’
45 Kama basi Daudi anamwita yeye ‘Bwana,’
awezaje kuwa mwanawe?” 46 Hakuna mtu
aliyeweza kumjibu Yesu neno. Tena tangu
siku hiyo hakuna aliyethubutu kumuuliza tena
maswali.

* **22:42** Kristo maana yake ni Masiya, yaani Aliyetiwa mafuta.

# 23

### *Yesu Awashutumu Walimu Wa Sheria Na Mafarisayo*
*(Marko 12:38-40; Luka 11:39-52; 20:45-47)*

1 Kisha Yesu akauambia umati wa watu
pamoja na wanafunzi wake: 2 “Walimu wa
sheria na Mafarisayo wameketi katika kiti cha
Mose, 3 hivyo inawapasa kuwatii na kufanya
kila kitu wanachowaambia. Lakini msifuate
yale wanayotenda, kwa sababu hawatendi yale
wanayohubiri. 4 Wao hufunga mizigo mikubwa
na kuiweka mabegani mwa watu, lakini wao
wenyewe hawako radhi hata kuinua kidole ili
kuisogeza.

5 “Wao hutenda mambo yao yote ili
waonekane na watu. Hupanua vikasha vyao
vyenye maandiko ya sheria na kurefusha
matamvua ya mavazi yao. 6 Wanapenda kukalia
viti vya heshima katika karamu, na vile viti
maalum sana katika masinagogi. 7 Hupenda
kusalimiwa masokoni na kutaka watu wawaite
‘Rabi.’*

8 “Lakini ninyi msiitwe ‘Rabi,’ kwa sababu
mnaye Bwana mmoja na ninyi nyote ni ndugu.
9 Nanyi msimwite mtu yeyote ‘Baba,’ hapa
duniani, kwa maana mnaye Baba mmoja, naye
yuko mbinguni. 10 Wala msiitwe ‘Mwalimu,’
kwa maana mnaye mwalimu mmoja tu, ndiye
Kristo.† 11 Yeye aliye mkuu kuliko ninyi ny-
ote miongoni mwenu atakuwa mtumishi wenu.

---

* **23:7** Rabi maana yake Bwana, Mwalimu. † **23:10** Kristo maana yake ni Masiya, yaani Aliyetiwa mafuta.

12 Kwa kuwa yeyote anayejikweza atashushwa,
na yeyote anayejinyenyekeza atakwezwa.

13 "Lakini ole wenu, walimu wa sheria na Ma-
farisayo, enyi wanafiki! Kwa maana mnawafun-
gia watu milango ya Ufalme wa Mbinguni. Ninyi
wenyewe hamuingii humo, nao wale wanaotaka
kuingia mnawazuia. [ 14 Ole wenu walimu wa
sheria na Mafarisayo, enyi wanafiki! Mnakula
katika nyumba za wajane, nanyi kwa kujifanya
kuwa wema, mnasali sala ndefu. Kwa hiyo
hukumu yenu itakuwa kuu zaidi.]

15 "Ole wenu walimu wa sheria na Mafarisayo,
enyi wanafiki! Ninyi mnasafiri baharini na
nchi kavu ili kumfanya mtu mmoja mwongofu,
lakini baada ya kumpata, mnamfanya mwana
wa jehanamu mara mbili kuliko ninyi!

16 "Ole wenu, viongozi vipofu! Ninyi
mwasema, 'Mtu akiapa kwa Hekalu, kiapo hicho
si kitu; lakini mtu akiapa kwa dhahabu ya
Hekalu, amefungwa kwa kiapo chake.' 17 Ninyi
vipofu wapumbavu! Ni kipi kilicho kikuu zaidi:
ni ile dhahabu, au ni lile Hekalu linaloifanya
hiyo dhahabu kuwa takatifu? 18 Pia mnasema,
'Mtu akiapa kwa madhabahu, si kitu; lakini
mtu akiapa kwa sadaka iliyo juu ya madhabahu,
amefungwa kwa kiapo chake' 19 Ninyi vipofu! Ni
kipi kikuu zaidi: ni sadaka, au ni madhabahu
yanayoifanya hiyo sadaka kuwa takatifu? 20 Kwa
hiyo, mtu aapaye kwa madhabahu, huapa kwa
hayo madhabahu na vitu vyote vilivyo juu yake.
21 Naye mtu aapaye kwa Hekalu, huapa kwa hilo
Hekalu na kwa huyo akaaye ndani yake. 22 Naye

aapaye kwa mbingu, huapa kwa kiti cha enzi cha
Mungu na kwa yeye aketiye juu ya kiti hicho.

23 “Ole wenu walimu wa sheria na Mafarisayo,
ninyi wanafiki! Kwa maana mnatoa zaka ya
mnanaa, bizari na jira, lakini mmeacha mambo
makuu zaidi ya sheria, yaani haki, huruma na
uaminifu. Iliwapasa kufanya haya makuu ya
sheria bila kupuuza hayo matoleo. 24 Ninyi vion-
gozi vipofu, mnachuja kiroboto lakini mnameza
ngamia!

25 “Ole wenu, walimu wa sheria na Ma-
farisayo, ninyi wanafiki! Kwa maana mnasafisha
kikombe na sahani kwa nje, lakini ndani mmejaa
unyang’anyi na kutokuwa na kiasi. 26 Ewe
Farisayo kipofu! Safisha ndani ya kikombe na
sahani kwanza, ndipo nje itakuwa safi pia.

27 “Ole wenu, walimu wa sheria na Mafarisayo,
ninyi wanafiki! Mnafanana na makaburi yaliy-
opakwa chokaa, ambayo yanapendeza kwa nje,
lakini ndani yamejaa mifupa ya wafu na kila
aina ya uchafu. 28 Vivyo hivyo, kwa nje ninyi
mnaonekana kwa watu kuwa wenye haki, lakini
kwa ndani mmejaa unafiki na uovu.

29 “Ole wenu, walimu wa sheria na Mafarisayo,
ninyi wanafiki! Mnajenga makaburi ya man-
abii na kuyapamba makaburi ya wenye haki.
30 Nanyi mwasema, ‘Kama tungaliishi wakati
wa baba zetu, tusingalikuwa tumeshiriki katika
kumwaga damu ya manabii!’ 31 Hivyo mna-
jishuhudia wenyewe kwamba ninyi ni wana wa
wale waliowaua manabii. 32 Haya basi, kijazeni
kipimo cha dhambi ya baba zenu!

33 “Ninyi nyoka, ninyi uzao wa nyoka wenye
sumu! Mtaiepukaje hukumu ya jehanamu?
34 Kwa sababu hii, tazameni, natuma kwenu
manabii na wenye hekima na walimu. Baadhi
yao mtawaua na kuwasulubisha, na wengine
wao mtawapiga mijeledi katika masinagogi yenu
na kuwafuatia kutoka mji mmoja hadi mji
mwingine. 35 Hivyo ile damu ya wenye haki
wote iliyomwagwa hapa duniani, tangu damu ya
Abeli, ambaye alikuwa hana hatia, hadi damu
ya Zekaria mwana wa Barakia, mliyemuua kati
ya patakatifu na madhabahu, itawajia juu yenu.
36 Amin, nawaambia, haya yote yatakuja juu ya
kizazi hiki.

### *Yesu Aililia Yerusalemu (Luka 13:34-35)*

37 “Ee Yerusalemu, Yerusalemu, uwauaye
manabii na kuwapiga mawe wale waliotumwa
kwako! Mara ngapi nimetamani kuwakusanya
watoto wako pamoja, kama vile kuku aku-
sanyavyo vifaranga wake chini ya mabawa yake,
lakini hukutaka! 38 Tazama nyumba yenu
imeachwa ukiwa. 39 Kwa maana nawaam-
bia, hamtaniona tena tangu sasa mpaka mtaka-
posema, ‘Amebarikiwa yeye ajaye kwa Jina la
Bwana.’ ”

# 24

### *Kubomolewa Kwa Hekalu Kwatabiriwa (Marko 13:1-2; Luka 21:5-6)*

1 Yesu akatoka Hekaluni na alipokuwa akienda
zake, wanafunzi wake wakamwendea ili kum-
wonyesha majengo ya Hekalu. 2 Ndipo Yesu

akawauliza, "Je, mnayaona haya yote? Amin, nawaambia, hakuna hata jiwe moja hapa litakalobaki juu ya jingine, bali kila moja litabomolewa."

### *Ishara Za Nyakati Za Mwisho (Marko 13:3-23; Luka 21:7-24)*

3 Yesu alipokuwa ameketi kwenye Mlima wa Mizeituni, wanafunzi wake wakamjia faraghani, wakamuuliza, "Tuambie, mambo haya yatatukia lini, nayo dalili ya kuja kwako na ya mwisho wa dunia ni gani?"

4 Yesu akawajibu, "Jihadharini, mtu yeyote asi-
wadanganye. 5 Kwa maana wengi watakuja kwa
Jina langu, wakidai, 'Mimi ndiye Kristo,'*nao
watawadanganya wengi. 6 Mtasikia habari za
vita na matetesi ya vita. Angalieni msitishike, kwa maana haya hayana budi kutukia. Lakini
ule mwisho bado. 7 Taifa litainuka dhidi ya taifa,
na ufalme dhidi ya ufalme. Kutakuwa na njaa na
mitetemeko ya ardhi sehemu mbalimbali. 8 Haya
yote yatakuwa ndio mwanzo wa utungu.

9 "Ndipo mtasalitiwa, ili mteswe na kuuawa, nanyi mtachukiwa na mataifa yote kwa ajili
yangu. 10 Wakati huo, wengi wataacha imani
yao, nao watasalitiana kila mmoja na mwenzake
na kuchukiana. 11 Watatokea manabii wengi
wa uongo, nao watawadanganya watu wengi.
12 Kwa sababu ya kuongezeka kwa uovu upendo
wa watu wengi utapoa, 13 lakini yule atakaye-
vumilia hadi mwisho ataokolewa. 14 Injili ya

* **24:5** Kristo maana yake ni Masiya, yaani Aliyetiwa mafuta.

Ufalme itahubiriwa ulimwenguni kote kuwa
ushuhuda kwa mataifa yote. Ndipo mwisho
utakapokuja.

15 "Hivyo mtakapoona lile 'chukizo la uharib-
ifu' lililonenwa na nabii Danieli limesimama
mahali patakatifu (asomaye na afahamu), 16 basi
wale walioko Uyahudi wakimbilie milimani.
17 Yeyote aliye juu ya dari ya nyumba asishuke
ili kuchukua chochote kutoka ndani ya nyumba.
18 Aliye shambani asirudi nyumbani kuchukua
vazi lake. 19 Ole wao wenye mimba na wale
wanaonyonyesha watoto siku hizo! 20 Ombeni
ili kukimbia kwenu kusiwe wakati wa baridi
au siku ya Sabato. 21 Kwa maana wakati
huo kutakuwa na dhiki kuu ambayo haijapata
kuwako tangu mwanzo wa dunia mpaka sasa:
wala haitakuwako tena kamwe. 22 Kama siku
hizo zisingefupishwa, hakuna hata mtu mmoja
ambaye angeokoka. Lakini kwa ajili ya wateule,
siku hizo zitafupizwa. 23 Wakati huo kama mtu
yeyote akiwaambia, 'Tazama, Kristo huyu hapa!'
Au, 'Kristo yuko kule,' msisadiki. 24 Kwa maana
watatokea makristo wa uongo na manabii wa
uongo, nao watafanya ishara kubwa na maa-
jabu mengi ili kuwapotosha, ikiwezekana, hata
wale wateule hasa. 25 Angalieni, nimekwisha
kuwaambia mapema.

26 "Kwa hiyo mtu yeyote akiwaambia,
'Yule kule nyikani,' msiende huko. Au
akisema, 'Yuko kwenye chumba,' msisadiki.
27 Kwa maana kama vile umeme utokeavyo
mashariki na kuonekana hata magharibi, ndivyo
itakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu.

28 Kwa maana popote ulipo mzoga, huko ndiko
wakusanyikapo tai.

### *Kuja Kwa Mwana Wa Adamu*
*(Marko 13:24-31; Luka 21:25-33)*

29 “Mara baada ya dhiki ya siku zile,
“ ‘jua litatiwa giza,
nao mwezi hautatoa nuru yake;
nazo nyota zitaanguka kutoka angani,
na nguvu za anga zitatikisika.’
30 “Ndipo itakapotokea ishara ya Mwana wa
Adamu angani, na makabila yote ya dunia
yataomboleza. Nao watamwona Mwana wa
Adamu akija juu ya mawingu ya angani, katika
uwezo na utukufu mkuu. 31 Naye atawatuma
malaika zake kwa sauti kuu ya tarumbeta, nao
watawakusanya wateule wake kutoka pande
zote nne za dunia, kutoka mwisho mmoja wa
mbingu hadi mwisho mwingine.
32 “Basi jifunzeni somo hili kutokana na mtini:
Matawi yake yanapoanza kuchipua na kutoa ma-
jani, mnatambua kwamba wakati wa kiangazi
umekaribia. 33 Vivyo hivyo, myaonapo mambo
haya yote, mnatambua kwamba wakati u karibu,
hata malangoni. 34 Amin, nawaambia, kizazi
hiki hakitapita hadi mambo haya yote yawe
yametimia. 35 Mbingu na nchi zitapita, lakini
maneno yangu hayatapita kamwe.

### *Hakuna Ajuaye Siku Wala Saa*
*(Marko 13:32-37; Luka 17:26-30, 34-36)*

36 “Kwa habari ya siku ile na saa, hakuna
ajuaye, hata malaika walio mbinguni wala
Mwana, ila Baba peke yake. 37 Kama ilivyokuwa

wakati wa Noa, ndivyo itakavyokuwa kuja
kwake Mwana wa Adamu. 38 Kwa maana siku
zile kabla ya gharika, watu walikuwa wakila
na kunywa, wakioa na kuolewa, mpaka siku ile
Noa alipoingia katika safina. 39 Nao hawaku-
jua lolote mpaka gharika ilipokuja ikawakumba
wote. Hivyo ndivyo itakavyokuwa atakapokuja
Mwana wa Adamu. 40 Watu wawili watakuwa
shambani, naye mmoja atatwaliwa na mwingine
ataachwa. 41 Wanawake wawili watakuwa
wanasaga pamoja, naye mmoja atatwaliwa na
mwingine ataachwa.

42 “Basi kesheni, kwa sababu hamjui ni siku
gani atakapokuja Bwana wenu. 43 Lakini fa-
hamuni jambo hili: Kama mwenye nyumba
angejua ni wakati gani wa usiku ambao mwizi
atakuja, angekesha na hangekubali nyumba
yake kuvunjwa. 44 Kwa hiyo ninyi pia hamna
budi kuwa tayari, kwa sababu Mwana wa
Adamu atakuja saa msiyotazamia.

### *Mfano Wa Mtumishi Mwaminifu (Luka 12:41-48)*

45 “Ni nani basi aliye mtumishi mwaminifu
na mwenye busara, ambaye bwana wake
amemweka kusimamia watumishi wengine
katika nyumba yake, ili awape chakula chao
kwa wakati unaofaa? 46 Heri mtumishi yule
ambaye bwana wake atakaporudi atamkuta
akifanya hivyo. 47 Amin, nawaambia, atamweka
mtumishi huyo kuwa msimamizi wa mali
yake yote. 48 Lakini kama huyo mtumishi ni
mwovu, naye akasema moyoni mwake, ‘Bwana
wangu atakawia muda mrefu,’ 49 kisha akaanza

kuwapiga watumishi wenzake, na kula na
kunywa pamoja na walevi. 50 Basi bwana
wa mtumishi huyo atakuja siku asiyodhani na
saa asiyoijua. 51 Atamkata vipande vipande
na kumweka katika sehemu moja pamoja na
wanafiki, mahali ambako kutakuwa ni kulia na
kusaga meno.

# 25

*Mfano Wa Wanawali Kumi*

1 “Wakati huo, Ufalme wa Mbinguni utakuwa
kama wanawali kumi waliochukua taa zao na
kwenda kumlaki bwana arusi. 2 Watano wao wa-
likuwa wapumbavu na watano walikuwa wenye
busara. 3 Wale wapumbavu walichukua taa zao
lakini hawakuchukua mafuta ya akiba, 4 lakini
wale wenye busara walichukua taa zao na
mafuta ya akiba kwenye vyombo. 5 Bwana arusi
alipokawia kuja wale wanawali wote wakasinzia
na kulala.

6 “Usiku wa manane pakawa na kelele: ‘Taza-
meni, huyu hapa bwana arusi! Tokeni nje
mkamlaki!’

7 “Ndipo wale wanawali wote wakaamka na
kuzitengeneza taa zao. 8 Wale wapumbavu
wakawaambia wale wenye busara, ‘Tupatieni
mafuta yenu kidogo; taa zetu zinazimika.’

9 “Lakini wale wenye busara wakawajibu,
‘Sivyo, hayatutoshi sisi na ninyi pia. Afad-
hali mwende kwa wauzao mkajinunulie mafuta
yenu.’

10 “Nao walipokuwa wakienda kununua
mafuta, bwana arusi akafika. Wale wanawali

waliokuwa tayari wakaingia ndani pamoja naye
kwenye karamu ya arusi na mlango ukafungwa.
11 “Baadaye wale wanawali wengine nao
wakaja, wakaita, ‘Bwana! Bwana! Tufungulie
mlango!’
12 “Lakini yeye bwana arusi akawajibu, ‘Amin,
amin nawaambia, siwajui ninyi!’
13 “Kwa hiyo kesheni, kwa sababu hamjui siku
wala saa.

### *Mfano Wa Watumishi Watatu Na Talanta (Luka 19:11-27)*

14 “Tena, Ufalme wa Mbinguni ni kama mtu
aliyetaka kusafiri, naye akawaita watumishi
wake na kuweka mali yake kwenye uangalizi
wao. 15 Mmoja akampa talanta*tano, mwingine
talanta mbili, na mwingine talanta moja. Kila
mmoja alipewa kwa kadiri ya uwezo wake.
Kisha yeye akasafiri. 16 Yule aliyepewa talanta
tano akaenda mara moja akafanya nazo biashara
akapata talanta nyingine tano zaidi. 17 Yule
aliyepewa talanta mbili akafanya vivyo hivyo,
akapata nyingine mbili zaidi. 18 Lakini yule
mtumishi aliyekuwa amepokea talanta moja,
alikwenda akachimba shimo ardhini na kuificha
ile fedha ya bwana wake.
19 “Baada ya muda mrefu, yule bwana wa
wale watumishi akarudi na kufanya hesabu nao.
20 Yule mtumishi aliyepokea talanta tano akaja,
akaleta nyingine tano zaidi. Akasema, ‘Bwana

---

* **25:15** Talanta moja ilikuwa sawa na mshahara wa kibarua wa miaka 15.

uliweka kwenye uangalizi wangu talanta tano. Tazama, nimepata faida ya talanta tano zaidi.’

21 “Bwana wake akamwambia, ‘Umefanya vizuri sana, mtumishi mwema na mwaminifu! Umekuwa mwaminifu kwa vitu vichache; nami nitakuweka kuwa msimamizi wa vitu vingi. Njoo ushiriki katika furaha ya bwana wako!’

22 “Yule mwenye talanta mbili naye akaja. Akasema, ‘Bwana, uliweka kwenye uangalizi wangu talanta mbili. Tazama nimepata hapa talanta mbili zaidi.’

23 “Bwana wake akajibu, ‘Umefanya vizuri sana, mtumishi mwema na mwaminifu. Umekuwa mwaminifu kwa vitu vichache; nami nitakuweka kuwa msimamizi wa vitu vingi. Njoo ushiriki katika furaha ya bwana wako!’

24 “Kisha yule mtumishi aliyepokea talanta
moja akaja, akasema, ‘Bwana, nilijua kwamba
wewe ni mtu mgumu, unayevuna mahali
usipopanda na kukusanya mahali usipotawanya
mbegu. 25 Kwa hiyo niliogopa, nikaenda,
nikaificha talanta yako ardhini. Tazama, hii
hapa ile iliyo mali yako.’

26 “Bwana wake akajibu, ‘Wewe mtumishi
mwovu na mvivu! Ulijua kwamba ninavuna
mahali nisipopanda na kukusanya mahali
nisipotawanya mbegu. 27 Vyema basi,
ingekupasa kuweka fedha yangu kwa watoa
riba, ili nirudipo, nichukue ile iliyo yangu na
faida yake.

28 “ ‘Basi mnyang’anyeni hiyo talanta, mkampe
yule mwenye talanta kumi. 29 Kwa maana kila
mtu aliye na kitu atapewa zaidi, naye atakuwa

navyo tele. Lakini yule asiye na kitu, hata kile
alicho nacho atanyang'anywa. 30 Nanyi mtupeni
huyo mtumishi asiyefaa nje, kwenye giza, mahali
ambako kutakuwa na kilio na kusaga meno.'

*Kondoo Na Mbuzi*

31 “Mwana wa Adamu atakapokuja katika
utukufu wake na malaika wote watakatifu
pamoja naye, ndipo atakapoketi juu ya kiti
cha enzi cha utukufu wake. 32 Mataifa yote
watakusanyika mbele zake, naye atawatenga
kama mchungaji anavyotenga kondoo na mbuzi.
33 Atawaweka kondoo upande wake wa kuume,
na mbuzi upande wake wa kushoto.

34 “Ndipo Mfalme atawaambia wale walioko
upande wake wa kuume, ‘Njooni, ninyi mlio-
barikiwa na Baba yangu; urithini Ufalme ulioan-
daliwa kwa ajili yenu tangu kuumbwa kwa
ulimwengu. 35 Kwa maana nilikuwa na njaa
mkanipa chakula, nilikuwa na kiu mkaninywe-
sha, nilikuwa mgeni mkanikaribisha, 36 nilikuwa
uchi mkanivika, nilikuwa mgonjwa mkanitunza,
nami nilikuwa kifungoni mkaja kunitembelea.'

37 “Ndipo wale wenye haki watakapomjibu,
‘Bwana, ni lini tulikuona ukiwa na njaa tukakul-
isha, au ukiwa na kiu tukakunywesha? 38 Lini tu-
likuona ukiwa mgeni tukakukaribisha, au ukiwa
uchi tukakuvika? 39 Tena ni lini tulikuona
ukiwa mgonjwa tukakutunza, au ukiwa kifun-
goni tukakutembelea?'

40 “Naye Mfalme atawajibu, ‘Amin nawaam-
bia, kwa jinsi mlivyomtendea mmojawapo wa

hawa ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea
mimi.'
41 "Kisha atawaambia wale walio upande
wake wa kushoto, 'Ondokeni kwangu, ninyi
mliolaaniwa, nendeni kwenye moto wa milele
ulioandaliwa kwa ajili ya ibilisi na malaika
zake. 42 Kwa maana nilikuwa na njaa hamku-
nipa chakula, nilikuwa na kiu hamkuninywe-
sha, 43 nilikuwa mgeni nanyi hamkunikaribisha,
nilikuwa uchi hamkunivika, nilikuwa mgonjwa
hamkunitunza, na nilikuwa gerezani nanyi
hamkuja kunitembelea.'
44 "Ndipo wao pia watajibu, 'Bwana ni lini
tulikuona ukiwa na njaa au kiu, au ukiwa mgeni
au uchi, au ukiwa mgonjwa na kifungoni na
hatukukuhudumia?'
45 "Naye atawajibu, 'Amin nawaambia, kwa
jinsi ambavyo hamkumtendea mmojawapo wa
hawa ndugu zangu walio wadogo, hamkuniten-
dea mimi.'
46 "Ndipo hawa watakapoingia kwenye ad-
habu ya milele, lakini wale wenye haki watain-
gia katika uzima wa milele."

# 26

*Shauri Baya La Kumuua Yesu*
*(Marko 14:1-2; Luka 22:1-2; Yohana 11:45-53)*
1 Yesu alipomaliza kusema hayo yote,
akawaambia wanafunzi wake, 2 "Kama
mnavyojua, baada ya siku mbili itakuwa
Pasaka, naye Mwana wa Adamu atasalitiwa
ili asulubiwe."

3 Basi viongozi wa makuhani na wazee wa
watu wakakusanyika katika jumba la utawala
la kuhani mkuu, jina lake Kayafa. 4 Wakafanya
shauri ili kumkamata Yesu kwa siri na kumuua.
5 Lakini wakasema, "Isiwe wakati wa Sikukuu,
kusitokee ghasia miongoni mwa watu."

### *Yesu Anapakwa Mafuta Huko Bethania (Marko 14:3-9; Yohana 12:1-8)*

6 Yesu alikuwa Bethania nyumbani mwa Si-
moni aliyekuwa na ukoma, 7 naye mwanamke
mmoja akamjia akiwa na chupa ya marhamu
yenye manukato ya thamani kubwa; akayamim-
ina kichwani mwa Yesu alipokuwa ameketi
mezani kula chakula.
8 Lakini wanafunzi wake walipoona hayo
wakakasirika, wakasema, "Upotevu huu wote ni
wa nini? 9 Manukato haya yangeuzwa kwa bei
kubwa, na fedha hizo wakapewa maskini."
10 Yesu, akijua jambo hili, akawaambia,
"Mbona mnamsumbua huyu mwanamke? Yeye
amenitendea jambo zuri sana. 11 Maskini
mtakuwa nao siku zote, lakini mimi hamtakuwa
nami siku zote. 12 Alipomiminia haya manukato
kwenye mwili wangu, amefanya hivyo ili ku-
niandaa kwa ajili ya maziko yangu. 13 Amin,
nawaambia, mahali popote ulimwenguni am-
bapo hii Injili itahubiriwa, jambo hili alilolitenda
huyu mwanamke litatajwa pia kwa ukumbusho
wake."

### *Yuda Akubali Kumsaliti Yesu (Marko 14:10-11; Luka 22:3-6)*

14 Kisha mmojawapo wa wale kumi na wawili,
aitwaye Yuda Iskariote, alikwenda kwa viongozi
wa makuhani 15 na kuuliza, "Mtanipa nini nikim-
tia Yesu mikononi mwenu?" Wakamlipa vipande
thelathini vya fedha. 16 Tangu wakati huo Yuda
akawa anatafuta wakati uliofaa wa kumsaliti
Yesu.

### *Yesu Ala Pasaka Pamoja Na Wanafunzi (Marko 14:12-21; Luka 22:7-23; Yohana 13:21-30)*

17 Siku ya kwanza ya Sikukuu ya Mikate Isiy-
otiwa Chachu, wanafunzi walimjia Yesu waka-
muuliza, "Unataka twende wapi ili tukuandalie
mahali pa kula Pasaka?"

18 Akajibu, "Nendeni kwa mtu fulani huko
mjini, mkamwambie, 'Mwalimu asema hivi:
Saa yangu imekaribia. Nitaiadhimisha Pasaka
pamoja na wanafunzi wangu katika nyumba
yako.' " 19 Hivyo wanafunzi wakafanya kama vile
Yesu alivyokuwa amewaelekeza, nao wakaandaa
Pasaka.

20 Ilipofika jioni, Yesu alikuwa ameketi mezani
pamoja na wale wanafunzi wake kumi na waw-
ili. 21 Nao walipokuwa wakila, Yesu akasema,
"Amin, nawaambia, mmoja wenu atanisaliti."

22 Wakahuzunika sana, wakaanza kumuuliza
mmoja baada ya mwingine, "Je, ni mimi
Bwana?"

23 Yesu akawaambia, "Yule aliyechovya
mkono wake katika bakuli pamoja nami
ndiye atakayenisaliti. 24 Mwana wa Adamu
anaenda zake kama vile alivyoandikiwa. Lakini
ole wake mtu yule amsalitiye Mwana wa

Adamu. Ingekuwa heri kwake mtu huyo kama hangezaliwa!”

25 Kisha Yuda, yule mwenye kumsaliti, akasema, “Je, ni mimi Rabi?”

Yesu akajibu, “Naam, wewe mwenyewe umesema.”

### *Kuanzishwa Kwa Meza Ya Bwana*
*(Marko 14:22-26; Luka 22:14-20; 1 Wakorintho 11:23-25)*

26 Walipokuwa wanakula, Yesu akachukua mkate, akashukuru, akaumega, na kuwapa wanafunzi wake, akisema, “Twaeni, mle; huu ndio mwili wangu.”

27 Kisha akakitwaa kikombe, akashukuru, akawapa, akisema, “Nyweni nyote katika
kikombe hiki. 28 Hii ndiyo damu yangu ya
Agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa
ondoleo la dhambi. 29 Lakini ninawaambia,
tangu sasa sitakunywa tena katika uzao huu wa mzabibu, hadi siku ile nitakapounywa mpya pamoja nanyi katika Ufalme wa Baba yangu.”

30 Walipokwisha kuimba wimbo, wakatoka wakaenda Mlima wa Mizeituni.

### *Yesu Atabiri Petro Kumkana*
*(Marko 14:27-31; Luka 22:31-34; Yohana 13:36-38)*

31 Kisha Yesu akawaambia, “Usiku huu, ninyi nyote mtaniacha, kwa maana imeandikwa:
“ ‘Nitampiga mchungaji,
nao kondoo wa hilo kundi watatawanyika.’
32 Lakini baada ya kufufuka kwangu, nitawatangulia kwenda Galilaya.”

33 Petro akajibu, “Hata kama wote
watakuacha, kamwe mimi sitakuacha.”
34 Yesu akamjibu, “Amin, nakuambia, usiku
huu, kabla jogoo hajawika, utanikana mara
tatu.”
35 Lakini Petro akasisitiza, “Hata kama itabidi
kufa pamoja nawe, sitakukana kamwe.” Nao
wanafunzi wale wengine wote wakasema vivyo
hivyo.

### *Yesu Anaomba Gethsemane (Marko 14:32-42; Luka 22:39-46)*

36 Kisha Yesu akaenda pamoja na wanafunzi
wake mpaka kwenye bustani iitwayo Gethse-
mane, akawaambia, “Kaeni hapa, nami niende
kule nikaombe.” 37 Akamchukua Petro pamoja
na wale wana wawili wa Zebedayo, akaanza
kuhuzunika na kufadhaika. 38 Kisha Yesu
akawaambia, “Moyo wangu umejawa na huzuni
kiasi cha kufa. Kaeni hapa na mkeshe pamoja
nami.”
39 Akaenda mbele kidogo, akaanguka kifud-
ifudi, akaomba akisema, “Baba yangu, kama
inawezekana, kikombe hiki na kiniondokee.
Lakini si kama nipendavyo mimi, bali kama
upendavyo wewe.”
40 Kisha akarudi kwa wanafunzi wake,
akawakuta wamelala. Akamuuliza Petro, “Je,
ninyi hamkuweza kukesha pamoja nami hata
kwa saa moja? 41 Kesheni na mwombe, msije
mkaingia majaribuni. Roho iko radhi, lakini
mwili ni mdhaifu.”
42 Akaenda tena mara ya pili na kuomba,
“Baba yangu, kama haiwezekani kikombe

hiki kiniepuke nisikinywe, basi mapenzi yako
yafanyike."
43 Aliporudi, akawakuta tena wamelala kwa
sababu macho yao yalikuwa mazito. 44 Hivyo
akawaacha akaenda zake tena mara ya tatu na
kuomba akisema maneno yale yale.
45 Kisha akarudi kwa wanafunzi wake,
akawaambia, "Bado mmelala na kupumzika?
Tazameni, saa imefika ambapo Mwana wa
Adamu anasalitiwa na kutiwa mikononi mwa
wenye dhambi. 46 Inukeni, twende zetu!
Tazameni, msaliti wangu yuaja!"

### *Yesu Akamatwa*

*(Marko 14:43-50; Luka 22:47-53; Yohana 18:3-12)*

47 Alipokuwa bado anazungumza, Yuda,
mmoja wa wale Kumi na Wawili, akafika.
Alikuwa amefuatana na umati mkubwa wa
watu wenye panga na marungu, waliokuwa
wametumwa na viongozi wa makuhani na
wazee wa watu. 48 Basi msaliti alikuwa
amewapa hao watu ishara, kwamba: "Yule
nitakayembusu ndiye. Mkamateni." 49 Mara
Yuda akamjia Yesu na kumsalimu, "Salamu,
Rabi!" Akambusu.
50 Yesu akamwambia, "Rafiki, fanya kile ulichokuja kufanya hapa."

Kisha wale watu wakasogea mbele, wakamka-
mata Yesu. 51 Ghafula mmoja wa wale
waliokuwa na Yesu alipoona hivyo, akaushika
upanga wake, akauchomoa na kumpiga mtumishi wa kuhani mkuu, akamkata sikio.

52 Ndipo Yesu akamwambia, “Rudisha upanga wako mahali pake, kwa maana wote watumiao
upanga watakufa kwa upanga. 53 Je, unadhani
siwezi kumwomba Baba yangu naye mara moja akaniletea zaidi ya majeshi kumi na mawili ya
malaika? 54 Lakini je, yale Maandiko yanayotabiri kwamba ni lazima itendeke hivi yatatimiaje?”

55 Wakati huo, Yesu akawaambia ule umati wa watu, “Je, mmekuja na panga na marungu kunikamata kana kwamba mimi ni mnyang’anyi? Siku kwa siku niliketi Hekaluni
nikifundisha, mbona hamkunikamata? 56 Lakini
haya yote yametukia ili maandiko ya manabii yapate kutimia.” Ndipo wanafunzi wake wote wakamwacha na kukimbia.

### *Yesu Mbele Ya Kuhani Mkuu*

*(Marko 14:53-65; Luka 22:54-71; Yohana 18:13-24)*

57 Wale waliokuwa wamemkamata Yesu wakampeleka kwa Kayafa, kuhani mkuu, mahali ambapo walimu wa sheria pamoja na wazee
walikuwa wamekusanyika. 58 Lakini Petro
akamfuata kwa mbali hadi uani kwa kuhani mkuu. Akaingia ndani, akaketi pamoja na walinzi ili aone litakalotukia.

59 Viongozi wa makuhani na Baraza la Wayahudi lote wakatafuta ushahidi wa uongo
dhidi ya Yesu ili wapate kumuua. 60 Lakini
hawakupata jambo lolote, ingawa mashahidi wengi wa uongo walijitokeza.

Hatimaye wakajitokeza mashahidi wawili wa
uongo 61 na kusema, “Huyu mtu alisema, ‘Ni-
naweza kulivunja Hekalu la Mungu na kulijenga
tena kwa siku tatu.’ ”
62 Kisha kuhani mkuu akasimama na
kumwambia Yesu, “Je, wewe hutajibu? Ni
ushahidi gani hawa watu wanauleta dhidi
yako?” 63 Lakini Yesu akakaa kimya.

Ndipo kuhani mkuu akamwambia,
“Nakuapisha mbele za Mungu aliye hai.
Tuambie kama wewe ndiwe Kristo,* Mwana
wa Mungu.”
64 Yesu akajibu, “Wewe umenena. Lakini ni-
nawaambia nyote: Siku za baadaye, mtamwona
Mwana wa Adamu akiwa ameketi mkono wa
kuume wa Mwenye Nguvu, na akija juu ya
mawingu ya mbinguni.”
65 Ndipo kuhani mkuu akararua mavazi yake
na kusema, “Amekufuru! Tuna haja gani tena ya
mashahidi zaidi? Tazama, sasa ninyi mmesikia
hayo makufuru. 66 Uamuzi wenu ni gani?”

Wakajibu, “Anastahili kufa.”
67 Kisha wakamtemea mate usoni na wengine
wakampiga ngumi. Wengine wakampiga makofi
68 na kusema, “Tutabirie, wewe Kristo! Ni nani
aliyekupiga?”

### *Petro Amkana Bwana Yesu*

*(Marko 14:66-72; Luka 22:56-62; Yohana 18:15-18, 25-27)*

69 Wakati huu Petro alikuwa amekaa nje
uani. Mtumishi mmoja wa kike akamjia na

* **26:63** Kristo maana yake ni Masiya, yaani Aliyetiwa mafuta.

kumwambia, “Wewe pia ulikuwa pamoja na Yesu wa Galilaya.”
70 Lakini Petro akakana mbele yao wote akisema, “Sijui hilo usemalo.”
71 Alipotoka nje kufika kwenye lango, mtumishi mwingine wa kike alimwona, akawaambia watu waliokuwepo, “Huyu mtu alikuwa pamoja na Yesu, Mnazareti.”
72 Akakana tena kwa kiapo akisema, “Mimi simjui huyo!”
73 Baada ya muda mfupi, wale waliokuwa wamesimama pale wakamwendea Petro, wakamwambia, “Hakika wewe ni mmoja wao, kwa maana usemi wako ni kama wao.”
74 Ndipo Petro akaanza kujilaani na kuwaapia, “Mimi simjui mtu huyo!”

Papo hapo jogoo akawika.
75 Ndipo Petro akakumbuka lile neno Yesu alilokuwa amesema: “Kabla jogoo hajawika, utanikana mara tatu.” Naye akaenda nje, akalia kwa majonzi.

# 27

### *Yesu Aletwa Mbele Ya Pilato*
### *(Marko 15:1; Luka 23:1-2; Yohana 18:28-32)*

1 Asubuhi na mapema, viongozi wa makuhani wote na wazee wa watu wakafanya shauri pamoja dhidi ya Yesu ili kumuua.
2 Wakamfunga, wakampeleka na kumkabidhi kwa Pilato, ambaye alikuwa mtawala wa Kirumi.

### *Yuda Ajinyonga*
### *(Matendo 1:18-19)*

3 Yuda, ambaye alikuwa amemsaliti Yesu,
alipoona kuwa Yesu amehukumiwa, akajuta na
akarudisha vile vipande thelathini vya fedha
alivyopewa na viongozi wa makuhani na wazee
wa watu. 4 Akasema, “Nimetenda dhambi, kwa
maana nimeisaliti damu isiyo na hatia.”

Wakamjibu, “Hilo latuhusu nini sisi? Ni shauri yako.”

5 Basi Yuda akavitupa vile vipande vya fedha ndani ya Hekalu akaondoka akaenda kujinyonga.

6 Wale viongozi wa makuhani wakazichukua
zile fedha wakasema, “Si halali kuchanganya
fedha hizi na sadaka kwa sababu hizi ni fedha
zenye damu.” 7 Kwa hiyo baada ya kushau-
riana, waliamua kuzitumia kununulia shamba
la mfinyanzi, liwe mahali pa kuzikia wageni.
8 Hii ndiyo sababu lile shamba likaitwa Shamba
la Damu hadi leo. 9 Ndipo likatimia lile lililo-
nenwa na nabii Yeremia, kwamba, “Walichukua
vile vipande thelathini vya fedha, thamani aliy-
opangiwa na watu wa Israeli, 10 wakanunulia
shamba la mfinyanzi, kama vile Bwana alivyoni-
agiza.”

*Yesu Mbele Ya Pilato*
*(Marko 15:2-15; Luka 23:3-25; Yohana 18:33–19:16)*

11 Wakati huo Yesu akiwa amesimama mbele ya mtawala, mtawala akamuuliza, “Wewe ndiye mfalme wa Wayahudi?”

Yesu akasema, “Wewe wasema hivyo.”

12 Lakini viongozi wa makuhani na wazee
walipomshtaki, hakujibu neno. 13 Ndipo Pi-
lato akamuuliza, “Je, husikii ni mambo man-
gapi wanayokushtaki nayo?” 14 Lakini Yesu
hakumjibu hata kwa shtaka moja, kiasi kwamba
mtawala alishangaa sana.

15 Basi ilikuwa ni desturi ya mtawala kumfun-
gua mfungwa mmoja aliyechaguliwa na umati
wa watu wakati wa sikukuu. 16 Wakati huo
alikuwepo mfungwa mmoja mwenye sifa mbaya,
aliyeitwa Baraba. 17 Hivyo umati wa watu
walipokusanyika, Pilato akawauliza, “Mnataka
niwafungulie nani, Baraba au Yesu yeye aitwaye
Kristo?” 18 Kwa kuwa alitambua Yesu alikuwa
amekabidhiwa kwake kwa ajili ya wivu.

19 Pilato akiwa ameketi kwenye kiti cha
hukumu, mkewe akampelekea ujumbe huu:
“Usiwe na jambo lolote juu ya mtu huyu asiye
na hatia, kwa kuwa leo nimeteseka sana katika
ndoto kwa sababu yake.”

20 Lakini viongozi wa makuhani na wazee
wakaushawishi ule umati wa watu kwamba
waombe Baraba afunguliwe, naye Yesu auawe.

21 Mtawala akawauliza tena, “Ni yupi kati ya
hawa wawili mnayetaka niwafungulie?”

Wakajibu, “Baraba.”

22 Pilato akawaambia, “Basi nifanye nini na
huyu Yesu aitwaye Kristo?”

Wakajibu wote, “Msulubishe!”

23 Pilato akauliza, “Kwa nini? Amefanya kosa
gani?”

Lakini wao wakazidi kupiga kelele, wakisema,
“Msulubishe!”

24 Pilato alipoona kwamba hawezi kufanya
lolote, lakini badala yake ghasia zilikuwa zi-
naanza, akachukua maji, akanawa mikono yake
mbele ya ule umati wa watu, akasema, "Sina
hatia juu ya damu ya mtu huyu, hili ni jukumu
lenu!"
25 Watu wote wakajibu, "Damu yake na iwe juu
yetu na juu ya watoto wetu!"
26 Basi akawafungulia Baraba. Lakini baada
ya kuamuru Yesu achapwe mijeledi, akamtoa ili
asulubishwe.

### *Askari Wamdhihaki Yesu*
*(Marko 15:16-20; Yohana 19:2-3)*

27 Kisha askari wa mtawala wakampeleka
Yesu kwenye Praitorio* na wakakusanya kikosi
kizima cha askari kumzunguka. 28 Wakamvua
nguo zake na kumvika vazi la rangi nyekundu,
kisha 29 wakasokota taji ya miiba, wakaiweka
kichwani pake. Wakamwekea fimbo katika
mkono wake wa kuume, na wakapiga magoti
mbele zake na kumdhihaki, wakisema, "Salamu,
mfalme wa Wayahudi!" 30 Wakamtemea mate,
wakachukua ile fimbo wakampiga kichwani tena
na tena. 31 Baada ya kumdhihaki, wakamvua
lile joho, wakamvika tena nguo zake. Kisha
wakampeleka ili wakamsulubishe.

### *Yesu Asulubishwa*
*(Marko 15:21-32; Luka 23:26-43; Yohana 19:17-27)*

---

* **27:27** Praitorio maana yake ni makao makuu ya mtawala, jumba la kifalme lililokuwa linakaliwa na Pontio Pilato huko Yerusalemu, palipokuwa na kiti cha hukumu.

32 Walipokuwa wakienda, wakakutana na
mtu mmoja kutoka Kirene, jina lake Simoni,
nao wakamlazimisha kuubeba ule msalaba.
33 Wakafika mahali palipoitwa Golgotha (maana
yake ni Mahali pa Fuvu la Kichwa). 34 Hapo
wakampa Yesu divai iliyochanganywa na nyongo ili anywe; lakini alipoionja, akakataa
kuinywa. 35 Walipokwisha kumsulubisha wakagawana mavazi yake kwa kuyapigia kura. [Hili
lilifanyika ili litimie lile neno lililonenwa na
nabii, “Waligawa nguo zangu miongoni mwao na
vazi langu wakalipigia kura.”] 36 Kisha wakaketi,
wakamchunga. 37 Juu ya kichwa chake, kwenye
msalaba, wakaandika shtaka lake hivi: HUYU NI
YESU, MFALME WA WAYAHUDI. 38 Wanyang’anyi
wawili walisulubiwa pamoja naye, mmoja
upande wake wa kuume na mwingine upande
wa kushoto. 39 Watu waliokuwa wakipita njiani
wakamtukana huku wakitikisa vichwa vyao
40 na kusema, “Wewe ambaye utalivunja Hekalu
na kulijenga kwa siku tatu, jiokoe mwenyewe
basi! Kama wewe ni Mwana wa Mungu, shuka
kutoka msalabani.”

41 Vivyo hivyo, viongozi wa makuhani, walimu wa sheria pamoja na wazee wakamdhihaki wakisema, 42 “Aliwaokoa wengine, lakini
hawezi kujiokoa mwenyewe! Yeye ni Mfalme
wa Israeli! Ashuke sasa kutoka msalabani,
nasi tutamwamini. 43 Anamwamini Mungu,
basi Mungu na amwokoe sasa kama anamtaka, kwa maana alisema, ‘Mimi ni Mwana wa
Mungu.’ ” 44 Hata wale wanyang’anyi waliosulubiwa pamoja naye wakamtukana vivyo hivyo.

### *Kifo Cha Yesu*

*(Marko 15:33-41; Luka 23:44-49; Yohana 19:28-30)*

45 Tangu saa sita hadi saa tisa giza liliifunika
nchi yote. 46 Ilipofika saa tisa, Yesu akapaza sauti
akalia, *“Eloi, Eloi, lama sabakthani?”* (maana
yake, “Mungu wangu, Mungu wangu, mbona
umeniacha?”)

47 Baadhi ya watu waliokuwa wamesimama
pale waliposikia hayo, wakasema, “Anamwita
Eliya.”

48 Ghafula mmoja wao akaenda mbio na
kuleta sifongo, akaichovya kwenye siki, akai-
weka kwenye mwanzi na akampa Yesu ili anywe.
49 Wengine wakasema, “Basi mwacheni. Hebu
tuone kama Eliya atakuja kumwokoa.”

50 Yesu alipolia tena kwa sauti kuu, akaitoa
roho yake.

51 Wakati huo huo pazia la Hekalu likachanika
vipande viwili, kuanzia juu hadi chini. Dunia
ikatetemeka na miamba ikapasuka. 52 Makaburi
yakafunguka na miili ya watakatifu waliokuwa
wamekufa ikafufuliwa. 53 Wakatoka mak-
aburini, na baada ya Yesu kufufuka, waliingia
kwenye Mji Mtakatifu na kuwatokea watu wengi.

54 Basi yule jemadari na wale waliokuwa
pamoja naye wakimlinda Yesu walipoona lile
tetemeko na yale yote yaliyokuwa yametukia,
waliogopa, wakasema, “Hakika huyu alikuwa
Mwana wa Mungu!”

55 Walikuwako wanawake huko wakiangalia
kwa mbali. Hawa walikuwa wamemfuata Yesu
tangu Galilaya ili kushughulikia mahitaji yake.

56 Miongoni mwao walikuwepo Maria Magda-
lene, na Maria mama yao Yakobo na Yosefu, na
mama yao wana wa Zebedayo.

### *Maziko Ya Yesu*
*(Marko 15:42-47; Luka 23:50-56; Yohana 19:38-42)*

57 Ilipofika jioni, alifika mtu mmoja tajiri
kutoka Arimathaya aitwaye Yosefu, ambaye pia
alikuwa mwanafunzi wa Yesu. 58 Akamwendea
Pilato ili kumwomba mwili wa Yesu. Pilato akaa-
muru apewe. 59 Yosefu akauchukua mwili wa
Yesu, akaufunga katika kitambaa cha kitani safi,
60 na kuuweka katika kaburi lake mwenyewe
jipya, alilokuwa amelichonga kwenye mwamba.
Kisha akavingirisha jiwe kubwa katika ingilio la
kaburi, akaenda zake. 61 Maria Magdalene na
yule Maria mwingine walikuwepo mahali pale,
wakiwa wameketi mkabala na kaburi.

### *Walinzi Pale Kaburini*

62 Kesho yake, yaani siku iliyofuata ile ya
Maandalizi ya Sabato, viongozi wa makuhani na
Mafarisayo wakamwendea Pilato 63 na kusema,
“Bwana, tumekumbuka kwamba yule mdan-
ganyifu wakati alikuwa bado hai alisema, ‘Baada
ya siku tatu nitafufuka.’ 64 Kwa hiyo uamuru
kaburi lilindwe kwa uthabiti mpaka baada ya
siku tatu. La sivyo, wanafunzi wake wanaweza
kuja kuuiba mwili wake na kuwaambia watu
kwamba amefufuliwa kutoka kwa wafu. Udan-
ganyifu huu wa mwisho utakuwa mbaya kuliko
ule wa kwanza.”

65 Pilato akawaambia, “Ninyi mnao askari
walinzi. Nendeni, liwekeeni ulinzi kadri mweza-
vyo.” 66 Kwa hiyo wakaenda na walinzi ili
kulilinda kaburi kwa uthabiti, wakatia muhuri
kwenye lile jiwe na kuweka ulinzi.

# 28

*Yesu Afufuka*
*(Marko 16:1-10; Luka 24:1-12; Yohana 20:1-10)*

1 Baada ya Sabato, alfajiri mapema siku ya
kwanza ya juma, Maria Magdalene na yule
Maria mwingine walikwenda kulitazama kaburi.

2 Ghafula, pakawa na tetemeko kubwa la
ardhi, kwa sababu malaika wa Bwana al-
ishuka kutoka mbinguni, akaenda penye kaburi,
akalivingirisha lile jiwe na kulikalia. 3 Sura ya
huyo malaika ilikuwa kama umeme, na mavazi
yake yalikuwa meupe kama theluji. 4 Wale
walinzi wa kaburi walimwogopa sana, wakatete-
meka hata wakawa kama wafu.

5 Yule malaika akawaambia wale wanawake,
“Msiogope, kwa maana ninajua kuwa
mnamtafuta Yesu aliyesulubiwa. 6 Hayupo hapa,
kwa kuwa amefufuka, kama vile alivyosema.
Njooni mpatazame mahali alipokuwa amelazwa.
7 Kisha nendeni upesi mkawaambie wanafunzi
wake kwamba, ‘Amefufuka kutoka kwa wafu,
naye awatangulia kwenda Galilaya. Huko ndiko
mtamwona. Sasa nimekwisha kuwaambia.’ ”

8 Hivyo wale wanawake wakaondoka pale
kaburini wakiwa wamejawa na hofu, bali
wakiwa na furaha nyingi. Wakaenda mbio
kuwaeleza wanafunzi wake habari hizo.

9 Ghafula, Yesu akakutana nao, akasema,
“Salamu!” Wale wanawake wakamkaribia,
wakaishika miguu yake, wakamwabudu.
10 Ndipo Yesu akawaambia, “Msiogope. Nendeni
mkawaambie ndugu zangu waende Galilaya,
ndiko watakakoniona.”

### *Taarifa Ya Walinzi*

11 Wakati wale wanawake walikuwa njiani
wakienda, baadhi ya wale askari waliokuwa
wakilinda kaburi walienda mjini na kuwaeleza
viongozi wa makuhani kila kitu kilichokuwa
kimetukia. 12 Baada ya viongozi wa makuhani
kukutana na wazee na kutunga hila, wali-
wapa wale askari kiasi kikubwa cha fedha
13 wakiwaambia, “Inawapasa mseme, ‘Wana-
funzi wake walikuja wakati wa usiku na
kumwiba sisi tulipokuwa tumelala.’ 14 Kama
habari hizi zikimfikia mtawala, sisi tutamwon-
dolea mashaka nanyi hamtapata tatizo lolote.”
15 Kwa hiyo wale askari wakazipokea hizo fedha
nao wakafanya kama walivyoelekezwa. Habari
hii imeenea miongoni mwa Wayahudi mpaka
leo.

### *Yesu Awatuma Wanafunzi Wake*

*(Marko 16:14-18; Luka 24:36-49; Yohana 20:19-23; Matendo 1:6-8)*

16 Basi wale wanafunzi kumi na mmoja
wakaenda hadi Galilaya kwenye ule mlima am-
bao Yesu alikuwa amewaagiza. 17 Walipomwona,
wakamwabudu; lakini baadhi yao wakaona
shaka. 18 Yesu akawajia na kusema, “Nimepewa
mamlaka yote mbinguni na duniani. 19 Kwa

sababu hii, enendeni mkawafanye mataifa yote
kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa Jina la Baba
na la Mwana na la Roho Mtakatifu, 20 nanyi
wafundisheni kuyashika mambo yote niliyowaa-
muru ninyi. Hakika mimi niko pamoja nanyi
siku zote, hadi mwisho wa nyakati.”

# Marko

*Mahubiri Ya Yohana Mbatizaji*
*(Mathayo 3:1-12; Luka 3:1-8; Yohana 1:19-28)*

1 Mwanzo wa Injili ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu.

2 Kama ilivyoandikwa katika kitabu cha nabii Isaya:

"Tazama, nitamtuma mjumbe wangu mbele yako,
atakayetengeneza njia mbele yako":
3 "sauti ya mtu aliaye nyikani.
'Itengenezeni njia ya Bwana,
yanyoosheni mapito yake.' "

4 Yohana alikuja, akibatiza huko nyikani, akihu-
biri ubatizo wa toba kwa ajili ya msamaha wa
dhambi. 5 Watu kutoka Uyahudi wote na se-
hemu zote za Yerusalemu walikuwa wakimwen-
dea. Nao wakaziungama dhambi zao, akawa-
batiza katika Mto Yordani. 6 Yohana alivaa
mavazi yaliyotengenezwa kwa singa za ngamia
na mkanda wa ngozi kiunoni mwake. Chakula
chake kilikuwa nzige na asali ya mwitu. 7 Naye
alihubiri akisema, "Baada yangu atakuja yeye
aliye na uwezo kuniliko mimi, ambaye sistahili
hata kuinama na kulegeza kamba za viatu vyake.
8 Mimi nawabatiza kwa maji, lakini yeye atawa-
batiza kwa Roho Mtakatifu."

*Ubatizo Wa Yesu*
*(Mathayo 3:13-17; Luka 3:21-22)*

9 Wakati huo Yesu akaja kutoka Nazareti ya
Galilaya, naye akabatizwa na Yohana katika
Mto Yordani. 10 Yesu alipokuwa akitoka ndani
ya maji, aliona mbingu zikifunguka na Roho
akishuka juu yake kama hua. 11 Nayo sauti
kutoka mbinguni ikasema, "Wewe ni Mwanangu
mpendwa; nami nimependezwa nawe sana."

### *Majaribu Ya Yesu*
### *(Mathayo 4:1-11; Luka 4:1-13)*

12 Wakati huo huo, Roho akamwongoza Yesu
kwenda nyikani, 13 naye akawa huko nyikani
kwa muda wa siku arobaini, akijaribiwa na
Shetani. Alikaa na wanyama wa mwituni, nao
malaika wakamhudumia.

### *Yesu Aanza Kuhubiri*

14 Baada ya Yohana kukamatwa na kutiwa
gerezani, Yesu aliingia Galilaya akaanza kuhu-
biri habari njema ya Mungu, 15 akisema, "Wakati
umewadia, Ufalme wa Mungu umekaribia.
Tubuni na kuiamini Habari Njema."

### *Yesu Awaita Wanafunzi Wanne*
### *(Mathayo 4:12-22; Luka 4:14-15; 5:1-11)*

16 Yesu alipokuwa akitembea kando ya Bahari
ya Galilaya, aliwaona Simoni na Andrea nduguye
wakizitupa nyavu zao baharini, kwa kuwa wao
walikuwa wavuvi. 17 Yesu akawaambia, "Njooni,
nifuateni nami nitawafanya mwe wavuvi wa
watu." 18 Mara wakaacha nyavu zao, wakamfu-
ata.
19 Alipokwenda mbele kidogo, akamwona
Yakobo mwana wa Zebedayo na Yohana
nduguye, wakiwa kwenye mashua yao

wakizitengeneza nyavu zao. [20] Papo hapo
akawaita, nao wakamwacha Zebedayo baba
yao kwenye mashua pamoja na watumishi wa
kuajiriwa, nao wakamfuata Yesu.

### *Yesu Amtoa Pepo Mchafu (Luka 4:31-37)*

[21] Wakaenda mpaka Kapernaumu. Ilipofika
siku ya Sabato, mara Yesu akaingia sinagogi,
akaanza kufundisha. [22] Watu wakashangaa
sana kwa mafundisho yake, kwa maana aliwa-
fundisha kama yeye aliye na mamlaka, wala si
kama walimu wa sheria. [23] Wakati huo huo
katika sinagogi lao palikuwa na mtu aliyekuwa
amepagawa na pepo mchafu, [24] naye akapiga
kelele akisema, "Tuna nini nawe, Yesu wa
Nazareti? Je, umekuja kutuangamiza? Ninaku-
jua wewe ni nani. Wewe ndiwe Aliye Mtakatifu
wa Mungu!"

[25] Lakini Yesu akamkemea, akamwambia,
"Nyamaza kimya! Nawe umtoke!" [26] Yule pepo
mchafu akamtikisatikisa huyo mtu kwa nguvu,
kisha akamtoka akipiga kelele kwa sauti kubwa.
[27] Watu wote wakashangaa, hata wakaulizana
wao kwa wao, "Haya ni mambo gani? Ni
mafundisho mapya, tena yenye mamlaka! Anaa-
muru hata pepo wachafu, nao wanamtii!" [28] Sifa
zake zikaanza kuenea haraka katika eneo lote la
karibu na Galilaya.

### *Yesu Amponya Mama Mkwe Wa Simoni (Mathayo 8:14-15; Luka 4:38-39)*

[29] Mara walipotoka katika sinagogi, walik-
wenda pamoja na Yakobo na Yohana hadi

nyumbani kwa Simoni na Andrea. 30 Mama
mkwe wa Simoni alikuwa kitandani, ana
homa, nao wakamweleza Yesu habari zake.
31 Hivyo Yesu akamwendea, akamshika mkono
na kumwinua. Kisha homa ikamwacha, naye
akaanza kuwahudumia.

### *Yesu Aponya Wengi*
### *(Mathayo 8:16-17; Luka 4:40-41)*

32 Jioni ile baada ya jua kutua, watu wakam-
letea Yesu wagonjwa wote na waliopagawa na
pepo wachafu. 33 Mji wote ukakusanyika mbele
ya nyumba hiyo. 34 Yesu akawaponya watu
wengi waliokuwa na magonjwa ya aina mbal-
imbali. Akawatoa pepo wachafu wengi, lakini
hakuwaacha hao pepo wachafu waseme, kwa
sababu walimjua yeye ni nani.

### *Yesu Aenda Galilaya*
### *(Luka 4:42-44)*

35 Alfajiri na mapema sana kulipokuwa bado
kuna giza, Yesu akaamka, akaondoka, akaenda
mahali pa faragha ili kuomba. 36 Simoni na wen-
zake wakaenda kumtafuta, 37 nao walipomwona,
wakamwambia, “Kila mtu anakutafuta!”

38 Yesu akawajibu, “Twendeni mahali pengine
kwenye vijiji jirani, ili niweze kuhubiri huko
pia, kwa sababu hicho ndicho nilichokuja kuk-
ifanya.” 39 Kwa hiyo akazunguka Galilaya kote,
akihubiri katika masinagogi yao na kutoa pepo
wachafu.

### *Yesu Amtakasa Mwenye Ukoma*
### *(Mathayo 8:1-4; Luka 5:12-16)*

40 Mtu mmoja mwenye ukoma alimjia Yesu,
akamwomba akipiga magoti, akamwambia, “Uk-
itaka, waweza kunitakasa.”
41 Yesu, akiwa amejawa na huruma, akany-
oosha mkono wake akamgusa, akamwambia,
“Nataka. Takasika!” 42 Mara ukoma ukamtoka,
naye akatakasika. 43 Baada ya Yesu kumwonya
vikali, akamruhusu aende zake 44 akimwambia,
“Hakikisha humwambii mtu yeyote habari hizi,
bali nenda ukajionyeshe kwa kuhani, na uka-
toe sadaka alizoagiza Mose kwa utakaso wako,
ili kuwa ushuhuda kwao.” 45 Lakini yule
mtu akaenda akaanza kutangaza habari za
kuponywa kwake waziwazi. Kwa hiyo, Yesu
hakuweza tena kuingia katika miji waziwazi
lakini alikaa sehemu zisizo na watu. Hata hivyo
watu wakamfuata huko kutoka kila upande.

# 2

### *Yesu Amponya Mtu Aliyepooza*
### *(Mathayo 9:1-8; Luka 5:17-26)*

1 Baada ya siku kadhaa Yesu alirudi Kaper-
naumu, watu wakasikia kwamba amerudi
nyumbani. 2 Hivyo watu wengi wakakusanyika
kiasi kwamba hapakubaki nafasi yoyote hata
mlangoni! Naye akawahubiria Neno. 3 Ndipo
baadhi ya watu wakaja wakamletea Yesu mtu
aliyepooza, akiwa amebebwa na watu wanne.
4 Kwa kuwa walikuwa hawawezi kumfikisha
kwa Yesu kwa ajili ya umati wa watu, walitoboa
tundu kwenye paa mahali pale alipokuwa Yesu,
wakamshusha yule aliyepooza kwa kitanda ali-
chokuwa amelalia. 5 Yesu alipoiona imani yao,

alimwambia yule mtu aliyepooza, “Mwanangu,
dhambi zako zimesamehewa.”
6 Basi baadhi ya walimu wa sheria waliokuwa
wameketi huko wakawaza mioyoni mwao,
7 “Kwa nini mtu huyu anasema hivi? Huyu
anakufuru! Ni nani awezaye kusamehe dhambi
isipokuwa Mungu peke yake?”
8 Mara moja Yesu akatambua rohoni mwake
kile walichokuwa wanawaza mioyoni mwao,
naye akawaambia, “Kwa nini mnawaza hivyo
mioyoni mwenu? 9 Je, ni lipi lililo rahisi zaidi:
kumwambia huyu aliyepooza, ‘Umesamehewa
dhambi zako,’ au kusema, ‘Inuka, uchukue
mkeka wako, uende’? 10 Lakini ili mpate
kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anayo
mamlaka duniani kusamehe dhambi…” Yesu
akamwambia yule aliyepooza, 11 “Nakuambia,
inuka, chukua mkeka wako, uende nyumbani
kwako.” 12 Yule mtu aliyekuwa amepooza
akasimama, akachukua mkeka wake, akatembea
machoni pao wote! Jambo hili likawashangaza
wote, wakamtukuza Mungu, wakisema, “Hatu-
japata kuona jambo kama hili kamwe!”

### *Yesu Amwita Lawi*
### *(Mathayo 9:9-13; Luka 5:27-32)*

13 Yesu akaenda tena kandokando ya Bahari
ya Galilaya. Umati mkubwa wa watu ukamfu-
ata, naye akaanza kuwafundisha. 14 Alipokuwa
akitembea, akamwona Lawi mwana wa Alfayo
ameketi forodhani mahali pa kutoza ushuru,
akamwambia, “Nifuate.” Lawi akaondoka,
akamfuata Yesu.

15 Yesu alipokuwa akila chakula nyumbani
mwa Lawi, watoza ushuru wengi pamoja na
“wenye dhambi” walikuwa wakila pamoja naye
na wanafunzi wake, kwa maana kulikuwa na
watu wengi waliokuwa wakimfuata. 16 Baadhi
ya walimu wa sheria waliokuwa Mafarisayo
walipomwona akila pamoja na watoza ushuru
na “wenye dhambi,” wakawauliza wanafunzi
wake: “Mbona Yesu anakula pamoja na watoza
ushuru na ‘wenye dhambi’?”
17 Yesu aliposikia haya akawaambia, “Watu
wenye afya hawahitaji tabibu, bali walio wag-
onjwa. Sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye
dhambi.”

### *Yesu Aulizwa Kuhusu Kufunga (Mathayo 9:14-17; Luka 5:33-39)*

18 Basi wanafunzi wa Yohana pamoja na Ma-
farisayo walikuwa wakifunga. Baadhi ya watu
wakamjia Yesu na kumuuliza, “Mbona wana-
funzi wa Yohana na wa Mafarisayo hufunga
lakini wanafunzi wako hawafungi?”
19 Yesu akawajibu, “Wageni wa bwana arusi
wawezaje kufunga wakati angali pamoja nao?
Wakati bwana arusi bado yuko pamoja nao,
hawawezi kufunga. 20 Lakini wakati utafika
ambapo bwana arusi ataondolewa kwao. Siku
hiyo ndipo watakapofunga.
21 “Hakuna mtu ashoneaye kiraka cha nguo
mpya kwenye nguo iliyochakaa. Akifanya hivyo,
kile kiraka kipya kitachanika kutoka ile nguo
iliyochakaa, nayo itachanika zaidi. 22 Wala
hakuna mtu awekaye divai mpya kwenye viriba

vikuukuu. Akifanya hivyo, ile divai mpya itavipasua hivyo viriba, nayo hiyo divai itamwagika na viriba vitaharibika. Lakini divai mpya huwekwa kwenye viriba vipya."

### *Bwana Wa Sabato*
### *(Mathayo 12:1-8; Luka 6:1-5)*

23 Siku moja ya Sabato, Yesu pamoja na wanafunzi wake walikuwa wakipita katikati ya mashamba ya nafaka. Walipokuwa wakitembea, wanafunzi wake wakaanza kuvunja masuke.
24 Mafarisayo wakamwambia, "Tazama, mbona wanafanya jambo lisilo halali kufanywa siku ya Sabato?"
25 Yesu akawajibu, "Je, hamjasoma kamwe alivyofanya Daudi wakati yeye na wenzake walikuwa na njaa, wakahitaji chakula? 26 Daudi
aliingia katika nyumba ya Mungu, wakati Abiathari alikuwa kuhani mkuu, akaila ile mikate iliyowekwa wakfu, ambayo ni halali kuliwa na makuhani peke yao. Naye pia akawapa wenzake."
27 Kisha Yesu akawaambia, "Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu, lakini si mwanadamu
kwa ajili ya Sabato. 28 Hivyo, Mwana wa Adamu
ndiye Bwana wa Sabato."

# 3

### *Mtu Aliyepooza Mkono Aponywa*
### *(Mathayo 12:9-14; Luka 6:6-11)*

1 Yesu akaingia tena ndani ya sinagogi, na huko palikuwa na mtu aliyepooza mkono.

2 Wakawa wanamwangalia waone kama atam-
ponya siku ya Sabato, ili wapate sababu ya
kumshtaki. 3 Yesu akamwambia yule mwenye
mkono uliopooza, “Njoo hapa mbele ya watu
wote.”
4 Kisha Yesu akawauliza, “Je, ni lipi lililo halali
siku ya Sabato: Ni kutenda mema au kutenda
mabaya? Ni kuokoa maisha au kuua?” Lakini
wao wakanyamaza kimya.
5 Yesu akawatazama pande zote kwa hasira,
akahuzunika sana kwa ajili ya ugumu wa mioyo
yao. Akamwambia yule mtu mwenye mkono
uliopooza, “Nyoosha mkono wako.” Akauny-
oosha, nao ukaponywa kabisa! 6 Kisha Ma-
farisayo wakatoka nje, nao wakaanza kufanya
shauri la kumuua Yesu wakiwa na Maherode.

### *Umati Wa Watu Wamfuata Yesu*

7 Yesu pamoja na wanafunzi wake wakaon-
doka huko wakaenda baharini, nao umati
mkubwa wa watu kutoka Galilaya ukamfu-
ata. 8 Waliposikia mambo yote aliyokuwa
akiyafanya, umati mkubwa wa watu ukamjia
kutoka Uyahudi, Yerusalemu, Idumaya, na
ng’ambo ya Yordani, pamoja na wale wa sehemu
za karibu na Tiro na Sidoni. 9 Kwa sababu ya
umati mkubwa wa watu, aliwaambia wanafunzi
wake waweke tayari mashua ndogo kwa ajili
yake, ili kuwazuia watu kumsonga. 10 Kwa kuwa
alikuwa amewaponya wagonjwa wengi, wale
wenye magonjwa walikuwa wanasukumana ili
wapate kumgusa. 11 Kila mara pepo wachafu
walipomwona, walianguka chini mbele yake na
kupiga kelele wakisema, “Wewe ndiwe Mwana

wa Mungu.” 12 Lakini aliwaonya wasimseme
yeye ni nani.

### *Yesu Achagua Mitume Kumi Na Wawili*
### *(Mathayo 10:1-4; Luka 6:12-16)*

13 Yesu akapanda mlimani na kuwaita wale
aliowataka, nao wakamjia. 14 Akawachagua
kumi na wawili, ambao aliwaita mitume, ili
wapate kuwa pamoja naye, na awatume kwenda
kuhubiri 15 na kuwa na mamlaka ya kutoa pepo
wachafu. 16 Hawa ndio wale kumi na wawili
aliowachagua: Simoni (ambaye alimwita Petro);
17 Yakobo mwana wa Zebedayo, na Yohana
nduguye (ambao aliwaita Boanerge, maana yake
Wana wa Ngurumo); 18 Andrea, Filipo, Bartholo-
mayo, Mathayo, Tomaso, Yakobo mwana wa
Alfayo, Thadayo, Simoni Mkananayo, 19 na Yuda
Iskariote aliyemsaliti Yesu.

### *Yesu Na Beelzebuli*
### *(Mathayo 12:22-32; Luka 11:14-23; 12:10)*

20 Kisha Yesu aliporudi nyumbani, umati wa
watu ukakusanyika tena, kiasi kwamba yeye
na wanafunzi wake hawakuweza kula chakula.
21 Ndugu zake walipopata habari wakaja ili kum-
chukua kwa maana watu walikuwa wakisema,
“Amerukwa na akili.”

22 Walimu wa sheria walioteremka kutoka
Yerusalemu walisema, “Amepagawa na Beelze-
buli!* Anatoa pepo wachafu kwa kutumia mkuu
wa pepo wachafu!”

---

* **3:22** Beelzebuli kwa Kiyunani ni Beelzebubu, yaani mkuu wa pepo wachafu.

23 Basi Yesu akawaita na kuzungumza nao
kwa mifano akasema: “Shetani awezaje kum-
toa Shetani? 24 Kama ufalme ukigawanyika
dhidi yake wenyewe, ufalme huo hauwezi kusi-
mama. 25 Nayo nyumba kama ikigawanyika
dhidi yake yenyewe, nyumba hiyo haiwezi
kusimama. 26 Naye Shetani kama akijipinga
mwenyewe na awe amegawanyika, hawezi kusi-
mama bali mwisho wake umewadia. 27 Hakuna
mtu yeyote awezaye kuingia kwenye nyumba
ya mtu mwenye nguvu na kuteka nyara mali
zake asipomfunga kwanza yule mwenye nguvu.
Ndipo ataweza kuteka nyara mali zake. 28 Amin,
nawaambia, dhambi zote na makufuru yote ya
wanadamu watasamehewa. 29 Lakini yeyote
anayemkufuru Roho Mtakatifu hatasamehewa
kamwe, atakuwa na hatia ya dhambi ya milele.”

30 Yesu alisema hivi kwa sababu walikuwa
wanasema, “Ana pepo mchafu.”

### *Mama Na Ndugu Zake Yesu (Mathayo 12:46-50; Luka 8:19-21)*

31 Kisha wakaja ndugu zake Yesu pamoja na
mama yake. Wakasimama nje, wakamtuma mtu
kumwita. 32 Umati wa watu ulikuwa umeketi
kumzunguka, nao wakamwambia, “Mama yako
na ndugu zako wako nje, wanakutafuta.”

33 Akawauliza, “Mama yangu na ndugu zangu
ni nani?”

34 Kisha akawatazama wale watu waliokuwa
wameketi kumzunguka pande zote, akasema,
“Hawa ndio mama yangu na ndugu zangu.
35 Mtu yeyote anayetenda mapenzi ya Mungu,

huyo ndiye ndugu yangu, na dada yangu na
mama yangu."

# 4

*Mfano Wa Mpanzi*
*(Mathayo 13:1-9; Luka 8:4-8)*

1 Yesu akaanza kufundisha tena kando ya
bahari. Umati wa watu uliokuwa umekusanyika
kumzunguka ulikuwa mkubwa, kiasi kwamba il-
imbidi Yesu aingie kwenye mashua iliyokuwa ba-
harini na kuketi humo, nao watu wote walikuwa
ufuoni mwa bahari. 2 Akawafundisha mambo
mengi kwa mifano, naye katika mafundisho yake
akasema: 3 "Sikilizeni! Mpanzi alitoka kwenda
kupanda mbegu zake. 4 Alipokuwa akitawanya
mbegu, nyingine zilianguka kando ya njia, nao
ndege wakaja na kuzila. 5 Nyingine zilianguka
kwenye ardhi yenye mwamba isiyo na udongo
wa kutosha. Zikaota haraka, kwa kuwa udongo
ulikuwa haba. 6 Lakini jua lilipozidi, mimea
ikanyauka na kukauka kwa kuwa mizizi yake
haikuwa na kina. 7 Mbegu nyingine zilian-
guka kwenye miiba, nayo miiba hiyo ikakua,
ikaisonga hiyo mimea, hivyo haikutoa mazao.
8 Mbegu nyingine zilianguka kwenye udongo
mzuri, zikaota vizuri na kukua, zikatoa mazao,
moja mara thelathini, nyingine mara sitini, na
nyingine mara mia moja."

9 Kisha Yesu akasema, "Mwenye masikio ya
kusikia, na asikie."

*Sababu Za Mifano*
*(Mathayo 13:10-17; Luka 8:9-10)*

10 Alipokuwa peke yake, watu waliokuwepo
naye pamoja na wanafunzi wake kumi na wawili
wakamuuliza kuhusu mifano yake. 11 Naye
akawaambia, "Ninyi mmepewa kujua siri ya
Ufalme wa Mungu. Lakini kwa wale walioko nje,
kila kitu husemwa kwao kwa mifano, 12 ili,
" 'daima waone lakini wasitambue,
daima wasikie lakini wasielewe;
wasije wakageuka, wakatubu na kusamehewa!' "

*Yesu Afafanua Maana Ya Mfano Wa Mbegu*
*(Mathayo 13:18-23; Luka 8:11-15)*

13 Kisha Yesu akawauliza, "Hamwelewi maana
ya mfano huu? Basi mtaelewaje mifano
mingine? 14 Yule mpanzi hupanda neno. 15 Hawa
ndio wale walio kando ya njia ambako neno
lilipandwa. Walisikiapo neno, Shetani huja mara
na kulinyakua lile neno lililopandwa ndani yao.
16 Nazo zile mbegu zilizoanguka kwenye udongo
wenye miamba, ni wale wanaolisikia neno, na
mara hulipokea kwa furaha. 17 Lakini kwa kuwa
hawana mizizi, wao hudumu kwa muda mfupi
tu. Kisha dhiki au mateso yanapoinuka kwa ajili
ya lile neno, mara wao huiacha imani. 18 Lakini
wengine, kama mbegu iliyopandwa kwenye mi-
iba, hulisikia lile neno; 19 lakini masumbufu ya
maisha haya, na udanganyifu wa mali na tamaa
ya mambo mengine huja na kulisonga lile neno
na kulifanya lisizae. 20 Wengine, kama mbegu
iliyopandwa kwenye udongo mzuri, hulisikia lile
neno, wakalipokea na kuzaa mazao. Wao huzaa
mara thelathini, au mara sitini, au mara mia ya
mbegu iliyopandwa."

### *Mfano Wa Taa*
### *(Luka 8:16-18)*

21 Akawaambia, "Je, taa huwashwa na kufu-
nikwa chini ya kikapu au mvunguni mwa ki-
tanda? Je, haiwashwi na kuwekwa juu ya kinara
chake? 22 Kwa kuwa hakuna kilichofichika am-
bacho hakitafunuliwa, wala hakuna jambo lolote
la siri ambalo halitaletwa nuruni. 23 Mwenye
masikio ya kusikia, na asikie."

24 Naye akawaambia, "Kuweni waangalifu na
yale mnayosikia. Kipimo kile mpimacho, ndicho
mtakachopimiwa ninyi, hata na zaidi. 25 Kwa
maana kila mtu aliye na kitu atapewa zaidi, naye
atakuwa navyo tele. Lakini yule asiye na kitu,
hata kile alicho nacho atanyang'anywa."

### *Mfano Wa Mbegu Inayoota*

26 Pia akawaambia, "Ufalme wa Mungu un-
afanana na mtu apandaye mbegu shambani.
27 Akiisha kuzipanda, usiku na mchana, akiwa
amelala au ameamka, mbegu huota na kukua
pasipo yeye kujua ikuavyo. 28 Udongo huifanya
iote kuwa mche, halafu suke, kisha nafaka
kamili kwenye suke. 29 Lakini nafaka inapokuwa
imekomaa, mara mkulima huingia shambani na
mundu wa kuvunia, maana mavuno yamekuwa
tayari."

### *Mfano Wa Mbegu Ya Haradali*
### *(Mathayo 13:31-32, 34; Luka 13:18-19)*

30 Akawaambia tena, "Tuufananishe Ufalme
wa Mungu na nini? Au tutumie mfano gani ili
kuueleza? 31 Ni kama punje ya haradali, ambayo

ni mbegu ndogo sana kuliko mbegu zote zina-
zopandwa ardhini. 32 Lakini ikishaota, hukua
ikawa mmea mkubwa kuliko yote ya bustanini,
ikawa na matawi makubwa hata ndege wa
angani wanaweza kujenga viota kwenye matawi
yake."
33 Kwa mifano mingine mingi kama hii Yesu
alinena nao neno lake, kwa kadiri walivyoweza
kulielewa. 34 Hakusema nao neno lolote pasipo
mfano. Lakini alipokuwa na wanafunzi wake,
aliwafafanulia kila kitu.

### *Yesu Atuliza Dhoruba*
### *(Mathayo 8:23-27; Luka 8:22-25)*

35 Siku hiyo ilipokaribia jioni, aliwaambia
wanafunzi wake, "Tuvukeni twende mpaka
ng'ambo." 36 Wakauacha ule umati wa watu, na
wakamchukua vile alivyokuwa kwenye mashua.
Palikuwa pia na mashua nyingine nyingi pamoja
naye. 37 Kukawa na dhoruba kali, nayo maw-
imbi yakaipiga ile mashua hata ikawa karibu
kujaa maji. 38 Yesu alikuwa katika shetri,
akiwa analala juu ya mto. Wanafunzi wake
wakamwamsha, wakamwambia, "Mwalimu, hu-
jali kama tunazama?"
39 Akaamka, akaukemea ule upepo, akayaam-
bia yale mawimbi, "Uwe kimya! Tulia!" Ule
upepo ukatulia, kukawa shwari kabisa.
40 Yesu akawaambia wanafunzi wake, "Kwa
nini mnaogopa hivyo? Je, bado hamna imani?"
41 Nao wakawa wameogopa sana,
wakaulizana, "Ni nani huyu ambaye hata upepo
na mawimbi vinamtii?"

# 5

## *Yesu Amponya Mtu Mwenye Pepo (Mathayo 8:28-34; Luka 8:26-39)*

1 Wakafika upande wa pili wa ziwa wakaingia
katika nchi ya Wagerasi. 2 Yesu alipotoka kwenye
mashua, mara mtu mmoja mwenye pepo mchafu
akatoka makaburini akakutana naye. 3 Mtu
huyu aliishi makaburini, wala hakuna aliyeweza
kumzuia hata kwa kumfunga minyororo. 4 Kwa
kuwa mara kwa mara alikuwa amefungwa miny-
ororo mikononi na miguuni, lakini akaikata
hiyo minyororo na kuzivunja zile pingu miguuni
mwake. Hapakuwa na mtu yeyote aliyekuwa
na nguvu za kumzuia. 5 Usiku na mchana
alikuwa makaburini na milimani, akipiga kelele
na kujikatakata kwa mawe.

6 Alipomwona Yesu kwa mbali, alimkimbilia,
akapiga magoti mbele yake. 7 Akapiga kelele kwa
nguvu akisema, "Una nini nami, Yesu, Mwana
wa Mungu Aliye Juu Sana? Ninakusihi kwa jina
la Mungu, usinitese!" 8 Kwa kuwa Yesu alikuwa
amemwambia, "Mtoke mtu huyu, wewe pepo
mchafu!"

9 Yesu akamuuliza, "Jina lako ni nani?"

Akamjibu, "Jina langu ni Legioni,* kwa kuwa
tuko wengi." 10 Akamsihi Yesu sana asiwapeleke
nje ya nchi ile.

11 Palikuwa na kundi kubwa la nguruwe
lililokuwa likilisha karibu kando ya kilima.
12 Wale pepo wachafu wakamsihi Yesu
wakisema, "Tuamuru twende kwenye wale

---

* **5:9** Legioni maana yake ni Jeshi.

nguruwe. Turuhusu tuwaingie.” 13 Basi
Yesu akawaruhusu, nao wale pepo wachafu wakatoka, wakawaingia hao nguruwe. Lile kundi lilikuwa na nguruwe wapatao 2,000, nao wote wakateremkia gengeni kwa kasi, nao wakatumbukia ziwani na kuzama.

14 Wale watu waliokuwa wakichunga hao
nguruwe wakakimbilia mjini na vijijini kueleza yaliyotukia. Watu wakatoka kwenda kuona
hayo yaliyokuwa yametukia. 15 Walipofika kwa
Yesu, wakamwona yule mtu aliyekuwa amepagawa na pepo wachafu legioni akiwa ameketi hapo, amevaa nguo na mwenye akili timamu.
Wakaogopa. 16 Wale walioyaona mambo hayo
wakawaeleza watu wengine yaliyomtokea yule mtu aliyekuwa amepagawa na pepo wachafu, na
habari za lile kundi la nguruwe pia. 17 Basi watu
wakaanza kumwomba Yesu aondoke katika nchi yao.

18 Yesu alipokuwa anaingia kwenye mashua,
yule mtu aliyekuwa amepagawa na pepo wachafu akamsihi Yesu waende pamoja.
19 Yesu hakumruhusu, bali alimwambia,
“Nenda nyumbani kwa jamaa yako ukawaeleze mambo makuu aliyokutendea Bwana, na jinsi
alivyokuhurumia.” 20 Yule mtu akaenda zake,
akaanza kutangaza katika Dekapoli mambo makuu Yesu aliyomtendea. Nao watu wote wakastaajabu.

### *Mwanamke Aponywa*
### *(Mathayo 9:18-26; Luka 8:40-56)*

21 Yesu alipokwisha kuvuka tena na kufika
ng'ambo, umati mkubwa wa watu ukamzunguka
yeye akiwa hapo kando ya bahari. 22 Kisha
mmoja wa viongozi wa sinagogi aliyeitwa Yairo
akafika pale. Naye alipomwona Yesu, akapiga
magoti miguuni pake, 23 akamsihi akisema,
"Binti yangu mdogo ni mgonjwa mahututi.
Tafadhali nakusihi, njoo uweke mikono yako
juu yake ili apate kupona, naye atakuwa hai."
24 Hivyo Yesu akaenda pamoja naye.

Umati mkubwa wa watu ukamfuata, nao watu
wakawa wanamsonga. 25 Hapo palikuwa na
mwanamke aliyekuwa amesumbuliwa na tatizo
la kutokwa damu kwa miaka kumi na miwili.
26 Mwanamke huyu alikuwa ameteseka sana
kwa mikono ya matabibu wengi, na kutumia
kila kitu alichokuwa nacho. Lakini badala ya
kupona, hali yake ilizidi kuwa mbaya. 27 Alikuwa
amesikia habari za Yesu, naye akaja kwa nyuma
yake kwenye umati wa watu, akaligusa vazi lake,
28 kwa maana alisema moyoni mwake, "Kama
nikiweza kuligusa vazi lake tu, nitaponywa."
29 Mara kutoka damu kwake kukakoma, naye
akajisikia mwilini mwake amepona kabisa.

30 Ghafula Yesu akatambua kuwa nguvu
zimemtoka. Akaugeukia ule umati wa watu na
kuuliza, "Ni nani aliyegusa mavazi yangu?"

31 Wanafunzi wake wakamjibu, "Unaona jinsi
umati wa watu unavyokusonga. Wawezaje
kuuliza, 'Ni nani aliyenigusa?' "

32 Lakini Yesu akaangalia pande zote ili aone
ni nani aliyemgusa. 33 Yule mwanamke, ak-
ijua kilichomtokea, akaja, akaanguka miguuni

pake akitetemeka kwa hofu, akamweleza ukweli
wote. 34 Yesu akamwambia, “Binti, imani yako
imekuponya. Nenda kwa amani, upone kabisa
ugonjwa wako.”

### *Yesu Amfufua Binti Yairo*

35 Alipokuwa bado anaongea, watu wakafika
kutoka nyumbani kwa Yairo. Wakamwambia,
“Binti yako amekufa. Kwa nini kuendelea kum-
sumbua Mwalimu?”
36 Aliposikia hayo waliyosema, Yesu
akamwambia huyo kiongozi wa sinagogi,
“Usiogope. Amini tu.”
37 Hakumruhusu mtu mwingine yeyote am-
fuate isipokuwa Petro, Yakobo na Yohana,
nduguye Yakobo. 38 Walipofika nyumbani kwa
yule kiongozi wa sinagogi, Yesu akaona gha-
sia, watu wakilia na kuomboleza kwa sauti
kubwa. 39 Alipokwisha kuingia ndani, akawaam-
bia, “Kwa nini mnafanya ghasia na kulia? Mtoto
hajafa, bali amelala tu.” 40 Wale watu wakam-
cheka kwa dharau.
Lakini yeye akawatoa wote nje, akawachukua
baba na mama wa yule mtoto, pamoja na
wale wanafunzi aliokuwa nao. Wakain-
gia ndani mpaka pale alipokuwa yule mtoto.
41 Akamshika mtoto mkono, akamwambia, *“Tal-
itha koum!”*† (maana yake ni, “Msichana,
nakuambia: amka!”) 42 Mara yule msichana
akasimama, akaanza kutembea (alikuwa na
umri wa miaka kumi na miwili). Walipoona

† **5:41** Talitha koum ni lugha ya Kiaramu.

haya, wakastaajabu sana. 43 Yesu akawaag-
iza kwa ukali wasimweleze mtu yeyote jambo
hilo, naye akawaambia wampe yule msichana
chakula.

# 6

## *Nabii Hana Heshima Kwao (Mathayo 13:53-58; Luka 4:16-30)*

1 Yesu akaondoka huko na kwenda mji
wa kwao, akiwa amefuatana na wanafunzi
wake. 2 Ilipofika siku ya Sabato, akaanza ku-
fundisha katika sinagogi, na wengi waliomsikia
wakashangaa.

Nao wakauliza, "Mtu huyu ameyapata wapi
mambo haya yote? Tazama ni hekima ya namna
gani hii aliyopewa? Tazama matendo ya miujiza
ayafanyayo kwa mikono yake! 3 Huyu si yule
seremala, mwana wa Maria? Na ndugu zake si
Yakobo, Yose,* Yuda na Simoni? Dada zake wote
si tuko nao hapa kwetu?" Nao wakachukizwa
sana kwa ajili yake, wakakataa kumwamini.

4 Yesu akawaambia, "Nabii hakosi heshima
isipokuwa katika mji wake mwenyewe, na mion-
goni mwa jamaa na ndugu zake, na nyum-
bani kwake." 5 Hakufanya miujiza yoyote
huko isipokuwa kuweka mikono yake juu ya
wagonjwa wachache na kuwaponya. 6 Naye
akashangazwa sana kwa jinsi wasivyokuwa na
imani.

## *Yesu Awatuma Wale Kumi Na Wawili (Mathayo 10:5-15; Luka 9:1-6)*

* **6:3** Yosefu kwa Kiyunani ni Joses.

Kisha Yesu akawa anakwenda kutoka kijiji
kimoja hadi kingine akifundisha. 7 Akawaita
wale kumi na wawili, akawatuma wawili wawili,
na kuwapa mamlaka kutoa pepo wachafu.

8 Akawaagiza akisema, “Msichukue chochote
kwa ajili ya safari isipokuwa fimbo tu.
Msichukue mkate, wala mkoba, wala fedha
kwenye mikanda yenu. 9 Vaeni viatu, lakini
msivae nguo ya ziada.” 10 Akawaambia,
“Mkiingia kwenye nyumba yoyote, kaeni
humo hadi mtakapoondoka katika mji huo.
11 Kama mahali popote hawatawakaribisha wala
kuwasikiliza, mtakapoondoka huko, kung’uteni
mavumbi kutoka kwenye miguu yenu ili kuwa
ushuhuda dhidi yao.”

12 Kwa hiyo wakatoka na kuhubiri kwamba
inawapasa watu kutubu na kuacha dhambi.
13 Wakatoa pepo wachafu wengi, wakawapaka
wagonjwa wengi mafuta na kuwaponya.

### *Yohana Mbatizaji Akatwa Kichwa*
### *(Mathayo 14:1-12; Luka 9:7-9)*

14 Mfalme Herode akasikia habari hizi, kwa
maana jina la Yesu lilikuwa limejulikana sana.
Watu wengine walikuwa wakisema, “Yohana
Mbatizaji amefufuliwa kutoka kwa wafu, ndiyo
sababu nguvu za kutenda miujiza zinafanya kazi
ndani yake.”

15 Wengine wakasema, “Yeye ni Eliya.”

Nao wengine wakasema, “Yeye ni nabii, kama
mmojawapo wa wale manabii wa zamani.”

16 Lakini Herode aliposikia habari hizi,
akasema, “Huyo ni Yohana Mbatizaji,

niliyemkata kichwa, amefufuliwa kutoka kwa
wafu!"

17 Kwa kuwa Herode alikuwa ameagiza
kwamba Yohana Mbatizaji akamatwe, afungwe
na kutiwa gerezani. Alifanya hivi kwa sababu
ya Herodia, mke wa Filipo, ndugu yake, ambaye
Herode alikuwa amemwoa. 18 Yohana alikuwa
amemwambia Herode, "Si halali kwako kuwa
na mke wa ndugu yako." 19 Kwa hiyo Herodia
alikuwa amemwekea Yohana kinyongo akataka
kumuua. Lakini hakuweza, 20 kwa sababu
Herode alimwogopa Yohana akijua kwamba ni
mtu mwenye haki na mtakatifu, hivyo akam-
linda. Herode alifadhaika sana alipomsikia
Yohana, lakini bado alipenda kumsikiliza.

21 Mfalme Herode alifanya karamu kubwa
wakati wa sikukuu ya kuzaliwa kwake. Akawaa-
lika maafisa wake wakuu, majemadari wa jeshi
na watu mashuhuri wa Galilaya. Hatimaye Hero-
dia alipata wasaa aliokuwa akiutafuta. 22 Binti
yake Herodia alipoingia na kucheza, akamfu-
rahisha Herode pamoja na wageni wake walioa-
likwa chakulani.

Mfalme Herode akamwambia yule binti,
"Niombe kitu chochote utakacho, nami ni-
takupa." 23 Tena akamwahidi kwa kiapo,
akamwambia, "Chochote utakachoomba ni-
takupa, hata kama ni nusu ya ufalme wangu."

24 Yule binti akatoka nje, akaenda kumuuliza
mama yake, "Niombe nini?"

Mama yake akamjibu, "Omba kichwa cha
Yohana Mbatizaji."

25 Yule binti akarudi haraka kwa mfalme,
akamwambia, “Nataka unipe sasa hivi kichwa
cha Yohana Mbatizaji kwenye sinia.”

26 Mfalme akasikitika sana, lakini kwa sababu
alikuwa ameapa viapo mbele ya wageni wake,
hakutaka kumkatalia. 27 Mara mfalme akatuma
askari mmojawapo wa walinzi wake kukileta
kichwa cha Yohana. Akaenda na kumkata
Yohana kichwa humo gerezani, 28 akakileta
kichwa chake kwenye sinia na kumpa yule
msichana, naye yule msichana akampa mama
yake. 29 Wanafunzi wa Yohana walipopata
habari hizi, wakaja na kuuchukua mwili wake,
wakauzika kaburini.

### *Yesu Awalisha Wanaume 5,000*

*(Mathayo 14:13-21; Luka 9:10-17; Yohana 6:1-14)*

30 Wale mitume wakakusanyika kwa Yesu
na kumpa taarifa ya mambo yote waliyokuwa
wamefanya na kufundisha. 31 Basi kwa kuwa
watu wengi mno walikuwa wakija na kutoka,
hata wakawa hawana nafasi ya kula, Yesu
akawaambia wanafunzi wake, “Twendeni peke
yetu mahali pa faragha, mpate kupumzika.”

32 Hivyo wakaondoka kwa mashua peke yao,
wakaenda mahali pasipo na watu. 33 Lakini watu
wengi waliowaona wakiondoka, wakawatam-
bua, nao wakaenda haraka kwa miguu kutoka
miji yote, nao wakatangulia kufika. 34 Yesu
alipofika kando ya bahari, aliona makutano
makubwa ya watu, akawahurumia kwa maana

walikuwa kama kondoo wasiokuwa na mchun-
gaji. Kwa hiyo akaanza kuwafundisha mambo
mengi.

35 Mchana ulipokuwa umeendelea sana, wana-
funzi wake walienda kwake, wakamwambia,
“Mahali hapa ni nyikani, nazo saa zimekwenda
sana. 36 Waage watu ili waende mashambani na
vijijini jirani, wakajinunulie chakula.”

37 Lakini Yesu akawajibu, “Ninyi wapeni
chakula.”

Wakamwambia, “Je, twende tukanunue
mikate ya dinari 200† ili tuwape watu hawa
wale?”

38 Akawauliza, “Kuna mikate mingapi? Nen-
deni mkaangalie.”

Walipokwisha kujua wakarudi,
wakamwambia, “Kuna mikate mitano na samaki
wawili.”

39 Kisha Yesu akawaamuru wawaketishe watu
makundi makundi kwenye majani, 40 nao
wakaketi kwenye makundi ya watu mia mia na
wengine hamsini hamsini. 41 Yesu akaichukua
ile mikate mitano na wale samaki wawili,
akainua macho yake akatazama mbinguni, akav-
ibariki na kuimega ile mikate. Kisha akawapa
wanafunzi wake ili wawagawie wale watu wote.
Pia akawagawia wote wale samaki wawili.
42 Watu wote wakala, wakashiba. 43 Nao wana-
funzi wake wakakusanya vipande vilivyosalia
vya mikate na samaki, wakajaza vikapu kumi na

† **6:37** Dinari moja ilikuwa kama mshahara wa kibarua wa siku moja; hivyo dinari 200 ni sawa na mshahara wa siku 200.

viwili. 44 Idadi ya wanaume waliokula walikuwa
5,000.

### *Yesu Atembea Juu Ya Maji (Mathayo 14:22-33; Yohana 6:15-21)*

45 Mara Yesu akawaambia wanafunzi wake
waingie kwenye mashua watangulie kwenda
Bethsaida, wakati yeye alikuwa akiwaaga wale
makutano. 46 Baada ya kuwaaga wale watu,
akaenda mlimani kuomba.
47 Ilipofika jioni, ile mashua ilikuwa imefika
katikati ya bahari, na Yesu alikuwa peke yake
katika nchi kavu. 48 Akawaona wanafunzi wake
wanahangaika na kupiga makasia kwa nguvu,
kwa sababu upepo ulikuwa wa mbisho. Wakati
wa zamu ya nne ya usiku, Yesu akawaendea
wanafunzi wake, akiwa anatembea juu ya maji.
Alikuwa karibu kuwapita, 49 lakini walipom-
wona akitembea juu ya maji, wakadhani ni
mzimu. Wakapiga yowe, 50 kwa sababu wote
walipomwona waliogopa.
Mara Yesu akasema nao, akawaambia, “Jipeni
moyo! Ni mimi. Msiogope!” 51 Akapanda
ndani ya mashua nao, na ule upepo ukakoma!
Wakashangaa kabisa, 52 kwa kuwa walikuwa
hawajaelewa kuhusu ile mikate. Mioyo yao
ilikuwa migumu.
53 Walipokwisha kuvuka, wakafika nchi ya
Genesareti, wakatia nanga. 54 Mara wali-
poshuka kutoka mashua yao, watu wakam-
tambua Yesu. 55 Wakaenda katika vijiji vyote
upesi, wakawabeba wagonjwa kwenye mikeka
ili kuwapeleka mahali popote waliposikia kuwa
Yesu yupo. 56 Kila mahali Yesu alipokwenda,

iwe vijijini, mijini au mashambani, watu waliwaweka wagonjwa wao masokoni. Wakamwomba awaruhusu hao wagonjwa waguse japo upindo wa vazi lake. Nao wote waliomgusa waliponywa.

# 7

### *Kilicho Safi Na Kilicho Najisi (Mathayo 15:1-20)*

1 Mafarisayo na baadhi ya walimu wa sheria waliokuwa wametoka Yerusalemu wakakusanyika mbele ya Yesu.
2 Wakawaona baadhi ya wanafunzi wake wakila chakula kwa mikono iliyo najisi, yaani, bila kunawa kama ilivyotakiwa na sheria ya dini ya Wayahudi.
3 (Kwa kuwa Mafarisayo na Wayahudi wote hawali chakula pasipo kunawa kwa kufuata desturi za wazee wao.
4 Wanapotoka sokoni hawawezi kula pasipo kunawa. Pia kuna desturi nyingine nyingi wanazofuata kama vile jinsi ya kuosha vikombe, vyungu na vyombo vya shaba.)

5 Kwa hiyo wale Mafarisayo na walimu wa sheria wakamuuliza Yesu, “Mbona wanafunzi wako hawafuati desturi za wazee, na badala yake wanakula kwa mikono najisi?”

6 Yesu akawajibu, “Nabii Isaya alisema ukweli alipotabiri juu yenu, ninyi wanafiki. Kama ilivyoandikwa:

“ ‘Watu hawa huniheshimu kwa midomo yao,
lakini mioyo yao iko mbali nami.
7 Huniabudu bure,
nayo mafundisho yao ni maagizo ya wanadamu tu.’

8 Ninyi mmeziacha amri za Mungu na kushika
desturi za watu.”
9 Naye akawaambia, “Ninyi mnayo njia nzuri
ya kukataa amri za Mungu ili mpate kuyashika
mapokeo yenu! 10 Kwa mfano, Mose alisema,
‘Waheshimu baba yako na mama yako,’ na, ‘Yey-
ote amtukanaye baba yake au mama yake, na
auawe.’ 11 Lakini ninyi mwafundisha kwamba
mtu akimwambia baba yake au mama yake,
‘Kile ambacho ningeweza kukusaidia ni Korbani’
(yaani kimewekwa wakfu kwa Mungu), 12 basi
hawajibiki tena kumsaidia baba yake au mama
yake. 13 Kwa njia hiyo ninyi mnabatilisha neno la
Mungu kwa mapokeo yenu mliyojiwekea. Nanyi
mnafanya mambo mengi ya aina hiyo.”
14 Yesu akaita tena ule umati wa watu,
akawaambia, “Nisikilizeni, kila mmoja wenu
na mwelewe jambo hili. 15 Hakuna kitu kina-
chomwingia mtu kimtiacho unajisi, lakini kile
kimtokacho ndicho kimtiacho unajisi. [ 16 Kama
mtu yeyote ana masikio ya kusikia na asikie.]”
17 Akiisha kuuacha ule umati wa watu na
kuingia ndani, wanafunzi wake wakamuuliza
maana ya mfano ule. 18 Akawajibu, “Je, hata
nanyi hamwelewi? Je, hamfahamu kwamba kitu
kimwingiacho mtu hakimtii unajisi? 19 Mtu akila
kitu hakiingii moyoni mwake bali tumboni, na
baadaye hutolewa nje ya mwili wake.” (Kwa
kusema hivi, Yesu alivihalalisha vyakula vyote
kuwa ni “safi.”)
20 Akaendelea kusema, “Kile kimtokacho mtu
ndicho kimtiacho unajisi. 21 Kwa maana kutoka
ndani ya moyo wa mtu hutoka mawazo mabaya,

uasherati, wizi, uuaji, uzinzi, 22 tamaa mbaya,
uovu, udanganyifu, ufisadi, wivu, matukano,
kiburi na upumbavu. 23 Maovu haya yote hutoka
ndani ya mtu, nayo ndiyo yamtiayo mtu unajisi."

### *Imani Ya Mwanamke Msirofoinike (Mathayo 15:21-28)*

24 Ndipo Yesu akaondoka hapo akaenda sehemu za Tiro. Akaingia katika nyumba moja, naye hakutaka mtu yeyote ajue kwamba yuko
humo. Lakini hakuweza kujificha. 25 Mara
mwanamke mmoja, ambaye binti yake mdogo alikuwa na pepo mchafu, akaja na kumpigia
magoti miguuni pake. 26 Basi huyo mwanamke
alikuwa Myunani, aliyezaliwa Foinike ya Siria.* Akamsihi Yesu amtoe binti yake huyo pepo mchafu.

27 Yesu akamwambia, "Waache watoto washibe kwanza, kwa maana si vyema kuchukua chakula cha watoto na kuwatupia mbwa."

28 Lakini yule mwanamke akamjibu, "Bwana, hata mbwa walio chini ya meza hula makombo ya chakula cha watoto."

29 Ndipo Yesu akamjibu, "Kwa sababu ya jibu lako, nenda zako nyumbani; yule pepo mchafu amemtoka binti yako."

30 Akaenda zake nyumbani akamkuta binti yake amelala kitandani, yule pepo mchafu akiwa amemtoka.

### *Yesu Amponya Mtu Aliyekuwa Kiziwi Na Bubu*

* **7:26** Kulikuwa na Foinike ya Siria (ndio Shamu) na Foinike ya Libya.

31 Kisha Yesu akaondoka sehemu za Tiro,
akapita katikati ya Sidoni, hadi Bahari ya
Galilaya na kuingia eneo la Dekapoli. 32 Huko,
watu wakamletea Yesu mtu mmoja kiziwi, am-
baye pia alikuwa na kigugumizi, wakamwomba
aweke mkono wake juu ya huyo mtu na am-
ponye.

33 Baadaye Yesu akampeleka yule kiziwi
kando mbali na watu, Yesu akatia vidole vyake
masikioni mwa yule mtu. Kisha akatema mate
na kuugusa ulimi wa yule mtu. 34 Ndipo
Yesu akatazama mbinguni, akavuta hewa ndani
kwa nguvu akamwambia, *“Efatha!”* (yaani,
“Funguka!”) 35 Mara masikio yake yakafunguka
na ulimi wake ukaachiliwa, akaanza kuongea
sawasawa.

36 Yesu akawaamuru wasimwambie mtu
yeyote habari hizi. Lakini kadiri alivyowazuia,
ndivyo walivyozidi kutangaza kwa bidii.
37 Walistaajabu mno. Wakasema, “Amefanya
mambo yote vizuri mno! Amewawezesha viziwi
wasikie na bubu waseme!”

# 8

### *Yesu Alisha Wanaume 4,000*
### *(Mathayo 15:32-39)*

1 Katika siku hizo, umati mkubwa wa watu
ulikusanyika tena. Kwa kuwa walikuwa
hawana chakula, Yesu akawaita wanafunzi
wake akawaambia, 2 “Ninauhurumia huu umati
wa watu, kwa sababu sasa wamekuwa nami
kwa muda wa siku tatu na hawana chakula.

3 Nikiwaaga waende nyumbani bila kula, wataz-
imia njiani kwa sababu baadhi yao wametoka
mbali.”

4 Wanafunzi wake wakamjibu, “Lakini hapa
nyikani tutapata wapi mikate ya kutosha kuwal-
isha?”

5 Yesu akawauliza, “Mna mikate mingapi?”

Wakajibu, “Tuna mikate saba.”

6 Akawaambia watu waketi chini. Akiisha
kuichukua mikate saba na kushukuru, akaimega
na kuwapa wanafunzi wake ili wawagawie watu.
Wanafunzi wake wakafanya hivyo. 7 Walikuwa
pia na visamaki vichache, Yesu akavibariki,
akawaamuru wanafunzi wake wawagawie watu.
8 Wale watu walikula na kutosheka. Baa-
daye wanafunzi wakakusanya vipande vilivyos-
alia, wakajaza vikapu saba. 9 Watu waliokula
walikuwa wapata 4,000. Akiisha kuwaaga,
10 aliingia kwenye mashua pamoja na wanafunzi
wake, akaenda sehemu za Dalmanutha.

### *Mafarisayo Waomba Ishara (Mathayo 12:38-42; 16:1-4)*

11 Mafarisayo wakaja, wakaanza kumhoji Yesu.
Ili kumtega, wakamwomba awaonyeshe ishara
kutoka mbinguni. 12 Akahuzunika moyoni,
akawaambia, “Kwa nini kizazi hiki kinataka
ishara? Amin nawaambieni, hakitapewa ishara
yoyote.” 13 Kisha akawaacha, akarudi kwenye
mashua, akavuka hadi ng’ambo.

### *Chachu Ya Mafarisayo Na Ya Herode (Mathayo 16:5-12)*

14 Wanafunzi walikuwa wamesahau kuchukua
mikate ya kutosha. Walikuwa na mkate mmoja
tu kwenye mashua. 15 Yesu akawaonya: "Jihad-
harini na chachu ya Mafarisayo na ya Herode."
16 Wakajadiliana wao kwa wao, na kusema,
"Anasema hivi kwa sababu hatukuleta mikate."
17 Yesu, akifahamu majadiliano yao,
akawauliza: "Mbona mnajadiliana kuhusu
kutokuwa na mikate? Je, bado hamtambui
wala hamwelewi? Je, mbona mioyo yenu
ni migumu kiasi hicho? 18 Je, mna macho
lakini mnashindwa kuona, na mna masikio
lakini mnashindwa kusikia? Je, hamkumbuki?
19 Nilipoimega ile mikate mitano kuwalisha watu
5,000, mlikusanya vikapu vingapi vilivyojaa vya
masazo?"

Wakamjibu, "Kumi na viwili."

20 "Je, nilipoimega ile mikate saba kuwalisha
watu 4,000, mlikusanya vikapu vingapi vilivyo-
jaa vya masazo?"

Wakamjibu, "Saba."

21 Ndipo akawauliza, "Je, bado hamwelewi?"

### *Yesu Amponya Kipofu Huko Bethsaida*

22 Wakafika Bethsaida na baadhi ya watu
wakamleta mtu mmoja kipofu wakamsihi Yesu
amguse. 23 Yesu akamshika mkono huyo kipofu
akampeleka nje ya kijiji. Baada ya kuyate-
mea mate macho ya yule kipofu na kumwekea
mikono, Yesu akamuuliza, "Unaona chochote?"
24 Yule kipofu akaangalia, akasema, "Ninaona
watu, wanaonekana kama miti inayotembea."
25 Yesu akamwekea tena mikono machoni.
Kisha macho yake yakafunguka, kuona kwake

kukarejea naye akaona kila kitu dhahiri.
26 Yesu akamuaga aende nyumbani kwake,
akimwambia, "Hata kijijini usiingie."

### *Petro Amkiri Yesu Kuwa Ndiye Kristo (Mathayo 16:13-20; Luka 9:18-21)*

27 Yesu na wanafunzi wake wakaondoka kwenda katika vijiji vya Kaisaria-Filipi. Walipokuwa njiani, Yesu akawauliza, "Watu husema mimi ni nani?"
28 Wakamjibu, "Baadhi husema wewe ni Yohana Mbatizaji, wengine husema ni Eliya, na bado wengine husema wewe ni mmojawapo wa manabii."
29 Akawauliza, "Je, ninyi mnasema mimi ni nani?"

Petro akajibu, "Wewe ndiwe Kristo."*

30 Yesu akawaonya wasimwambie mtu yeyote habari zake.

### *Yesu Atabiri Kifo Chake (Mathayo 16:21-28; Luka 9:22-27)*

31 Ndipo akaanza kuwafundisha wanafunzi wake kuwa Mwana wa Adamu lazima atapata mateso mengi na kukataliwa na wazee, viongozi wa makuhani, na walimu wa sheria, na kwamba itampasa auawe lakini baada ya siku tatu afu-
fuke. 32 Aliyasema haya waziwazi, ndipo Petro
akamchukua kando na akaanza kumkemea.
33 Lakini Yesu alipogeuka na kuwaangalia wanafunzi wake, akamkemea Petro. Akasema, "Rudi nyuma yangu, Shetani! Moyo wako hauwazi yaliyo ya Mungu, bali ya wanadamu."

---

* **8:29** Kristo maana yake ni Masiya, yaani Aliyetiwa mafuta.

34 Ndipo akauita ule umati wa watu pamoja
na wanafunzi wake, akasema, “Mtu yeyote ak-
itaka kunifuata, ni lazima ajikane mwenyewe,
auchukue msalaba wake, anifuate. 35 Kwa
maana yeyote anayetaka kuyaokoa maisha
yake atayapoteza, lakini yeyote atakayeyapoteza
maisha yake kwa ajili yangu na kwa ajili ya Injili
atayaokoa. 36 Je, itamfaidi nini mtu kuupata
ulimwengu wote, lakini akayapoteza maisha
yake? 37 Au mtu atatoa nini badala ya nafsi
yake? 38 Mtu yeyote akinionea aibu mimi na
maneno yangu katika kizazi hiki cha uzinzi na dhambi, Mwana wa Adamu naye atamwonea aibu wakati atakapokuja katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika watakatifu.”

# 9

1 Yesu akaendelea kuwaambia, “Amin, nawaambia, kuna watu waliosimama hapa ambao hawataonja mauti kabla ya kuuona Ufalme wa Mungu ukija kwa nguvu.”

### *Yesu Ageuka Sura*
### *(Mathayo 17:1-13; Luka 9:28-36)*

2 Baada ya siku sita, Yesu akawachukua Petro,
Yakobo na Yohana, akawapeleka juu ya mlima
mrefu, mahali walipokuwa faraghani. Huko,
Yesu akageuka sura mbele yao. 3 Mavazi yake
yakawa na weupe wa kuzima macho, meupe
kuliko ambavyo mtu yeyote duniani angaliweza
kuyang’arisha. 4 Mose na Eliya wakawatokea,
wakawa wanazungumza na Yesu.

5 Petro akamwambia Yesu, “Rabi, ni vyema sisi
tukae hapa. Turuhusu tujenge vibanda vitatu:
kimoja chako, kingine cha Mose na kingine cha
Eliya.” 6 Petro hakujua aseme nini kwa maana
yeye na wenzake walikuwa wameogopa sana.

7 Ndipo pakatokea wingu, likawafunika, nayo
sauti kutoka lile wingu ikasema, “Huyu ni
Mwanangu mpendwa. Msikieni yeye.”

8 Mara walipotazama huku na huku,
hawakuona tena mtu mwingine yeyote pamoja
nao isipokuwa Yesu.

9 Walipokuwa wakishuka kutoka mlimani,
Yesu akawakataza wasimwambie mtu yeyote
mambo waliyoona, mpaka Mwana wa Adamu
atakapokuwa amefufuka kutoka kwa wafu.
10 Wakalihifadhi jambo hilo wao wenyewe, lakini
wakawa wanajiuliza, “Huku kufufuka kwa wafu
maana yake nini?”

11 Wakamuuliza, “Kwa nini walimu wa sheria
husema kwamba ni lazima Eliya aje kwanza?”

12 Yesu akawajibu, “Ni kweli, Eliya yuaja
kwanza ili kutengeneza mambo yote. Mbona
basi imeandikwa kwamba Mwana wa Adamu
ni lazima ateseke sana na kudharauliwa?
13 Lakini ninawaambia, Eliya amekwisha
kuja, nao wakamtendea walivyopenda, kama
ilivyoandikwa kumhusu yeye.”

### *Mvulana Mwenye Pepo Mchafu Aponywa (Mathayo 17:14-21; Luka 9:37-43)*

14 Walipowafikia wale wanafunzi wengine,
wakawakuta wamezungukwa na umati mkubwa

wa watu na baadhi ya walimu wa sheria wak-
ibishana nao. 15 Mara wale watu walipomwona
Yesu, wakastaajabu sana, wakamkimbilia ili
kumsalimu.

16 Akawauliza wanafunzi wake, “Mnabishana
nao kuhusu nini?”

17 Mtu mmoja miongoni mwa ule umati
wa watu akajibu, “Mwalimu, nilimleta kwako
mwanangu ambaye ana pepo mchafu anayem-
fanya asiweze kuongea. 18 Kila mara huyo pepo
mchafu ampagaapo mwanangu, humwangusha chini na kumfanya atokwe povu mdomoni na kusaga meno, kisha mwili wake hukauka. Niliwaomba wanafunzi wako wamtoe huyo pepo mchafu, lakini hawakuweza.”

19 Yesu akawaambia, “Enyi kizazi kisicho na imani! Nitakuwa pamoja nanyi mpaka lini? Nitawavumilia mpaka lini? Mleteni mvulana kwangu.”

20 Nao wakamleta yule mvulana. Yule pepo mchafu alipomwona Yesu, mara akamtia yule mvulana kifafa, akaanguka, akagaagaa chini huku akitokwa na povu kinywani.

21 Yesu akamuuliza baba yake, “Mwanao amekuwa katika hali hii tangu lini?”

Akamjibu, “Tangu utoto wake. 22 Mara
kwa mara huyo pepo mchafu amekuwa akimwangusha kwenye moto au kwenye maji ili kumwangamiza. Lakini kama unaweza kufanya jambo lolote, tafadhali tuhurumie utusaidie.”

23 Yesu akamwambia, “Kama ukiweza kuamini, yote yawezekana kwake yeye aaminiye.”

24 Mara baba yake yule mvulana akapiga kelele
akisema, “Ninaamini. Nisaidie kutokuamini
kwangu!” 25 Yesu alipoona kwamba umati
wa watu unakusanyika pamoja mbio, akamke-
mea yule pepo mchafu, akimwambia, “Wewe
pepo bubu na kiziwi, nakuamuru umtoke, wala
usimwingie tena!”
26 Yule pepo mchafu akiisha kupiga kelele,
akamtia kifafa kwa nguvu, na akamtoka. Yule
mvulana alikuwa kama maiti, hivyo watu
wengi wakasema, “Amekufa.” 27 Lakini Yesu
akamshika mkono, akamwinua, naye akasi-
mama.
28 Baada ya Yesu kuingia ndani ya nyumba,
wanafunzi wake wakamuuliza wakiwa peke yao,
“Mbona sisi hatukuweza kumtoa huyo pepo
mchafu?”
29 Yesu akawajibu, “Hali hii haiwezi kutoka
isipokuwa kwa kuomba na kufunga.”

### *Yesu Atabiri Tena Kifo Chake Na Ufufuo*
### *(Mathayo 17:22-23; Luka 9:43-45)*

30 Wakaondoka huko, wakapitia Galilaya. Yesu
hakutaka mtu yeyote afahamu mahali walipo,
31 kwa maana alikuwa anawafundisha wana-
funzi wake. Akawaambia, “Mwana wa Adamu
atasalitiwa na kutiwa mikononi mwa watu. Nao
watamuua, lakini siku tatu baada ya kuuawa
atafufuka.” 32 Lakini wao hawakuelewa kile
alimaanisha, nao waliogopa kumuuliza maana
yake.

### *Mabishano Kuhusu Aliye Mkuu Zaidi*
### *(Mathayo 18:1-5; Luka 9:46-48)*

33 Basi wakafika Kapernaumu na baada
ya kuingia nyumbani akawauliza, “Mlikuwa
mnabishana nini kule njiani?” 34 Lakini
hawakumjibu, kwa sababu njiani walikuwa
wakibishana kuhusu nani miongoni mwao
alikuwa mkuu zaidi ya wote.
35 Akaketi chini, akawaita wote kumi na waw-
ili, akawaambia: “Kama mtu yeyote akitaka
kuwa wa kwanza, hana budi kuwa wa mwisho
na mtumishi wa wote.”
36 Kisha akamchukua mtoto mdogo,
akamsimamisha katikati yao. Akamkumbatia,
akawaambia, 37 “Mtu yeyote amkaribishaye
mmoja wa hawa watoto wadogo kwa Jina langu,
anikaribisha mimi. Naye anikaribishaye mimi,
amkaribisha Baba yangu aliyenituma.”

### *Yeyote Asiye Kinyume Nasi Yuko Upande Wetu (Luka 9:49-50)*

38 Yohana akamwambia, “Mwalimu, tumem-
wona mtu akitoa pepo wachafu kwa jina lako,
nasi tukamkataza, kwa sababu yeye si mmoja
wetu.”
39 Yesu akasema, “Msimkataze, kwa kuwa
hakuna yeyote atendaye miujiza kwa Jina langu
ambaye baada ya kitambo kidogo aweza kunena
lolote baya dhidi yangu. 40 Kwa maana yey-
ote asiye kinyume chetu, yuko upande wetu.
41 Amin, nawaambia, yeyote awapaye ninyi
kikombe cha maji kwa Jina langu kwa sababu
ninyi ni mali ya Kristo, hakika hataikosa
thawabu yake.”

### *Kusababisha Kutenda Dhambi (Mathayo 18:6-9; Luka 17:1-2)*

42 “Kama mtu yeyote akimsababisha mmo-
jawapo wa wadogo hawa wanaoniamini kutenda
dhambi, ingekuwa bora kwake afungiwe jiwe
kubwa la kusagia shingoni mwake, na kutoswa
baharini. 43 Kama mkono wako ukikusababisha
kutenda dhambi, ukate. Ni afadhali kwako
kuingia katika uzima ukiwa na mkono mmoja,
kuliko kuwa na mikono miwili lakini ukain-
gia jehanamu, mahali ambako moto hauzimiki.
[ 44 Mahali ambako funza wake hawafi wala
moto wake hauzimiki.] 45 Kama mguu wako
ukikusababisha kutenda dhambi, ukate. Ni afad-
hali kwako kuingia katika uzima ukiwa kiwete,
kuliko kuwa na miguu miwili lakini ukaingia
jehanamu. [ 46 Mahali ambako funza wake
hawafi wala moto hauzimiki.] 47 Nalo jicho lako
likikusababisha kutenda dhambi, ling’oe. Ni
afadhali kwako kuingia katika Ufalme wa Mungu
ukiwa na jicho moja, kuliko kuwa na macho
mawili lakini ukatupwa jehanamu, 48 mahali
ambako
“ ‘funza wake hawafi,
wala moto wake hauzimiki.’
49 Kila mmoja atatiwa chumvi kwa moto.

50 “Chumvi ni nzuri, lakini ikipoteza ladha
yake utaifanyaje ili iweze kukolea tena? Mwe
na chumvi ndani yenu, mkaishi kwa amani, kila
mmoja na mwenzake.”

# 10

### *Mafundisho Kuhusu Talaka (Mathayo 19:1-12; Luka 16:18)*

1 Yesu akaondoka huko, akavuka Mto Yordani, akaenda sehemu za Uyahudi. Umati mkubwa wa watu ukaenda kwake tena, naye kama ilivyokuwa desturi yake, akawafundisha.

2 Baadhi ya Mafarisayo wakaja ili kumjaribu kwa kumuuliza, "Je, ni halali mtu kumwacha mke wake?"

3 Yesu akawajibu, "Je, Mose aliwaamuru nini?"

4 Wakajibu, "Mose aliruhusu kwamba mume anaweza kumwandikia mkewe hati ya talaka na kumwacha."

5 Yesu akawaambia, "Mose aliwaandikia sheria
hiyo kwa sababu ya ugumu wa mioyo yenu.
6 Lakini tangu mwanzo wa uumbaji, 'Mungu
aliwaumba mwanaume na mwanamke. 7 Kwa
sababu hii mwanaume atamwacha baba yake
na mama yake na kuambatana na mkewe, na
hao wawili watakuwa mwili mmoja.' 8 Kwa hiyo
hawatakuwa wawili tena, bali mwili mmoja.
9 Basi, alichokiunganisha Mungu, mwanadamu
asikitenganishe."

10 Walipokuwa tena ndani ya nyumba, wana-
funzi wake wakamuuliza kuhusu jambo hili.
11 Akawajibu, "Mtu yeyote amwachaye mkewe
na kuoa mke mwingine, anazini naye. 12 Naye
mwanamke amwachaye mumewe na kuolewa
na mume mwingine, anazini."

### *Yesu Anawabariki Watoto Wadogo (Mathayo 19:13-15; Luka 18:15-17)*

13 Watu walikuwa wakimletea Yesu watoto
wadogo ili awaguse, lakini wanafunzi wake
wakawakemea. 14 Yesu alipoona yaliyokuwa

yakitukia, akachukizwa. Akawaambia wana-
funzi wake, “Waacheni watoto wadogo waje
kwangu, wala msiwazuie, kwa maana Ufalme
wa Mungu ni wa wale walio kama hawa.
15 Amin, nawaambia, mtu yeyote asiyeupokea
Ufalme wa Mungu kama mtoto mdogo, hatauin-
gia kamwe.” 16 Akawachukua watoto mikononi
mwake, akawakumbatia, akaweka mikono yake
juu yao, akawabariki.

### *Kijana Tajiri*
### *(Mathayo 19:16-30; Luka 18:18-30)*

17 Yesu alipokuwa anaondoka, mtu mmoja
akamkimbilia, akapiga magoti mbele yake, aka-
muuliza, “Mwalimu mwema, nifanye nini ili
niurithi uzima wa milele?”

18 Yesu akamwambia, “Mbona unaniita
mwema? Hakuna yeyote aliye mwema ila
Mungu peke yake. 19 Unazijua amri: ‘Usiue,
usizini, usiibe, usishuhudie uongo, usidanganye,
waheshimu baba yako na mama yako.’ ”

20 Akamjibu, “Mwalimu, amri hizi zote
nimezishika tangu nikiwa mtoto.”

21 Yesu akamtazama na kumpenda,
akamwambia, “Umepungukiwa na kitu kimoja.
Nenda ukauze kila kitu ulicho nacho uwape
maskini hizo fedha, nawe utakuwa na hazina
mbinguni. Kisha njoo, unifuate.”

22 Yule mtu aliposikia hayo, akasikitika sana.
Akaondoka kwa huzuni kwa sababu alikuwa na
mali nyingi.

23 Yesu akatazama pande zote, akawaambia
wanafunzi wake, “Itakuwa vigumu sana kwa
wenye mali kuingia katika Ufalme wa Mungu!”

24 Wanafunzi wake wakashangazwa sana na
maneno hayo. Lakini Yesu akawaambia tena,
“Wanangu, tazama jinsi ilivyo vigumu kwa
wale wanaotumainia mali kuingia katika Ufalme
wa Mungu. 25 Ni rahisi zaidi kwa ngamia
kupita kwenye tundu la sindano kuliko mtu
tajiri*kuingia katika Ufalme wa Mungu.”

26 Wanafunzi wake wakashangaa sana.
Wakaulizana wao kwa wao, “Ni nani basi
awezaye kuokoka?”

27 Yesu akawatazama, akawaambia, “Kwa
mwanadamu jambo hili haliwezekani, lakini
kwa Mungu sivyo. Mambo yote yanawezekana
kwa Mungu.”

28 Ndipo Petro akamjibu, “Tazama, tumeacha
kila kitu na kukufuata wewe!”

29 Yesu akasema, “Amin, nawaambia, hakuna
mtu yeyote aliyeacha nyumba, ndugu wa kiume
au wa kike, au mama au baba, au watoto
au mashamba kwa ajili yangu na kwa ajili ya
Injili, 30 ambaye hatalipwa mara mia katika
ulimwengu huu: nyumba, ndugu wa kiume na
wa kike, mama na baba na watoto, mashamba
pamoja na mateso, kisha uzima wa milele katika
ulimwengu ujao. 31 Lakini wengi walio wa
kwanza watakuwa wa mwisho, na wa mwisho
watakuwa wa kwanza.”

---

* **10:25** Tajiri ina maana wale wanaotumainia mali.

### *Yesu Atabiri Mara Ya Tatu Kufa Na Kufufuka Kwake*
### *(Mathayo 20:17-19; Luka 18:31-34)*

32 Walikuwa njiani wakipanda kwenda Yerusalemu, na Yesu alikuwa ametangulia. Wanafunzi wake walishangaa, nao watu waliowafuata walijawa na hofu. Yesu akawachukua tena wale wanafunzi wake kumi na wawili kando na kuwaambia yatakayompata.
33 Akasema, “Tunapanda kwenda Yerusalemu, na Mwana wa Adamu atasalitiwa kwa viongozi wa makuhani na walimu wa sheria. Wao watamhukumu kifo na kumtia mikononi mwa
watu wa Mataifa, 34 ambao watamdhihaki na
kumtemea mate, watampiga na kumuua. Siku tatu baadaye atafufuka.”

### *Ombi La Yakobo Na Yohana*
### *(Mathayo 20:20-28)*

35 Kisha Yakobo na Yohana, wana wa Zebedayo, wakaja kwake na kumwambia, “Mwalimu, tunataka utufanyie lolote tutakalokuomba.”

36 Naye akawaambia, “Je, mwataka niwafanyie jambo gani?”

37 Wakamwambia, “Tupe kukaa mmoja upande wako wa kuume na mwingine upande wako wa kushoto katika utukufu wako.”

38 Lakini Yesu akawaambia, “Ninyi hamjui mnaloliomba. Je, mnaweza kukinywea kikombe ninyweacho mimi, au kubatizwa ubatizo nibatizwao mimi?”

39 Wakajibu, “Tunaweza.”

Kisha Yesu akawaambia, “Kikombe nikinywea-
cho mtakinywea na ubatizo nibatizwao mtaba-
tizwa, 40 lakini kuketi mkono wangu wa kuume
au wa kushoto si juu yangu mimi kuwapa. Nafasi
hizi ni kwa ajili ya wale walioandaliwa.”
41 Wale wanafunzi wengine kumi waliposikia
hayo, wakaanza kuwakasirikia Yakobo na
Yohana. 42 Lakini Yesu akawaita wote pamoja
na kuwaambia, “Mnafahamu kuwa wale
wanaodhaniwa kuwa watawala wa watu
wa Mataifa huwatawala watu kwa nguvu,
nao wenye vyeo huonyesha mamlaka yao.
43 Lakini isiwe hivyo kwenu. Badala yake,
yeyote anayetaka kuwa mkuu miongoni mwenu
hana budi kuwa mtumishi wenu, 44 na yeyote
anayetaka kuwa wa kwanza, hana budi kuwa
mtumwa wa wote. 45 Kwa kuwa hata Mwana wa
Adamu hakuja ili kutumikiwa, bali kutumika na
kuutoa uhai wake uwe fidia kwa ajili ya wengi.”

### *Yesu Amponya Kipofu Bartimayo (Mathayo 20:29-34; Luka 18:35-43)*

46 Kisha wakafika Yeriko. Yesu alipokuwa
akiondoka mjini na wanafunzi wake pamoja na
umati mkubwa wa watu, kipofu mmoja, jina lake
Bartimayo, mwana wa Timayo, alikuwa ameketi
kando ya njia akiomba msaada. 47 Aliposikia
kuwa ni Yesu wa Nazareti aliyekuwa anapita,
akaanza kupaza sauti akisema, “Yesu, Mwana
wa Daudi, nihurumie!”
48 Watu wengi wakamkemea, wakamwambia
akae kimya, lakini yeye akazidi kupaza sauti,
akisema, “Mwana wa Daudi, nihurumie!”

49 Yesu akasimama na kusema, “Mwiteni.”
Hivyo wakamwita yule mtu kipofu,
wakamwambia, “Jipe moyo! Inuka, anakuita.”
50 Akiwa analivua lile joho lake, alisimama na
kumwendea Yesu.
51 Yesu akamuuliza, “Unataka nikufanyie
nini?”
Yule kipofu akajibu, “Mwalimu, nataka
kuona.”
52 Yesu akamwambia, “Nenda zako, imani yako
imekuponya.” Mara akapata kuona, akamfuata
Yesu njiani.

# 11

### *Yesu Aingia Yerusalemu Kwa Shangwe*
*(Mathayo 21:1-11; Luka 19:28-40; Yohana 12:12-19)*

1 Walipokaribia Yerusalemu, wakafika
Bethfage na Bethania katika Mlima wa Mizeituni.
Yesu akawatuma wawili wa wanafunzi wake,
2 akawaambia, “Nendeni katika kijiji kilichoko
mbele yenu. Na hapo mtakapoingia kijijini,
mtamkuta mwana-punda amefungwa hapo,
ambaye hajapandwa na mtu bado. Mfungueni,
mkamlete hapa. 3 Kama mtu yeyote akiwauliza,
‘Mbona mnamfungua?’ Mwambieni, ‘Bwana
anamhitaji, na atamrudisha hapa baada ya
muda mfupi.’ ”
4 Wakaenda, wakamkuta mwana-punda
amefungwa kando ya barabara, karibu
na mlango wa nyumba. 5 Walipokuwa
wanamfungua, watu waliokuwa wamesimama
karibu wakawauliza, “Mna maana gani

mnapomfungua huyo mwana-punda?”
6 Wakawajibu kama vile Yesu alivyokuwa
amewaagiza, nao wale watu wakawaruhusu.
7 Kisha wakamleta huyo mwana-punda kwa
Yesu na kutandika mavazi yao juu yake, naye
akampanda. 8 Watu wengi wakatandaza mavazi
yao barabarani, na wengine wakatandaza
matawi waliyokuwa wamekata mashambani.
9 Kisha wale waliokuwa wametangulia mbele
na wale waliokuwa wakifuata nyuma wakapaza
sauti, wakisema,

“Hosana!”*

“Amebarikiwa yeye ajaye kwa Jina la Bwana!”

10 “Umebarikiwa Ufalme unaokuja wa baba yetu Daudi!”

“Hosana kwake yeye aliye juu!”

11 Yesu akaingia Yerusalemu na kwenda
Hekaluni. Akaangalia kila kitu kilichokuwamo,
lakini kwa kuwa ilishakuwa jioni, akaenda zake
Bethania pamoja na wale kumi na wawili.

### *Yesu Alaani Mtini Usiozaa (Mathayo 21:18-19)*

12 Kesho yake walipokuwa wakitoka Bethania,
Yesu alikuwa na njaa. 13 Akauona mtini kwa
mbali, naye akaenda ili aone kama ulikuwa
na matunda. Alipoufikia, akakuta una majani tu, kwa kuwa hayakuwa majira ya tini.
14 Akauambia ule mti, “Tangu leo mtu yeyote

* **11:9** Kiebrania kusema Okoa, basi likawa neno la shangwe.

asile kamwe matunda kutoka kwako." Wana-
funzi wake walimsikia akisema hayo.

### *Yesu Atakasa Hekalu*
### *(Mathayo 21:12-17; Luka 19:45-48; Yohana 2:13-22)*

15 Walipofika Yerusalemu, Yesu akaingia katika
eneo la Hekalu, akaanza kuwafukuza wale
waliokuwa wakinunua na kuuza humo ndani.
Akazipindua meza za wale waliokuwa wak-
ibadilisha fedha, na pia viti vya wale waliokuwa
wakiuza njiwa, 16 wala hakumruhusu mtu yey-
ote kuchukua bidhaa kupitia ukumbi wa Hekalu.
17 Naye alipokuwa akiwafundisha, akasema, "Je,
haikuandikwa kuwa:
" 'Nyumba yangu itaitwa
nyumba ya sala kwa mataifa yote'?
Lakini ninyi mmeifanya kuwa 'pango la
wanyang'anyi.' "
18 Viongozi wa makuhani na walimu wa
sheria wakapata habari hizi, nao wakaanza
kutafuta njia ya kumuua, kwa kuwa walikuwa
wakimwogopa, kwa sababu umati wote ulikuwa
unashangazwa na mafundisho yake.
19 Ilipofika jioni, Yesu na wanafunzi wake
wakatoka nje ya mji.

### *Mtini Ulionyauka*
### *(Mathayo 21:20-22)*

20 Asubuhi yake walipokuwa wakipita,
wakauona ule mtini umenyauka kutoka juu
hadi kwenye mizizi yake. 21 Petro akakumbuka
na kumwambia Yesu, "Rabi, tazama! Ule mtini
ulioulaani umenyauka!"

22 Yesu akawajibu, “Mwaminini Mungu.
23 Amin, nawaambia, mtu yeyote atakayeuambia
mlima huu, ‘Ng’oka ukatupwe baharini,’ wala
asione shaka moyoni mwake, bali aamini
kwamba hayo asemayo yametukia, atatimiziwa.
24 Kwa sababu hiyo nawaambia, yoyote
mtakayoyaomba mkisali, aminini ya kwamba
mmeyapokea, nayo yatakuwa yenu. 25 Nanyi
kila msimamapo kusali, sameheni mkiwa na
neno na mtu, ili naye Baba yenu aliye mbinguni
awasamehe ninyi makosa yenu. [ 26 Lakini
kama ninyi msiposamehe, wala Baba yenu aliye
mbinguni hatawasamehe ninyi makosa yenu.]”

### *Swali Kuhusu Mamlaka Ya Yesu (Mathayo 21:23-27; Luka 20:1-8)*

27 Wakafika tena Yerusalemu, na Yesu
alipokuwa akitembea Hekaluni, viongozi wa
makuhani, walimu wa sheria pamoja na wazee
wa watu wakamjia. 28 Wakamuuliza, “Unafanya
mambo haya kwa mamlaka gani? Na ni nani
aliyekupa mamlaka ya kufanya hayo?”
29 Yesu akawajibu, “Nitawauliza swali moja.
Nijibuni, nami nitawaambia ni kwa mamlaka
gani ninafanya mambo haya. 30 Niambieni, je,
ubatizo wa Yohana ulitoka mbinguni au kwa
wanadamu?”
31 Wakahojiana wao kwa wao, wakisema,
“Kama tukisema, ‘Ulitoka mbinguni,’ atatu-
uliza, ‘Mbona hamkumwamini?’ 32 Lakini
tukisema, ‘Ulitoka kwa wanadamu,’…” (Wali-
waogopa watu, kwa sababu kila mtu aliamini
kwamba Yohana alikuwa nabii wa kweli.)
33 Kwa hiyo wakamjibu Yesu, “Hatujui.”

Naye Yesu akawaambia, “Wala mimi sitawaambia ni kwa mamlaka gani ninatenda mambo haya.”

# 12

### *Mfano Wa Wapangaji Waovu (Mathayo 21:33-46; Luka 20:9-19)*

1 Yesu akaanza kusema nao kwa mifano,
akawaambia: “Mtu mmoja alipanda shamba
la mizabibu. Akajenga ukuta kulizunguka,
akachimba shimo ndani yake kwa ajili ya
shinikizo la kusindika divai, na akajenga mnara
wa ulinzi. Kisha akalikodisha shamba hilo la
mizabibu kwa wakulima fulani, kisha akasafiri
kwenda nchi nyingine. 2 Wakati wa mavuno
ulipofika, mwenye shamba akamtuma mtumishi
wake kwa hao wapangaji ili kuchukua sehemu
yake ya mavuno ya shamba la mizabibu kutoka
kwa hao wapangaji. 3 Lakini wale wakulima wal-
imkamata yule mtumishi, wakampiga, wakam-
fukuza mikono mitupu. 4 Kisha yule mwenye
shamba akamtuma mtumishi mwingine kwao;
nao wale wakulima wakampiga kichwani na
kumfanyia mambo ya aibu. 5 Kisha akam-
tuma mtumishi mwingine, naye huyo waka-
muua. Akawatuma wengine wengi; baadhi yao
wakawapiga, na wengine wakawaua.

6 “Mwenye shamba alikuwa bado na mmoja
wa kumtuma, mwanawe aliyempenda. Ha-
timaye akamtuma akisema, ‘Watamheshimu
mwanangu.’

7 “Lakini wale wapangaji wakasemezana
pamoja, ‘Huyu ndiye mrithi. Njooni tumuue, nao

urithi utakuwa wetu.’ 8 Hivyo wakamchukua
na kumuua, wakamtupa nje ya lile shamba la
mizabibu.
9 “Sasa basi yule mwenye shamba atafanya
nini? Atakuja na kuwaua hao wapangaji, kisha
atawapa wapangaji wengine hilo shamba la
mizabibu. 10 Je, hamjasoma Andiko hili:

“ ‘Jiwe walilolikataa waashi
limekuwa jiwe kuu la pembeni;
11 Bwana ndiye alitenda jambo hili,
nalo ni ajabu machoni petu’?”

12 Walipotambua kuwa amesema mfano huo
kwa ajili yao, wakataka kumkamata, lakini
wakaogopa ule umati wa watu. Wakamwacha,
wakaondoka, wakaenda zao.

### *Swali Kuhusu Kulipa Kodi (Mathayo 22:15-22; Luka 20:20-26)*

13 Baadaye wakawatuma baadhi ya Mafarisayo
na Maherode ili kwenda kumtega Yesu katika
yale anayosema. 14 Wakamjia, wakamwambia,
“Mwalimu, tunajua kwamba wewe ni mtu
mwadilifu. Wewe huyumbishwi na wanadamu,
kwa kuwa huna upendeleo. Lakini wewe hui-
fundisha njia ya Mungu katika kweli. Je, ni halali
kulipa kodi kwa Kaisari, au la? 15 Je, tulipe kodi
au tusilipe?”

Lakini Yesu alijua unafiki wao. Akawauliza
“Mbona mnajaribu kunitega? Nileteeni hiyo
dinari*niione.” 16 Wakamletea hiyo sarafu. Naye

---

* **12:15** Dinari moja ilikuwa sawa na mshahara wa kibarua wa siku moja.

akawauliza, “Sura hii ni ya nani? Na maandishi haya ni ya nani?”

Wakamjibu, “Ni vya Kaisari.”

17 Ndipo Yesu akawaambia, “Mpeni Kaisari kilicho cha Kaisari, naye Mungu mpeni kilicho cha Mungu.”

Nao wakamstaajabia sana.

### *Ndoa Wakati Wa Ufufuo*
### *(Mathayo 22:23-33; Luka 20:27-40)*

18 Kisha Masadukayo, wale wasemao kuwa hakuna ufufuo wa wafu, wakamjia Yesu,
19 wakasema, “Mwalimu, Mose alituandikia kuwa kama ndugu wa mtu akifa na kumwacha mkewe bila mtoto, basi huyo mtu inampasa amwoe huyo mjane ili amzalie ndugu yake watoto.
20 Basi palikuwepo ndugu saba. Yule wa kwanza akaoa mke, naye akafa pasipo kuwa na mtoto
yeyote. 21 Wa pili akamwoa yule mjane, lakini naye akafa bila kuacha mtoto yeyote. Ikawa
vivyo hivyo kwa yule wa tatu. 22 Hakuna hata mmojawapo wa hao ndugu wote saba aliyeacha mtoto. Hatimaye yule mwanamke naye akafa.
23 Kwa hiyo wakati wa ufufuo, yeye atakuwa mke wa nani, maana aliolewa na ndugu wote saba?”

24 Yesu akawajibu, “Je, hampotoki kwa sababu hamfahamu Maandiko wala uweza wa
Mungu? 25 Wafu watakapofufuka, hawataoa wala kuolewa, bali watakuwa kama malaika
wa mbinguni. 26 Basi kuhusu wafu kufufuliwa, je hamjasoma katika Kitabu cha Mose jinsi Mungu alivyosema na Mose kutoka kile kichaka akisema, ‘Mimi ni Mungu wa Abrahamu, na

Mungu wa Isaki, na Mungu wa Yakobo?' 27 Yeye
si Mungu wa wafu, bali ni Mungu wa walio hai.
Kwa hiyo mmekosea kabisa."

### *Amri Iliyo Kuu*
*(Mathayo 22:34-40; Luka 10:25-28)*

28 Mwalimu mmoja wa sheria akaja,
akawasikia wakijadiliana. Akiona kwamba Yesu
amewajibu vyema, naye akamuuliza, "Katika
amri zote, ni ipi iliyo kuu?"

29 Yesu akajibu, "Amri iliyo kuu ndiyo hii:
'Sikia ee Israeli. Bwana Mungu wetu, Bwana
ndiye mmoja. 30 Mpende Bwana Mungu wako
kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote, kwa
akili zako zote, na kwa nguvu zako zote.' 31 Ya
pili ndiyo hii: 'Mpende jirani yako kama nafsi
yako.' Hakuna amri nyingine iliyo kuu kuliko
hizi."

32 Yule mwalimu wa sheria akamwambia Yesu,
"Mwalimu, umejibu vyema kwamba Mungu
ni mmoja, wala hakuna mwingine ila yeye.
33 Kumpenda Mungu kwa moyo wote na kwa
akili zote na kwa nguvu zote, na kumpenda
jirani kama mtu anavyojipenda mwenyewe ni
bora zaidi kuliko kutoa sadaka za kuteketezwa
na dhabihu zote."

34 Yesu alipoona kwamba amejibu kwa busara,
akamwambia, "Wewe hauko mbali na Ufalme
wa Mungu." Tangu wakati huo, hakuna mtu
yeyote aliyethubutu kumuuliza maswali tena.

### *Kristo Ni Mwana Wa Nani?*
*(Mathayo 22:41-46; Luka 20:41-44)*

35 Yesu alipokuwa akifundisha Hekaluni,
akauliza, "Imekuwajewalimu wa sheria
wanasema kwamba Kristo† ni Mwana wa Daudi?
36 Kwa maana Daudi mwenyewe, akinena kwa
kuongozwa na Roho Mtakatifu, alisema:

" 'BWANA alimwambia Bwana wangu:
"Keti mkono wangu wa kuume,
hadi nitakapowaweka adui zako
chini ya miguu yako." '

37 Kwa hiyo Daudi mwenyewe anamwita
'Bwana.' Awezaje basi yeye kuwa mwanawe?"

Ule umati wote wa watu wakamsikiliza kwa furaha.

### *Yesu Awatahadharisha Watu Kuhusu Walimu Wa Sheria*
*(Mathayo 23:1-36; Luka 20:45-47)*

38 Alipokuwa akifundisha, Yesu alisema, "Ji-
hadharini na walimu wa sheria. Wao hupenda
kutembea wakiwa wamevaa mavazi marefu, na
kusalimiwa kwa heshima masokoni. 39 Pia wao
hupenda kukaa kwenye viti vya mbele katika
masinagogi, na kupewa nafasi za heshima katika
karamu. 40 Wao hula nyumba za wajane, na
ili waonekane kuwa wema wanasali sala ndefu.
Watu kama hawa watapata hukumu iliyo kuu
sana."

### *Sadaka Ya Mjane*
*(Luka 21:1-4)*

41 Kisha Yesu akaketi mkabala na sehemu ambapo sadaka zilikuwa zinawekwa na kuangalia umati wa watu wakiweka fedha zao kwenye sanduku la hazina ya Hekalu. Matajiri wengi

† **12:35** Kristo maana yake ni Masiya, yaani Aliyetiwa mafuta.

wakaweka kiasi kikubwa cha fedha. 42 Lakini
mjane mmoja maskini akaja na kuweka sarafu
mbili ndogo za shaba zenye thamani ya senti
mbili.
43 Yesu akawaita wanafunzi wake, akawaam-
bia, "Amin, nawaambia, huyu mjane maskini
ameweka katika sanduku la hazina zaidi ya watu
wengine wote. 44 Wengine wote wametoa ku-
tokana na ziada ya mali zao. Lakini huyu mjane
ametoa kutokana na umaskini wake, akaweka
kila kitu alichokuwa nacho, hata kile alichohitaji
ili kuishi."

# 13

### *Dalili Za Siku Za Mwisho (Mathayo 24:1-2; Luka 21:5-6)*

1 Yesu alipokuwa akitoka Hekaluni, mmo-
jawapo wa wanafunzi wake akamwambia,
"Mwalimu! Tazama jinsi mawe haya yalivyo
makubwa, na majengo haya yalivyo mazuri!"
2 Ndipo Yesu akajibu akasema, "Je, unayaona
majengo haya yalivyo makubwa? Hakuna hata
jiwe moja litakalobaki juu ya jingine, bali yote
yatabomolewa."

### *Mateso Yatabiriwa (Mathayo 24:3-14; Luka 21:7-19)*

3 Yesu alipokuwa ameketi kwenye Mlima wa
Mizeituni mkabala na Hekalu, Petro, Yakobo,
Yohana na Andrea wakamuuliza faraghani,
4 "Tafadhali tuambie, mambo haya yatatukia
lini? Nayo dalili ya kuwa hayo yote yanakaribia
kutimia itakuwa gani?"

5 Yesu akawaambia: “Jihadharini mtu yeyote
asiwadanganye. 6 Wengi watakuja kwa Jina
langu wakidai, ‘Mimi ndiye,’ nao watawadan-
ganya wengi. 7 Msikiapo habari za vita na
uvumi wa vita, msiwe na hofu. Mambo haya
hayana budi kutukia, lakini ule mwisho bado.
8 Taifa litainuka dhidi ya taifa na ufalme dhidi ya
ufalme. Kutakuwa na mitetemeko sehemu mbalimbali na njaa. Haya yatakuwa ndio mwanzo wa utungu.

9 “Lakini ninyi jihadharini. Kwa maana
watawapeleka katika mabaraza yao na kupigwa
mijeledi katika masinagogi. Mtashtakiwa mbele
ya watawala na wafalme kwa ajili yangu, ili
kuwa ushuhuda kwao. 10 Nayo habari njema laz-
ima ihubiriwe kwanza kwa mataifa yote kabla
ule mwisho haujawadia. 11 Mtakapokamatwa
na kushtakiwa, msisumbuke awali kuhusu
mtakalosema. Semeni tu lolote mtakalopewa
wakati huo, kwa kuwa si ninyi mtakaokuwa
mkinena, bali ni Roho Mtakatifu.

12 “Ndugu atamsaliti ndugu yake ili auawe,
naye baba atamsaliti mtoto wake. Watoto nao
wataasi dhidi ya wazazi wao na kusababisha
wauawe. 13 Watu wote watawachukia kwa ajili
ya Jina langu. Lakini yule atakayevumilia hadi
mwisho ataokolewa.

### *Chukizo La Uharibifu*
### *(Mathayo 24:15-28; Luka 21:20-24)*

14 “Mtakapoona ‘chukizo la uharibifu’ limes-
imama mahali pasipolipasa (asomaye na afa-
hamu), basi wale walioko Uyahudi wakimbilie
milimani. 15 Yeyote aliye juu ya dari ya

nyumba asishuke au kuingia ndani ili kuchukua
chochote. 16 Aliye shambani asirudi nyum-
bani kuchukua vazi lake. 17 Ole wao wenye
mimba na wale wanaonyonyesha watoto siku
hizo! 18 Ombeni mambo haya yasitokee wakati
wa baridi. 19 Kwa maana siku hizo zitakuwa
za dhiki kuu ambayo haijapata kuwako tangu
mwanzo, hapo Mungu alipoumba ulimwengu,
mpaka leo, na wala haitakuwako tena kamwe.
20 Kama Bwana asingelifupisha siku hizo, kamwe
asingeliokoka mtu yeyote. Lakini kwa ajili ya
wateule, wale aliowachagua, amezifupisha siku
hizo. 21 Wakati huo mtu yeyote akiwaambia,
'Tazama, Kristo*huyu hapa!' au, 'Tazama, yuko
kule,' msisadiki. 22 Kwa maana watatokea
makristo wa uongo na manabii wa uongo, nao
watafanya ishara na maajabu ili kuwapotosha,
ikiwezekana, hata wale wateule. 23 Hivyo jihad-
harini. Nimekwisha kuwaambia mambo haya
yote mapema kabla hayajatukia.

*Kuja Kwa Mwana Wa Adamu*
*(Mathayo 24:29-31; Luka 21:25-28)*

24 "Lakini katika siku hizo, baada ya hiyo dhiki,
" 'jua litatiwa giza
nao mwezi hautatoa nuru yake;
25 nazo nyota zitaanguka kutoka angani,
na nguvu za anga zitatikisika.'
26 "Ndipo watu wote watakapomwona Mwana
wa Adamu akija mawinguni kwa nguvu nyingi
na utukufu. 27 Naye atawatuma malaika wake

* **13:21** Kristo maana yake ni Masiya, yaani Aliyetiwa mafuta.

wawakusanye wateule wake kutoka pande zote
nne za dunia, kutoka miisho ya dunia hadi
miisho ya mbingu.

### *Somo Kuhusu Mtini*
### *(Mathayo 24:32-35; Luka 21:29-33)*

28 "Basi jifunzeni somo hili kutokana na mtini:
Matawi yake yanapoanza kuchipua na kutoa ma-
jani, mnatambua kwamba wakati wa kiangazi
umekaribia. 29 Vivyo hivyo, myaonapo mambo
haya yakitukia, mnatambua kwamba wakati u
karibu, hata malangoni. 30 Amin, nawaambia,
kizazi hiki hakitapita hadi mambo haya yote
yawe yametimia. 31 Mbingu na nchi zitapita,
lakini maneno yangu hayatapita kamwe.

### *Hakuna Ajuaye Siku Wala Saa*
### *(Mathayo 24:36-44)*

32 "Kwa habari ya siku ile na saa hakuna yey-
ote ajuaye, hata malaika walio mbinguni wala
Mwana, ila Baba peke yake. 33 Jihadharini! Kesh-
eni! Kwa maana hamjui wakati ule utakapowa-
dia. 34 Ni kama mtu anayesafiri. Anaiacha
nyumba yake na kuwaachia watumishi wake
kuiangalia, kila mtu na kazi yake, kisha akamwa-
muru yule bawabu aliye mlangoni akeshe.

35 "Basi kesheni kwa sababu hamjui ni lini
mwenye nyumba atakaporudi: iwapo ni jioni,
au ni usiku wa manane, au alfajiri awikapo
jogoo, au mapambazuko. 36 Kama akija ghafula,
asije akawakuta mmelala. 37 Lile ninalowaambia
ninyi, nawaambia watu wote: 'Kesheni!' "

# 14

### *Shauri La Kumuua Yesu*
### *(Mathayo 26:1-5; Luka 22:1-2; Yohana 11:45-53)*

1 Zilikuwa zimebaki siku mbili tu kabla ya
Sikukuu ya Pasaka, na Sikukuu ya Mikate Isiy-
otiwa Chachu. Viongozi wa makuhani na wal-
imu wa sheria walikuwa wakitafuta njia ya
kumkamata Yesu kwa hila na kumuua. 2 Lakini
walisema, "Tusilifanye jambo hili wakati wa
Sikukuu, maana watu wanaweza wakafanya
ghasia."

### *Yesu Kupakwa Mafuta Huko Bethania*
### *(Mathayo 26:6-13; Yohana 12:1-8)*

3 Yesu alikuwa Bethania nyumbani kwa Simoni
aliyekuwa na ukoma. Wakati alipokuwa ameketi
mezani akila chakula cha jioni, mwanamke
mmoja aliingia akiwa na chupa ya marhamu
yenye manukato ya nardo* safi ya thamani
kubwa. Akaivunja hiyo chupa, akamiminia hayo
manukato kichwani mwa Yesu.
4 Baadhi ya watu waliokuwepo pale walikuwa
wakisemezana wao kwa wao, "Upotevu huu
wote ni wa nini? 5 Mafuta haya yangeweza
kuuzwa kwa zaidi ya dinari† 300, na fedha hizo
wakapewa maskini." Wakamkemea vikali huyo
mwanamke.
6 Lakini Yesu akawaambia, "Mbona mnam-
sumbua huyu mwanamke? Mwacheni! Yeye

---

* **14:3** Nardo ni aina ya manukato yaliyotengenezwa kutokana na mimea yenye mizizi inayotoa harufu nzuri. † **14:5** Dinari 300 ni sawa na mshahara wa kibarua wa siku 300.

amenitendea jambo zuri sana. 7 Maskini
mtakuwa nao siku zote na mnaweza kuwasaidia
wakati wowote mnaotaka. Lakini mimi ham-
takuwa nami siku zote. 8 Huyu mwanamke
amenitendea lile aliloweza. Ameumiminia mwili
wangu manukato ili kuniandaa kwa maziko
yangu. 9 Amin, nawaambia, mahali popote
ulimwenguni ambapo Injili itahubiriwa, jambo
hili alilolitenda huyu mwanamke litatajwa pia
kwa ukumbusho wake."

### *Yuda Akubali Kumsaliti Yesu (Mathayo 26:14-16; Luka 22:3-6)*

10 Kisha Yuda Iskariote, mmoja wa wale wana-
funzi kumi na wawili, akaenda kwa viongozi wa
makuhani ili kumsaliti Yesu kwao. 11 Walifurahi
sana kusikia jambo hili na wakaahidi kumpa
fedha. Hivyo yeye akawa anatafuta wakati
uliofaa wa kumsaliti.

### *Yesu Ala Pasaka Na Wanafunzi Wake (Mathayo 26:17-25; Luka 22:7-14, 21-23; Yohana 13:21-30)*

12 Siku ya kwanza ya Sikukuu ya Mikate Isiy-
otiwa Chachu, siku ambayo kwa desturi mwana-
kondoo wa Pasaka huchinjwa, wanafunzi wa
Yesu wakamuuliza, "Unataka twende wapi ili
tukuandalie mahali pa kula Pasaka?"
13 Basi akawatuma wawili miongoni mwa
wanafunzi wake, akawaambia, "Nendeni mjini.
Huko mtakutana na mwanaume amebeba
mtungi wa maji. Mfuateni. 14 Mwambieni
mwenye nyumba ile atakayoingia, 'Mwalimu
anauliza: Kiko wapi chumba changu cha wageni,
ambamo mimi na wanafunzi wangu tutakula

Pasaka?’ 15 Atawaonyesha chumba kikubwa ghorofani, kilichopambwa tena kilicho tayari. Tuandalieni humo.”
16 Wale wanafunzi wakaondoka na kwenda mjini, nao wakakuta kila kitu kama Yesu alivyowaambia. Hivyo wakaiandaa Pasaka.
17 Ilipofika jioni, Yesu akaja pamoja na wale
wanafunzi wake kumi na wawili. 18 Walipoketi
mezani wakila, Yesu akawaambia, “Amin, nawaambia, mmoja wenu atanisaliti, mmoja anayekula pamoja nami.”
19 Wakaanza kuhuzunika na kumuuliza mmoja baada ya mwingine, “Je, ni mimi Bwana?”
20 Akawajibu, “Ni mmoja miongoni mwenu
ninyi kumi na wawili, yule anayechovya mkate
kwenye bakuli pamoja nami. 21 Mwana wa
Adamu anaenda zake kama vile alivyoandikiwa. Lakini ole wake mtu yule amsalitiye Mwana wa Adamu! Ingekuwa heri kwake mtu huyo kama hangezaliwa.”

*Kuanzishwa Kwa Meza Ya Bwana*

*(Mathayo 26:26-30; Luka 22:14-20; 1 Wakorintho 11:23-25)*

22 Walipokuwa wanakula, Yesu akachukua mkate, akashukuru, akaumega na kuwapa wanafunzi wake, akisema, “Twaeni mle; huu ndio mwili wangu.”
23 Kisha akakitwaa kikombe, akashukuru, akawapa, nao wote wakanywa kutoka humo.
24 Akawaambia, “Hii ndiyo damu yangu ya
agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi. 25 Amin,
nawaambia, sitakunywa tena katika uzao wa

mzabibu, hadi siku ile nitakapounywa mpya
katika Ufalme wa Mungu."
26 Walipokwisha kuimba wimbo, wakatoka
wakaenda Mlima wa Mizeituni.

### *Yesu Atabiri Kuwa Petro Atamkana*
*(Mathayo 26:31-35; Luka 22:31-34; Yohana 13:36-38)*

27 Yesu akawaambia, "Ninyi nyote mtaniacha,
kwa maana imeandikwa:
" 'Nitampiga mchungaji,
nao kondoo watatawanyika.'
28 Lakini baada ya kufufuka kwangu, nitawatan-
gulia kwenda Galilaya."
29 Petro akasema, "Hata kama wengine wote
watakuacha, mimi sitakuacha."
30 Yesu akamwambia, "Amin, nakuambia; leo,
usiku huu, kabla jogoo hajawika mara mbili,
wewe mwenyewe utanikana mara tatu."
31 Lakini Petro akasisitiza zaidi, "Hata kama
itabidi kufa pamoja nawe, sitakukana kamwe."
Nao wale wengine wote wakasema vivyo hivyo.

### *Yesu Aomba Katika Bustani Ya Gethsemane*
*(Mathayo 26:36-46; Luka 22:39-46)*

32 Wakaenda mahali paitwapo Gethsemane.
Yesu akawaambia wanafunzi wake, "Kaeni hapa,
nami niende nikaombe." 33 Kisha akawachukua
pamoja naye Petro, Yakobo na Yohana. Akaanza
kuhuzunika sana na kutaabika. 34 Akawaambia,
"Moyo wangu umejawa na huzuni kiasi cha kufa.
Kaeni hapa na mkeshe."
35 Akaenda mbele kidogo, akaanguka kifud-
ifudi, akaomba kwamba kama ingewezekana
saa hiyo ya mateso imwondokee. 36 Akasema,

"*Abba,*‡Baba, mambo yote yawezekana kwako. Niondolee kikombe hiki. Lakini si kama nipendavyo mimi, bali vile upendavyo wewe."
37 Akarudi kwa wanafunzi wake, akawakuta wamelala. Akamwambia Petro, "Simoni, umelala? Je, hukuweza kukesha hata kwa saa
moja? 38 Kesheni na mwombe, msije mkaingia majaribuni. Roho iko radhi, lakini mwili ni mdhaifu."
39 Akaenda tena kuomba, akisema maneno
yale yale. 40 Aliporudi, akawakuta tena wamelala kwa sababu macho yao yalikuwa mazito. Nao hawakujua la kumwambia.
41 Akaja mara ya tatu, akawaambia, "Bado mmelala na kupumzika? Imetosha! Saa imewadia. Tazameni, Mwana wa Adamu anasalitiwa na kutiwa mikononi mwa wenye dhambi.
42 Inukeni, twende zetu! Tazameni, msaliti wangu yuaja!"

### *Yesu Akamatwa*

*(Mathayo 26:47-56; Luka 22:47-53; Yohana 18:3-12)*

43 Yesu alipokuwa bado anazungumza, Yuda, mmoja wa wale wanafunzi Kumi na Wawili, akatokea. Alikuwa amefuatana na umati wa watu wenye panga na marungu, waliokuwa wametumwa na viongozi wa makuhani, walimu wa sheria, na wazee.
44 Basi msaliti alikuwa amewapa hao watu ishara, kwamba: "Yule nitakayembusu ndiye. Mkamateni, mkamchukue chini ya ulinzi."

‡ **14:36** Abba ni neno la Kiaramu ambalo maana yake ni Baba; ni mtoto wa kuzaa tu angeweza kulitumia kwa baba yake.

45 Mara Yuda akamjia Yesu na kusema, "Rabi."§
Akambusu. 46 Wale watu wakamkamata Yesu,
wakamweka chini ya ulinzi. 47 Ndipo mmoja
wa wale waliokuwa wamesimama karibu aliu-
chomoa upanga wake na kumpiga mtumishi wa
kuhani mkuu, akamkata sikio.

48 Kisha Yesu akawaambia, "Mmekuja na
panga na marungu kunikamata kana kwamba
mimi ni mnyang'anyi? 49 Siku kwa siku ni-
likuwa pamoja nanyi nikifundisha Hekaluni,
wala hamkunikamata. Lakini Maandiko sharti
yatimie." 50 Ndipo wanafunzi wake wote
wakamwacha, wakakimbia.

51 Kijana mmoja, ambaye hakuwa amevaa kitu
isipokuwa alijitanda nguo ya kitani, alikuwa
akimfuata Yesu. Walipomkamata, 52 alikimbia
uchi, akaliacha vazi lake.

### *Yesu Mbele Ya Baraza La Wayahudi*
*(Mathayo 26:57-68; Luka 22:54-71; Yohana 18:13-24)*

53 Wakampeleka Yesu kwa kuhani mkuu, nao
viongozi wa makuhani wote, na wazee na wal-
imu wa sheria wote wakakusanyika pamoja.
54 Petro akamfuata kwa mbali, hadi uani kwa
kuhani mkuu. Huko akaketi pamoja na walinzi,
akiota moto.

---

§ **14:45** *Rabi* ni neno la Kiebrania ambalo maana yake ni daktari, mwalimu au bwana. Walikuwa na madaraja matatu: La chini kabisa *Rab* (bwana), la pili *Rabi* (bwana wangu), na la juu kabisa *Raboni* (mkuu wangu, bwana wangu mkuu).

55 Viongozi wa makuhani na Baraza la
Wayahudi* lote wakatafuta ushahidi dhidi ya
Yesu ili wapate kumuua. Lakini hawaku-
pata jambo lolote. 56 Wengi walitoa ushahidi
wa uongo dhidi yake, lakini maelezo yao
hayakukubaliana.

57 Ndipo wengine wakasimama wakatoa
ushahidi wa uongo dhidi yake, wakisema:
58 “Sisi tulimsikia akisema, ‘Mimi nitalibomoa
Hekalu hili lililojengwa na wanadamu, na katika
siku tatu nitajenga jingine ambalo halikujengwa
na wanadamu.’ ” 59 Lakini hata hivyo, ushahidi
wao haukukubaliana.

60 Basi kuhani mkuu akasimama mbele yao,
akamuuliza Yesu, “Je, wewe hutajibu? Ni
ushahidi gani hawa watu wanauleta dhidi
yako?” 61 Lakini Yesu akakaa kimya, hakusema
neno lolote.

Kuhani mkuu akamuuliza tena, “Je, wewe ndiwe Kristo,† Mwana wa Mungu Aliyebarikiwa?”

62 Yesu akajibu, “Mimi ndimi. Nanyi mtamwona Mwana wa Adamu akiwa ameketi mkono wa kuume wa Mwenye Nguvu, na akija juu ya mawingu ya mbinguni.”

63 Kuhani mkuu akararua mavazi yake,
akasema, “Tuna haja gani tena ya mashahidi
zaidi? 64 Ninyi mmesikia hayo makufuru. Ua-
muzi wenu ni gani?”

* **14:55** Baraza la Wayahudi hapa ina maana ya Sanhedrin ambalo lilikuwa ndilo baraza la juu kabisa la utawala wa Kiyahudi, lililoundwa na wazee 70 pamoja na kuhani mkuu.
† **14:61** Kristo maana yake ni Masiya, yaani Aliyetiwa mafuta.

Wote wakamhukumu kwamba anastahili kifo.
65 Kisha baadhi ya watu wakaanza kumtemea mate; wakamfunga kitambaa machoni, wakampiga kwa ngumi na kumwambia, “Tabiri!” Walinzi wakamchukua na kumpiga makofi.

### *Petro Amkana Yesu*
*(Mathayo 26:69-75; Luka 22:56-62; Yohana 18:15-18, 25-27)*

66 Petro alipokuwa bado yuko chini kwenye ua wa jumba la kifalme, tazama akaja mmoja wa watumishi wa kike wa kuhani mkuu.
67 Alipomwona Petro akiota moto, akamtazama sana, akamwambia,

“Wewe pia ulikuwa pamoja na Yesu, Mnazareti.”

68 Lakini Petro akakana, akasema, “Sijui wala sielewi unalosema.” Naye akaondoka kuelekea kwenye njia ya kuingilia.

69 Yule mtumishi wa kike alipomwona mahali pale, akawaambia tena wale waliokuwa wamesimama hapo, “Huyu mtu ni mmoja wao.”
70 Lakini Petro akakana tena.

Baada ya muda kidogo wale waliokuwa wamesimama hapo karibu na Petro wakamwambia, “Hakika wewe ni mmoja wao, kwa maana wewe pia ni Mgalilaya!” 71 Petro
akaanza kujilaani na kuwaapia, “Mimi simjui huyu mtu mnayesema habari zake!”

72 Papo hapo jogoo akawika mara ya pili. Ndipo Petro akakumbuka lile neno Yesu alikuwa amemwambia: “Kabla jogoo hajawika mara

mbili, utanikana mara tatu." Akavunjika moyo, akalia sana.

# 15

*Yesu Mbele Ya Pilato*
*(Mathayo 27:1-14; Luka 23:1-5; Yohana 18:28-38)*

1 Asubuhi na mapema, viongozi wa makuhani, pamoja na wazee, walimu wa sheria na Baraza lote, wakafikia uamuzi. Wakamfunga Yesu, wakamchukua na kumkabidhi kwa Pilato.
2 Pilato akamuuliza, "Je, wewe ndiye Mfalme wa Wayahudi?"

Yesu akajibu, "Wewe umesema."
3 Viongozi wa makuhani wakamshtaki kwa
mambo mengi. 4 Pilato akamuuliza tena, "Je, huna la kujibu? Tazama ni mashtaka mangapi wanayaleta juu yako."
5 Lakini Yesu hakujibu lolote, hivyo Pilato akashangaa.

*Pilato Amtoa Yesu Asulubiwe*
*(Mathayo 27:15-26; Luka 23:13-25; Yohana 18:39–19:16)*

6 Ilikuwa desturi wakati wa Sikukuu ya Pasaka kumfungulia mfungwa yeyote ambaye watu
wangemtaka. 7 Wakati huo, mtu aliyeitwa Baraba alikuwa amefungwa gerezani pamoja na waasi wengine waliokuwa wametekeleza
uuaji wakati wa maasi. 8 Ule umati wa watu ukamjia Pilato na kumwomba awafanyie kama ilivyokuwa desturi yake.
9 Pilato akawauliza, "Mnataka niwafungulie
huyu Mfalme wa Wayahudi?" 10 Kwa maana

yeye alitambua kuwa viongozi wa makuhani
walikuwa wamemtia Yesu mikononi mwake kwa
ajili ya wivu. 11 Lakini viongozi wa makuhani
wakauchochea ule umati wa watu wamwombe
awafungulie Baraba badala yake.

12 Pilato akawauliza tena, “Basi mnataka nifanye nini na huyu mtu mnayemwita Mfalme wa Wayahudi?”

13 Wakapiga kelele wakisema, “Msulubishe!”

14 Pilato akawauliza, “Kwa nini? Amefanya kosa gani?”

Lakini wao wakapiga kelele kwa nguvu zaidi, wakisema, “Msulubishe!”

15 Pilato, akitaka kuuridhisha ule umati wa watu, akawafungulia Baraba. Naye baada ya kuamuru Yesu achapwe mijeledi, akamtoa ili asulubishwe.

### *Askari Wamdhihaki Yesu (Mathayo 27:27-31; Yohana 19:2-3)*

16 Askari wakampeleka Yesu hadi kwenye
ukumbi wa ndani wa jumba la kifalme, ndio
Praitorio,* wakakusanya kikosi kizima cha
askari. 17 Wakamvalisha Yesu joho la zam-
barau, wakasokota taji ya miiba, wakamvika
kichwani. 18 Wakaanza kumsalimu kwa dhihaka,
“Salamu, mfalme wa Wayahudi!” 19 Wakampiga
kwa fimbo ya mwanzi tena na tena kich-
wani na kumtemea mate. Wakapiga magoti
mbele yake, wakamsujudia kwa kumdhihaki.

---

* **15:16** Praitorio maana yake ni makao makuu ya mtawala; ni jumba la kifalme lililokuwa linakaliwa na Pontio Pilato huko Yerusalemu, palipokuwa na kiti cha hukumu.

20 Walipokwisha kumdhihaki, wakamvua lile
joho la zambarau, wakamvika tena nguo zake.
Kisha wakamtoa nje ili wakamsulubishe.

*Kusulubiwa Kwa Yesu*
*(Mathayo 27:32-44; Luka 23:26-43; Yohana 19:17-27)*

21 Mtu mmoja kutoka Kirene, jina lake Si-
moni, baba yao Aleksanda na Rufo, alikuwa
anapita zake kuingia mjini kutoka shamba, nao
wakamlazimisha kuubeba ule msalaba. 22 Kisha
wakampeleka Yesu mpaka mahali palipoitwa
Golgotha (maana yake ni Mahali pa Fuvu
la Kichwa). 23 Nao wakampa divai iliy-
ochanganywa na manemane, lakini hakuinywa.
24 Basi wakamsulubisha, nazo nguo zake waka-
gawana miongoni mwao kwa kuzipigia kura ili
kuamua ni gani kila mtu ataichukua.

25 Ilikuwa yapata saa tatu asubuhi walipom-
sulubisha. 26 Tangazo likaandikwa la mash-
taka dhidi yake lenye maneno haya: “MFALME
WA WAYAHUDI.” 27 Pamoja naye walisulubiwa
wanyang’anyi wawili, mmoja upande wake wa
kuume na mwingine upande wa kushoto. [
28 Nayo maandiko yakatimizwa, yale yasemayo,
“Alihesabiwa pamoja na watenda dhambi.]”
29 Watu waliokuwa wakipita njiani wakam-
tukana huku wakitikisa vichwa vyao na kusema,
“Aha! Wewe ambaye utalivunja Hekalu na
kulijenga kwa siku tatu, 30 basi shuka kutoka
msalabani na ujiokoe mwenyewe!”

31 Vivyo hivyo, viongozi wa makuhani pamoja
na walimu wa sheria wakamdhihaki miongoni

mwao wakisema, “Aliwaokoa wengine, lakini
hawezi kujiokoa mwenyewe! 32 Basi huyu
Kristo,† huyu Mfalme wa Israeli, ashuke sasa
kutoka msalabani, ili tupate kuona na kuamini.”
Wale waliosulubiwa pamoja naye pia wakam-
tukana.

### *Kifo Cha Yesu Msalabani*
*(Mathayo 27:45-56; Luka 23:44-49; Yohana 19:28-30)*

33 Ilipofika saa sita, giza liliifunika nchi yote
hadi saa tisa. 34 Mnamo saa tisa, Yesu aka-
paza sauti, akalia, *“Eloi, Eloi, lama sabakthani?”*
(maana yake, “Mungu wangu, Mungu wangu,
mbona umeniacha?”)

35 Baadhi ya watu waliokuwa wamesimama
karibu waliposikia hayo, wakasema, “Msikieni,
anamwita Eliya.”

36 Mtu mmoja akaenda mbio, akachovya si-
fongo kwenye siki, akaiweka kwenye mwanzi
na akampa Yesu ili anywe, akisema, “Basi
mwacheni. Hebu tuone kama Eliya atakuja
kumshusha kutoka hapo msalabani.”

37 Kisha Yesu akatoa sauti kuu, akakata roho.

38 Pazia la Hekalu likachanika vipande viwili
kuanzia juu hadi chini. 39 Basi yule jemadari
aliyekuwa amesimama hapo mbele ya msalaba
wa Yesu aliposikia ile sauti yake na kuona jinsi
alivyokata roho, akasema, “Hakika mtu huyu
alikuwa Mwana wa Mungu!”

† **15:32** Kristo maana yake ni Masiya, yaani Aliyetiwa mafuta.

40 Walikuwepo pia wanawake waliokuwa
wakiangalia kwa mbali. Miongoni mwao wa-
likuwepo Maria Magdalene, na Maria mama
yao Yakobo mdogo na Yose, pia na Salome.
41 Hawa walifuatana na Yesu na kushughulikia
mahitaji yake alipokuwa Galilaya. Pia wa-
likuwepo wanawake wengine wengi waliokuwa
wamekuja pamoja naye Yerusalemu.

### *Maziko Ya Yesu*
*(Mathayo 27:57-61; Luka 23:50-56; Yohana 19:38-42)*

42 Ilipofika jioni, kwa kuwa ilikuwa Siku ya
Maandalizi, yaani siku moja kabla ya Sabato,
43 Yosefu wa Arimathaya, mtu aliyeheshimiwa
katika Baraza, na ambaye alikuwa anautarajia
Ufalme wa Mungu, akamwendea Pilato kwa
ujasiri na kumwomba mwili wa Yesu. 44 Pilato
alikuwa akijiuliza kama Yesu alikuwa amek-
wisha kufa. Hivyo akamwita yule jemadari,
akamuuliza iwapo Yesu alikuwa amekwisha
kufa. 45 Baada ya kupata habari kutoka kwa
yule jemadari kwamba kweli amekwisha kufa,
Pilato akampa Yosefu ruhusa ya kuuchukua huo
mwili. 46 Hivyo Yosefu akanunua kitambaa cha
kitani safi, akaushusha mwili kutoka msalabani,
akaufunga katika kile kitambaa cha kitani, na
kuuweka ndani ya kaburi lililochongwa kwenye
mwamba. Kisha akavingirisha jiwe kwenye
ingilio la kaburi. 47 Maria Magdalene na Maria
mamaye Yose walipaona mahali pale alipolazwa.

# 16

*Kufufuka Kwa Yesu*
*(Mathayo 28:1-8; Luka 24:1-12; Yohana 20:1-10)*

1 Sabato ilipomalizika, Maria Magdalene,
Maria mama yake Yakobo, na Salome walin-
unua manukato ili wakaupake mwili wa Yesu.
2 Asubuhi na mapema, siku ya kwanza ya juma,
mara tu baada ya kuchomoza jua, walikwenda
kaburini. 3 Njiani wakawa wanaulizana wao
kwa wao, "Ni nani atakayetuvingirishia lile jiwe
kutoka kwenye ingilio la kaburi?"

4 Lakini walipotazama, wakaona lile jiwe,
ambalo lilikuwa kubwa sana, limekwisha kuvin-
girishwa kutoka pale penye ingilio la kaburi.
5 Walipokuwa wakiingia mle kaburini, wakam-
wona kijana mmoja aliyevaa joho jeupe akiwa
ameketi upande wa kuume, nao wakastaajabu.

6 Yule malaika akawaambia, "Msistaajabu.
Mnamtafuta Yesu, Mnazareti, aliyesulubiwa.
Amefufuka! Hayuko hapa. Tazameni mahali
walipomlaza. 7 Lakini nendeni mkawaambie
wanafunzi wake pamoja na Petro, kwamba,
'Anawatangulia kwenda Galilaya. Huko ndiko
mtamwona, kama alivyowaambia.' "

8 Hivyo wakatoka, wakakimbia kutoka mle
kaburini wakiwa na hofu kuu na mshangao. Nao
hawakumwambia mtu yeyote neno lolote, kwa
sababu waliogopa.

*Yesu Anamtokea Maria Magdalene*
*(Mathayo 28:9-10; Yohana 20:11-18)*

[9] Yesu alipofufuka alfajiri na mapema siku
ya kwanza ya juma alimtokea kwanza Maria
Magdalene, yule ambaye alikuwa amemtoa pepo
wachafu saba. [10] Maria akaenda, naye akawaam-
bia wale waliokuwa wamefuatana na Yesu,
waliokuwa wanaomboleza na kulia. [11] Lakini
waliposikia kwamba Yesu yu hai na kwamba
Maria alikuwa amemwona, hawakusadiki.

*Yesu Awatokea Wanafunzi Wawili*
*(Luka 24:13-35)*

[12] Baadaye Yesu akawatokea wawili miongoni
mwa wanafunzi wake walipokuwa wakienda
shambani akiwa katika sura nyingine. [13] Nao
wakarudi na kuwaambia wenzao. Lakini
hawakuwasadiki wao pia.

*Yesu Awaagiza Wale Wanafunzi Kumi Na Mmoja*
*(Mathayo 28:16-20; Luka 24:36-49; Yohana 20:19-23; Matendo 1:6-8)*

[14] Baadaye Yesu akawatokea wale wanafunzi kumi na mmoja walipokuwa wakila chakula. Akawakemea kwa kutoamini kwao na kwa ugumu wa mioyo yao kwa kutosadiki wale waliomwona baada yake kufufuka.

[15] Akawaambia, “Enendeni ulimwenguni kote,
mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. [16] Yeyote
aaminiye na kubatizwa ataokoka. Lakini yeyote
asiyeamini atahukumiwa. [17] Nazo ishara hizi
zitafuatana na wanaoamini: Kwa Jina langu
watatoa pepo wachafu; watasema kwa lugha
mpya; [18] watashika nyoka kwa mikono yao; na

hata wakinywa kitu chochote cha kuua, hakitawadhuru kamwe; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapona."

### *[Yesu Apaa Kwenda Mbinguni (Luka 24:50-53; Matendo 1:9-11)*

19 Baada ya Bwana Yesu kusema nao,
alichukuliwa juu mbinguni na kuketi mkono
wa kuume wa Mungu. 20 Kisha wanafunzi wake
wakatoka, wakahubiri kila mahali, naye Bwana
akatenda kazi pamoja nao na kulithibitisha neno
lake kwa ishara zilizofuatana nalo.]

# Luka

[1] Kwa kuwa watu wengi wamekaa ili kuandika
habari za mambo yaliyotukia katikati yetu,
[2] kama vile yalivyokabidhiwa kwetu na wale
waliokuwa mashahidi walioyaona na watumishi
wa Bwana, [3] mimi nami baada ya kuchun-
guza kila kitu kwa uangalifu kuanzia mwanzo,
niliamua kukuandikia habari za mambo hayo,
ewe mtukufu Theofilo, [4] ili upate kujua ukweli
kuhusu yale uliyofundishwa.

### *Kuzaliwa Kwa Yohana Mbatizaji Kwatabiriwa*

[5] Wakati wa Herode mfalme wa Uyahudi,
palikuwa na kuhani mmoja jina lake Zekaria,
ambaye alikuwa wa ukoo wa kikuhani wa Abiya.
Elizabeti mkewe alikuwa pia mzao wa Aroni.
[6] Zekaria na Elizabeti mkewe wote walikuwa
watu wanyofu mbele za Mungu, wakizishika
amri zote za Bwana na maagizo yote bila
lawama. [7] Lakini walikuwa hawana watoto, kwa
sababu Elizabeti alikuwa tasa; nao wote wawili
walikuwa wazee sana.

[8] Siku moja ilipokuwa zamu ya kikundi cha
Zekaria, yeye akifanya kazi ya ukuhani Hekaluni
mbele za Mungu, [9] alichaguliwa kwa kura kwa
kufuata desturi za ukuhani, kuingia Hekaluni
mwa Bwana ili kufukiza uvumba. [10] Nao
wakati wa kufukiza uvumba ulipowadia, wale
wote waliokuwa wamekusanyika ili kuabudu
walikuwa nje wakiomba.

11 Ndipo malaika wa Bwana, akiwa
amesimama upande wa kuume wa madhabahu
ya kufukizia uvumba, akamtokea Zekaria.
12 Zekaria alipomwona huyo malaika,
akafadhaika sana, akajawa na hofu. 13 Lakini
malaika akamwambia, “Usiogope, Zekaria, kwa
maana Mungu amesikia maombi yako. Mkeo
Elizabeti atakuzalia mtoto wa kiume, nawe
utamwita jina lake Yohana. 14 Yeye atakuwa
furaha na shangwe kwako, nao watu wengi
watashangilia kwa sababu ya kuzaliwa kwake.
15 Kwa kuwa atakuwa mkuu mbele za Bwana,
kamwe hataonja mvinyo wala kinywaji chochote
cha kulevya, naye atajazwa Roho Mtakatifu hata
kabla ya kuzaliwa kwake. 16 Naye atawageuza
wengi wa wana wa Israeli warudi kwa Bwana
Mungu wao. 17 Naye atatangulia mbele za Bwana
katika roho na nguvu ya Eliya, ili kuigeuza
mioyo ya baba kuwaelekea watoto wao, na
wasiotii warejee katika hekima ya wenye haki,
ili kuliweka tayari taifa lililoandaliwa kwa ajili
ya Bwana.”

18 Zekaria akamuuliza malaika, “Jambo hilo
linawezekanaje? Mimi ni mzee na mke wangu
pia ana umri mkubwa.”

19 Malaika akamjibu, akamwambia, “Mimi ni
Gabrieli, nisimamaye mbele za Mungu, nami
nimetumwa kwako ili nikuambie habari hizi
njema. 20 Basi sasa kwa kuwa hujaamini ma-
neno yangu ambayo yatatimizwa kwa wakati
wake, utakuwa bubu hadi siku ile mambo haya
yatakapotukia.”

21 Wakati huo watu walikuwa wanamngojea

Zekaria nje huku wakishangaa kukawia kwake
mle Hekaluni.
22 Alipotoka akawa hawezi kusema nao, wao wakatambua kuwa ameona maono ndani ya Hekalu. Lakini kwa kuwa alikuwa bubu, akawa anawaashiria kwa mikono.
23 Muda wake wa kuhudumu Hekaluni ulipomalizika, akarudi nyumbani kwake.
24 Baada ya muda usio mrefu, Elizabeti mkewe akapata mimba, naye akajitenga kwa miezi mitano.
25 Akasema, “Hili ndilo Bwana alilonitendea aliponiangalia kwa upendeleo na kuniondolea aibu yangu mbele ya watu.”

### *Kuzaliwa Kwa Yesu Kwatabiriwa*

26 Mwezi wa sita baada ya Elizabeti kupata mimba, Mungu alimtuma malaika Gabrieli aende Galilaya katika mji wa Nazareti,
27 kwa mwanamwali bikira aliyekuwa ameposwa na mtu mmoja jina lake Yosefu wa nyumba ya Daudi. Jina la huyu mwanamwali bikira ni Maria.
28 Naye malaika akaja kwake akamwambia: “Salamu, wewe uliyebarikiwa, Bwana yu pamoja nawe!”
29 Maria akafadhaishwa sana na maneno haya, akajiuliza moyoni, “Salamu hii ni ya namna gani?”
30 Ndipo malaika akamwambia, “Usiogope, Maria, umepata kibali kwa Mungu.
31 Tazama, utachukua mimba, nawe utamzaa mtoto mwanaume na utamwita jina lake Yesu.
32 Yeye atakuwa mkuu, naye ataitwa Mwana wa Aliye Juu Sana. BWANA Mungu atampa kiti cha enzi cha Daudi baba yake.
33 Ataimiliki nyumba ya Yakobo milele, na ufalme wake hautakuwa na mwisho.”

34 Maria akamuuliza huyo malaika, “Maadamu
mimi ni bikira, jambo hili litawezekanaje?”
35 Malaika akamjibu, “Roho Mtakatifu ataku-
jilia juu yako, nazo nguvu zake Yeye Aliye
Juu Sana zitakufunika kama kivuli. Kwa hiyo
mtoto atakayezaliwa atakuwa mtakatifu, naye
ataitwa Mwana wa Mungu. 36 Tazama, jamaa
yako Elizabeti amechukua mimba katika uzee
wake, na huu ni mwezi wake wa sita, yeye
aliyeitwa tasa. 37 Kwa maana kwa Mungu
hakuna lisilowezekana.”
38 Maria akasema, “Tazama, mimi ni mtumishi
wa Bwana. Na iwe kwangu kama ulivyosema.”
Kisha malaika akaondoka, akamwacha.

### *Maria Aenda Kumtembelea Elizabeti*

39 Wakati huo Maria akajiandaa, akaharakisha
kwenda katika mji mmoja kwenye vilima vya
Uyahudi. 40 Akaingia nyumbani kwa Zekaria na
kumsalimu Elizabeti. 41 Naye Elizabeti aliposikia
salamu ya Maria, mtoto aliyekuwa tumboni
mwake akaruka. Elizabeti akajazwa na Roho
Mtakatifu, 42 akapaza sauti kwa nguvu akasema,
“Umebarikiwa wewe miongoni mwa wanawake,
naye mtoto utakayemzaa amebarikiwa. 43 Lakini
ni kwa nini mimi nimepata upendeleo kiasi hiki,
hata mama wa Bwana wangu afike kwangu?
44 Mara tu niliposikia sauti ya salamu yako,
mtoto aliyeko tumboni mwangu aliruka kwa fu-
raha. 45 Amebarikiwa yeye aliyeamini kwamba
lile Bwana alilomwambia litatimizwa.”

### *Wimbo Wa Maria Wa Sifa*

46 Naye Maria akasema:

“Moyo wangu wamwadhimisha Bwana,
47 nayo roho yangu inamfurahia
Mungu Mwokozi wangu,
48 kwa kuwa ameangalia kwa fadhili
unyonge wa mtumishi wake.
Hakika tangu sasa vizazi vyote vitaniita aliye-
barikiwa,
49 kwa maana yeye Mwenye Nguvu
amenitendea mambo ya ajabu:
jina lake ni takatifu.
50 Rehema zake huwaendea wale wamchao,
kutoka kizazi hadi kizazi.
51 Kwa kuwa ametenda mambo ya ajabu kwa
mkono wake;
amewatawanya wale wenye kiburi
ndani ya mioyo yao.
52 Amewashusha watawala toka kwenye viti
vyao vya enzi,
lakini amewainua wanyenyekevu.
53 Amewashibisha wenye njaa kwa vitu vizuri,
bali matajiri amewafukuza mikono mitupu.
54 Amemsaidia mtumishi wake Israeli,
kwa kukumbuka ahadi yake ya kumrehemu
55 Abrahamu na uzao wake milele,
kama alivyowaahidi baba zetu.”

56 Maria akakaa na Elizabeti karibu miezi
mitatu, kisha akarudi nyumbani kwake.

### *Kuzaliwa Kwa Yohana Mbatizaji*

57 Ulipowadia wakati wa Elizabeti kujifungua,
alizaa mtoto mwanaume. 58 Majirani zake na
jamii zake wakasikia jinsi Bwana alivyomfanyia
rehema kuu, nao wakafurahi pamoja naye.

59 Siku ya nane wakaja kumtahiri mtoto,
wakataka yule mtoto aitwe Zekaria, ambalo
ndilo jina la baba yake. 60 Lakini mama yake
akakataa na kusema, “Hapana! Jina lake ataitwa
Yohana.”
61 Wakamwambia, “Hakuna mtu yeyote katika
jamaa yako mwenye jina kama hilo.”
62 Basi wakamfanyia Zekaria baba yake ishara
ili kujua kwamba yeye angependa kumpa mtoto
jina gani. 63 Akaomba wampe kibao cha
kuandikia na kwa mshangao wa kila mtu
akaandika: “Jina lake ni Yohana.” 64 Papo
hapo kinywa chake kikafunguliwa na ulimi wake
ukaachiwa, akawa anaongea akimsifu Mungu.
65 Majirani wote wakajawa na hofu ya Mungu,
na katika nchi yote ya vilima vya Uyahudi watu
walikuwa wakinena juu ya mambo haya yote.
66 Kila aliyesikia habari hizi alishangaa akauliza,
“Je, mtoto huyu atakuwa mtu wa namna gani?”
Maana mkono wa Bwana ulikuwa pamoja naye.

### *Unabii Wa Zekaria*

67 Zekaria, baba yake, akajazwa na Roho
Mtakatifu, naye akatoa unabii, akisema:

68 “Ahimidiwe Bwana, Mungu wa Israeli,
kwa kuwa amewajilia watu wake na kuwakomboa.
69 Naye ametusimamishia pembe* ya wokovu
katika nyumba ya Daudi mtumishi wake,
70 kama alivyonena kwa vinywa vya manabii
wake watakatifu tangu zamani,
71 kwamba atatuokoa kutoka kwa adui zetu,

---

* **1:69** Pembe hapa inamaanisha nguvu.

na kutoka mikononi mwao wote watuchukiao:
72 ili kuonyesha rehema kwa baba zetu
na kukumbuka Agano lake takatifu,
73 kiapo alichomwapia baba yetu Abrahamu:
74 kutuokoa kutoka mikononi mwa adui zetu,
tupate kumtumikia yeye pasipo hofu
75 katika utakatifu na haki mbele zake,
siku zetu zote.

76 “Nawe mtoto wangu, utaitwa nabii wa Aliye Juu Sana;
kwa kuwa utamtangulia Bwana
na kuandaa njia kwa ajili yake,
77 kuwajulisha watu wake juu ya wokovu
utakaopatikana kwa kusamehewa dhambi zao,
78 kwa ajili ya wingi wa rehema za Mungu wetu,
nuru itokayo juu itatuzukia
79 ili kuwaangazia wale waishio gizani
na katika uvuli wa mauti,
kuiongoza miguu yetu katika njia ya amani.”
80 Yule mtoto akakua na kuongezeka nguvu katika roho; akaishi nyikani hadi siku ile alipojionyesha hadharani kwa Waisraeli.

# 2

*Kuzaliwa Kwa Yesu*
*(Mathayo 1:18-25)*

1 Siku zile Kaisari Augusto alitoa amri kwamba watu wote waandikishwe katika ulimwengu wa Kirumi.
2 (Orodha hii ndiyo ya kwanza iliyofanyika wakati Krenio alikuwa mtawala wa

Shamu[*]). 3 Kila mtu alikwenda kuandikishwa
katika mji wake alikozaliwa.

4 Hivyo Yosefu akapanda kutoka mji wa
Nazareti ulioko Galilaya kwenda Uyahudi,
mpaka Bethlehemu, mji wa Daudi, kwa sababu
yeye alikuwa wa ukoo na wa nyumba ya Daudi.
5 Alikwenda huko kujiandikisha pamoja na
Maria, ambaye alikuwa amemposa naye alikuwa
mjamzito. 6 Wakiwa Bethlehemu, wakati
wa Maria wa kujifungua ukawa umetimia,
7 naye akamzaa mwanawe, kifungua mimba.
Akamfunika nguo za kitoto na kumlaza katika
hori ya kulia ng'ombe, kwa sababu hapakuwa
na nafasi katika nyumba ya wageni.

### *Wachungaji Na Malaika*

8 Katika eneo lile walikuwako wachungaji
waliokuwa wakikaa mashambani, wakilinda
makundi yao ya kondoo usiku. 9 Ghafula tazama,
malaika wa Bwana akawatokea, nao utukufu wa
Bwana ukawang'aria kotekote, wakaingiwa na
hofu. 10 Lakini malaika akawaambia: "Msio-
gope. Kwa maana tazama nawaletea habari
njema za furaha itakayokuwa kwa watu wote.
11 Leo katika mji wa Daudi kwa ajili yenu
amezaliwa Mwokozi, ndiye Kristo[†] Bwana. 12 Hii
ndiyo itakayokuwa ishara kwenu: Mtamkuta
mtoto mchanga amefunikwa nguo za kitoto na
kulazwa katika hori ya kulia ng'ombe."

---

[*] **2:2** Shamu inamaanisha Syria. [†] **2:11** Kristo maana yake ni Masiya, yaani Aliyetiwa mafuta.

13 Ghafula pakawa na jeshi kubwa la mbinguni pamoja na huyo malaika wakimsifu Mungu wakisema,

14 "Atukuzwe Mungu juu mbinguni,
na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia."

15 Hao malaika walipokwisha kuondoka na kwenda zao mbinguni, wale wachungaji wakasemezana wao kwa wao, "Twendeni Bethlehemu tukaone mambo haya ya ajabu yaliyotukia, ambayo Bwana ametuambia habari zake."

16 Hivyo wakaenda haraka Bethlehemu,
wakawakuta Maria na Yosefu na yule mtoto
mchanga akiwa amelala katika hori la kulia
ng'ombe. 17 Walipomwona yule mtoto,
wakawaeleza yale waliyokuwa wameambiwa
kuhusu huyo mtoto. 18 Nao wote waliosikia
habari hizi wakastaajabia yale waliyoambiwa
na wale wachungaji wa kondoo. 19 Lakini Maria
akayaweka mambo haya yote moyoni mwake
na kuyatafakari. 20 Wale wachungaji wakarudi,
huku wakimtukuza Mungu na kumsifu kwa ajili ya mambo yote waliyokuwa wameambiwa na kuyaona.

21 Hata zilipotimia siku nane, ulikuwa ndio wakati wa kumtahiri mtoto, akaitwa Yesu, jina alilokuwa amepewa na malaika kabla hajatungwa mimba.

*Yesu Apelekwa Hekaluni*

22 Ulipotimia wakati wa utakaso wake Maria kwa mujibu wa Sheria ya Mose, basi Yosefu na Maria walimpeleka mtoto Yerusalemu,
ili kumweka wakfu kwa Bwana 23 (kama

ilivyoandikwa katika Sheria ya Bwana, kwamba,
“Kila mtoto wa kiume kifungua mimba
atawekwa wakfu kwa Bwana”), 24 na pia kutoa
dhabihu kulingana na yale yaliyonenwa katika
Sheria ya Bwana: “Hua wawili au makinda
mawili ya njiwa.”

25 Basi alikuwako huko Yerusalemu mtu
mmoja jina lake Simeoni, ambaye alikuwa
mwenye haki na mcha Mungu, akitarajia faraja
ya Israeli, na Roho Mtakatifu alikuwa juu yake.
26 Roho Mtakatifu alikuwa amemfunulia kuwa
hatakufa kabla hajamwona Kristo wa Bwana.
27 Simeoni, akiwa ameongozwa na Roho Mtakat-
ifu, alikwenda Hekaluni. Wazazi walipomleta
mtoto Yesu ili kumfanyia kama ilivyokuwa des-
turi ya Sheria, 28 ndipo Simeoni akampokea
mtoto mikononi mwake na kumsifu Mungu,
akisema:

29 “Bwana Mwenyezi, kama ulivyoahidi,
sasa wamruhusu mtumishi wako
aende zake kwa amani.
30 Kwa maana macho yangu yameuona wokovu
wako,
31 ulioweka tayari machoni pa watu wote,
32 nuru kwa ajili ya ufunuo kwa watu wa Mataifa
na kwa ajili ya utukufu kwa watu wako
Israeli.”

33 Naye Yosefu na mama yake mtoto wakastaa-
jabu kwa yale yaliyokuwa yamesemwa kumhusu
huyo mtoto. 34 Kisha Simeoni akawabariki,
akamwambia Maria mama yake, “Mtoto huyu
amewekwa kwa makusudi ya kuanguka na
kuinuka kwa wengi katika Israeli. Atakuwa

ishara ambayo watu watanena dhidi yake,
35 ili
mawazo ya mioyo mingi yadhihirike. Nao
upanga utauchoma moyo wako.”
36 Tena alikuwako Hekaluni nabii mmoja
mwanamke, jina lake Ana binti Fanueli, wa kabila la Asheri. Alikuwa mzee sana; naye alikuwa
ameolewa na kuishi na mume kwa miaka saba
tu, kisha mumewe akafa.
37 Hivyo alikuwa
mjane na umri wake ulikuwa miaka themanini
na minne. Yeye hakuondoka humo Hekaluni
usiku wala mchana, bali alikuwa akimwabudu
Mungu, akifunga na kuomba.
38 Wakati huo
huo, Ana alikuja akaanza kusifu, akimshukuru
Mungu na kusema habari za huyo mtoto kwa
watu wote waliokuwa wakitarajia ukombozi wa
Yerusalemu.
39 Yosefu na Maria walipokuwa wamekamilisha mambo yote yaliyotakiwa na Sheria ya
Bwana, walirudi mjini kwao Nazareti huko
Galilaya.
40 Naye yule mtoto akakua na
kuongezeka nguvu, akiwa amejaa hekima, na
neema ya Mungu ilikuwa juu yake.

### *Kijana Yesu Hekaluni*

41 Kila mwaka Yosefu na Maria mama
yake Yesu walikuwa na desturi ya kwenda
Yerusalemu kwa ajili ya Sikukuu ya Pasaka.
42 Yesu alipokuwa na umri wa miaka kumi
na miwili, walipanda kwenda kwenye Sikukuu
hiyo kama ilivyokuwa desturi.
43 Baada ya
Sikukuu kumalizika, wakati Yosefu na Maria
mama yake walipokuwa wakirudi nyumbani,
Yesu alibaki Yerusalemu lakini hawakutambua.
44 Wao wakidhani kuwa yuko miongoni mwa

wasafiri, walienda mwendo wa kutwa nzima.
Ndipo wakaanza kumtafuta miongoni mwa ja-
maa zao na marafiki. 45 Walipomkosa walirudi
Yerusalemu ili kumtafuta. 46 Baada ya siku tatu
wakamkuta ndani ya Hekalu, akiwa ameketi
katikati ya walimu wa sheria, akiwasikiliza
na kuwauliza maswali. 47 Wote waliomsikia
walistaajabishwa na uwezo wake mkubwa wa
kuelewa, na majibu aliyoyatoa. 48 Yosefu na
Maria mama yake walipomwona walishangaa.
Mama yake akamuuliza, “Mwanangu, mbona
umetufanyia hivi? Tazama, mimi na baba yako
tumekuwa tukikutafuta kwa wasiwasi mkubwa
kila mahali.”

49 Yesu akawaambia, “Kwa nini kunitafuta?
Hamkujua kwamba imenipasa kuwa katika
nyumba ya Baba yangu?”

50 Lakini wao hawakuelewa maana ya lile
alilowaambia.

51 Ndipo akashuka pamoja nao hadi Nazareti,
naye alikuwa mtiifu kwao. Lakini mama yake
akayaweka moyoni mwake mambo haya yote.
52 Naye Yesu akakua katika hekima na kimo,
akimpendeza Mungu na wanadamu.

# 3

### *Yohana Mbatizaji Aanza Kuhubiri*
### *(Mathayo 3:1-12; Marko 1:1-8; Yohana 1:19-28)*

1 Katika mwaka wa kumi na tano wa utawala
wa Kaisari Tiberio, Pontio Pilato akiwa mtawala
wa Uyahudi, Herode akiwa mfalme wa Galilaya,
Filipo ndugu yake akiwa mfalme wa Iturea na
nchi ya Trakoniti, na Lisania akiwa mfalme

wa Abilene, 2 nao Anasi na Kayafa wakiwa
makuhani wakuu, neno la Mungu likamjia
Yohana, mwana wa Zekaria huko jangwani.
3 Akaenda katika nchi yote kandokando ya Mto
Yordani, akihubiri ubatizo wa toba kwa ajili ya
msamaha wa dhambi. 4 Kama ilivyoandikwa
katika kitabu cha nabii Isaya:

"Sauti ya mtu aliaye nyikani,
'Itengenezeni njia ya Bwana,
yanyoosheni mapito yake.
5 Kila bonde litajazwa,
kila mlima na kilima vitashushwa.
Njia zilizopinda zitanyooshwa,
na zilizoparuza zitasawazishwa.
6 Nao watu wote watauona
wokovu wa Mungu.' "

7 Yohana akauambia ule umati wa watu
uliokuwa unakuja ili kubatizwa naye, "Ninyi
watoto wa nyoka! Ni nani aliyewaonya kuikim-
bia ghadhabu inayokuja? 8 Basi zaeni matunda
yastahiliyo toba. Wala msianze kusema mioyoni
mwenu kuwa, 'Sisi tunaye Abrahamu, baba
yetu.' Kwa maana nawaambia kuwa Mungu
anaweza kumwinulia Abrahamu watoto kutoka
mawe haya. 9 Hata sasa shoka limeshawekwa
tayari kwenye shina la kila mti. Basi kila mti
usiozaa matunda mazuri hukatwa na kutupwa
motoni."

10 Ule umati wa watu ukamuuliza, "Inatupasa
tufanyeje basi?"

11 Yohana akawaambia, "Aliye na kanzu mbili
amgawie asiye nayo, naye aliye na chakula na
afanye vivyo hivyo."

12 Watoza ushuru nao wakaja ili wabatizwe, wakamuuliza, "Bwana na sisi inatupasa tufanyeje?"

13 Akawaambia, "Msichukue zaidi ya kiwango mlichopangiwa."

14 Askari nao wakamuuliza, "Je, nasi inatupasa tufanye nini?"

Akawaambia, "Msimdhulumu mtu wala msimshtaki mtu kwa uongo, bali mridhike na mishahara yenu."

15 Watu walikuwa na matazamio makubwa.
Wakawa wanajiuliza mioyoni mwao iwapo
Yohana angeweza kuwa ndiye Kristo.* 16 Yohana
akawajibu akawaambia, "Mimi nawabatiza kwa
maji.† Lakini atakuja aliye na nguvu kuniliko
mimi, ambaye sistahili hata kufungua kamba za
viatu vyake. Yeye atawabatiza kwa Roho Mtakat-
ifu na kwa moto. 17 Pepeto lake liko mkononi,
tayari kusafisha sakafu yake ya kupuria na
kuikusanya ngano ghalani, lakini makapi atay-
ateketeza kwa moto usiozimika." 18 Basi, kwa
maonyo mengine mengi Yohana aliwasihi na
kuwahubiria watu Habari Njema.

19 Lakini Yohana alipomkemea Mfalme Herode
kuhusu uhusiano wake na Herodia, mke wa
ndugu yake, na maovu mengine aliyokuwa ame-
fanya, 20 Herode aliongezea jambo hili kwa hayo
mengine yote: alimfunga Yohana gerezani.

### *Kubatizwa Kwa Bwana Yesu*
### *(Mathayo 3:13-17; Marko 1:9-11)*

---

* **3:15** Kristo maana yake ni Masiya, yaani Aliyetiwa mafuta.

† **3:16** Tafsiri nyingine zinasema ndani ya maji.

21 Baada ya watu wote kubatizwa, Yesu naye
akabatizwa. Naye alipokuwa akiomba, mbingu
zilifunguka. 22 Roho Mtakatifu akashuka juu
yake kwa umbo kama la hua, nayo sauti ku-
toka mbinguni ikasema: “Wewe ni Mwanangu
mpendwa; nami nimependezwa nawe sana.”

### *Ukoo Wa Bwana Yesu*
### *(Mathayo 1:1-17)*

23 Yesu alikuwa na umri wa miaka thelathini
alipoanza huduma yake. Alikuwa akidhaniwa
kuwa mwana wa Yosefu,

Yosefu alikuwa mwana wa Eli,
24 Eli alikuwa mwana wa Mathati,
Mathati alikuwa mwana wa Lawi,
Lawi alikuwa mwana wa Melki,
Melki alikuwa mwana wa Yanai,
Yanai alikuwa mwana wa Yosefu,
25 Yosefu alikuwa mwana wa Matathia,
Matathia alikuwa mwana wa Amosi,
Amosi alikuwa mwana wa Nahumu,
Nahumu alikuwa mwana wa Esli,
Esli alikuwa mwana wa Nagai,
26 Nagai alikuwa mwana wa Maathi,
Maathi alikuwa mwana wa Matathia,
Matathia alikuwa mwana wa Semeini,
Semeini alikuwa mwana wa Yoseki,
Yoseki alikuwa mwana wa Yoda,
27 Yoda alikuwa mwana wa Yoanani,
Yoanani alikuwa mwana wa Resa,
Resa alikuwa mwana wa Zerubabeli,
Zerubabeli alikuwa mwana wa Shealtieli,
Shealtieli alikuwa mwana wa Neri,
28 Neri alikuwa mwana wa Melki,

Melki alikuwa mwana wa Adi,
Adi alikuwa mwana wa Kosamu,
Kosamu alikuwa mwana wa Elmadamu,
Elmadamu alikuwa mwana wa Eri,
29 Eri alikuwa mwana wa Yoshua,
Yoshua alikuwa mwana wa Eliezeri,
Eliezeri alikuwa mwana wa Yorimu,
Yorimu alikuwa mwana wa Mathati,
Mathati alikuwa mwana wa Lawi,
30 Lawi alikuwa mwana wa Simeoni,
Simeoni alikuwa mwana wa Yuda,
Yuda alikuwa mwana wa Yosefu,
Yosefu alikuwa mwana wa Yonamu,
Yonamu alikuwa mwana wa Eliakimu,
Eliakimu alikuwa mwana wa Melea,
31 Melea alikuwa mwana wa Mena,
Mena alikuwa mwana wa Matatha,
Matatha alikuwa mwana wa Nathani,
Nathani alikuwa mwana wa Daudi,
32 Daudi alikuwa mwana wa Yese,
Yese alikuwa mwana wa Obedi,
Obedi alikuwa mwana wa Boazi,
Boazi alikuwa mwana wa Salmoni,
Salmoni alikuwa mwana wa Nashoni,
33 Nashoni alikuwa mwana wa Aminadabu,
Aminadabu alikuwa mwana wa Aramu,
Aramu alikuwa mwana wa Hesroni,
Hesroni alikuwa mwana wa Peresi,
Peresi alikuwa mwana wa Yuda,
34 Yuda alikuwa mwana wa Yakobo,
Yakobo alikuwa mwana wa Isaki,
Isaki alikuwa mwana wa Abrahamu,
Abrahamu alikuwa mwana wa Tera,
Tera alikuwa mwana wa Nahori,
35 Nahori alikuwa mwana wa Serugi,

Serugi alikuwa mwana wa Reu,
Reu alikuwa mwana wa Pelegi,
Pelegi alikuwa mwana wa Eberi,
Eberi alikuwa mwana wa Sala,
36 Sala alikuwa mwana wa Kenani,
Kenani alikuwa mwana wa Arfaksadi,
Arfaksadi alikuwa mwana wa Shemu,
Shemu alikuwa mwana wa Noa,
Noa alikuwa mwana wa Lameki,
37 Lameki alikuwa mwana wa Methusela,
Methusela alikuwa mwana wa Enoki,
Enoki alikuwa mwana wa Yaredi,
Yaredi alikuwa mwana wa Mahalaleli,
Mahalaleli alikuwa mwana wa Kenani,
38 Kenani alikuwa mwana wa Enoshi,
Enoshi alikuwa mwana wa Sethi,
Sethi alikuwa mwana wa Adamu,
Adamu alikuwa mwana wa Mungu.

# 4

### *Yesu Ajaribiwa Na Shetani (Mathayo 4:1-11; Marko 1:12-13)*

1 Yesu, akiwa amejaa Roho Mtakatifu, akarudi
kutoka Yordani. Akaongozwa na Roho Mtakatifu
hadi nyikani, 2 mahali ambako kwa siku arobaini
alikuwa akijaribiwa na ibilisi. Kwa siku zote
hizo hakula chochote, hivyo baada ya muda huo
akaona njaa.

3 Ibilisi akamwambia, "Ikiwa wewe ni Mwana
wa Mungu, amuru jiwe hili liwe mkate."

4 Yesu akajibu akamwambia, "Imeandikwa:
'Mtu haishi kwa mkate tu.' "

5 Ibilisi akampeleka hadi juu ya mlima mrefu
akamwonyesha milki zote za dunia kwa mara

moja. 6 Akamwambia, “Nitakupa mamlaka
juu ya milki hizi na fahari zake zote, kwa
maana zimekabidhiwa mkononi mwangu nami
ninaweza kumpa yeyote ninayetaka. 7 Hivyo
ikiwa utanisujudia na kuniabudu, vyote vi-
takuwa vyako.”

8 Yesu akamjibu, “Imeandikwa: ‘Mwabudu
Bwana Mungu wako na umtumikie yeye peke
yake.’ ”

9 Kisha ibilisi akampeleka mpaka Yerusalemu,
akamweka juu ya mnara mrefu wa Hekalu,
akamwambia, “Kama wewe ndiwe Mwana wa
Mungu, jitupe chini kutoka hapa, 10 kwa maana
imeandikwa:

“ ‘Atakuagizia malaika zake
ili wakulinde;
11 nao watakuchukua mikononi mwao,
usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe.’ ”

12 Yesu akamjibu, “Imesemwa, ‘Usimjaribu
Bwana Mungu wako.’ ”

13 Ibilisi alipomaliza kila jaribu, akamwacha
Yesu mpaka wakati mwingine ufaao.

### *Mwanzo Wa Huduma Ya Galilaya (Mathayo 4:12-17; Marko 1:14-15)*

14 Kisha Yesu akarudi mpaka Galilaya, akiwa
amejaa nguvu za Roho Mtakatifu, nazo habari
zake zikaenea katika sehemu zote za nchi za
kandokando. 15 Akaanza kufundisha kwenye
masinagogi yao, na kila mmoja akamsifu.

### *Yesu Akataliwa Nazareti (Mathayo 13:53-58; Marko 6:1-6)*

16 Yesu akaenda Nazareti, alipolelewa, na
siku ya Sabato alikwenda katika sinagogi kama
ilivyokuwa desturi yake. Akasimama ili asome,
17 naye akapewa kitabu cha nabii Isaya, akaki-
fungua na kukuta mahali palipoandikwa:
18 "Roho wa Bwana yu juu yangu,
kwa sababu amenitia mafuta
kuwahubiria maskini habari njema.
Amenituma kuwatangazia wafungwa
kufunguliwa kwao,
na vipofu kupata kuona tena,
kuwaweka huru wanaoonewa,
19 na kutangaza mwaka wa Bwana uliokuba-
lika."
20 Kisha akakifunga kitabu, akamrudishia mtu-
mishi na akaketi. Watu wote waliokuwamo
katika sinagogi wakamkazia macho. 21 Ndipo
akaanza kwa kuwaambia, "Leo Andiko hili lime-
timia mkiwa mnasikia."
22 Wote waliokuwako wakamsifu na
kuyastaajabia maneno yake yaliyojaa neema,
wakaulizana, "Je, huyu si mwana wa Yosefu?"
23 Yesu akawaambia, "Bila shaka mtatu-
mia mithali hii: 'Tabibu, jiponye mwenyewe!
Mambo yale tuliyosikia kwamba uliyafanya
huko Kapernaumu, yafanye na hapa kwenye mji
wako.' "
24 Yesu akasema, "Amin, nawaambia,
hakuna nabii anayekubalika katika mji wake
mwenyewe. 25 Lakini ukweli ni kwamba
palikuwa na wajane wengi katika Israeli wakati
wa Eliya, mbingu zilipofungwa kwa miaka
mitatu na miezi sita pakawa na njaa kuu katika
nchi nzima. 26 Hata hivyo Eliya hakutumwa hata

kwa mmoja wao, bali kwa mjane mmoja wa
Sarepta katika nchi ya Sidoni. 27 Pia palikuwa
na wengi wenye ukoma katika Israeli katika
siku za nabii Elisha, lakini hakuna hata mmoja
wao aliyetakaswa, isipokuwa Naamani mtu wa
Shamu."*

28 Watu wote katika sinagogi waliposikia ma-
neno haya, wakakasirika sana. 29 Wakasimama,
wakamtoa nje ya mji, wakamchukua hadi
kwenye kilele cha mlima mahali ambapo mji huo
ulikuwa umejengwa, ili wamtupe chini kutoka
kwenye mteremko mkali. 30 Lakini yeye akapita
papo hapo katikati ya huo umati wa watu
akaenda zake.

### *Yesu Atoa Pepo Mchafu (Marko 1:21-28)*

31 Kisha Yesu akashuka kwenda Kapernaumu,
mji wa Galilaya, na katika siku ya Sabato akawa
anafundisha. 32 Wakashangazwa sana na ma-
fundisho yake, maana maneno yake yalikuwa na
mamlaka.

33 Ndani ya sinagogi palikuwa na mtu
aliyekuwa amepagawa na pepo mchafu. Naye
akapiga kelele kwa nguvu akisema, 34 "Tuache!
Tuna nini nawe, Yesu wa Nazareti? Je, umekuja
kutuangamiza? Ninakujua wewe ni nani. Wewe
ndiwe Aliye Mtakatifu wa Mungu!"

35 Basi Yesu akamkemea yule pepo mchafu,
akisema, "Nyamaza kimya! Nawe umtoke!" Yule
pepo mchafu akamwangusha yule mtu chini
mbele yao wote, akatoka pasipo kumdhuru.

---

* **4:27** Shamu hapa inamaanisha Syria.

36 Watu wote wakashangaa, wakaambiana, “Ma-
fundisho haya ni ya namna gani? Anawaamuru
pepo wachafu kwa mamlaka na nguvu, nao
wanatoka!” 37 Habari zake zikaanza kuenea kila
mahali katika sehemu ile.

### *Yesu Awaponya Wengi*
### *(Mathayo 8:14-17; Marko 1:29-34)*

38 Yesu akatoka katika sinagogi, akaenda
nyumbani kwa Simoni. Basi huko alimkuta
mama mkwe wa Simoni akiwa ameshikwa na
homa kali, nao wakamwomba Yesu amsaidie.
39 Hivyo Yesu akamwinamia na kukemea ile
homa, nayo ikamwacha. Akaamka saa ile ile,
naye akaanza kuwahudumia.

40 Jua lilipokuwa linatua, watu wakamletea
Yesu watu wote waliokuwa na maradhi mbal-
imbali, naye akaweka mikono yake juu ya kila
mgonjwa, naye akawaponya. 41 Pepo wachafu
pia wakawatoka watu wengi, nao walipokuwa
wakitoka wakapiga kelele, wakisema: “Wewe ni
Mwana wa Mungu!” Lakini Yesu akawakemea
na kuwazuia wasiseme, kwa maana walimjua
kuwa yeye ndiye Kristo.†

42 Kesho yake, kulipopambazuka, Yesu alik-
wenda mahali pa faragha. Watu wengi wakawa
wanamtafuta kila mahali, nao walipomwona
wakajaribu kumzuia asiondoke. 43 Lakini yeye
akawaambia, “Imenipasa kuhubiri habari njema
za Ufalme wa Mungu katika miji mingine
pia, kwa maana kwa kusudi hili nilitumwa.”

† **4:41** Kristo maana yake ni Masiya, yaani Aliyetiwa mafuta.

44 Naye aliendelea kuhubiri katika masinagogi ya
Uyahudi.

# 5

### *Kuitwa Kwa Wanafunzi Wa Kwanza (Mathayo 4:18-22; Marko 1:16-20)*

1 Siku moja Yesu alipokuwa amesimama
karibu na Ziwa la Genesareti,* watu wengi
wakiwa wanasongana kumzunguka ili wapate
kusikia neno la Mungu, 2 akaona mashua mbili
ukingoni mwa ziwa, zikiwa zimeachwa hapo
na wavuvi waliokuwa wanaosha nyavu zao.
3 Akaingia katika mojawapo ya hizo mashua
ambayo ilikuwa ya Simoni, akamwomba aiso-
geze ndani ya maji kidogo kutoka ufuoni. Kisha
akaketi na kufundisha watu akiwa mle ndani ya
mashua.

4 Alipomaliza kunena, akamwambia Simoni,
"Sasa peleka mashua hadi kilindini kisha
mshushe nyavu zenu mkavue samaki."

5 Simoni akamjibu, "Bwana, tumefanya kazi ya
kuchosha usiku kucha na hatukuvua chochote.
Lakini, kwa neno lako nitazishusha nyavu."

6 Nao walipozishusha nyavu zao, wakavua
samaki wengi sana, nyavu zao zikajaa zikaanza
kukatika. 7 Wakawaashiria wavuvi wenzao
kwenye ile mashua nyingine ili waje kuwasaidia.
Wakaja, wakajaza mashua zote mbili samaki
hata zikaanza kuzama.

8 Simoni Petro alipoona haya yaliyotukia,
alianguka miguuni mwa Yesu na kumwambia,

---

* **5:1** Yaani Bahari ya Galilaya.

“Bwana, ondoka kwangu. Mimi ni mtu mwenye
dhambi!” 9 Kwa kuwa yeye na wavuvi wenzake
walikuwa wameshangazwa sana na wingi wa
samaki waliokuwa wamepata. 10 Vivyo hivyo
wenzake Simoni, yaani Yakobo na Yohana, wana
wa Zebedayo, walishangazwa pia.

Ndipo Yesu akamwambia Simoni, “Usiogope,
tangu sasa utakuwa mvuvi wa watu.” 11 Hivyo
wakasogeza mashua zao mpaka ufuoni mwa
bahari, wakaacha kila kitu na kumfuata.

### *Yesu Amtakasa Mtu Mwenye Ukoma (Mathayo 8:1-4; Marko 1:40-45)*

12 Ikawa siku moja Yesu alipokuwa katika
mji fulani, mtu mmoja mwenye ukoma mwili
mzima akamjia. Alipomwona Yesu, alianguka
chini mpaka uso wake ukagusa ardhi, akamsihi
akisema, “Bwana, ukitaka, waweza kunitakasa.”
13 Yesu akanyoosha mkono wake, akamgusa
yule mtu, akamwambia, “Nataka. Takasika!” Na
mara ukoma wake ukatakasika.
14 Yesu akamwagiza akisema, “Usimwambie
mtu yeyote, bali nenda ukajionyeshe kwa kuhani
na ukatoe sadaka alizoagiza Mose kwa utakaso
wako, ili kuwa ushuhuda kwao.”
15 Lakini habari zake Yesu zikazidi sana kue-
nea kotekote kuliko wakati mwingine wowote.
Makutano makubwa ya watu yalikuwa yakiku-
sanyika ili kumsikiliza na kuponywa magonjwa
yao. 16 Lakini mara kwa mara Yesu alijitenga nao
ili kwenda mahali pa faragha kuomba.

### *Yesu Amponya Mtu Mwenye Kupooza (Mathayo 9:1-8; Marko 2:1-12)*

17 Siku moja Yesu alipokuwa akifundisha, Ma-
farisayo na walimu wa sheria, waliokuwa wame-
toka kila kijiji cha Galilaya na kutoka Uyahudi
na Yerusalemu, walikuwa wameketi huko. Nao
uweza wa Bwana ulikuwa juu yake kuponya
wagonjwa. 18 Wakaja watu wamembeba
mgonjwa aliyepooza kwenye mkeka. Waka-
jaribu kumwingiza ndani ili wamweke mbele
ya Yesu. 19 Walipokuwa hawawezi kufanya
hivyo kwa sababu ya umati wa watu, waka-
panda juu ya paa, wakaondoa baadhi ya mato-
fali, wakamteremsha yule mgonjwa kwa mkeka
wake hadi katikati ya ule umati pale mbele ya
Yesu.

20 Yesu alipoiona imani yao, akamwambia yule
mgonjwa, "Rafiki, dhambi zako zimesamehewa."

21 Mafarisayo na wale walimu wa she-
ria wakaanza kuuliza, "Ni nani mtu huyu
anayesema maneno ya kukufuru? Ni nani
awezaye kusamehe dhambi isipokuwa Mungu
peke yake?"

22 Yesu akijua mawazo yao akawauliza, "Kwa
nini mnawaza hivyo mioyoni mwenu? 23 Je,
ni lipi lililo rahisi zaidi, kumwambia, 'Ume-
samehewa dhambi zako,' au kusema, 'Inuka,
uende'? 24 Lakini ili mpate kujua kwamba
Mwana wa Adamu anayo mamlaka duniani
kusamehe dhambi…" Akamwambia yule aliye-
pooza, "Nakuambia, inuka, chukua mkeka wako,
uende nyumbani kwako." 25 Mara yule mtu
aliyekuwa amepooza akasimama mbele yao
wote, akachukua mkeka wake, akaenda zake
nyumbani, huku akimtukuza Mungu. 26 Kila

mmoja akashangaa na kumtukuza Mungu.
Wakajawa na hofu ya Mungu, wakasema, “Leo
tumeona mambo ya ajabu.”

### *Yesu Amwita Lawi*
### *(Mathayo 9:9-13; Marko 2:13-17)*

27 Baada ya haya, Yesu alitoka na kum-
wona mtoza ushuru mmoja jina lake Lawi
akiwa amekaa forodhani, mahali pake pa kutoza
ushuru. Akamwambia, “Nifuate.” 28 Naye Lawi
akaacha kila kitu, akaondoka, akamfuata.
29 Kisha Lawi akamfanyia Yesu karamu kubwa
nyumbani kwake, nao umati mkubwa wa
watoza ushuru na watu wengine walikuwa
wakila pamoja nao. 30 Lakini Mafarisayo
na walimu wa sheria waliokuwa wa dhe-
hebu lao wakawalalamikia wanafunzi wa Yesu,
wakisema, “Mbona mnakula na kunywa pamoja
na watoza ushuru na ‘wenye dhambi’?”
31 Yesu akawajibu, “Wenye afya hawahitaji
tabibu, bali walio wagonjwa. 32 Sikuja kuwaita
wenye haki, bali wenye dhambi wapate kutubu.”

### *Yesu Aulizwa Kuhusu Kufunga*
### *(Mathayo 9:14-17; Marko 2:18-22)*

33 Wakamwambia Yesu, “Wanafunzi wa
Yohana na wa Mafarisayo mara kwa mara
hufunga na kuomba, lakini wanafunzi wako
wanaendelea kula na kunywa.”
34 Yesu akawajibu, “Je, mnaweza kuwafanya
wageni wa bwana arusi kufunga wakati yuko
pamoja nao? 35 Lakini wakati utafika ambapo
bwana arusi ataondolewa kwao. Hapo ndipo
watakapofunga.”

36 Yesu akawapa mfano huu, akawaambia:
"Hakuna mtu achanaye kiraka kutoka kwenye
nguo mpya na kukishonea kwenye nguo iliy-
ochakaa. Akifanya hivyo, atakuwa amechana
nguo mpya, na kile kiraka hakitalingana na ile
nguo iliyochakaa. 37 Hakuna mtu awekaye divai
mpya kwenye viriba vikuukuu. Akifanya hivyo,
hiyo divai mpya itavipasua hivyo viriba, nayo
yote itamwagika. 38 Divai mpya lazima iwekwe
kwenye viriba vipya. 39 Wala hakuna mtu
anayependelea divai mpya baada ya kunywa
divai ya zamani, bali husema, 'Ile ya zamani ni
nzuri zaidi.' "

# 6

### *Bwana Wa Sabato*
### *(Mathayo 12:1-8; Marko 2:23-28)*

1 Ikawa siku moja ya Sabato Yesu alikuwa
akipita katika mashamba ya nafaka, nao wana-
funzi wake wakaanza kuvunja masuke ya
nafaka, wakayafikicha kwa mikono yao na
kula punje zake. 2 Baadhi ya Mafarisayo
wakawauliza, "Mbona mnafanya mambo yasiyo
halali kufanywa siku ya Sabato?"

3 Yesu akawajibu, "Je, ninyi hamjasoma
kamwe alivyofanya Daudi wakati yeye na wen-
zake walikuwa na njaa? 4 Aliingia ndani
ya nyumba ya Mungu, akaichukua na kuila
ile mikate iliyowekwa wakfu, ambayo ni ha-
lali kuliwa na makuhani peke yao. Naye
pia akawapa wenzake." 5 Yesu akawaambia,
"Mwana wa Adamu ndiye Bwana wa Sabato."

### *Mtu Aliyepooza Mkono Aponywa (Mathayo 12:9-14; Marko 3:1-6)*

6 Ikawa siku nyingine ya Sabato, Yesu aliingia ndani ya sinagogi na akawa anafundisha. Huko palikuwa na mtu ambaye mkono wake
wa kuume ulikuwa umepooza. 7 Mafarisayo
na walimu wa sheria walikuwa wakitafuta sababu ya kumshtaki Yesu. Kwa hivyo wakawa wanamwangalia sana ili waone kama ataponya
katika siku ya Sabato. 8 Lakini Yesu alijua
mawazo yao, hivyo akamwambia yule mwenye mkono uliopooza, "Inuka usimame mbele ya watu wote." Hivyo yule mtu akainuka, akasimama mbele yao wote.
9 Ndipo Yesu akawaambia wale walimu wa
sheria na Mafarisayo, "Nawauliza ninyi, ni lipi lililo halali siku ya Sabato? Ni kutenda mema au kutenda mabaya? Ni kuokoa maisha au kuyaangamiza?"
10 Akawatazama watu wote waliokuwepo,
kisha akamwambia yule aliyepooza mkono, "Nyoosha mkono wako!" Akaunyoosha na mkono
wake ukaponywa kabisa. 11 Wale wakuu
wakakasirika sana, wakashauriana wao kwa wao ni nini watakachomtendea Yesu.

### *Yesu Achagua Mitume Kumi Na Wawili (Mathayo 10:1-4; Marko 3:13-19)*

12 Ikawa katika siku hizo Yesu alikwenda
mlimani kuomba, akakesha usiku kucha akimwomba Mungu. 13 Kulipopambazuka, akawaita
wanafunzi wake, naye akachagua kumi na
wawili, ambao pia aliwaita mitume: 14 Simoni
aliyemwita Petro, Andrea nduguye, Yakobo,

Yohana, Filipo, Bartholomayo,
15 Mathayo,
Tomaso, Yakobo mwana wa Alfayo, Simoni
aliyeitwa Zelote,
16 Yuda mwana wa Yakobo, na
Yuda Iskariote ambaye alikuwa msaliti.

### *Yesu Aponya Wengi*
### *(Mathayo 4:23-25)*

17 Akashuka pamoja nao, akasimama mahali penye uwanja tambarare. Hapo palikuwa na idadi kubwa ya wanafunzi wake na umati mkubwa wa watu kutoka sehemu zote za Uyahudi, kutoka Yerusalemu, na kutoka pwani ya Tiro na Sidoni.
18 Walikuwa
wamekuja kumsikiliza na kuponywa magonjwa yao. Wale waliokuwa wakiteswa na pepo wachafu akawaponya.
19 Watu wote walikuwa
wanajitahidi kumgusa kwa sababu nguvu zilikuwa zikimtoka na kuwaponya wote.

### *Baraka Na Ole*
### *(Mathayo 5:1-12)*

20 Akawatazama wanafunzi wake, akasema:
"Mmebarikiwa ninyi mlio maskini,
kwa sababu Ufalme wa Mungu ni wenu.
21 Mmebarikiwa ninyi mlio na njaa sasa,
kwa sababu mtashibishwa.
Mmebarikiwa ninyi mnaolia sasa,
kwa sababu mtacheka.
22 Mmebarikiwa ninyi, watu watakapowachukia,
watakapowatenga na kuwatukana
na kulikataa jina lenu kama neno ovu,
kwa ajili ya Mwana wa Adamu.
23 "Furahini na kurukaruka kwa shangwe, kwa
sababu thawabu yenu ni kubwa mbinguni, kwa

kuwa hivyo ndivyo baba zao walivyowatenda manabii.
24 “Lakini ole wenu ninyi mlio matajiri,
kwa sababu mmekwisha kupokea faraja yenu.
25 Ole wenu ninyi mlioshiba sasa,
maana mtaona njaa.
Ole wenu ninyi mnaocheka sasa,
maana mtaomboleza na kulia.
26 Ole wenu watu watakapowasifu,
kwani ndivyo baba zao walivyowasifu
manabii wa uongo.

*Wapendeni Adui Zenu*
*(Mathayo 5:38-48)*

27 “Lakini nawaambia ninyi mnaonisikia:
Wapendeni adui zenu. Watendeeni
mema wanaowachukia. 28 Wabarikini
wale wanaowalaani, waombeeni wale
wanaowatendea mabaya. 29 Kama mtu
akikupiga shavu moja, mgeuzie na la pili
pia. Mtu akikunyang’anya koti lako, usimzuie
kuchukua joho pia. 30 Mpe kila akuombaye,
na kama mtu akichukua mali yako usitake
akurudishie. 31 Watendeeni wengine kama
ambavyo mngetaka wawatendee ninyi.
32 “Kama mkiwapenda tu wale
wanaowapenda, mwapata sifa gani? Hata
‘wenye dhambi’ huwapenda wale wawapendao.
33 Tena mkiwatendea mema wale tu
wanaowatendea ninyi mema, mwapata sifa
gani? Hata ‘wenye dhambi’ hufanya vivyo
hivyo. 34 Tena mnapowakopesha wale tu
mnaotegemea wawalipe, mwapata sifa gani?

Hata 'wenye dhambi' huwakopesha 'wenye
dhambi' wenzao wakitarajia kulipwa mali
yao yote. 35 Lakini wapendeni adui zenu,
watendeeni mema, wakopesheni bila kutegemea
kurudishiwa mlichokopesha. Ndipo thawabu
yenu itakapokuwa kubwa, nanyi mtakuwa
wana wa Aliye Juu Sana, kwa sababu yeye ni
mwema kwa watu wasio na shukrani na kwa
wale waovu. 36 Kuweni na huruma, kama Baba
yenu alivyo na huruma.

### *Kuwahukumu Wengine (Mathayo 7:1-5)*

37 "Msihukumu, nanyi hamtahukumiwa. Msi-
laumu, nanyi hamtalaumiwa. Sameheni, nanyi
mtasamehewa. 38 Wapeni watu vitu, nanyi
mtapewa. Kipimo cha kujaa na kushindiliwa na
kusukwasukwa hata kumwagika, ndicho watu
watakachowapa vifuani mwenu. Kwa kuwa kip-
imo kile mpimacho, ndicho mtakachopimiwa."

39 Pia akawapa mfano akasema, "Je, kipofu
aweza kumwongoza kipofu? Je, wote waw-
ili hawatatumbukia shimoni? 40 Mwanafunzi
hawezi kumzidi mwalimu wake, ila yule aliye-
hitimu aweza kuwa kama mwalimu wake.

41 "Mbona unatazama kibanzi kilicho ndani
ya jicho la ndugu yako, wala huoni boriti iliyo
ndani ya jicho lako mwenyewe? 42 Utawezaje
kumwambia ndugu yako, 'Ndugu yangu, acha
nitoe kibanzi kilicho ndani ya jicho lako,' wakati
wewe mwenyewe huoni boriti iliyo ndani ya
jicho lako? Ewe mnafiki, ondoa boriti ndani ya
jicho lako kwanza, ndipo utaweza kuona dhahiri

jinsi ya kuondoa kibanzi kilicho ndani ya jicho la
ndugu yako.

### *Mti Na Mazao Yake*
### *(Mathayo 7:16-20; Marko 12:33-35)*

43 “Hakuna mti mzuri uzaao matunda mabaya,
wala hakuna mti mbaya uzaao matunda mazuri.
44 Kila mti hujulikana kwa matunda yake. Kwa
maana watu hawachumi tini kwenye miiba,
wala zabibu kwenye michongoma. 45 Vivyo
hivyo mtu mwema hutoa mambo mema kutoka
kwenye hazina ya moyo wake, naye mtu mwovu
hutoa mambo maovu kutoka kwenye hazina ya
moyo wake. Kwa kuwa mtu hunena kwa kinywa
chake yale yaliyoujaza moyo wake.

### *Mjenzi Mwenye Busara Na Mjenzi Mpumbavu*
### *(Mathayo 7:24-27)*

46 “Kwa nini mnaniita, ‘Bwana, Bwana,’ nanyi
hamfanyi ninayowaambia? 47 Nitawaonyesha
jinsi alivyo mtu yule anayekuja kwangu na
kusikia maneno yangu na kuyatenda. 48 Yeye
ni kama mtu aliyejenga nyumba, akachimba
chini sana, na kuweka msingi kwenye mwamba.
Mafuriko yalipokuja, maji ya ghafula yaliipiga
ile nyumba, lakini haikutikisika, kwa sababu
ilikuwa imejengwa vizuri. 49 Lakini yeye
anayesikia maneno yangu wala asiyatende, ni
kama mtu aliyejenga nyumba juu ya ardhi
bila kuweka msingi. Mafuriko yalipoikumba
nyumba ile, ikaanguka mara na kubomoka
kabisa.”

# 7

*Yesu Amponya Mtumishi Wa Jemadari*
*(Mathayo 8:5-13)*

1 Baada ya Yesu kumaliza kusema haya yote
watu wakiwa wanamsikiliza, akaingia Kaper-
naumu. 2 Mtumishi wa jemadari mmoja
wa Kirumi, ambaye bwana wake alimthamini
sana, alikuwa mgonjwa sana karibu kufa.
3 Jemadari huyo aliposikia habari za Yesu, aliwa-
tuma wazee wa Kiyahudi kwake, wakamwomba
aje kumponya mtumishi wa huyo jemadari.
4 Wale wazee walipofika kwa Yesu, wakam-
sihi sana amsaidie yule jemadari wakisema,
“Mtu huyu anastahili wewe umfanyie jambo
hili, 5 kwa sababu analipenda taifa letu tena
ametujengea sinagogi.” 6 Hivyo Yesu akaon-
gozana nao, lakini alipokuwa hayuko mbali
na nyumbani, yule jemadari akatuma rafiki
zake kumwambia Yesu, “Bwana, usijisumbue,
kwani mimi sistahili wewe kuingia chini ya
dari yangu. 7 Ndiyo maana sikujiona hata
ninastahili kuja kwako wewe. Lakini sema
neno tu, naye mtumishi wangu atapona. 8 Kwa
kuwa mimi mwenyewe ni mtu niliyewekwa
chini ya mamlaka, nikiwa na askari chini yangu.
Nikimwambia huyu, ‘Nenda,’ yeye huenda;
na mwingine nikimwambia, ‘Njoo,’ yeye huja.
Nikimwambia mtumishi wangu, ‘Fanya hivi,’
yeye hufanya.”

9 Yesu aliposikia maneno haya, alishangazwa
naye sana. Akaugeukia ule umati wa watu
uliokuwa unamfuata, akawaambia, “Sijaona

imani kubwa namna hii hata katika Israeli.”
10 Nao wale watu waliokuwa wametumwa kwa
Yesu waliporudi nyumbani walimkuta yule mtu-
mishi amepona.

### *Yesu Amfufua Mwana Wa Mjane*

11 Baadaye kidogo, Yesu alikwenda katika mji
mmoja ulioitwa Naini. Nao wanafunzi wake
na umati mkubwa wa watu walikwenda pamoja
naye. 12 Alipokaribia lango la mji, alikutana na
watu waliokuwa wamebeba maiti wakitoka nje
ya mji. Huyu aliyekufa alikuwa mwana pekee
wa mwanamke mjane. Umati mkubwa wa watu
wa mji ule ulikuwa pamoja na huyo mwanamke.
13 Bwana Yesu alipomwona yule mjane, moyo
wake ulimhurumia, akamwambia, “Usilie.”
14 Kisha akasogea mbele akaligusa lile jeneza
na wale waliokuwa wamelibeba wakasimama
kimya. Akasema, “Kijana, nakuambia inuka.”
15 Yule aliyekuwa amekufa akaketi akaanza
kuongea, naye Yesu akamkabidhi kwa mama
yake.
16 Watu wote wakajawa na hofu ya Mungu, nao
wakamtukuza Mungu wakisema, “Nabii mkuu
ametokea miongoni mwetu, Mungu amekuja
kuwakomboa watu wake.” 17 Habari hizi za
mambo aliyoyafanya Yesu zikaenea Uyahudi
wote na sehemu zote za jirani.

### *Yesu Na Yohana Mbatizaji (Mathayo 11:2-19)*

18 Wanafunzi wa Yohana Mbatizaji
wakamweleza Yohana mambo haya yote. Hivyo
Yohana akawaita wanafunzi wake wawili

19 na kuwatuma kwa Bwana ili kumuuliza,
“Wewe ndiye yule aliyekuwa aje, au tumngojee
mwingine?”
20 Wale watu walipofika kwa Yesu
wakamwambia, “Yohana Mbatizaji ametutuma tukuulize, ‘Wewe ndiye yule aliyekuwa aje, au tumngojee mwingine?’ ”
21 Wakati huo huo, Yesu aliwaponya wengi
waliokuwa na magonjwa, maradhi na pepo
wachafu, na pia akawafungua vipofu wengi
macho wakapata kuona. 22 Hivyo akawajibu
wale wajumbe, “Rudini mkamwambie Yohana yote mnayoyaona na kuyasikia: Vipofu wanapata kuona, viwete wanatembea, wenye ukoma wanatakaswa, viziwi wanasikia, wafu wanafufuliwa na maskini wanahubiriwa habari njema.
23 Amebarikiwa mtu yule asiyechukizwa na
mimi.”
24 Wajumbe wa Yohana walipoondoka, Yesu
akaanza kusema na makutano kuhusu Yohana Mbatizaji. Akawauliza, “Mlipokwenda kule nyikani, mlikwenda kuona nini? Je, ni unyasi
ukipeperushwa na upepo? 25 Kama sivyo, mlik-
wenda kuona nini basi? Mtu aliyevaa mavazi ya kifahari? La hasha, watu wanaovaa mavazi ya kifahari na kuishi maisha ya anasa wako
katika majumba ya kifalme. 26 Lakini mlikwenda
kuona nini? Mlikwenda kumwona nabii? Naam,
nawaambia, yeye ni zaidi ya nabii. 27 Huyu ndiye
ambaye habari zake zimeandikwa:

“ ‘Tazama, nitamtuma mjumbe wangu mbele yako,
atakayetengeneza njia mbele yako.’

28 Nawaambia, miongoni mwa wale waliozaliwa na wanawake, hakuna aliye mkuu kuliko Yohana. Lakini yeye aliye mdogo kabisa katika Ufalme wa Mungu ni mkuu kuliko Yohana.”

29 (Watu wote hata watoza ushuru waliposikia
maneno ya Yesu, walikubali kwamba mpango
wa Mungu ni haki, maana walikuwa wame-
batizwa na Yohana. 30 Lakini Mafarisayo na
wataalamu wa sheria walikataa mpango wa Mungu kwao kwa kutokubali kubatizwa na Yohana.)

31 Yesu akawauliza, “Niwafananishe na nini
watu wa kizazi hiki? Wanafanana na nini?
32 Wao ni kama watoto waliokaa sokoni wakiitana wao kwa wao, wakisema:

“ ‘Tuliwapigia filimbi,
lakini hamkucheza;
tuliwaimbia nyimbo za maombolezo,
lakini hamkulia.’

33 Kwa maana Yohana Mbatizaji alikuja, alikuwa
hali mkate wala hanywi divai, nanyi mkasema,
‘Yeye ana pepo mchafu.’ 34 Mwana wa Adamu
alikuja akila na kunywa, nanyi mnasema: ‘Tazameni huyu mlafi na mlevi, rafiki wa watoza
ushuru na “wenye dhambi.”’ 35 Nayo hekima
huthibitishwa kuwa kweli na watoto wake wote.”

*Yesu Apakwa Mafuta Na Mwanamke Mwenye Dhambi*

36 Basi Farisayo mmoja alimwalika Yesu nyumbani kwake kwa chakula. Hivyo Yesu akaenda nyumbani mwa yule Farisayo na kukaa katika
nafasi yake mezani. 37 Naye mwanamke mmoja

kwenye ule mji, ambaye alikuwa mwenye dhambi, alipojua kwamba Yesu alikuwa akila chakula nyumbani kwa yule Farisayo, akaleta chupa ya marhamu yenye manukato.
38 Yule mwanamke akasimama nyuma ya miguu ya Yesu akilia. Akailowanisha miguu yake kwa machozi yake, kisha akaifuta kwa nywele zake, akaibusu na kuimiminia manukato.

39 Yule Farisayo aliyemwalika Yesu alipoona yanayotendeka, akawaza moyoni mwake, "Kama huyu mtu angekuwa nabii, angejua kwamba ni nani anayemgusa, na kwamba yeye ni mwanamke wa namna gani, na ya kuwa huyu mwanamke ni mwenye dhambi."

40 Yesu akanena akamwambia, "Simoni, nina jambo la kukuambia."

Simoni akajibu, "Mwalimu, sema."

41 "Palikuwa na mtu mmoja aliyewakopesha watu wawili fedha: Mmoja alidaiwa dinari 500*na mwingine dinari hamsini.
42 Wote wawili walipokuwa hawawezi kulipa, aliyafuta madeni yao wote wawili. Sasa ni yupi kati yao atakayempenda yule aliyewasamehe zaidi?"

43 Simoni akajibu, "Nadhani ni yule aliyesamehewa deni kubwa zaidi."

Naye Yesu akamwambia, "Umehukumu kwa usahihi."

44 Kisha akamgeukia yule mwanamke, akamwambia Simoni, "Je, unamwona mwanamke huyu? Nilipoingia nyumbani mwako, hukunipa maji ya kunawa miguu

---

* **7:41** Dinari 500 ni sawa na mshahara wa kibarua wa siku mia tano.

yangu, lakini huyu ameninawisha miguu
kwa machozi yake, na kunifuta kwa nywele
zake. 45 Hukunisalimu kwa busu, lakini huyu
mwanamke hajaacha kuibusu miguu yangu
tangu nilipoingia. 46 Hukunipaka mafuta
kichwani mwangu, lakini yeye ameipaka miguu
yangu manukato. 47 Kwa hiyo, nakuambia,
dhambi zake zilizokuwa nyingi zimesamehewa,
kwani ameonyesha upendo mwingi. Lakini yule
aliyesamehewa kidogo, hupenda kidogo."

48 Kisha akamwambia yule mwanamke,
"Dhambi zako zimesamehewa."

49 Lakini wale waliokuwa wameketi pamoja
naye chakulani wakaanza kusemezana wao kwa
wao, "Huyu ni nani ambaye hata anasamehe
dhambi?"

50 Yesu akamwambia yule mwanamke, "Imani
yako imekuokoa; nenda kwa amani."

# 8

*Mfano Wa Mpanzi*
*(Mathayo 13:1-9; Marko 4:1-9)*

1 Baada ya haya Yesu alikwenda, akawa
anazunguka katika miji na vijiji akihubiri habari
njema za Ufalme wa Mungu. Wale wanafunzi
wake kumi na wawili walikuwa pamoja naye,
2 pia baadhi ya wanawake waliokuwa wame-
tolewa pepo wachafu na kuponywa magonjwa.
Miongoni mwao alikuwepo Maria Magdalene,
aliyetolewa pepo wachafu saba; 3 Yoana mkewe
Kuza, msimamizi wa nyumba ya watu wa nyum-
bani mwa Herode; Susana; na wengine wengi
waliokuwa wakimhudumia kwa mali zao.

[4] Umati mkubwa wa watu ulipokuwa ukija
kwa Yesu kutoka kila mji, akawaambia mfano
huu: [5] “Mpanzi alitoka kwenda kupanda mbegu
zake. Alipokuwa akitawanya mbegu, nyingine
zilianguka kando ya njia; zikakanyagwa, nao
ndege wa angani wakazila. [6] Mbegu nyingine
zilianguka penye miamba, nazo zilipoota, hiyo
mimea ikakauka kwa kukosa unyevu. [7] Nazo
mbegu nyingine zilianguka kwenye miiba, nayo
ile miiba ikakua pamoja nazo, na kuisonga hiyo
mimea. [8] Mbegu nyingine zilianguka kwenye
udongo mzuri. Zikaota na kuzaa mara mia moja
zaidi ya mbegu alizopanda.”

Baada ya kusema haya, Yesu akapaza sauti, akasema, “Mwenye masikio ya kusikia, na asikie.”

[9] Wanafunzi wake wakamuuliza maana ya
mfano huo. [10] Naye akasema, “Ninyi mmepewa
kufahamu siri za Ufalme wa Mungu, lakini kwa
wengine nazungumza kwa mifano, ili,

“ ‘ingawa wanatazama, wasione;
ingawa wanasikiliza, wasielewe.’

[11] “Maana ya mfano huu ni hii: Mbegu ni neno
la Mungu. [12] Zile zilizoanguka kando ya njia ni
wale ambao husikia neno, naye ibilisi anakuja
na kuliondoa neno kutoka mioyoni mwao, ili
wasije wakaamini na kuokoka. [13] Zile mbegu
zilizoanguka kwenye mwamba ni wale ambao
hulipokea neno kwa furaha wanapolisikia, lakini
hawana mizizi. Wanaamini kwa muda mfupi,
lakini wakati wa kujaribiwa huiacha imani.
[14] Zile mbegu zilizoanguka kwenye miiba ni

mfano wa wale wanaosikia, lakini wanapoende-
lea husongwa na masumbufu ya maisha haya,
utajiri na anasa, nao hawakui. 15 Lakini zile
mbegu zilizoanguka kwenye udongo mzuri ni
mfano wa wale ambao hulisikia neno la Mungu
na kulishika kwa moyo mnyofu wa utiifu, nao
kwa kuvumilia kwingi huzaa matunda.

### *Mfano Wa Taa*
*(Marko 4:21-25)*

16 “Hakuna mtu awashaye taa na kuificha
ndani ya gudulia au kuiweka mvunguni mwa
kitanda. Badala yake, huiweka juu ya kinara,
ili wale waingiao ndani waone mwanga. 17 Kwa
maana hakuna jambo lolote lililofichika ambalo
halitafichuliwa, wala lolote lililositirika ambalo
halitajulikana na kuwekwa wazi. 18 Kwa hiyo,
kuweni waangalifu mnavyosikia. Kwa maana
yeyote aliye na kitu atapewa zaidi. Lakini yule
asiye na kitu, hata kile anachodhani anacho
atanyang’anywa.”

### *Mama Yake Yesu Na Ndugu Zake*
*(Mathayo 12:46-50; Marko 3:31-35)*

19 Wakati mmoja mama yake Yesu na ndugu
zake walikuja kumwona, lakini hawakuweza
kumfikia kwa sababu ya msongamano wa watu.
20 Mtu mmoja akamwambia, “Mama yako na
ndugu zako wako nje wanataka kukuona.”

21 Yesu akamjibu, “Mama yangu na ndugu
zangu ni wale wote wanaolisikia neno la Mungu
na kulifanya.”

### *Yesu Atuliza Dhoruba*
### *(Mathayo 8:23-27; Marko 4:35-41)*

22 Siku moja Yesu alipanda ndani ya mashua
pamoja na wanafunzi wake, akawaambia, “Tu-
vukeni twende mpaka ng’ambo ya ziwa.” Nao
wakaondoka. 23 Hivyo walipokuwa wakienda,
akalala usingizi. Dhoruba kali ikatokea mle
ziwani, hata mashua ikawa inajaa maji, nao
walikuwa katika hatari kubwa.

24 Wanafunzi wake wakamwendea na
kumwamsha, wakisema, “Bwana, Bwana,
tunaangamia!”

Yeye akaamka, akaukemea ule upepo na
yale mawimbi; dhoruba ikakoma, nako kukawa
shwari. 25 Akawauliza wanafunzi wake, “Imani
yenu iko wapi?”

Kwa woga na mshangao wakaulizana, “Huyu
ni nani, ambaye anaamuru hata upepo na maji,
navyo vikamtii?”

### *Yesu Amponya Mtu Mwenye Pepo Mchafu*
### *(Mathayo 8:28-34; Marko 5:1-20)*

26 Basi wakafika katika nchi ya Wagerasi,
ambayo iko upande wa pili wa ziwa kutoka
Galilaya. 27 Yesu aliposhuka kutoka mashua na
kukanyaga ufuoni, alikutana na mtu mmoja wa
mji ule aliyekuwa amepagawa na pepo mchafu,
naye kwa muda mrefu alikuwa havai nguo
wala kuishi nyumbani, bali aliishi makaburini.
28 Alipomwona Yesu, alipiga kelele, akajitupa
chini mbele yake na kusema kwa sauti kuu, “Una
nini nami, Yesu, Mwana wa Mungu Aliye Juu
Sana? Nakuomba, usinitese!” 29 Wakati huo
Yesu alikuwa amemwamuru yule pepo mchafu

amtoke huyo mtu. Mara nyingi huyo pepo
mchafu alimpagaa, na hata alipofungwa kwa
minyororo mikono na miguu na kuwekwa chini
ya ulinzi, alikata hiyo minyororo na kupelekwa
na huyo pepo mchafu kwenda nyikani.
30 Yesu akamuuliza, “Jina lako ni nani?”

Akamjibu, “Legioni,”* kwa kuwa alikuwa
ameingiwa na pepo wachafu wengi mno. 31 Wale
pepo wachafu wakamsihi sana asiwaamuru
kwenda katika Shimo.†
32 Palikuwa na kundi kubwa la nguruwe hapo
likilisha kando ya kilima. Wale pepo wachafu
wakamsihi Yesu awaruhusu wawaingie hao ngu-
ruwe, naye akawaruhusu. 33 Wale pepo wachafu
walipomtoka yule mtu, wakawaingia wale ngu-
ruwe, nalo kundi lote likateremkia gengeni kwa
kasi, likatumbukia ziwani na kuzama.
34 Wale watu waliokuwa wakichunga lile
kundi la nguruwe walipoona yaliyotukia,
wakakimbia, wakaeneza habari hizi mjini na
mashambani. 35 Nao watu wakatoka kwenda
kujionea wenyewe yaliyotukia. Walipofika
hapo alipokuwa Yesu, wakamkuta yule mtu
aliyetokwa na pepo wachafu amekaa karibu
na Yesu, akiwa amevaa nguo na mwenye akili
timamu! Wakaogopa. 36 Wale walioyaona
mambo hayo wakawaeleza watu wengine
jinsi yule mtu aliyekuwa amepagawa na
pepo wachafu alivyoponywa. 37 Ndipo watu
wote wa nchi ile ya Wagerasi wakamwomba

* **8:30** Legioni maana yake ni Jeshi. † **8:31** Shimo hapa ina maana Abyss (shimo lisilo na mwisho), yaani Kuzimu; kwa Kiebrania ni Sheol.

Yesu aondoke kwao, kwa sababu walikuwa wamejawa na hofu. Basi akaingia katika mashua, akaondoka zake.
38 Yule mtu aliyetokwa na pepo wachafu akam-
sihi Yesu afuatane naye, lakini Yesu akamuaga,
akamwambia: 39 "Rudi nyumbani ukawaeleze
mambo makuu Mungu aliyokutendea." Kwa hiyo yule mtu akaenda, akatangaza katika mji wote mambo makuu ambayo Yesu alimtendea.

### *Msichana Afufuliwa, Na Mwanamke Aponywa (Mathayo 9:18-26; Marko 5:21-43)*

40 Basi Yesu aliporudi, umati mkubwa wa
watu ukampokea kwa furaha, kwani walikuwa
wakimngojea. 41 Kisha mtu mmoja, jina lake
Yairo, aliyekuwa kiongozi wa sinagogi, akaja na
kuanguka miguuni mwa Yesu, akimwomba afike
nyumbani kwake, 42 kwa kuwa binti yake wa
pekee, mwenye umri wa miaka kumi na miwili, alikuwa anakufa.

Yesu alipokuwa akienda, umati wa watu
ukamsonga sana. 43 Katika umati huo palikuwa
na mwanamke mmoja aliyekuwa na tatizo la kutokwa damu kwa muda wa miaka kumi na miwili. Tena alikuwa amegharimia yote aliyokuwa nayo kwa ajili ya matibabu, wala hakuna yeyote
aliyeweza kumponya. 44 Huyo mwanamke akaja
kwa nyuma ya Yesu na kugusa upindo wa vazi lake. Mara kutokwa damu kwake kukakoma.
45 Yesu akauliza, "Ni nani aliyenigusa?"

Watu wote walipokana, Petro akasema, "Bwana, huu umati wa watu unakusonga na kukusukuma kila upande."

46 Lakini Yesu akasema, "Kuna mtu aliyeni-
gusa, kwa maana nimetambua kuwa nguvu
zimenitoka."

47 Yule mwanamke alipofahamu ya kuwa
hawezi kuendelea kujificha, alikuja akitetemeka,
akaanguka miguuni mwa Yesu. Akaeleza mbele
ya watu wote kwa nini alimgusa na jinsi alivyo-
ponywa mara. 48 Basi Yesu akamwambia, "Binti,
imani yako imekuponya. Nenda kwa amani."

49 Yesu alipokuwa bado anasema, akaja mtu-
mishi kutoka nyumbani kwa Yairo, yule kiongozi
wa sinagogi, kumwambia, "Binti yako amek-
wisha kufa. Usiendelee kumsumbua Mwalimu."

50 Yesu aliposikia jambo hili, akamwambia
Yairo, "Usiogope. Amini tu, naye binti yako
atapona."

51 Walipofika nyumbani kwa Yairo, hakum-
ruhusu mtu yeyote aingie ndani naye isipokuwa
Petro, Yakobo na Yohana, pamoja na baba na
mama wa yule binti. 52 Wakati ule ule watu
wote walikuwa wakilia na kuomboleza kwa ajili
ya huyo binti. Yesu akawaambia, "Acheni kulia.
Huyu binti hajafa, ila amelala."

53 Wao wakamcheka kwa dharau, wakijua
kuwa amekwisha kufa. 54 Yesu akamshika yule
binti mkono na kuita, "Binti, amka!" 55 Roho
yake ikamrudia, naye akainuka mara moja.
Akaamuru apewe kitu cha kula. 56 Wazazi wake
wakastaajabu sana, lakini Yesu akawakataza
wasimwambie mtu yeyote juu ya yale yaliy-
otukia.

# 9

### *Yesu Awatuma Wale Kumi Na Wawili*
### *(Mathayo 10:5-15; Marko 6:7-13)*

1 Yesu kisha akawaita wale kumi na wawili
pamoja, akawapa mamlaka na uwezo wa kutoa
pepo wachafu wote na kuponya magonjwa yote,
2 kisha akawatuma waende wakahubiri Ufalme
wa Mungu na kuponya wagonjwa. 3 Akawaagiza
akisema, "Msichukue chochote safarini: sio
fimbo, wala mkoba, wala mkate, wala fedha,
hata msichukue kanzu ya ziada. 4 Katika
nyumba yoyote mwingiayo, kaeni humo hadi
mtakapoondoka katika mji huo. 5 Kama watu
wasipowakaribisha, mnapoondoka katika mji
wao, kung'uteni mavumbi kutoka kwenye miguu
yenu ili kuwa ushuhuda dhidi yao." 6 Hivyo wale
wanafunzi wakaondoka wakaenda kutoka kijiji
hadi kijiji, wakihubiri habari njema na kuponya
wagonjwa kila mahali.

### *Herode Afadhaika*
### *(Mathayo 14:1-12; Marko 6:14-29)*

7 Basi Mfalme Herode, mtawala wa Galilaya,
alisikia habari za yote yaliyotendeka. Naye
akafadhaika, kwa kuwa baadhi ya watu wa-
likuwa wakisema Yohana Mbatizaji amefufuliwa
kutoka kwa wafu. 8 Wengine wakasema Eliya
amewatokea, na wengine wakasema kwamba
mmoja wa manabii wa kale amefufuka. 9 Herode
akasema, "Yohana nilimkata kichwa. Lakini ni
nani huyu ambaye ninasikia mambo kama haya
kumhusu?" Akatamani sana kumwona.

*Yesu Awalisha Wanaume 5,000*
*(Mathayo 14:13-21; Marko 6:30-44; Yohana 6:1-14)*

10 Mitume wake waliporudi, wakamweleza
Yesu yote waliyofanya. Akawachukua, akaenda
nao faraghani mpaka mji uitwao Bethsaida.
11 Lakini umati wa watu ukafahamu alikok-
wenda, ukamfuata. Akawakaribisha na kunena
nao kuhusu Ufalme wa Mungu na kuwaponya
wale wote waliokuwa wanahitaji uponyaji.

12 Ilipokaribia jioni, wale mitume kumi na wawili wakaenda kwa Yesu na kumwambia, "Waage makutano ili waende vijijini jirani na mashambani, ili wapate chakula na mahali pa kulala, kwa maana hapa tuko nyikani."

13 Yesu akawajibu, "Ninyi wapeni chakula."

Nao wakajibu, "Hatuna zaidi ya mikate mi-
tano na samaki wawili. Labda twende tuka-
nunue chakula cha kuwatosha watu hawa wote."
14 Walikuwako wanaume wapatao 5,000.

Yesu akawaambia wanafunzi wake,
"Waketisheni katika makundi ya watu hamsini
hamsini." 15 Wanafunzi wakafanya hivyo,
wakawaketisha wote. 16 Yesu akaichukua
ile mikate mitano na wale samaki wawili,
akatazama mbinguni, akavibariki na kuvimega.
Kisha akawapa wanafunzi ili wawagawie watu.
17 Wote wakala, wakashiba. Nao wanafunzi
wakakusanya vipande vilivyosalia, wakajaza
vikapu kumi na viwili.

*Petro Amkiri Yesu Kuwa Ndiye Kristo*
*(Mathayo 16:13-19; Marko 8:27-29)*

18 Wakati mmoja, Yesu alipokuwa akiomba
faraghani, nao wanafunzi wake wakiwa pamoja
naye, akawauliza, "Watu husema mimi ni nani?"
19 Wakamjibu, "Baadhi husema wewe ni
Yohana Mbatizaji, wengine husema ni Eliya, na
bado wengine husema kwamba ni mmoja wa
manabii wa kale amefufuka kutoka kwa wafu."
20 Kisha akawauliza, "Je, ninyi mnasema mimi
ni nani?"

Petro akajibu, "Wewe ndiwe Kristo* wa
Mungu."
21 Yesu akawakataza wasimwambie mtu yey-
ote jambo hilo. 22 Yesu akasema, "Imempasa
Mwana wa Adamu kupata mateso mengi na
kukataliwa na wazee, viongozi wa makuhani, na
walimu wa sheria, na itampasa auawe, lakini
siku ya tatu kufufuliwa kutoka mauti."
23 Kisha akawaambia wote, "Mtu yeyote
akitaka kunifuata, ni lazima ajikane mwenyewe,
auchukue msalaba wake kila siku, anifuate.
24 Kwa maana yeyote anayetaka kuyaokoa
maisha yake atayapoteza, lakini yeyote
atakayeyapoteza maisha yake kwa ajili
yangu atayaokoa. 25 Je, itamfaidi nini mtu
kuupata ulimwengu wote, lakini akapoteza
au kuangamiza nafsi yake? 26 Mtu yeyote
akinionea aibu mimi na maneno yangu, Mwana
wa Adamu naye atamwonea aibu atakapokuja
katika utukufu wake na katika utukufu wa
Baba, pamoja na malaika watakatifu. 27 Amin,
nawaambia, wako baadhi ya watu waliosimama

* **9:20** Kristo maana yake ni Masiya, yaani Aliyetiwa mafuta.

hapa ambao hawataonja mauti kabla ya kuuona
Ufalme wa Mungu.”

### *Bwana Yesu Abadilika Sura (Mathayo 17:1-8; Marko 9:2-8)*

28 Yapata siku nane baada ya Yesu kusema
hayo, aliwachukua Petro, Yakobo na Yohana,
akaenda nao mlimani kuomba. 29 Alipokuwa
akiomba, sura ya uso wake ikabadilika, nayo
mavazi yake yakametameta kama mwanga wa
umeme wa radi. 30 Ghafula wakawaona watu
wawili, ndio Mose na Eliya, wakizungumza
naye. 31 Walionekana katika utukufu wak-
izungumza na Yesu kuhusu kifo chake amba-
cho kingetokea huko Yerusalemu. 32 Petro na
wenzake walikuwa wamelala usingizi mzito.
Walipoamka, wakaona utukufu wa Yesu na wale
watu wawili waliokuwa wamesimama pamoja
naye. 33 Mose na Eliya walipokuwa wanaondoka,
Petro akamwambia Yesu, “Bwana, ni vizuri
tukae hapa! Tutajenga vibanda vitatu: kimoja
chako, kingine cha Mose na kingine cha Eliya.”
Lakini Petro alikuwa hajui asemacho.

34 Alipokuwa bado anazungumza, pakatokea
wingu, likawafunika, nao wakaogopa
walipoingia mle kwenye wingu. 35 Sauti ikatoka
kwenye lile wingu ikisema, “Huyu ni Mwanangu
mpendwa, niliyemchagua. Msikieni yeye.”
36 Baada ya sauti hiyo kusema, walimkuta
Yesu akiwa peke yake. Wale wanafunzi
wakalihifadhi jambo hili, wala kwa wakati huo
hawakumwambia mtu yeyote yale waliyokuwa
wameyaona.

### *Kuponywa Kwa Kijana Mwenye Pepo Mchafu (Mathayo 17:1-8; Marko 9:2-8)*

37 Kesho yake waliposhuka kutoka mlimani,
alikutana na umati mkubwa wa watu. 38 Mtu
mmoja katika ule umati wa watu akapaza
sauti, akasema, “Mwalimu, naomba umwangalie
mwanangu, kwani ndiye mtoto wangu wa pekee.
39 Mara kwa mara pepo mchafu humpagaa na
kumfanya apige kelele, kisha humwangusha na
kumtia kifafa hata akatokwa na povu kiny-
wani. Huyo pepo mchafu anamtesa sana, na
hamwachi ila mara chache. 40 Niliwaomba
wanafunzi wako wamtoe huyo pepo mchafu,
lakini hawakuweza.”

41 Yesu akawajibu, “Enyi kizazi kisichoamini
na kilichopotoka! Nitakaa nanyi na kuwavumilia
mpaka lini? Mlete mwanao hapa.”

42 Hata yule mtoto alipokuwa akija, yule pepo
mchafu akamwangusha, akamtia kifafa. Lakini
Yesu akamkemea yule pepo mchafu amtoke,
akamponya yule mtoto, na akamrudisha kwa
baba yake. 43 Watu wote wakastaajabia uweza
mkuu wa Mungu.

Wakati bado watu walikuwa wanastaajabia
hayo yote aliyokuwa akiyafanya Yesu, yeye
akawaambia wanafunzi wake: 44 “Sikilizeni kwa
makini haya nitakayowaambia sasa: Mwana wa
Adamu atasalitiwa na kutiwa mikononi mwa
watu.” 45 Lakini wao hawakuelewa alimaan-
isha nini. Maana ya maneno hayo ilifichika
kwao, hivyo hawakuyaelewa, nao wakaogopa
kumuuliza maana yake.

### *Ni Nani Atakayekuwa Mkubwa Kuliko Wote (Mathayo 18:1-5; Marko 9:33-37)*

46 Kukazuka mabishano miongoni mwa
wanafunzi kuhusu ni nani miongoni mwao
atakayekuwa mkuu kuliko wote. 47 Lakini Yesu
akayatambua mawazo yao, naye akamchukua
mtoto mdogo, akamsimamisha kando yake.
48 Kisha akawaambia, “Yeyote amkaribishaye
mtoto huyu mdogo kwa Jina langu, anikaribisha
mimi, na yeyote atakayenikaribisha mimi,
atakuwa amemkaribisha yeye aliyenituma.
Kwa maana yeye aliye mdogo miongoni mwenu,
ndiye aliye mkuu kuliko wote.”

49 Yohana akasema, “Bwana, tumemwona
mtu akitoa pepo wachafu kwa jina lako, nasi
tukamzuia, kwa sababu yeye si mmoja wetu.”

50 Yesu akasema, “Msimzuie, kwa sababu yey-
ote ambaye si kinyume nanyi, yu upande wenu.”

### *Yesu Akataliwa Samaria*

51 Wakati ulipokaribia wa yeye kuchukuliwa
mbinguni, alikaza uso wake kwenda
Yerusalemu. 52 Akatuma watu wamtangulie,
nao wakaenda katika kijiji kimoja cha Samaria
kumwandalia kila kitu; 53 lakini watu wa kijiji
kile hawakumkaribisha kwa sababu alikuwa
anakwenda zake Yerusalemu. 54 Wanafunzi
wake, yaani Yakobo na Yohana, walipoona hayo,
wakasema: “Bwana, unataka tuagize moto
kutoka mbinguni ili uwaangamize?” 55 Yesu
akageuka na kuwakemea, 56 nao wakaenda kijiji
kingine.

*Gharama Ya Kumfuata Yesu*
*(Mathayo 8:19-22)*

57 Walipokuwa njiani wakienda, mtu mmoja akamwambia Yesu, “Nitakufuata kokote uendako.”

58 Yesu akamjibu, “Mbweha wana mapango, nao ndege wa angani wana viota, lakini Mwana wa Adamu hana mahali pa kulaza kichwa chake.”

59 Yesu akamwambia mtu mwingine, “Nifuate.”

Mtu huyo akamjibu, “Bwana, niruhusu kwanza nikamzike baba yangu.”

60 Yesu akamwambia, “Waache wafu wawazike wafu wao, bali wewe nenda ukautangaze Ufalme wa Mungu.”

61 Mtu mwingine akamwambia, “Bwana, nitakufuata lakini naomba kwanza nikawaage jamaa yangu.”

62 Yesu akamwambia, “Mtu yeyote atiaye mkono wake kulima, kisha akatazama nyuma, hafai kwa Ufalme wa Mungu.”

# 10

*Yesu Awatuma Wale Sabini Na Wawili*

1 Baada ya hayo, Bwana akawachagua wengine
sabini na wawili, akawatuma wawili wawili
katika kila mji na kila sehemu aliyokusudia
kwenda baadaye. 2 Akawaambia, “Mavuno ni
mengi, lakini watendakazi ni wachache. Kwa
hiyo mwombeni Bwana wa mavuno, ili apeleke
watendakazi katika shamba lake la mavuno.

3 Haya! nendeni. Ninawatuma kama wana-
kondoo katikati ya mbwa mwitu. 4 Msichukue
mkoba, wala mfuko, wala viatu, na msimsalimu
mtu yeyote njiani.
5 “Mkiingia katika nyumba yoyote, kwanza
semeni, ‘Amani iwe kwenu.’ 6 Kama kuna mtu
wa amani humo, basi amani yenu itakuwa juu
yake. La sivyo, itawarudia. 7 Kaeni katika
nyumba hiyo, mkila na kunywa kile wataka-
chowapa, kwa sababu kila mtendakazi anastahili
malipo yake. Msihamehame kutoka nyumba
hadi nyumba.
8 “Mkienda katika mji na watu wake
wakawakaribisha, kuleni chochote kiwekwacho
mbele yenu, 9 waponyeni wagonjwa
waliomo na waambieni: ‘Ufalme wa Mungu
umekaribia.’ 10 Lakini mkiingia katika mji,
nao hawakuwakaribisha, tokeni mwende katika
barabara zake mkaseme: 11 ‘Hata mavumbi ya
mji wenu yaliyoshikamana na miguu yetu,
tunayakung’uta dhidi yenu. Lakini mjue
kwamba Ufalme wa Mungu umekaribia.’
12 Ninawaambia, itakuwa rahisi zaidi kwa
Sodoma kustahimili katika siku ile kuliko mji
ule.

*Onyo Kwa Miji Isiyotubu*
*(Mathayo 11:20-24)*

13 “Ole wako Korazini! Ole wako Bethsaida!
Kwa kuwa kama miujiza iliyofanyika kwenu
ingefanyika Tiro na Sidoni, miji hiyo ingekuwa
imetubu zamani, kwa kuvaa magunia na ku-
jipaka majivu. 14 Lakini itakuwa rahisi zaidi
kwa Tiro na Sidoni kustahimili katika siku ya

hukumu, kuliko ninyi. [15] Nawe, Kapernaumu,
je, utainuliwa hadi mbinguni? La hasha,
utashushwa mpaka kuzimu."
[16] "Yeye awasikilizaye ninyi anisikiliza mimi;
naye awakataaye ninyi amenikataa mimi. Lakini
yeye anikataaye mimi amkataa yeye aliyeni-
tuma."
[17] Wale sabini na wawili wakarudi kwa furaha,
na kusema, "Bwana, hata pepo wachafu wanatu-
tii kwa jina lako."
[18] Yesu akawaambia, "Nilimwona Shetani
akianguka kutoka mbinguni kama umeme wa
radi. [19] Tazama nimewapa mamlaka ya
kukanyaga nyoka na nge na juu ya nguvu zote za
adui; wala hakuna kitu chochote kitakachowad-
huru. [20] Basi, msifurahi kwa kuwa pepo wachafu
wanawatii, bali furahini kwa kuwa majina yenu
yameandikwa mbinguni."

### *Yesu Anashangilia*
### *(Mathayo 11:25-27; 13:16-17)*

[21] Wakati huo Yesu akashangilia katika Roho
Mtakatifu, akasema, "Nakuhimidi Baba, Bwana
wa mbingu na nchi, kwa kuwa umewaficha
mambo haya wenye hekima na wenye elimu,
nawe ukawafunulia watoto wadogo. Naam,
Baba, kwa kuwa hivyo ndivyo ilivyokupendeza.
[22] "Nimekabidhiwa vitu vyote na Baba yangu.
Hakuna mtu amjuaye Mwana ni nani ila Baba,
wala hakuna amjuaye Baba ni nani ila Mwana na
yeyote ambaye Mwana anapenda kumfunulia."
[23] Basi Yesu akawageukia wanafunzi wake
akanena nao faraghani, akawaambia, "Heri

macho yanayoona yale mambo mnayoyaona.
24 Kwa maana nawaambia, manabii wengi na
wafalme walitamani kuona yale mnayoyaona
lakini hawakuyaona, na walitamani kusikia yale
mnayoyasikia lakini hawakuyasikia.”

### *Mfano Wa Msamaria Mwema*

25 Wakati huo mtaalamu mmoja wa sheria alisimama ili kumjaribu Yesu, akamuuliza, “Mwalimu, nifanye nini ili niurithi uzima wa milele?”

26 Yesu akamjibu, “Imeandikwaje katika Sheria? Kwani unasoma nini humo?”

27 Akajibu, “ ‘Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote, kwa nguvu zako zote, na kwa akili zako zote’; tena, ‘Mpende jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe.’ ”

28 Yesu akamwambia, “Umejibu vyema. Fanya hivyo nawe utaishi.”

29 Lakini yule mtaalamu wa sheria, akitaka kujionyesha kuwa mwenye haki, akamuuliza Yesu, “Jirani yangu ni nani?”

30 Yesu akamjibu akasema, “Mtu mmoja
alikuwa akiteremka kutoka Yerusalemu kwenda
Yeriko, naye akaangukia mikononi mwa
wanyang’anyi. Wakampiga, wakaondoka,
wakamwacha akiwa karibu kufa. 31 Kuhani
mmoja alikuwa akipitia njia ile, alipomwona
huyo mtu, akapita upande mwingine,
akamwacha hapo barabarani. 32 Vivyo
hivyo, Mlawi mmoja naye alipofika mahali
pale, alimwona, akapita upande mwingine,
akamwacha hapo barabarani 33 Lakini Msamaria

mmoja aliyekuwa akisafiri alipomwona,
alimhurumia. 34 Akaenda alipokuwa na
akasafisha majeraha yake kwa divai na mafuta,
kisha akayafunga. Ndipo akampandisha kwenye
punda wake, akampeleka mpaka kwenye
nyumba ya wageni na kumtunza. 35 Kesho yake,
yule Msamaria akachukua dinari mbili*akampa
yule mwenye nyumba ya wageni na kusema,
'Mtunze, nami nirudipo nitakulipa gharama
yoyote ya ziada uliyotumia kwa ajili yake.'
36 "Ni yupi basi miongoni mwa hawa watatu
wewe unadhani ni jirani yake yule mtu aliyean-
gukia mikononi mwa wanyang'anyi?"
37 Yule mtaalamu wa sheria akajibu, "Ni yule
aliyemhurumia."

Ndipo Yesu akamwambia, "Nenda, ukafanye vivyo hivyo."

### *Yesu Awatembelea Martha Na Maria*

38 Ikawa Yesu na wanafunzi wake walipokuwa
wakienda Yerusalemu, akaingia kwenye kijiji
kimoja ambapo mwanamke mmoja aliyeitwa
Martha alimkaribisha nyumbani kwake.
39 Martha alikuwa na mdogo wake aliyeitwa
Maria, ambaye aliketi chini miguuni mwa Bwana
akisikiliza yale aliyokuwa akisema. 40 Lakini
Martha alikuwa akihangaika na maandalizi yote
yaliyokuwa yafanyike. Martha akaja kwa Yesu
na kumuuliza, "Bwana, hujali kwamba ndugu
yangu ameniachia kazi zote mwenyewe? Basi
mwambie anisaidie."

---

* **10:35** Dinari mbili ni sawa na mshahara wa kibarua wa siku mbili.

41 Lakini Bwana akamjibu, “Martha, Martha,
mbona unasumbuka na kuhangaika na mengi?
42 Lakini kunahitajika kitu kimoja tu. Maria
amechagua kile kilicho bora, wala hakuna mtu
atakayemwondolea.”

# 11

*Yesu Afundisha Wanafunzi Wake Kuomba*
*(Mathayo 6:9-13; 7:7-11)*

1 Siku moja, Yesu alikuwa mahali fulani
akiomba. Alipomaliza kuomba, mmoja wa
wanafunzi wake akamwambia, “Bwana, tu-
fundishe kuomba, kama vile Yohana alivyowa-
fundisha wanafunzi wake.”
2 Akawaambia, “Mnapoomba, semeni:

“ ‘Baba yetu (uliye mbinguni),
jina lako litukuzwe,
ufalme wako uje.
(Mapenzi yako yafanyike
hapa duniani kama huko mbinguni.)
3 Utupatie kila siku riziki yetu.
4 Utusamehe dhambi zetu,
kwa kuwa na sisi huwasamehe wote wanao-
tukosea.
Wala usitutie majaribuni
(bali utuokoe kutoka kwa yule mwovu).’ ”

5 Kisha akawaambia, “Ni nani miongoni
mwenu mwenye rafiki yake, naye akamwen-
dea usiku wa manane na kumwambia, ‘Rafiki,
nikopeshe mikate mitatu. 6 Kwa sababu rafiki
yangu amekuja kutoka safarini, nami sina kitu
cha kumpa.’

7 “Kisha yule aliyeko ndani amjibu, ‘Usin-
isumbue. Mlango umefungwa, nami na wa-
toto wangu tumelala. Siwezi kuamka nikupe
chochote.’ 8 Nawaambia, ingawa huyo mtu
hataamka na kumpa hiyo mikate kwa sababu
ni rafiki yake, lakini kwa sababu ya kuendelea
kwake kuomba, ataamka na kumpa kiasi ana-
chohitaji.

9 “Kwa hiyo nawaambia: Ombeni nanyi
mtapewa; tafuteni nanyi mtapata; bisheni nanyi
mtafunguliwa mlango. 10 Kwa kuwa kila aom-
baye hupewa; naye kila atafutaye hupata; na kila
abishaye hufunguliwa mlango.

11 “Je, kuna yeyote miongoni mwenu ambaye
mtoto wake akimwomba samaki, atampa nyoka
badala yake? 12 Au mtoto akimwomba yai
atampa nge? 13 Basi ikiwa ninyi mlio waovu,
mnajua kuwapa watoto wenu vitu vizuri, si zaidi
sana Baba yenu aliye mbinguni atawapa Roho
Mtakatifu wale wamwombao!”

### *Yesu Na Beelzebuli*
### *(Mathayo 12:22-30; Marko 3:20-27)*

14 Basi Yesu alikuwa anamtoa pepo mchafu
kutoka kwa mtu aliyekuwa bubu. Yule
pepo mchafu alipomtoka yule mtu aliyekuwa
bubu, akaanza kuongea, nao umati wa watu
ukashangaa. 15 Lakini wengine wakasema, “Ana-
toa pepo wachafu kwa uwezo wa Beelzebuli,*
yule mkuu wa pepo wachafu wote.” 16 Wengine

* **11:15** Beelzebubu au Beelzebuli; ni mkuu wa pepo wachafu; pia 18, 19.

ili kumjaribu wakataka awaonyeshe ishara kutoka mbinguni.

17 Yesu akajua mawazo yao, naye akawaambia, “Kila ufalme ukigawanyika dhidi yake wenyewe huangamia. Nayo nyumba iliyogawanyika dhidi
yake yenyewe itaanguka.
18 Kama Shetani amegawanyika mwenyewe, ufalme wake utasimamaje? Nawaambia haya kwa sababu ninyi mnadai ya kuwa mimi ninatoa pepo wachafu
kwa uwezo wa Beelzebuli.
19 Kama mimi natoa pepo wachafu kwa nguvu za Beelzebuli, wafuasi wenu nao je, wao hutoa pepo wachafu kwa uwezo wa nani? Hivyo basi, wao ndio
watakaowahukumu.
20 Lakini kama mimi ninatoa pepo wachafu kwa kidole cha Mungu, basi Ufalme wa Mungu umewajia.

21 “Mtu mwenye nguvu aliyejifunga silaha anapoilinda nyumba yake, mali yake iko salama.
22 Lakini mtu mwenye nguvu zaidi kumliko akimshambulia na kumshinda, yeye humnyang’anya silaha zake zote alizozitegemea, na kuchukua nyara.

23 “Mtu asiyekuwa pamoja nami yu kinyume nami, na mtu ambaye hakusanyi pamoja nami, hutawanya.

### *Kurudi Kwa Pepo Mchafu (Mathayo 12:43-45)*

24 “Pepo mchafu amtokapo mtu, hutangatanga katika sehemu zisizo na maji akitafuta mahali pa kupumzika, lakini hapati. Ndipo husema, ‘Nitarudi kwenye nyumba yangu nilikotoka.’

25 Naye arudipo na kuikuta ile nyumba imefag-
iliwa na kupangwa vizuri, 26 ndipo huenda na
kuchukua pepo wachafu wengine saba wabaya
kuliko yeye mwenyewe, nao huingia na kukaa
humo. Nayo hali ya mwisho ya yule mtu huwa
ni mbaya kuliko ile ya kwanza."

27 Ikawa Yesu alipokuwa akisema hayo,
mwanamke mmoja katikati ya ule umati wa
watu akapaza sauti akasema, "Limebarikiwa
tumbo lililokuzaa na matiti uliyonyonya!"

28 Yesu akajibu, "Wamebarikiwa zaidi wale
wanaolisikia neno la Mungu na kulitii."

### *Ishara Ya Yona*
### *(Mathayo 12:38-42)*

29 Umati wa watu ulipokuwa unazidi
kuongezeka, Yesu akaendelea kusema, "Hiki
ni kizazi kiovu. Kinatafuta ishara, lakini
hakitapewa ishara yoyote isipokuwa ile ya
Yona. 30 Kwa maana kama vile Yona alivyokuwa
ishara kwa watu wa Ninawi, ndivyo Mwana
wa Adamu atakavyokuwa ishara kwa kizazi
hiki. 31 Malkia wa Kusini atasimama wakati wa
hukumu na kuwahukumu watu wa kizazi hiki.
Kwa kuwa yeye alikuja kutoka miisho ya dunia
ili kuisikiliza hekima ya Solomoni. Na hapa yupo
aliye mkuu kuliko Solomoni. 32 Siku ya hukumu,
watu wa Ninawi watasimama pamoja na kizazi
hiki na kukihukumu; kwa maana wao walitubu
waliposikia mahubiri ya Yona. Na tazama, hapa
yupo yeye aliye mkuu kuliko Yona.

### *Taa Ya Mwili*
### *(Mathayo 5:15; 6:22-23)*

33 “Hakuna mtu yeyote awashaye taa na kui-
weka mahali palipofichika au kuifunikia chini
ya bakuli. Badala yake huiweka juu ya kinara
chake, ili watu wote wanaoingia waone nuru.
34 Jicho lako ni taa ya mwili wako. Kama jicho
lako ni zima, mwili wako wote pia umejaa nuru.
Lakini kama jicho ni bovu, mwili wako wote pia
umejaa giza. 35 Kwa hiyo, hakikisha kwamba
nuru iliyoko ndani yako isiwe giza. 36 Basi ikiwa
mwili wako wote umejaa nuru, bila sehemu yake
yoyote kuwa gizani, basi utakuwa na nuru kama
vile taa ikuangazavyo kwa nuru yake.”

### *Yesu Awashutumu Mafarisayo Na Wanasheria (Mathayo 23:1-36; Marko 12:38-40)*

37 Yesu alipomaliza kuzungumza, Farisayo
mmoja alimwalika nyumbani mwake kwa
chakula. Yesu akaingia na kuketi katika sehemu
yake mezani. 38 Yule Farisayo akashangaa
kwamba Yesu hakunawa kwanza kabla ya kula.

39 Ndipo Bwana akamwambia, “Sasa, enyi
Mafarisayo, mnasafisha kikombe na sahani
kwa nje, lakini ndani mmejaa unyang’anyi na
uovu. 40 Enyi wapumbavu! Hamjui kuwa yeye
aliyetengeneza nje ndiye alitengeneza na ndani
pia? 41 Basi toeni sadaka ya vile mlivyo navyo,
na tazama, vitu vyote vitakuwa safi kwenu.

42 “Lakini ole wenu, Mafarisayo, kwa maana
mnampa Mungu zaka za mnanaa, mchicha na
kila aina ya mboga, lakini mnapuuza haki na
upendo wa Mungu. Iliwapasa kufanya haya ya
pili bila kupuuza hayo ya kwanza.

43 “Ole wenu Mafarisayo, kwa sababu ninyi
mnapenda kukalia viti vya mbele katika masi-
nagogi, na kusalimiwa kwa heshima masokoni.
44 “Ole wenu, kwa sababu ninyi ni kama
makaburi yasiyokuwa na alama, ambayo watu
huyakanyaga pasipo kujua.”
45 Mtaalamu mmoja wa sheria akamjibu,
akasema, “Mwalimu, unaposema mambo haya,
unatutukana na sisi pia.”
46 Yesu akamjibu, “Nanyi wataalamu wa she-
ria, ole wenu, kwa sababu mnawatwika watu
mizigo mizito ambayo hawawezi kubeba, wala
ninyi wenyewe hamwinui hata kidole kimoja
kuwasaidia.
47 “Ole wenu, kwa sababu ninyi mnajenga
makaburi ya manabii waliouawa na baba zenu.
48 Hivyo ninyi mwashuhudia na mnathibitisha
kile baba zenu walichofanya. Wao waliwaua
manabii, nanyi mnawajengea makaburi. 49 Kwa
sababu ya jambo hili, Mungu katika hekima
yake alisema, ‘Tazama, nitatuma kwao man-
abii na mitume, nao watawaua baadhi yao
na wengine watawatesa.’ 50 Kwa hiyo kizazi
hiki kitawajibika kwa ajili ya damu ya man-
abii iliyomwagwa tangu kuwekwa misingi ya
ulimwengu, 51 tangu damu ya Abeli mpaka damu
ya Zekaria, aliyeuawa kati ya madhabahu na
mahali patakatifu. Naam, nawaambia, kizazi
hiki kitawajibika kwa haya yote.
52 “Ole wenu ninyi wataalamu wa sheria,
kwa sababu mmeuondoa ufunguo wa maarifa.
Ninyi wenyewe hamkuingia, na wale waliokuwa
wanaingia mkawazuia.”

53 Yesu alipoondoka huko, walimu wa sheria
na Mafarisayo wakaanza kumpinga vikali na
kumsonga kwa maswali, 54 wakivizia kumka-
mata kwa kitu atakachosema ili wamshtaki.

# 12

*Maonyo Dhidi Ya Unafiki*
*(Mathayo 10:26-33)*

1 Wakati huo, umati mkubwa wa watu
maelfu, walipokuwa wamekusanyika hata
wakawa wanakanyagana, Yesu akaanza
kuzungumza kwanza na wanafunzi wake,
akawaambia: "Jihadharini na chachu ya
Mafarisayo, yaani, unafiki wao. 2 Hakuna jambo
lolote lililositirika ambalo halitafunuliwa, au
lililofichwa ambalo halitajulikana. 3 Kwa hiyo,
lolote mlilosema gizani litasikiwa nuruni. Na
kile mlichonong'ona masikioni mkiwa kwenye
vyumba vya ndani, kitatangazwa juu ya paa.

4 "Nawaambieni rafiki zangu, msiwaogope
wale wauao mwili, lakini baada ya hilo
hawawezi kufanya lolote zaidi. 5 Lakini
nitawaambia nani wa kumwogopa: Mwogopeni
yule ambaye baada ya kuua mwili, ana mam-
laka ya kuwatupa motoni. Naam, nawaambia,
mwogopeni huyo! 6 Mnajua kwamba shomoro
watano huuzwa kwa senti mbili? Lakini Mungu
hamsahau hata mmoja wao. 7 Naam, hata ny-
wele za vichwa vyenu zote zimehesabiwa. Hivyo
msiogope, kwa maana ninyi ni wa thamani
kubwa kuliko shomoro wengi.

8 "Ninawaambia kwamba yeyote atakayenikiri
mbele ya watu, Mwana wa Adamu naye atamkiri

mbele za malaika wa Mungu. 9 Lakini yeye
atakayenikana mimi mbele ya watu, Mwana
wa Adamu naye atamkana mbele ya malaika
wa Mungu. 10 Naye kila atakayenena neno
baya dhidi ya Mwana wa Adamu atasamehewa,
lakini yeyote atakayemkufuru Roho Mtakatifu
hatasamehewa.
11 "Watakapowapeleka katika masinagogi, na
mbele ya watawala na wenye mamlaka, msiwe
na wasiwasi kuhusu namna mtakavyojitetea au
mtakavyosema. 12 Kwa maana Roho Mtakatifu
atawafundisha wakati huo huo mnachopaswa
kusema."

### *Mfano Wa Tajiri Mpumbavu*

13 Mtu mmoja katika umati wa watu
akamwambia Yesu, "Mwalimu, mwambie ndugu
yangu tugawane naye urithi wetu."
14 Lakini Yesu akamwambia, "Rafiki, ni nani
aliyeniweka mimi kuwa hakimu wenu au msu-
luhishi juu yenu?" 15 Ndipo Yesu akawaambia,
"Jihadharini! Jilindeni na aina zote za choyo.
Kwa maana maisha ya mtu hayatokani na wingi
wa mali alizo nazo."
16 Kisha akawaambia mfano huu: "Shamba
la mtu mmoja tajiri lilizaa sana. 17 Akawaza
moyoni mwake, 'Nifanye nini? Sina mahali pa
kuhifadhi mavuno yangu.'
18 "Ndipo huyo tajiri akasema, 'Nitafanya hivi:
Nitabomoa ghala zangu za nafaka na kujenga
nyingine kubwa zaidi na huko nitayahifadhi
mavuno yangu yote na vitu vyangu. 19 Nami
nitaiambia nafsi yangu, "Nafsi, unavyo vitu vingi

vizuri ulivyojiwekea akiba kwa miaka mingi.
Pumzika; kula, unywe, ufurahi.” ’
20 “Lakini Mungu akamwambia, ‘Mpumbavu
wewe! Usiku huu uhai wako unatakiwa. Sasa
hivyo vitu ulivyojiwekea akiba vitakuwa vya
nani?’
21 “Hivyo ndivyo ilivyo kwa wale wanaoji-
wekea mali lakini hawajitajirishi kwa Mungu.”

### *Msiwe Na Wasiwasi*
*(Mathayo 6:25-34)*

22 Kisha Yesu akawaambia wanafunzi wake:
“Kwa hiyo nawaambia, msisumbukie maisha
yenu kwamba mtakula nini; au msumbukie miili
yenu kwamba mtavaa nini. 23 Maisha ni zaidi ya
chakula, na mwili ni zaidi ya mavazi. 24 Fikirini
ndege! Wao hawapandi wala hawavuni, hawana
ghala wala popote pa kuhifadhi nafaka; lakini
Mungu huwalisha. Ninyi ni wa thamani zaidi ku-
liko ndege! 25 Ni nani miongoni mwenu ambaye
kwa kujitaabisha kwake anaweza kujiongezea
hata saa moja zaidi katika maisha yake? 26 Kama
hamwezi kufanya jambo dogo kama hilo, kwa
nini basi kuyasumbukia hayo mengine?
27 “Angalieni maua jinsi yameavyo: Hayafanyi
kazi wala hayafumi. Lakini nawaambia, hata
Solomoni katika fahari yake yote hakuvikwa
vizuri kama mojawapo ya hayo maua. 28 Basi
ikiwa Mungu huyavika hivi majani ya shambani,
ambayo leo yapo, na kesho yanatupwa motoni,
si atawavika ninyi vizuri zaidi, enyi wa imani
haba! 29 Wala msisumbuke mioyoni mwenu
mtakula nini au mtakunywa nini. Msiwe na
wasiwasi juu ya haya. 30 Watu wa mataifa ya

duniani husumbuka sana kuhusu vitu hivi vyote,
lakini Baba yenu anafahamu kuwa mnahitaji
haya yote. 31 Bali utafuteni Ufalme wa Mungu,
na haya yote atawapa pia.

*Utajiri Wa Mbinguni*
*(Mathayo 6:19-21)*

32 "Msiogope enyi kundi dogo, kwa maana
Baba yenu ameona vyema kuwapa ninyi Ufalme.
33 Uzeni mali zenu mkawape maskini. Ji-
fanyieni mifuko isiyochakaa, mkajiwekee hazina
mbinguni isiyokwisha, mahali ambapo mwizi
hakaribii wala nondo haharibu. 34 Kwa sababu
mahali hazina yako ilipo, hapo ndipo moyo wako
utakapokuwa pia.

*Kukesha*

35 "Kuweni tayari mkiwa mmevikwa kwa
ajili ya huduma na taa zenu zikiwa zinawaka,
36 kama watumishi wanaomngojea bwana wao
arudi kutoka kwenye karamu ya arusi, ili
ajapo na kubisha mlango waweze kumfungulia
mara. 37 Heri wale watumishi ambao bwana
wao atakapokuja atawakuta wakiwa wanake-
sha. Amin, nawaambia, atajifunga mkanda
wake na kuwaketisha ili wale, naye atakuja na
kuwahudumia. 38 Itakuwa heri kwa watumwa
hao ikiwa bwana wao atakapokuja atawakuta
wamekesha hata kama atakuja mnamo usiku
wa manane, au karibu na mapambazuko.
39 Lakini fahamuni jambo hili: Kama mwenye
nyumba angalijua saa mwizi atakuja, asingali-
iacha nyumba yake kuvunjwa. 40 Ninyi nanyi

hamna budi kuwa tayari, kwa sababu Mwana wa Adamu atakuja saa msiyotazamia."

### *Mtumishi Mwaminifu Na Yule Asiye Mwaminifu*
*(Mathayo 24:45-51)*

41 Ndipo Petro akamuuliza, "Bwana, mfano huu unatuambia sisi peke yetu au watu wote?"

42 Yesu akamjibu, "Ni yupi basi wakili mwaminifu na mwenye busara, ambaye bwana wake atamfanya msimamizi juu ya watumishi wake wote, ili awape watumishi wengine chakula chao wakati unaofaa?
43 Heri mtu-
mishi yule ambaye bwana wake atakaporudi atamkuta akifanya hivyo.
44 Amin nawaambia,
atamweka mtumishi huyo kuwa msimamizi wa mali yake yote.
45 Lakini kama yule mtu-
mishi atasema moyoni mwake, 'Bwana wangu anakawia kurudi,' kisha akaanza kuwapiga wale watumishi wa kiume na wa kike, na kula na kunywa na kulewa.
46 Basi bwana wa mtumishi
huyo atakuja siku asiyodhani na saa asiyoijua. Atamkata vipande vipande na kumweka katika sehemu moja pamoja na wale wasioamini.

47 "Yule mtumishi anayefahamu vyema mapenzi ya bwana wake na asijiandae wala kufanya kama apendavyo bwana wake, atapigwa kwa mapigo mengi.
48 Lakini
yeyote ambaye hakujua naye akafanya yale yastahiliyo kupigwa, atapigwa kidogo. Yeyote aliyepewa vitu vingi, atadaiwa vingi; na yeyote aliyekabidhiwa vingi, kwake vitatakiwa vingi.

*Yesu Kuleta Mafarakano*
*(Mathayo 10:34-36)*

49 "Nimekuja kuleta moto duniani; laiti kama
ungekuwa tayari umewashwa! 50 Lakini ni-
nao ubatizo ambao lazima nibatizwe, nayo
dhiki yangu ni kuu mpaka ubatizo huo ukami-
like! 51 Mnadhani nimekuja kuleta amani
duniani? La, nawaambia sivyo, nimekuja
kuleta mafarakano. 52 Kuanzia sasa, kutakuwa
na watu watano katika nyumba moja, watatu
dhidi ya wawili, na wawili dhidi ya watatu.
53 Watafarakana baba dhidi ya mwanawe na
mwana dhidi ya babaye, mama dhidi ya bintiye
na binti dhidi ya mamaye, naye mama mkwe
dhidi ya mkwewe na mkwe dhidi ya mama
mkwe wake."

*Kutambua Majira*
*(Mathayo 16:2-3)*

54 Pia Yesu akauambia ule umati wa watu,
"Mwonapo wingu likitokea magharibi, mara
mwasema, 'Mvua itanyesha,' nayo hunyesha.
55 Nanyi mwonapo upepo wa kusini ukivuma,
ninyi husema, 'Kutakuwa na joto,' na huwa
hivyo. 56 Enyi wanafiki! Mnajua jinsi ya kutam-
bua kuonekana kwa dunia na anga. Inakuwaje
basi kwamba mnashindwa kutambua wakati
huu wa sasa?

57 "Kwa nini hamwamui wenyewe lililo haki?
58 Uwapo njiani na mshtaki wako kwenda kwa
hakimu, jitahidi kupatana naye mkiwa njiani. La
sivyo, atakupeleka kwa hakimu, naye hakimu
atakukabidhi kwa afisa, naye afisa atakutupa

gerezani. 59 Nakuambia, hautatoka humo hadi
uwe umelipa senti ya mwisho.”

# 13

### *Tubu, La Sivyo Utaangamia*

1 Wakati huo huo, kulikuwa na watu
waliomwambia Yesu habari za Wagalilaya
ambao Pilato aliwaua, na damu ya hao watu
akaichanganya na dhabihu yao waliyokuwa
wanatoa. 2 Yesu akawauliza, “Mnadhani
kwamba hawa Wagalilaya ambao walikufa kifo
cha namna hiyo walikuwa na dhambi kuwazidi
Wagalilaya wengine wote? 3 La hasha! Ninyi
nanyi msipotubu, mtaangamia vivyo hivyo.
4 Au wale watu kumi na wanane waliokufa
walipoangukiwa na mnara huko Siloamu:
mnadhani wao walikuwa waovu kuliko
watu wote waliokuwa wanaishi Yerusalemu?
5 Nawaambia, la hasha! Ninyi nanyi msipotubu,
wote mtaangamia vivyo hivyo.”

### *Mfano Wa Mti Usiozaa Matunda*

6 Kisha Yesu akawaambia mfano huu: “Mtu
mmoja alikuwa na mtini uliopandwa katika
shamba lake la mizabibu, akaja ili kutafuta tini
kwenye mti huo, lakini hakupata hata moja.
7 Hivyo akamwambia mtunza shamba: ‘Tazama,
kwa muda wa miaka mitatu sasa nimekuwa
nikija kutafuta matunda kwenye mtini huu,
nami sikupata hata moja. Ukate! Kwa nini
uendelee kuharibu ardhi?’
8 “Yule mtunza shamba akamjibu, ‘Bwana,
uache tena kwa mwaka mmoja zaidi, nami

nitaupalilia na kuuwekea mbolea. 9 Kama ukizaa
matunda mwaka ujao, vyema, la sivyo uukate.' "

### *Yesu Amponya Mwanamke Kilema Siku Ya Sabato*

10 Basi Yesu alikuwa akifundisha katika sin-
agogi mojawapo siku ya Sabato. 11 Wakati
huo huo akaja mwanamke mmoja aliyekuwa na
pepo mchafu, naye alikuwa amepinda mgongo
kwa muda wa miaka kumi na minane, wala
alikuwa hawezi kunyooka wima. 12 Yesu alipom-
wona, akamwita, akamwambia, "Mwanamke,
uwe huru, umepona ugonjwa wako." 13 Yesu
alipomwekea mikono yake, mara akasimama
wima akaanza kumtukuza Mungu.

14 Lakini kiongozi wa sinagogi akakasirika kwa
sababu Yesu alikuwa ameponya mtu siku ya
Sabato. Akaambia ule umati wa watu, "Kuna
siku sita ambazo watu wanapaswa kufanya kazi.
Katika siku hizo, njooni mponywe, lakini si
katika siku ya Sabato."

15 Lakini Bwana akamjibu, "Enyi wanafiki! Je,
kila mmoja wenu hamfungulii ng'ombe wake
au punda wake kutoka zizini akampeleka kum-
nywesha maji siku ya Sabato? 16 Je, huyu
mwanamke, ambaye ni binti wa Abrahamu,
aliyeteswa na Shetani akiwa amemfunga kwa
miaka yote hii kumi na minane, hakustahili ku-
funguliwa kutoka kifungo hicho siku ya Sabato?"

17 Aliposema haya, wapinzani wake
wakaaibika, lakini watu wakafurahi kwa ajili ya
mambo ya ajabu aliyoyafanya.

### *Mfano Wa Punje Ya Haradali (Mathayo 13:31-32; Marko 4:30-32)*

18 Kisha Yesu akauliza, “Ufalme wa Mungu
unafanana na nini? Nitaufananisha na nini?
19 Umefanana na punje ya haradali ambayo
mtu aliichukua na kuipanda katika shamba lake.
Nayo ikakua, ikawa mti nao ndege wa angani wakatengeneza viota vyao kwenye matawi yake.”

### *Mfano Wa Chachu (Mathayo 13:33)*

20 Yesu akauliza tena, “Nitaufananisha Ufalme
wa Mungu na nini? 21 Unafanana na chachu
ambayo mwanamke aliichukua akaichanganya katika kiasi kikubwa cha unga mpaka wote ukaumuka.”

### *Mlango Mwembamba (Mathayo 7:13-14, 21-23)*

22 Yesu akapita katika miji na vijiji, akifundisha
wakati alisafiri kwenda Yerusalemu. 23 Mtu
mmoja akamuuliza, “Bwana, ni watu wachache tu watakaookolewa?”
24 Yesu akawaambia, “Jitahidini sana kuingia kupitia mlango mwembamba, kwa maana nawaambia wengi watajaribu kuingia, lakini hawataweza.
25 Wakati mwenye nyumba
atakapoondoka na kufunga mlango, mtasimama nje mkibisha mlango na kusema, ‘Bwana! Tufungulie mlango!’

“Lakini yeye atawajibu, ‘Siwajui ninyi, wala mtokako.’

26 “Ndipo mtamjibu, ‘Tulikula na kunywa
pamoja nawe, tena ulifundisha katika mitaa
yetu.’

27 “Lakini yeye atawajibu, ‘Siwajui ninyi, wala
mtokako. Ondokeni kwangu, ninyi watenda
maovu!’

28 “Ndipo kutakuwako kilio na kusaga meno,
mtakapowaona Abrahamu, Isaki, Yakobo na
manabii wote wakiwa katika Ufalme wa Mungu,
lakini ninyi mkiwa mmetupwa nje. 29 Watu
watatoka mashariki na magharibi, kaskazini
na kusini, nao wataketi kwenye sehemu
walizoandaliwa karamuni katika Ufalme wa
Mungu. 30 Tazama, kunao walio wa mwisho
watakaokuwa wa kwanza, nao wa kwanza
watakaokuwa wa mwisho.”

### *Yesu Aomboleza Kwa Ajili Ya Yerusalemu (Mathayo 23:37-39)*

31 Wakati huo huo baadhi ya Mafarisayo
wakamwendea Yesu na kumwambia, “Ondoka
hapa uende mahali pengine kwa maana Herode
anataka kukuua.”

32 Yesu akawajibu, “Nendeni mkamwambie
yule mbweha, ‘Ninafukuza pepo wachafu na
kuponya wagonjwa leo na kesho, nami siku ya
tatu nitaikamilisha kazi yangu.’ 33 Sina budi
kuendelea na safari yangu leo, kesho na kesho
kutwa: kwa maana haiwezekani nabii kufa
mahali pengine isipokuwa Yerusalemu.

34 “Ee Yerusalemu, Yerusalemu, uwauaye
manabii na kuwapiga mawe wale waliotumwa
kwako! Mara ngapi nimetamani kuwakusanya

watoto wako pamoja, kama vile kuku aku-
sanyavyo vifaranga wake chini ya mabawa yake,
lakini hukutaka! 35 Tazama nyumba yenu
imeachwa ukiwa. Ninawaambia, hamtaniona
tena mpaka wakati ule mtakaposema, 'Ame-
barikiwa yeye ajaye kwa jina la Bwana.'"

# 14

*Yesu Nyumbani Mwa Farisayo*

1 Ikawa siku moja Yesu alipokuwa amek-
wenda kula chakula kwa mmoja wa viongozi
wa Mafarisayo siku ya Sabato, watu walikuwa
wakimchunguza kwa bidii. 2 Papo hapo mbele
yake palikuwa na mtu mmoja mwenye ugonjwa
wa kuvimba mwili. 3 Yesu akawauliza wale
Mafarisayo na walimu wa sheria, "Je, ni halali
kuponya watu siku ya Sabato au la?" 4 Wakakaa
kimya. Hivyo Yesu akamshika yule mgonjwa
mkono na kumponya, akamruhusu aende zake.

5 Kisha akawauliza, "Kama mmoja wenu
angekuwa na mtoto au ng'ombe wake aliyetum-
bukia katika kisima siku ya Sabato, je, ham-
tamvuta mara moja na kumtoa?" 6 Nao
hawakuwa na la kusema.

*Unyenyekevu Na Ukarimu*

7 Alipoona jinsi wageni walivyokuwa wanach-
agua mahali pa heshima wakati wa kula,
akawaambia mfano huu: 8 "Mtu akikualika
arusini, usikae mahali pa mgeni wa hes-
hima kwa kuwa inawezekana amealikwa mtu
mheshimiwa kuliko wewe. 9 Kama mkifanya
hivyo yule aliyewaalika ninyi wawili atakuja

na kukuambia, 'Mpishe huyu mtu kiti chako.'
Ndipo kwa aibu utalazimika kukaa katika nafasi
ya chini kabisa. 10 Badala yake, unapoalikwa,
chagua nafasi ya chini, ili yule mwenyeji wako
atakapokuona atakuja na kukuambia, 'Rafiki
yangu, nenda kwenye nafasi iliyo bora zaidi.'
Kwa jinsi hii utakuwa umepewa heshima mbele
ya wageni wenzako wote. 11 Kwa maana kila
mtu ajikwezaye atashushwa, naye ajishushaye
atakwezwa."

12 Kisha Yesu akamwambia yule aliyewaalika,
"Uandaapo karamu ya chakula cha mchana au
cha jioni, usialike rafiki zako au ndugu zako au
jamaa zako au majirani zako walio matajiri tu.
Ukifanya hivyo, wao nao wanaweza kukualika
kwao, nawe ukawa umelipwa kile ulichofanya
na kupata thawabu yako. 13 Bali ufanyapo
karamu, waalike maskini, vilema na vipofu,
14 nawe utabarikiwa kwa sababu hawa hawana
uwezo wa kukulipa. Mungu atakulipa wakati wa
ufufuo wa wenye haki."

### *Mfano Wa Karamu Kuu*
### *(Mathayo 22:1-10)*

15 Mmoja wa wale waliokuwa pamoja naye
mezani aliposikia hivi akamwambia Yesu, "Ame-
barikiwa mtu yule atakayekula katika karamu ya
Ufalme wa Mungu!"

16 Yesu akamjibu, "Mtu mmoja alikuwa anaan-
daa karamu kubwa, akaalika watu wengi.
17 Wakati wa karamu ulipofika, akamtuma
mtumishi wake akawaambie wale walioalikwa,
'Karibuni, kila kitu ki tayari sasa.'

18 “Lakini wote, kila mmoja, wakaanza kutoa
udhuru: Wa kwanza akasema, ‘Nimenunua
shamba, lazima niende kuliona. Tafadhali niwie
radhi.’
19 “Mwingine akasema, ‘Ndipo tu nimenunua
jozi tano za ng’ombe wa kulimia, nami ni-
nakwenda kuwajaribu, tafadhali niwie radhi.’
20 Naye mwingine akasema, ‘Nimeoa mke, kwa
hiyo siwezi kuja.’
21 “Yule mtumishi akarudi, akampa bwana
wake taarifa. Ndipo yule mwenye nyumba
akakasirika, akamwagiza yule mtumishi wake,
akisema, ‘Nenda upesi kwenye mitaa na vicho-
choro vya mjini uwalete maskini, vilema, vipofu
na viwete.’
22 “Yule mtumishi akamwambia, ‘Bwana, yale
uliyoniagiza nimefanya, lakini bado ipo nafasi.’
23 “Ndipo yule bwana akamwambia mtu-
mishi wake, ‘Nenda kwenye barabara na vijia
vilivyoko nje ya mji na uwalazimishe watu
waingie ili nyumba yangu ipate kujaa. 24 Kwa
maana nawaambia, hakuna hata mmoja wa wale
walioalikwa atakayeionja karamu yangu.’ ”

### *Gharama Ya Kuwa Mwanafunzi (Mathayo 10:37-38)*

25 Umati mkubwa wa watu ulikuwa ukisafiri
pamoja na Yesu, naye akageuka, akawaam-
bia, 26 “Mtu yeyote anayekuja kwangu hawezi
kuwa mwanafunzi wangu kama hatanipenda
mimi zaidi ya baba yake na mama yake, mke
wake na watoto wake, ndugu zake na dada
zake, naam, hata maisha yake mwenyewe.

27 Yeyote asiyeuchukua msalaba wake na kuni-
fuata hawezi kuwa mwanafunzi wangu.
28 “Ni nani miongoni mwenu ambaye kama
anataka kujenga nyumba, hakai kwanza chini
na kufanya makisio ya gharama aone kama ana
fedha za kutosha kukamilisha? 29 La sivyo,
akiisha kuweka msingi, naye akiwa hana uwezo
wa kuikamilisha, wote waionao wataanza kumd-
hihaki, 30 wakisema, ‘Mtu huyu alianza kujenga
lakini hakuweza kukamilisha.’
31 “Au ni mfalme gani atokaye kwenda kupi-
gana vita na mfalme mwingine, ambaye hakai
chini kwanza na kufikiri iwapo akiwa na jeshi
la watu 10,000 ataweza kupigana na yule
anayekuja na jeshi la watu 20,000? 32 Kama
hawezi, basi wakati yule mwingine akiwa bado
yuko mbali, yeye hutuma ujumbe wa watu na
kuomba masharti ya amani. 33 Vivyo hivyo,
yeyote miongoni mwenu ambaye hawezi kuacha
vyote alivyo navyo, hawezi kuwa mwanafunzi
wangu.

*Chumvi Isiyofaa*
*(Mathayo 5:13; Marko 9:50)*

34 “Chumvi ni nzuri, lakini chumvi ikiwa ime-
poteza ladha yake, itafanywaje ili iweze kukolea
tena? 35 Haifai ardhi wala kwa lundo la mbolea,
bali hutupwa nje.
“Mwenye masikio ya kusikia, na asikie.”

# 15

*Mfano Wa Kondoo Aliyepotea*
*(Mathayo 18:12-14)*

1 Basi watoza ushuru na wenye dhambi wote
walikuwa wanakusanyika ili wapate kumsik-
iliza Yesu. 2 Lakini Mafarisayo na walimu wa
sheria wakanung'unika wakisema, "Huyu mtu
anawakaribisha wenye dhambi na kula nao."
3 Ndipo Yesu akawaambia mfano huu: 4 "Ikiwa
mmoja wenu ana kondoo mia moja, naye
akapoteza mmoja wao, je, hawaachi wale tisini
na tisa nyikani na kwenda kumtafuta huyo
aliyepotea mpaka ampate? 5 Naye akishampata,
humbeba mabegani mwake kwa furaha 6 na
kwenda nyumbani. Kisha huwaita rafiki zake
na majirani, na kuwaambia, 'Furahini pamoja
nami; nimempata kondoo wangu aliyepotea.'
7 Nawaambieni, vivyo hivyo kutakuwa na furaha
zaidi mbinguni kwa sababu ya mwenye dhambi
mmoja atubuye, kuliko kwa wenye haki tisini na
tisa ambao hawana haja ya kutubu."

### *Mfano Wa Sarafu Iliyopotea*

8 "Au ikiwa mwanamke ana sarafu za fedha
kumi, naye akapoteza moja, je, hawashi taa
na kufagia nyumba na kuitafuta kwa bidii
mpaka aipate? 9 Naye akiisha kuipata, huwaita
rafiki zake na majirani na kuwaambia, 'Furahini
pamoja nami; nimeipata ile sarafu yangu ya
fedha iliyopotea.' 10 Vivyo hivyo, nawaambia,
kuna furaha mbele ya malaika wa Mungu juu
ya mwenye dhambi mmoja atubuye."

### *Mfano Wa Mwana Mpotevu*

11 Yesu akaendelea kusema: "Kulikuwa na
mtu mmoja aliyekuwa na wana wawili. 12 Yule
mdogo akamwambia baba yake, 'Baba, nipe

urithi wangu.’ Hivyo akawagawia wanawe mali
yake.
13 “Baada ya muda mfupi, yule mdogo akaku-
sanya vitu vyote alivyokuwa navyo, akaenda
nchi ya mbali, na huko akaitapanya mali yake
kwa maisha ya anasa. 14 Baada ya kutumia
kila kitu alichokuwa nacho, kukawa na njaa
kali katika nchi ile yote, naye akawa hana
chochote. 15 Kwa hiyo akaenda akaajiriwa na
mwenyeji mmoja wa nchi ile ambaye alimpeleka
shambani kwake kulisha nguruwe. 16 Akatamani
kujishibisha kwa maganda waliyokula wale ngu-
ruwe, wala hakuna mtu aliyempa chochote.
17 “Lakini alipozingatia moyoni mwake,
akasema, ‘Ni watumishi wangapi walioajiriwa
na baba yangu ambao wana chakula cha
kuwatosha na kusaza, bali mimi hapa nakufa
kwa njaa! 18 Nitaondoka na kurudi kwa baba
yangu na kumwambia: Baba, nimetenda dhambi
mbele za Mungu na mbele yako. 19 Sistahili
tena kuitwa mwanao; nifanye kama mmoja wa
watumishi wako.’ 20 Basi akaondoka, akaenda
kwa baba yake.

“Lakini alipokuwa bado yuko mbali, baba
yake akamwona, moyo wake ukajawa na hu-
ruma. Akamkimbilia mwanawe, akamkumbatia
na kumbusu.
21 “Yule mwana akamwambia baba yake,
‘Baba, nimekosa mbele za Mungu na mbele yako.
Sistahili kuitwa mwanao tena.’
22 “Lakini baba yake akawaambia watumishi,
‘Leteni upesi joho lililo bora sana, tieni pete
kidoleni mwake na viatu miguuni mwake.

23 Leteni ndama aliyenona, mkamchinje ili tuwe
na karamu, tule na kufurahi. 24 Kwa maana huyu
mwanangu alikuwa amekufa na sasa yu hai
tena; alikuwa amepotea na sasa amepatikana!'
Nao wakaanza kufanya tafrija.
25 "Wakati huo, yule mwana mkubwa
alikuwa shambani. Alipokaribia nyumbani,
akasikia sauti ya nyimbo na watu wakicheza.
26 Akamwita mmoja wa watumishi na
kumuuliza, 'Kuna nini?' 27 Akamwambia,
'Ndugu yako amekuja, naye baba yako
amemchinjia ndama aliyenona kwa sababu
mwanawe amerudi nyumbani akiwa salama na
mzima.'
28 "Yule mwana mkubwa akakasirika,
akakataa kuingia ndani. Basi baba yake akatoka
nje na kumsihi. 29 Lakini yeye akamjibu baba
yake, 'Tazama! Miaka yote hii nimekutumikia
na hata siku moja sijaacha kutii amri zako,
lakini hujanipa hata mwana-mbuzi ili nifurahi
na rafiki zangu. 30 Lakini huyu mwanao
ambaye ametapanya mali yako kwa makahaba
aliporudi nyumbani, wewe umemchinjia ndama
aliyenona!'
31 "Baba yake akamjibu, 'Mwanangu,
umekuwa nami siku zote na vyote nilivyo
navyo ni vyako. 32 Lakini ilitubidi tufurahi
na kushangilia kwa sababu huyu ndugu yako
alikuwa amekufa na sasa yu hai; alikuwa
amepotea naye amepatikana.' "

**16**

*Mfano Wa Msimamizi Mjanja*

1 Yesu akawaambia wanafunzi wake, "Pa-
likuwa na tajiri mmoja na msimamizi wake.
Ilisemekana kwamba huyo msimamizi alikuwa
anatumia vibaya mali ya tajiri yake. 2 Hivyo
huyo tajiri akamwita na kumuuliza, 'Ni mambo
gani haya ninayoyasikia kukuhusu? Toa taarifa
ya usimamizi wako, kwa sababu huwezi kuende-
lea kuwa msimamizi.'

3 "Yule msimamizi akawaza moyoni mwake,
'Nitafanya nini sasa? Bwana wangu ananiondoa
katika kazi yangu. Sina nguvu za kulima, nami
ninaona aibu kuombaomba. 4 Najua nitakalo-
fanya ili nikiachishwa kazi yangu hapa, watu
wanikaribishe nyumbani kwao.'

5 "Kwa hiyo akawaita wadeni wote wa bwana
wake, mmoja mmoja. Akamuuliza wa kwanza,
'Deni lako kwa bwana wangu ni kiasi gani?'

6 "Akajibu, 'Galoni 800*za mafuta ya
mizeituni.'

"Msimamizi akamwambia, 'Chukua hati ya
deni lako, ibadilishe upesi, uandike galoni 400.'

7 "Kisha akamuuliza wa pili, 'Wewe deni lako
ni kiasi gani?'

"Akajibu, 'Vipimo 1,000†vya ngano.'

"Yule msimamizi akamwambia, 'Chukua hati
yako, andika vipimo 800!'

8 "Yule bwana akamsifu yule msimamizi dhal-
imu kwa jinsi alivyotumia ujanja. Kwa maana
watu wa dunia hii wana ujanja zaidi wanapo-
jishughulisha na mambo ya dunia kuliko watu

---

* **16:6** Galoni 800 ni sawa na lita 4,000. † **16:7** Vipimo 1,000 ni kama magunia 100.

wa nuru. 9 Nawaambia, tumieni mali ya
kidunia kujipatia marafiki, ili itakapokwisha,
mkaribishwe katika makao ya milele.

10 “Yeyote aliye mwaminifu katika mambo
madogo, pia ni mwaminifu hata katika mambo
makubwa, naye mtu ambaye si mwaminifu
katika mambo madogo pia si mwaminifu
katika mambo makubwa. 11 Ikiwa hamkuwa
waaminifu katika mali ya kidunia, ni nani
atakayewaaminia mali ya kweli? 12 Nanyi kama
hamkuwa waaminifu na mali ya mtu mwingine,
ni nani atakayewapa iliyo yenu wenyewe?

13 “Hakuna mtumishi awezaye kuwatumikia
mabwana wawili. Kwa kuwa atamchukia huyu
na kumpenda yule mwingine, au atashikamana
sana na huyu na kumdharau yule mwingine.
Hamwezi kumtumikia Mungu pamoja na Mali.”‡

14 Mafarisayo, waliokuwa wapenda fedha,
waliyasikia hayo yote na wakamcheka kwa dha-
rau. 15 Yesu akawaambia, “Ninyi mnajionyesha
kuwa wenye haki mbele za wanadamu, lakini
Mungu anaijua mioyo yenu. Kwa maana vile
vitu ambavyo wanadamu wanavithamini sana,
kwa Mungu ni machukizo.

### *Sheria Na Ufalme Wa Mungu*

16 “Sheria na Manabii vilihubiriwa mpaka kuja
kwa Yohana Mbatizaji. Tangu wakati huo habari
njema za Ufalme wa Mungu zinahubiriwa, na
kila mmoja hujiingiza kwa nguvu. 17 Lakini ni

‡ **16:13** Mali (au Utajiri) hapa inatoka neno Mamoni kwa Kiaramu au Mamona kwa Kiyunani.

rahisi zaidi mbingu na dunia kupita kuliko hata
herufi moja kuondoka katika Sheria.

18 “Mtu yeyote amwachaye mkewe na kumwoa mwanamke mwingine anazini, naye mwanaume amwoaye mwanamke aliyetalikiwa anazini.

*Tajiri Na Lazaro*

19 “Palikuwa na mtu mmoja tajiri aliyevaa nguo za rangi ya zambarau na kitani safi, am-
baye aliishi kwa anasa kila siku. 20 Hapo penye
mlango wake aliishi maskini mmoja, jina lake
Lazaro, mwenye vidonda mwili mzima. 21 Huyo
Lazaro alitamani kujishibisha kwa makombo yaliyoanguka kutoka mezani kwa yule tajiri. Hata mbwa walikuwa wakija na kuramba vidonda vyake.

22 “Wakati ukafika yule maskini akafa, nao malaika wakamchukua akae pamoja na Abrahamu. Yule tajiri naye akafa na akazikwa.
23 Kule kuzimu alipokuwa akiteseka, alitazama
juu, akamwona Abrahamu kwa mbali, naye
Lazaro alikuwa karibu yake. 24 Hivyo yule
tajiri akamwita, ‘Baba Abrahamu, nihurumie na umtume Lazaro achovye ncha ya kidole chake ndani ya maji aupoze ulimi wangu, kwa sababu nina maumivu makuu kwenye moto huu.’

25 “Lakini Abrahamu akamjibu, ‘Mwanangu, kumbuka kwamba wakati wa uhai wako ulipata mambo mazuri, lakini Lazaro alipata mambo mabaya. Lakini sasa anafarijiwa hapa na wewe
uko katika maumivu makuu. 26 Zaidi ya hayo,
kati yetu na ninyi huko kumewekwa shimo kubwa, ili wale wanaotaka kutoka huku kuja

huko wasiweze, wala mtu yeyote asiweze ku-
vuka kutoka huko kuja kwetu.’
27 “Akasema, ‘Basi, nakuomba, umtume
Lazaro aende nyumbani kwa baba yangu,
28 maana ninao ndugu watano. Awaonye, ili
wasije nao wakafika mahali hapa pa mateso.’
29 “Abrahamu akamjibu, ‘Ndugu zako wana
Maandiko ya Mose na Manabii, wawasikilize
hao.’
30 “Yule tajiri akasema, ‘Hapana, baba Abra-
hamu, lakini mtu kutoka kwa wafu akiwaendea,
watatubu.’
31 “Abrahamu akamwambia, ‘Kama
wasipowasikiliza Mose na Manabii, hawataweza
kushawishika hata kama mtu akifufuka kutoka
kwa wafu.’ ”

# 17

*Yesu Afundisha Kuhusu Majaribu, Dhambi Na Imani*

*(Mathayo 18:6-7, 21-22; Marko 9:42)*

1 Yesu akawaambia wanafunzi wake, “Mambo
yanayosababisha watu watende dhambi hayana
budi kutukia. Lakini ole wake mtu yule
anayeyasababisha. 2 Ingekuwa heri kama mtu
huyo angefungiwa jiwe la kusagia shingoni na
kutoswa baharini, kuliko kumsababisha mmo-
jawapo wa hawa wadogo kutenda dhambi.
3 Kwa hiyo, jilindeni.

“Kama ndugu yako akikukosea mwonye, naye
akitubu, msamehe. 4 Kama akikukosea mara
saba kwa siku moja na mara saba kwa siku moja
akaja kwako akisema, ‘Ninatubu,’ msamehe.”

### *Imani*

5 Mitume wake wakamwambia Bwana,
"Tuongezee imani."

6 Bwana akawajibu, "Kama mkiwa na imani
ndogo kama punje ya haradali, mngeweza ku-
uambia mti huu wa mkuyu, 'Ng'oka ukaote
baharini,' nao ungewatii.

### *Wajibu Wa Mtumishi*

7 "Ikiwa mmoja wenu ana mtumishi anayelima
shambani au anayechunga kondoo, je, mtumishi
huyo arudipo atamwambia, 'Karibu hapa keti
ule chakula?' 8 Je, badala yake, hatamwambia,
'Niandalie chakula, nile, jifunge unitumikie ni-
napokula na kunywa; baadaye waweza kula na
kunywa?' 9 Je, huyo mtu atamshukuru mtumishi
huyo kwa kutimiza yale aliyoamriwa? 10 Vivyo
hivyo nanyi mkiisha kufanya mliyoagizwa, se-
meni, 'Sisi tu watumishi tusiostahili; tumefanya
tu yale tuliyopaswa kufanya.' "

### *Yesu Atakasa Wakoma Kumi*

11 Yesu alipokuwa njiani akienda Yerusalemu,
alipitia mpakani mwa Samaria na Galilaya.
12 Alipokuwa akiingia kwenye kijiji kimoja,
watu kumi waliokuwa na ukoma wakakutana
naye. Wakasimama mbali, 13 wakapaza sauti,
wakasema, "Yesu, Bwana, tuhurumie!"

14 Alipowaona akawaambia, "Nendeni mka-
jionyeshe kwa makuhani." Nao walipokuwa
njiani wakienda, wakatakasika.

15 Mmoja wao alipoona kwamba amepona,
akarudi kwa Yesu, akimsifu Mungu kwa

sauti kuu. 16 Akajitupa miguuni mwa Yesu
akamshukuru. Yeye alikuwa Msamaria.

17 Yesu akauliza, "Je, hawakutakaswa
wote kumi? Wako wapi wale wengine tisa?
18 Hakuna hata mmoja aliyeonekana kurudi ili
kumshukuru Mungu isipokuwa huyu mgeni?"
19 Yesu akamwambia, "Inuka na uende zako,
imani yako imekuponya."

### *Kuja Kwa Ufalme Wa Mungu*
### *(Mathayo 24:23-28, 37-41)*

20 Yesu alipoulizwa na Mafarisayo Ufalme wa
Mungu utakuja lini, yeye akawajibu, "Ufalme wa
Mungu hauji kwa kuchunguza kwa bidii, 21 wala
watu hawatasema, 'Huu hapa,' au 'Ule kule,'
kwa maana Ufalme wa Mungu umo ndani yenu."

22 Kisha Yesu akawaambia wanafunzi wake,
"Wakati utafika ambapo mtatamani kuiona moja
ya siku ya Mwana wa Adamu, lakini hamtaiona.
23 Watu watawaambia, 'Yule kule!' Au, 'Huyu
hapa!' Msiwakimbilie. 24 Kwa maana kama
vile umeme wa radi umulikavyo katika anga
kuanzia mwisho mmoja hadi mwingine, ndivyo
atakavyokuwa Mwana wa Adamu katika siku
yake. 25 Lakini kwanza itampasa kuteseka katika
mambo mengi na kukataliwa na kizazi hiki.

26 "Kama ilivyokuwa siku za Noa, ndivyo
itakavyokuwa katika siku za Mwana wa Adamu.
27 Watu walikuwa wakila na kunywa, wakioa na
kuolewa, mpaka siku ile Noa alipoingia katika
safina. Ndipo gharika ikaja na kuwaangamiza
wote.

28 “Ndivyo ilivyokuwa katika siku za Loti:
Watu walikuwa wakila na kunywa, wakinunua
na kuuza, wakilima na kujenga. 29 Lakini
siku ile Loti alipoondoka Sodoma, ikanyesha
mvua ya moto na kiberiti kutoka mbinguni
ukawaangamiza wote.
30 “Hivyo ndivyo itakavyokuwa siku ile Mwana
wa Adamu atakapofunuliwa. 31 Siku hiyo,
mtu yeyote aliye juu ya dari ya nyumba
yake, hata vitu vyake vikiwa ndani ya hiyo
nyumba, asishuke kuvichukua. Vivyo hivyo
mtu aliye shambani asirudi nyumbani kuchukua
chochote. 32 Mkumbukeni mke wa Loti!
33 Mtu yeyote anayejaribu kuyaokoa maisha
yake atayapoteza, na yeyote atakayeyapoteza
maisha yake atayaokoa. 34 Nawaambia, usiku
huo watu wawili watakuwa wamelala ki-
tanda kimoja; naye mmoja atatwaliwa na
mwingine ataachwa. 35 Wanawake waw-
ili watakuwa wanasaga nafaka pamoja; naye
mmoja atatwaliwa na mwingine ataachwa. [
36 Wanaume wawili watakuwa wanafanya kazi
pamoja shambani; mmoja atachukuliwa na
mwingine ataachwa.]”
37 Kisha wakamuuliza, “Haya yatatukia wapi
Bwana?”
Akawaambia, “Pale ulipo mzoga, huko ndiko
tai watakapokusanyika.”

# 18

*Mfano Wa Mjane Asiyekata Tamaa*

1 Kisha Yesu akawapa wanafunzi wake mfano
ili kuwaonyesha kuwa yawapasa kuomba pasipo

kukata tamaa. 2 Akawaambia, “Katika mji
mmoja alikuwepo hakimu ambaye hakum-
wogopa Mungu wala kumjali mtu. 3 Katika mji
huo alikuwako mjane mmoja ambaye alikuwa
akija kwake mara kwa mara akimwomba,
‘Tafadhali nipatie haki kati yangu na adui
yangu.’

4 “Kwa muda mrefu yule hakimu alikataa.
Lakini hatimaye akasema moyoni mwake,
‘Ijapokuwa simwogopi Mungu wala simjali
mwanadamu, 5 lakini kwa kuwa huyu mjane
ananisumbuasumbua, nitahakikisha amepata
haki yake ili asiendelee kunichosha kwa kunijia
mara kwa mara!’ ”

6 Bwana akasema, “Sikilizeni asemavyo huyu
hakimu dhalimu. 7 Je, Mungu hatawatendea haki
wateule wake wanaomlilia usiku na mchana? Je,
atakawia kuwasaidia? 8 Ninawaambia, atawa-
patia haki upesi. Lakini je, Mwana wa Adamu
atakapokuja ataikuta imani duniani?”

### *Mfano Wa Farisayo Na Mtoza Ushuru*

9 Yesu akatoa mfano huu kwa wale walio-
jiamini kuwa wao ni wenye haki na kuwad-
harau wengine: 10 “Watu wawili walikwenda
Hekaluni kusali, mmoja wao alikuwa Farisayo
na mwingine alikuwa mtoza ushuru. 11 Yule
Farisayo, akasimama, akasali hivi na kuomba
kwake mwenyewe: ‘Mungu, nakushukuru kwa
sababu mimi si kama watu wengine ambao
ni wanyang’anyi, wadhalimu, na wazinzi, wala
kama huyu mtoza ushuru. 12 Mimi nafunga mara

mbili kwa juma, na natoa sehemu ya kumi ya
mapato yangu.’
13 “Lakini yule mtoza ushuru akasimama
mbali, wala hakuthubutu hata kuinua uso wake
kutazama mbinguni, bali alijipigapiga kifuani
na kusema: ‘Mungu, nihurumie, mimi mwenye
dhambi.’
14 “Nawaambia, huyu mtoza ushuru alirudi
nyumbani akiwa amehesabiwa haki mbele
za Mungu zaidi ya yule Farisayo. Kwa
maana yeyote ajikwezaye atashushwa, na yeyote
ajishushaye atakwezwa.”

### *Yesu Awabariki Watoto Wadogo*
### *(Mathayo 19:13-15; Marko 10:13-16)*

15 Pia, watu walikuwa wakimletea Yesu wa-
toto wachanga ili awaguse. Wanafunzi wake
walipoona hivyo, wakawakemea. 16 Lakini Yesu
akawaita wale watoto waje kwake, akasema,
“Waacheni watoto wadogo waje kwangu, wala
msiwazuie, kwa maana Ufalme wa Mungu ni wa
wale walio kama hawa. 17 Amin, nawaambia,
mtu yeyote asiyeupokea Ufalme wa Mungu kama
mtoto mdogo, hatauingia kamwe.”

### *Mtawala Tajiri*
### *(Mathayo 19:16-30; Marko 10:17-31)*

18 Mtawala mmoja akamuuliza Yesu, “Mwal-
imu mwema, nifanye nini ili niurithi uzima wa
milele?”
19 Yesu akamjibu, “Mbona unaniita mwema?
Hakuna yeyote aliye mwema ila Mungu peke
yake. 20 Unazijua amri: ‘Usizini, usiue, usiibe,

usishuhudie uongo, waheshimu baba yako na mama yako.' "

21 Akajibu, "Amri hizi zote nimezishika tangu nikiwa mtoto."

22 Yesu aliposikia haya, akamwambia, "Bado kuna jambo moja ulilopungukiwa. Nenda ukauze kila kitu ulicho nacho, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni. Kisha njoo, unifuate."

23 Aliposikia jambo hili, alisikitika sana kwa
maana alikuwa mtu mwenye mali nyingi. 24 Yesu
akamtazama, akasema, "Tazama jinsi ilivyo vigumu kwa tajiri kuingia katika Ufalme wa
Mungu! 25 Hakika ni rahisi zaidi kwa ngamia
kupita kwenye tundu la sindano kuliko mtu tajiri kuingia katika Ufalme wa Mungu."

26 Wale waliosikia haya wakauliza, "Ni nani basi awezaye kuokoka?"

27 Yesu akajibu, "Yasiyowezekana kwa wanadamu yanawezekana kwa Mungu."

28 Ndipo Petro akamjibu, "Tazama, tumeacha vyote tulivyokuwa navyo tukakufuata!"

29 Yesu akajibu, "Amin, nawaambia, hakuna hata mtu aliyeacha nyumba yake, au mke, au ndugu, au wazazi au watoto kwa ajili ya Ufalme
wa Mungu 30 ambaye hatapewa mara nyingi
zaidi ya hivyo katika maisha haya, na hatimaye kupata uzima wa milele ujao."

### *Yesu Atabiri Kifo Chake Mara Ya Tatu (Mathayo 20:17-19; Marko 10:32-34)*

31 Yesu akawachukua wale wanafunzi wake
kumi na wawili kando na kuwaambia, “Tuna-
panda kwenda Yerusalemu, na kila kitu kili-
choandikwa na manabii kumhusu Mwana wa
Adamu kitatimizwa. 32 Kwa kuwa atatiwa
mikononi mwa watu wasiomjua Mungu, nao
watamdhihaki, watamtukana na kumtemea
mate, watampiga mijeledi na kumuua. 33 Naye
siku ya tatu atafufuka.”

34 Wanafunzi wake hawakuelewa mambo haya, kwa kuwa maana yake ilikuwa imefichika kwao, nao hawakujua Yesu alikuwa anazungumzia nini.

### *Yesu Amponya Kipofu Karibu Na Yeriko (Mathayo 20:29-34; Marko 10:46-52)*

35 Yesu alipokuwa anakaribia Yeriko, kipofu
mmoja alikuwa ameketi kando ya njia akiomba
msaada. 36 Kipofu huyo aliposikia umati
wa watu ukipita, akauliza, “Kuna nini?”
37 Wakamwambia, “Yesu wa Nazareti anapita.”

38 Akapaza sauti, akasema, “Yesu, Mwana wa Daudi, nihurumie!”

39 Wale waliokuwa wametangulia mbele wakamkemea, wakamwambia akae kimya. Lakini yeye akapaza sauti zaidi, “Mwana wa Daudi, nihurumie!”

40 Yesu akasimama, akawaamuru wamlete
huyo mtu kwake. Alipokaribia, Yesu akamuuliza,
41 “Unataka nikufanyie nini?”

Akajibu, “Bwana, nataka kuona.”

42 Yesu akamwambia, “Basi upate kuona.
Imani yako imekuponya.” 43 Akapata kuona saa
ile ile, akamfuata Yesu, huku akimsifu Mungu.

Watu wote walipoona mambo hayo, nao wakamsifu Mungu.

# 19

*Zakayo Mtoza Ushuru*

1 Yesu akaingia Yeriko, naye alikuwa anapita
katikati ya huo mji. 2 Tazama, palikuwa na mtu
mmoja mkuu wa watoza ushuru naye alikuwa
tajiri, jina lake Zakayo. 3 Yeye alikuwa akijitahidi
kumwona Yesu ni mtu wa namna gani. Lakini
kutokana na umati mkubwa wa watu hakuweza
kwa sababu alikuwa mfupi wa kimo. 4 Kwa
hiyo akatangulia mbio mbele ya umati wa watu
akapanda juu ya mkuyu ili amwone Yesu, kwa
sababu angeipitia njia ile.
5 Yesu alipofika pale chini ya huo mkuyu,
akatazama juu, akamwambia, "Zakayo, shuka
upesi, kwa maana leo nitakuwa mgeni nyumbani
kwako!" 6 Hivyo Zakayo akashuka upesi,
akamkaribisha Yesu nyumbani kwake kwa furaha kubwa.
7 Watu wote walipoona hivyo, wakaanza
kunung'unika wakisema, "Amekwenda kuwa
mgeni wa 'mtu mwenye dhambi.' "
8 Lakini Zakayo akasimama na kumwambia
Bwana, "Tazama, Bwana! Sasa hivi nusu ya mali
yangu ninawapa maskini, nami kama nimemdhulumu mtu yeyote kitu chochote, nitamrudishia
mara nne ya hicho kiwango."
9 Ndipo Yesu akamwambia, "Leo, wokovu
umeingia nyumbani humu, kwa sababu huyu
naye ni mwana wa Abrahamu. 10 Kwa maana

Mwana wa Adamu amekuja kutafuta na kuokoa
kile kilichopotea."

### *Mfano Wa Fedha (Mathayo 25:14-30)*

11 Walipokuwa wanasikiliza haya, Yesu
akaendelea kuwaambia mfano, kwa sababu
alikuwa anakaribia Yerusalemu na watu
walikuwa wakidhani ya kuwa Ufalme wa
Mungu ulikuwa unakuja saa iyo hiyo. 12 Hivyo
akawaambia: "Mtu mmoja mwenye cheo
kikubwa alisafiri kwenda nchi ya mbali ili
akapokee madaraka ya kuwa mfalme, kisha
arudi. 13 Hivyo akawaita kumi miongoni mwa
watumishi wake, na akawapa kila mmoja fungu
la fedha. Akawaambia, 'Fanyeni biashara na
fedha hizi mpaka nitakaporudi.'
14 "Lakini raiya wa nchi yake walimchukia
wakapeleka ujumbe na kusema, 'Hatutaki huyu
mtu awe mfalme wetu.'
15 "Hata hivyo alirudi akiwa amekwisha
kupokea mamlaka ya ufalme, akawaita wale
watumishi wake aliokuwa amewaachia fedha,
ili afahamu ni faida kiasi gani kila mmoja wao
aliyopata kwa kufanya biashara.
16 "Wa kwanza akaja na kusema, 'Bwana,
kutokana na fedha uliyoniachia, nimepata faida
mara kumi zaidi.'
17 "Yule bwana akamjibu, 'Umefanya vizuri
mtumishi mwema! Kwa sababu umekuwa
mwaminifu katika wajibu mdogo sana, nakupa
mamlaka juu ya miji kumi.'
18 "Wa pili naye akaja. Akasema, 'Bwana,
fedha yako imeleta faida mara tano zaidi.'

19 “Bwana wake akajibu, ‘Nakupa mamlaka
juu ya miji mitano.’
20 “Kisha akaja yule mtumishi mwingine,
akasema, ‘Bwana, hii hapa fedha yako. Nili-
itunza vizuri kwenye kitambaa. 21 Nilikuogopa,
kwa sababu wewe ni mtu mgumu. Unachukua
ambapo hukuweka kitu, na unavuna mahali
ambapo hukupanda kitu.’
22 “Bwana wake akamjibu, ‘Nitakuhukumu
kwa maneno yako mwenyewe, wewe mtumishi
mwovu! Kama ulifahamu kwamba mimi ni mtu
mgumu, nichukuaye mahali ambapo sikuweka
kitu na kuvuna mahali ambapo sikupanda,
23 kwa nini basi hukuweka fedha zangu kwa
watoa riba, ili nitakaporudi nichukue iliyo yangu
na riba yake?’
24 “Ndipo akawaambia wale waliokuwa
wamesimama karibu, ‘Mnyang’anyeni fungu
lake la fedha, mkampe yule mwenye kumi.’
25 “Wakamwambia, ‘Bwana, mbona; tayari
anayo mafungu kumi!’
26 “Akawajibu, ‘Nawaambia kwamba kila aliye
na kitu, ataongezewa. Lakini yule asiye na kitu,
hata alicho nacho atanyang’anywa. 27 Lakini
wale adui zangu ambao hawakutaka mimi niwe
mfalme juu yao. Waleteni hapa mkawaue mbele
yangu.’ ”

*Yesu Aingia Yerusalemu Kwa Ushindi*
*(Mathayo 21:1-11; Marko 11:1-11; Yohana 12:12-19)*

28 Baada ya Yesu kusema haya, alitangulia ku-
panda kwenda Yerusalemu. 29 Naye alipokaribia

Bethfage na Bethania kwenye mlima uitwao
Mlima wa Mizeituni, aliwatuma wanafunzi wake
wawili, akawaambia, 30 “Nendeni katika ki-
jiji kilichoko mbele yenu. Na mtakapokuwa
mnaingia kijijini, mtamkuta mwana-punda ame-
fungwa hapo, ambaye hajapandwa na mtu bado.
Mfungueni, mkamlete hapa. 31 Kama mtu aki-
wauliza, ‘Mbona mnamfungua?’ Mwambieni,
‘Bwana anamhitaji.’ ”

32 Wale waliotumwa wakaenda, wakakuta kila
kitu kama vile Yesu alivyokuwa amewaam-
bia. 33 Walipokuwa wanamfungua yule mwana-
punda, wenyewe wakawauliza, “Mbona mnam-
fungua huyo mwana-punda?”

34 Wale wanafunzi wakajibu, “Bwana anamhi-
taji.”

35 Wakamleta kwa Yesu, nao baada ya ku-
tandika mavazi yao juu ya huyo mwana-punda,
wakampandisha Yesu juu yake. 36 Alipokuwa
akienda akiwa amempanda, watu wakatandaza
mavazi yao barabarani.

37 Alipokaribia mahali yanapoanzia
materemko ya Mlima wa Mizeituni, umati wote
wa wafuasi wake wakaanza kumsifu Mungu
kwa furaha kwa sauti kuu kwa ajili ya matendo
yote ya miujiza waliyoyaona. Wakasema:

38 “Amebarikiwa Mfalme ajaye kwa Jina la
Bwana!”
“Amani mbinguni na utukufu huko juu
sana.”

39 Baadhi ya Mafarisayo waliokuwamo mion-
goni mwa ule umati wa watu wakamwambia,

“Mwalimu, waamuru wanafunzi wako wanya-
maze.”
40 Yesu akawajibu, “Nawaambia ninyi, kama
hawa wakinyamaza, mawe yatapiga kelele.”

### *Yesu Anaulilia Mji Wa Yerusalemu*

41 Alipokaribia Yerusalemu na kuuona mji,
aliulilia, 42 akisema, “Laiti ungalijua hata wewe
leo yale ambayo yangeleta amani, lakini sasa
yamefichika machoni pako. 43 Hakika siku
zinakujia, ambazo adui zako watakuzingira, nao
watakuzunguka pande zote na kukuzuilia ndani.
44 Watakuponda chini, wewe na watoto walioko
ndani ya kuta zako. Nao hawataacha hata jiwe
moja juu ya jingine, kwa sababu hukutambua
wakati wa kujiliwa kwako.”

### *Yesu Atakasa Hekaluni*

*(Mathayo 21:12-17; Marko 11:15-19; Yohana 2:13-22)*

45 Ndipo akaingia eneo la Hekalu, akaanza
kuwafukuza wale waliokuwa wakiuza vitu
humo. 46 Naye akawaambia, “Imeandikwa,
‘Nyumba yangu itakuwa nyumba ya sala,’
lakini ninyi mmeifanya kuwa ‘pango la
wanyang’anyi.’ ”

47 Kila siku alikuwa akifundisha Hekaluni.
Lakini viongozi wa makuhani, walimu wa sheria
na viongozi wa watu walikuwa wakitafuta njia
ili kumuua. 48 Lakini hawakupata nafasi kwa
sababu watu wote walimfuata wakiyasikiliza
maneno yake kwa usikivu mwingi.

# 20

### *Swali Kuhusu Mamlaka Ya Yesu*
### *(Mathayo 21:23-27; Marko 11:27-33)*

1 Siku moja, Yesu alipokuwa akifundisha watu
Hekaluni na kuhubiri habari njema, viongozi wa
makuhani, walimu wa sheria, pamoja na wazee
wa watu wakamjia. 2 Wakamuuliza, "Tuambie,
unafanya mambo haya kwa mamlaka gani? Ni
nani aliyekupa mamlaka haya?"
3 Akawajibu, "Nami nitawauliza swali. 4 Je,
ubatizo wa Yohana ulitoka mbinguni au kwa
wanadamu?"
5 Wakahojiana wao kwa wao wakisema,
"Kama tukisema, 'Ulitoka mbinguni,' atatuuliza,
'Mbona hamkumwamini?' 6 Lakini tukisema,
'Ulitoka kwa wanadamu,' watu wote watatupiga
mawe, kwa sababu wanaamini kwamba Yohana
alikuwa nabii."
7 Basi wakajibu, "Hatujui ulikotoka."
8 Yesu akawaambia, "Wala mimi sitawaambia
ni kwa mamlaka gani ninatenda mambo haya."

### *Mfano Wa Wapangaji Waovu*
### *(Mathayo 21:33-46; Marko 12:1-12)*

9 Akaendelea kuwaambia watu mfano huu:
"Mtu mmoja alipanda shamba la mizabibu,
akalikodisha kwa wakulima fulani, kisha
akasafiri kwa muda mrefu. 10 Wakati wa
mavuno ulipofika, akamtuma mtumishi wake
kwa hao wapangaji ili wampe sehemu ya
mavuno ya shamba la mizabibu. Lakini wale
wakulima wakampiga, wakamfukuza mikono
mitupu. 11 Akamtuma mtumishi mwingine, huyo
naye wakampiga, wakamfanyia mambo ya aibu

na kumfukuza. 12 Bado akamtuma na mwingine
wa tatu, huyu pia wakamjeruhi na kumtupa nje
ya shamba.

13 “Basi yule mwenye shamba la mizabibu
akasema, ‘Nifanye nini? Nitamtuma mwanangu
mpendwa, huenda yeye watamheshimu.’

14 “Lakini wale wapangaji walipomwona,
wakasemezana wao kwa wao. Wakasema, ‘Huyu
ndiye mrithi. Basi na tumuue ili urithi uwe
wetu.’ 15 Kwa hiyo wakamtupa nje ya shamba
la mizabibu, wakamuua.”

“Sasa basi yule mwenye shamba la mizabibu
atawafanyia nini wapangaji hawa? 16 Atakuja na
kuwaua hao wapangaji, na kuwapa wapangaji
wengine hilo shamba la mizabibu.”

Watu waliposikia hayo wakasema, “Mungu
apishie mbali jambo hili lisitokee!”

17 Lakini Yesu akawakazia macho, akasema,
“Basi ni nini maana ya yale yaliyoandikwa:

“ ‘Jiwe walilolikataa waashi,
limekuwa jiwe kuu la pembeni’?

18 Kila mtu aangukaye juu ya jiwe hilo atavunjika
vipande vipande, lakini yule litakayemwangukia
atasagwa kabisa.”

19 Walimu wa sheria na viongozi wa makuhani
wakatafuta njia ya kumkamata mara moja, kwa
sababu walifahamu kwamba amesema mfano
huo kwa ajili yao. Lakini waliwaogopa watu.

*Kumlipa Kaisari Kodi*
*(Mathayo 22:15-22; Marko 12:13-17)*

20 Kwa hiyo wakawa wanamchunguza na kutuma wapelelezi waliojifanya kuwa wenye haki

ili wapate kumtega kwa maneno asemayo, ili
wamtie katika uwezo na mamlaka ya mtawala.
21 Hivyo wale wapelelezi wakamuuliza, “Mwal-
imu, tunajua unasema na kufundisha yaliyo
kweli wala humpendelei mtu, bali wafundisha
njia ya Mungu katika kweli. 22 Je, ni halali sisi
kulipa kodi kwa Kaisari, au la?”
23 Lakini Yesu akatambua hila yao, kwa hiyo
akawaambia, 24 “Nionyesheni dinari. Je, sura
hii na maandishi haya yaliyoko juu yake ni vya
nani?”
25 Wakamjibu, “Ni vya Kaisari.”

Akawaambia, “Basi mpeni Kaisari kilicho cha Kaisari, naye Mungu mpeni kilicho cha Mungu.”

26 Wakashindwa kumkamata kwa yale
aliyokuwa amesema hadharani. Nao
wakashangazwa mno na majibu yake,
wakanyamaza kimya.

### *Ufufuo Na Ndoa*
### *(Mathayo 22:23-33; Marko 12:18-27)*

27 Baadhi ya Masadukayo, wale wasemao
kwamba hakuna ufufuo wa wafu, wakamjia
Yesu na kumuuliza, 28 “Mwalimu, Mose ali-
tuandikia kwamba kama ndugu wa mtu akifa
na kumwacha mkewe bila mtoto, basi huyo mtu
inampasa amwoe huyo mjane ili amzalie ndugu
yake watoto. 29 Basi palikuwepo ndugu saba.
Yule wa kwanza akaoa, akafa bila kuzaa mtoto.
30 Kisha yule wa pili akamwoa huyo mjane, naye
akafa bila mtoto, 31 naye wa tatu pia akam-
woa. Vivyo hivyo ndugu wote saba wakawa
wamemwoa huyo mwanamke, na wote wakafa

pasipo yeyote kupata mtoto. 32 Mwishowe, yule
mwanamke naye akafa. 33 Sasa basi, siku ya
ufufuo huyo mwanamke atakuwa mke wa nani,
maana aliolewa na ndugu wote saba?”
34 Yesu akawajibu, “Katika maisha haya watu
huoa na kuolewa. 35 Lakini wale ambao wame-
hesabiwa kwamba wanastahili kupata nafasi
katika ulimwengu ule na katika ufufuo wa wafu,
hawaoi wala hawaolewi. 36 Hawa hawawezi
kufa tena, kwa maana wao ni kama malaika.
Wao ni watoto wa Mungu, kwa sababu ni
watoto wa ufufuo. 37 Hata Mose alidhi-
hirisha kuwa wafu wanafufuka, kwa habari ya
kile kichaka kilichokuwa kikiwaka moto bila
kuteketea, alipomwita Bwana, ‘Mungu wa Abra-
hamu, Mungu wa Isaki, na Mungu wa Yakobo.’
38 Yeye si Mungu wa wafu, bali wa walio hai, kwa
kuwa kwake wote ni hai.”
39 Baadhi ya walimu wa sheria wakasema,
“Mwalimu, umesema sawasawa kabisa!”
40 Baada ya hayo hakuna mtu aliyethubutu
kumuuliza maswali tena.

### *Kristo Ni Mwana Wa Nani?*
### *(Mathayo 22:41-46; Marko 12:35-37)*

41 Kisha Yesu akawaambia, “Imekuwaje basi
wao husema Kristo*ni Mwana wa Daudi?
42 Daudi mwenyewe anasema katika Kitabu cha
Zaburi:
“ ‘Bwana alimwambia Bwana wangu:
“Keti mkono wangu wa kuume,
43 hadi nitakapowaweka adui zako
chini ya miguu yako.” ’

* **20:41** Kristo maana yake ni Masiya, yaani Aliyetiwa mafuta.

44 Ikiwa Daudi anamwita yeye 'Bwana,' basi
atakuwaje mwanawe?"

*Yesu Awashutumu Walimu Wa Sheria*
*(Mathayo 23:1-36; Marko 12:38-40)*

45 Wakati watu wote walikuwa wanam-
sikiliza, Yesu akawaambia wanafunzi wake,
46 "Jihadharini na walimu wa sheria. Wao
hupenda kutembea wakiwa wamevaa mavazi
marefu, na kusalimiwa kwa heshima masokoni.
Hupenda kukaa kwenye viti vya mbele katika
masinagogi, na kukaa kwenye nafasi za heshima
katika karamu. 47 Wao hula nyumba za wajane,
na ili waonekane kuwa wema, wanasali sala
ndefu. Watu kama hawa watapata hukumu iliyo
kuu sana."

# 21

*Sadaka Ya Mjane*
*(Marko 12:41-44)*

1 Yesu alipoinua macho yake, aliwaona mata-
jiri wakiweka sadaka zao kwenye sanduku la
hazina ya Hekalu. 2 Akamwona pia mjane
mmoja maskini akiweka humo sarafu mbili
ndogo za shaba. 3 Yesu akasema, "Amin,
nawaambia, huyu mjane maskini ameweka
humo zaidi ya watu wengine wote. 4 Hawa watu
wengine wote wametoa sadaka kutokana na
wingi wa mali zao. Lakini huyu mjane ametoa
kutokana na umaskini wake vyote alivyokuwa
navyo, hata kile alichohitaji ili kuishi."

*Dalili Za Siku Za Mwisho*
*(Mathayo 24:1-2; Marko 13:1-2)*

[5] Baadhi ya wanafunzi wake wakawa wanam-
wonyesha jinsi Hekalu lilivyopambwa kwa
mawe mazuri na kwa vitu vilivyotolewa kuwa
sadaka kwa Mungu. Lakini Yesu akawaam-
bia, [6] "Kuhusu haya mnayoyaona hapa, wakati
utafika ambapo hakuna jiwe moja litakalobaki
juu ya jingine, bali kila moja litabomolewa."

### *Mateso*
### *(Mathayo 24:3-14; Marko 13:3-13)*

[7] Wakamuuliza, "Mwalimu, mambo haya
yatatukia lini? Ni dalili gani itaonyesha kwamba
yanakaribia kutendeka?"
[8] Yesu akawajibu, "Jihadharini msije mkadan-
ganywa. Maana wengi watakuja kwa Jina langu,
wakidai, 'Mimi ndiye,' na, 'Wakati umekaribia.'
Msiwafuate. [9] Lakini msikiapo habari za vita na
machafuko, msiogope. Kwa maana hayo ni laz-
ima yatokee kwanza, ila ule mwisho hautakuja
wakati huo."
[10] Kisha akawaambia: "Taifa litainuka dhidi
ya taifa jingine, na ufalme mmoja dhidi ya
ufalme mwingine. [11] Kutakuwa na mitetemeko
mikubwa ya ardhi, na njaa kali, na magonjwa
ya kuambukiza katika sehemu mbalimbali. Pia
kutakuwa na matukio ya kutisha na ishara kuu
kutoka mbinguni.
[12] "Lakini kabla yote hayajatokea,
watawakamata ninyi na kuwatesa. Watawatia
mikononi mwa wakuu wa masinagogi na
kuwafunga magerezani. Nanyi mtapelekwa
mbele ya wafalme na watawala kwa ajili
ya Jina langu. [13] Hii itawapa nafasi ya
kushuhudia. [14] Lakini kusudieni mioyoni

mwenu msisumbuke awali kuhusu mtakalosema
mbele ya mashtaka. [15] Kwa maana nitawapa
maneno na hekima ambayo hakuna hata adui
yenu mmoja atakayeweza kushindana nayo wala
kuipinga. [16] Mtasalitiwa hata na wazazi, ndugu,
jamaa na marafiki, na baadhi yenu watawaua.
[17] Mtachukiwa na watu wote kwa ajili ya Jina
langu. [18] Lakini hapatakuwa na unywele mmoja
wa kichwa chenu utakaoangamia. [19] Kwa
kuvumilia mtaokoa roho zenu.

### *Kuharibiwa Kwa Yerusalemu Kwatabiriwa (Mathayo 24:15-21; Marko 13:14-19)*

[20] “Mtakapoona mji wa Yerusalemu umezun-
gukwa na majeshi, basi fahamuni kwamba
kuharibiwa kwake kumekaribia. [21] Wakati
huo, wale walio Uyahudi wakimbilie milimani,
walio mjini Yerusalemu watoke humo, nao wale
walioko mashambani wasiingie mjini. [22] Kwa
sababu huu utakuwa ni wakati wa adhabu ili
kutimiza yote yaliyoandikwa. [23] Ole wao wenye
mimba na wale wanaonyonyesha watoto siku
hizo! Kutakuwa na dhiki kuu katika nchi na
ghadhabu juu ya hawa watu. [24] Wataanguka kwa
makali ya upanga, na wengine watachukuliwa
kuwa mateka katika mataifa yote. Nao mji wa
Yerusalemu utakanyagwa na watu wa Mataifa
hadi muda wa hao watu wa Mataifa utimie.

### *Kuja Kwa Mwana Wa Adamu (Mathayo 24:29-35; Marko 13:24-31)*

[25] “Kutakuwa na ishara katika jua, mwezi
na nyota. Hapa duniani, mataifa yatakuwa
katika dhiki na fadhaa kutokana na ngurumo

na misukosuko ya bahari. 26 Watu wataz-
imia roho kutokana na hofu kuu na kuyaona
yale mambo yanayotokea duniani, kwa maana
nguvu za angani zitatikisika. 27 Wakati huo
ndipo watakapomwona Mwana wa Adamu akija
mawinguni pamoja na uweza na utukufu mkuu.
28 Mambo haya yatakapoanza kutendeka, sima-
meni na mkaviinue vichwa vyenu, kwa sababu
ukombozi wenu umekaribia.”

29 Akawaambia mfano huu: “Uangalieni mtini
na miti mingine yote. 30 Inapochipua ma-
jani, ninyi wenyewe mnaweza kuona na ku-
tambua wenyewe ya kuwa wakati wa kiangazi
umekaribia. 31 Vivyo hivyo, myaonapo mambo
haya yakitukia, mnatambua kwamba Ufalme wa
Mungu umekaribia.

32 “Amin, nawaambia, kizazi hiki haki-
tapita hadi mambo haya yote yawe yametimia.
33 Mbingu na nchi zitapita, lakini maneno yangu
hayatapita kamwe.”

### *Siku Ya Mwisho Itakuja Ghafula*

34 “Jihadharini mioyo yenu isije ikalemewa na
anasa, ulevi na fadhaa za maisha haya, nayo
siku ile ikawakuta ninyi bila kutazamia kama
vile mtego unasavyo. 35 Kwa maana kama vile
mtego unasavyo, ndivyo siku hiyo itakavyowa-
pata wanadamu wote waishio katika uso wa
dunia yote. 36 Kesheni daima na mwombe ili
mweze kuokoka na yale yote yatakayotokea na
kusimama mbele ya Mwana wa Adamu.”

37 Kila siku Yesu alikuwa akifundisha
Hekaluni, na jioni ilipofika, alikwenda zake

kwenye Mlima wa Mizeituni na kukaa huko
usiku kucha. 38 Nao watu wote walikuja asubuhi
na mapema Hekaluni ili kumsikiliza.

# 22

*Yuda Akubali Kumsaliti Yesu*
*(Mathayo 26:14-16; Marko 14:10-11)*

1 Wakati huu Sikukuu ya Mikate Isiyotiwa
Chachu, iitwayo Pasaka, ilikuwa imekaribia.
2 Viongozi wa makuhani na walimu wa sheria
walikuwa wanatafuta njia ya kumuua Yesu,
kwa sababu waliwaogopa watu. 3 Shetani
akamwingia Yuda, aliyeitwa Iskariote, mmoja
wa wale Kumi na Wawili. 4 Yuda akaenda kwa
viongozi wa makuhani na kwa maafisa wa wal-
inzi wa Hekalu, akazungumza nao jinsi ambavyo
angeweza kumsaliti Yesu. 5 Wakafurahi na
wakakubaliana kumpa fedha. 6 Naye akakubali,
akaanza kutafuta wakati uliofaa wa kumsaliti
Yesu kwao, wakati ambapo hakuna umati wa
watu.

*Maandalizi Ya Pasaka*
*(Mathayo 26:17-25; Marko 14:12-21; Yohana 13:21-30)*

7 Basi ikawadia siku ya Mikate Isiyotiwa
Chachu, siku ambayo mwana-kondoo wa Pasaka
huchinjwa. 8 Hivyo Yesu akawatuma Petro
na Yohana, akisema, "Nendeni mkatuandalie
chakula cha Pasaka ili tuweze kuila."

9 Wakamuuliza, "Unataka tukuandalie wapi?"

10 Yesu akawaambia, "Tazameni,
mtakapokuwa mkiingia mjini, mtakutana na
mwanaume amebeba mtungi wa maji. Mfuateni

mpaka kwenye nyumba atakayoingia. 11 Nanyi
mwambieni mwenye nyumba, 'Mwalimu
anauliza: Kiko wapi chumba cha wageni,
ambamo mimi na wanafunzi wangu tutakula
Pasaka?' 12 Atawaonyesha chumba kikubwa
ghorofani, kikiwa kimepambwa vizuri. Andaeni
humo."
13 Wakaenda, nao wakakuta kila kitu kama
Yesu alivyowaambia. Hivyo wakaiandaa Pasaka.

*Kuanzishwa Kwa Meza Ya Bwana*
*(Mathayo 26:31-35; Marko 14:27-31; Yohana 13:36-38)*

14 Wakati ulipowadia, Yesu akaketi mezani
pamoja na wale mitume wake. 15 Kisha
akawaambia, "Nimetamani sana kuila Pasaka hii
pamoja nanyi kabla ya kuteswa kwangu. 16 Kwa
maana, nawaambia, sitaila tena Pasaka mpaka
itakapotimizwa katika Ufalme wa Mungu."
17 Akiisha kukichukua kikombe, akashukuru,
akasema, "Chukueni hiki mnywe wote. 18 Kwa
maana nawaambia tangu sasa sitakunywa tena
katika uzao wa mzabibu, hadi Ufalme wa Mungu
utakapokuja."
19 Kisha akachukua mkate, akashukuru,
akaumega, na kuwapa, akisema, "Huu ni mwili
wangu unaotolewa kwa ajili yenu. Fanyeni hivi
kwa ukumbusho wangu."
20 Vivyo hivyo baada ya kula, akakitwaa
kikombe, akisema, "Kikombe hiki ni agano jipya
katika damu yangu, imwagikayo kwa ajili yenu.
21 Lakini mkono wake huyo atakayenisaliti uko
hapa mezani pamoja nami. 22 Mwana wa Adamu
anaenda zake kama ilivyokusudiwa. Lakini

ole wake mtu huyo amsalitiye." 23 Wakaanza
kuulizana wenyewe ni nani miongoni mwao
angeweza kufanya jambo hilo.

*Mabishano Kuhusu Ukuu*

24 Pia yakazuka mabishano katikati ya wana-
funzi kwamba ni nani aliyeonekana kuwa mkuu
kuliko wote miongoni mwao. 25 Yesu akawaam-
bia, "Wafalme na watu wa Mataifa huwatawala
watu kwa nguvu. Nao wenye mamlaka juu yao
hujiita 'Wafadhili.' 26 Lakini ninyi msifanane
nao. Bali yeye aliye mkuu kuliko wote miongoni
mwenu, inampasa kuwa kama yeye aliye mdogo
wa wote, naye atawalaye na awe kama yeye
ahudumuye. 27 Kwani ni nani aliye mkuu? Ni
yule aketiye mezani au ni yule ahudumuye? Si
ni yule aliyekaa mezani? Lakini mimi niko mion-
goni mwenu kama yule ahudumuye. 28 Ninyi
mmekuwa pamoja nami katika majaribu yangu.
29 Nami kama Baba yangu alivyonipa ufalme,
kadhalika mimi nami ninawapa ninyi, 30 ili
mpate kula na kunywa mezani pangu katika
karamu ya ufalme wangu, na kukaa katika viti
vya enzi, mkihukumu makabila kumi na mawili
ya Israeli."

*Yesu Atabiri Kuwa Petro Atamkana*

31 Yesu akasema, "Simoni, Simoni, sikiliza,
Shetani ameomba kuwapepeta ninyi wote kama
ngano. 32 Lakini nimekuombea wewe Simoni ili
imani yako isishindwe, nawe ukiisha kunirudia,
uwaimarishe ndugu zako."

33 Petro akajibu, "Bwana, niko tayari kwenda
pamoja nawe gerezani na hata kifoni."

34 Yesu akamjibu, "Ninakuambia Petro, kabla jogoo hajawika usiku wa leo, utakana mara tatu kwamba hunijui mimi."

### *Mfuko, Mkoba Na Upanga*

35 Kisha Yesu akawauliza, "Nilipowatuma bila mfuko, wala mkoba, wala viatu, mlipungukiwa na kitu chochote?"

Wakajibu, "La, hatukupungukiwa na kitu chochote."

36 Akawaambia, "Lakini sasa, aliye na mfuko
na auchukue, na aliye na mkoba vivyo hivyo.
Naye asiye na upanga, auze joho lake anunue
mmoja. 37 Kwa sababu, nawaambia, andiko
hili lazima litimizwe juu yangu, kwamba, 'Al-
ihesabiwa pamoja na wakosaji'; kwa kweli
yaliyoandikwa kunihusu mimi hayana budi ku-
timizwa."

38 Wanafunzi wake wakamwambia, "Bwana, tazama hapa kuna panga mbili."

Akawajibu, "Inatosha."

### *Yesu Aomba Kwenye Mlima Wa Mizeituni (Mathayo 26:36-46; Marko 14:32-42)*

39 Yesu akatoka, akaenda kwenye Mlima wa
Mizeituni kama ilivyokuwa kawaida yake, nao
wanafunzi wake wakamfuata. 40 Walipofika
huko, akawaambia wanafunzi wake, "Ombeni,
msije mkaingia majaribuni." 41 Akajitenga nao
kama umbali wa kutupa jiwe, akapiga magoti,
akaomba 42 akisema, "Baba, kama ni mapenzi
yako, niondolee kikombe hiki. Lakini si kama
nipendavyo, bali mapenzi yako yatendeke."
43 Malaika kutoka mbinguni akamtokea, akamtia

nguvu. 44 Naye akiwa katika maumivu makuu,
akaomba kwa bidii, nalo jasho lake likawa kama
matone ya damu yakidondoka ardhini.

45 Baada ya kuomba, akawarudia wanafunzi
wake akawakuta wamelala, wakiwa wamechoka
kutokana na huzuni. 46 Naye akawauliza,
"Mbona mmelala? Amkeni, mwombe ili msije
mkaingia majaribuni."

*Yesu Akamatwa*

*(Mathayo 26:47-56; Marko 14:43-50; Yohana 18:3-11)*

47 Yesu alipokuwa bado anazungumza, umati
mkubwa wa watu ukaja. Uliongozwa na Yuda,
ambaye alikuwa mmoja wa wale wanafunzi
Kumi na Wawili. Akamkaribia Yesu ili ambusu.
48 Lakini Yesu akamwambia, "Yuda, je, unamsaliti
Mwana wa Adamu kwa busu?"

49 Wafuasi wa Yesu walipoona yale yaliyokuwa
yanakaribia kutokea, wakasema, "Bwana,
tuwakatekate kwa panga zetu?" 50 Mmoja
wao akampiga mtumishi wa kuhani mkuu kwa
upanga, akamkata sikio la kuume.

51 Lakini Yesu akasema, "Acheni!" Akaligusa
lile sikio la yule mtu na kumponya.

52 Kisha Yesu akawaambia wale viongozi wa
makuhani, maafisa wa walinzi wa Hekalu,
pamoja na wazee waliokuwa wamekuja kumkamata,
"Mmekuja na panga na marungu, kana
kwamba mimi ni mnyang'anyi? 53 Siku kwa
siku nilikuwa pamoja nanyi Hekaluni lakini
hamkunikamata. Lakini hii ni saa yenu, wakati
giza linatawala!"

### *Petro Amkana Yesu*
### *(Mathayo 26:57-75; Marko 14:53-72; Yohana 18:12-27)*

54 Kisha wakamkamata Yesu, wakamchukua,
wakaenda naye mpaka nyumbani kwa kuhani
mkuu. Lakini Petro akafuata kwa mbali.
55 Walipokwisha kuwasha moto katikati ya ua
na kuketi pamoja, Petro naye akaketi pamoja
nao. 56 Mtumishi mmoja wa kike akamwona
kwa mwanga wa moto akiwa ameketi pale.
Akamtazama sana, akasema, “Huyu mtu pia
alikuwa pamoja na Yesu!”

57 Lakini Petro akakana, akasema, “Ewe
mwanamke, hata simjui!”

58 Baadaye kidogo, mtu mwingine alimwona
Petro akasema, “Wewe pia ni mmoja wao!”
Petro akajibu, “Wewe mtu, mimi sio mmoja
wao!”

59 Baada ya muda wa kama saa moja hivi, mtu
mwingine akazidi kusisitiza, “Kwa hakika huyu
mtu naye alikuwa pamoja na Yesu, kwa maana
yeye pia ni Mgalilaya.”

60 Petro akajibu, “Wewe mtu, mimi sijui
unalosema!” Wakati huo huo, akiwa bado
anazungumza, jogoo akawika. 61 Naye
Bwana akageuka, akamtazama Petro. Ndipo
Petro akakumbuka lile neno ambalo Bwana
alimwambia: “Kabla jogoo hajawika leo,
utanikana mara tatu.” 62 Naye akaenda nje,
akalia kwa majonzi.

### *Walinzi Wamdhihaki Yesu Na Kumpiga*
### *(Mathayo 26:67-68; Marko 14:65)*

63 Watu waliokuwa wanamlinda Yesu
wakaanza kumdhihaki na kumpiga.
64 Wakamfunga kitambaa machoni na
kumuuliza, “Tabiri! Tuambie ni nani
aliyekupiga?” 65 Wakaendelea kumtukana kwa
matusi mengi.

### *Yesu Apelekwa Mbele Ya Baraza*

*(Mathayo 26:59-66; Marko 14:55-64; Yohana 18:28-38)*

66 Kulipopambazuka, baraza la wazee wa
watu,* yaani viongozi wa makuhani na wal-
imu wa sheria, wakakutana pamoja, naye Yesu
akaletwa mbele yao. 67 Wakamwambia, “Kama
wewe ndiye Kristo,† tuambie.”

Yesu akawajibu, “Hata nikiwaambia ham-
taamini. 68 Nami nikiwauliza swali, hamtanijibu.
69 Lakini kuanzia sasa, Mwana wa Adamu ataketi
mkono wa kuume wa Mungu Mwenye Nguvu.”

70 Wote wakauliza, “Wewe basi ndiwe Mwana
wa Mungu?”

Yeye akawajibu, “Ninyi mwasema kwamba
mimi ndiye.”

71 Kisha wakasema, “Tuna haja gani tena ya
ushahidi zaidi? Tumesikia wenyewe kutoka
kinywani mwake.”

---

* **22:66** Baraza la wazee hapa ina maana ya Sanhedrin ambalo lilikuwa ndilo Baraza la juu kabisa la utawala wa Kiyahudi, lililoundwa na wazee 70 pamoja na kuhani mkuu. † **22:67** Kristo maana yake ni Masiya, yaani Aliyetiwa mafuta.

# 23

*Yesu Apelekwa Kwa Pilato*
*(Mathayo 27:1-14; Marko 15:1-5; Yohana 18:28-38)*

1 Kisha umati wote wa watu ukainuka na
kumpeleka Yesu kwa Pilato. 2 Nao wakaanza
kumshtaki wakisema: “Tumemwona huyu mtu
akipotosha taifa letu, akiwazuia watu wasilipe
kodi kwa Kaisari na kujiita kuwa yeye ni Kristo,*
mfalme.”

3 Basi Pilato akamuuliza Yesu, “Wewe ndiye
mfalme wa Wayahudi?”

Yesu akajibu, “Wewe wasema.”

4 Pilato akawaambia viongozi wa makuhani
na watu wote waliokuwepo, “Sioni sababu ya
kutosha kumshtaki mtu huyu!”

5 Lakini wao wakakazana kusema, “Anawachochea watu kwa mafundisho yake katika Uyahudi yote, tangu Galilaya alikoanzia, hadi sehemu hii!”

*Yesu Apelekwa Kwa Herode*

6 Pilato aliposikia hayo akauliza, “Huyu mtu
ni Mgalilaya?” 7 Alipofahamu kwamba Yesu
alikuwa chini ya mamlaka ya Herode, akampeleka kwa Herode, ambaye wakati huo alikuwa pia Yerusalemu.

8 Herode alipomwona Yesu alifurahi sana,
kwa sababu kwa muda mrefu alikuwa amesikia mambo mengi kumhusu yeye. Pia alitarajia kumwona akifanya miujiza kadha wa
kadha. 9 Herode akamuuliza maswali mengi,

* **23:2** Kristo maana yake ni Masiya, yaani Aliyetiwa mafuta.

lakini Yesu hakumjibu lolote. 10 Wakati huo
viongozi wa makuhani na walimu wa sheria
walikuwepo wakitoa mashtaka yao kwa nguvu
sana. 11 Herode na askari wake wakamdhihaki
Yesu na kumfanyia mzaha. Wakamvika vazi zuri
sana, wakamrudisha kwa Pilato. 12 Siku hiyo,
Herode na Pilato wakawa marafiki; kabla ya
jambo hili walikuwa na uadui kati yao.

*Yesu Ahukumiwa Kifo*

*(Mathayo 27:15-26; Marko 15:6-15; Yohana 18:39–19:16)*

13 Basi Pilato akawaita pamoja viongozi
wa makuhani, viongozi wengine na watu,
14 akawaambia, "Ninyi mlimleta huyu mtu
kwangu kana kwamba ni mtu anayewachochea
watu ili waasi. Nimemhoji mbele yenu nami
nimeona hakuna msingi wowote wa mashtaka
yenu dhidi yake. 15 Wala Herode hakumwona na
kosa lolote, ndiyo sababu amemrudisha kwetu.
Kama mnavyoona, mtu huyu hakufanya jambo
lolote linalostahili kifo. 16 Kwa hiyo nitaamuru
apigwe mijeledi na kumwachia." [ 17 Kwa kuwa
ilikuwa lazima kuwafungulia mfungwa mmoja
wakati wa Sikukuu.]

18 Ndipo watu wote wakapiga kelele kwa
pamoja, "Mwondoe mtu huyo! Tufungulie
Baraba!" 19 (Baraba alikuwa amefungwa
gerezani kwa sababu ya maasi yaliyokuwa
yametokea mjini, na kwa ajili ya uuaji.)

20 Pilato, akitaka kumwachia Yesu, akasema
nao tena. 21 Lakini wao wakaendelea kupiga
kelele wakisema, "Msulubishe! Msulubishe!"

22 Kwa mara ya tatu, Pilato akawauliza, "Kwani
amefanya kosa gani huyu mtu? Sikuona kwake
sababu yoyote inayostahili adhabu ya kifo. Kwa
hiyo nitaamuru apigwe mijeledi, na kisha nita-
mwachia."
23 Lakini watu wakazidi kupiga kelele kwa
nguvu zaidi, wakidai kwamba Yesu asulubiwe.
Hivyo, kelele zao zikashinda. 24 Kwa hiyo Pilato
akatoa hukumu kwamba madai yao yatimizwe.
25 Akamfungua yule mtu aliyekuwa amefungwa
gerezani kwa kuhusika katika uasi dhidi ya
serikali na mauaji. Akamkabidhi Yesu mikononi
mwao, wamfanyie watakavyo.

*Kusulubiwa Kwa Yesu*
*(Mathayo 27:32-44; Marko 15:21-32; Yohana 19:17-27)*

26 Walipokuwa wakienda naye, wakamkamata
mtu mmoja aitwaye Simoni mwenyeji wa Kirene,
aliyekuwa anapita zake kuingia mjini kutoka
shambani. Wakambebesha msalaba, wakam-
lazimisha auchukue nyuma ya Yesu. 27 Idadi
kubwa ya watu wakamfuata Yesu, wakiwamo
wanawake waliokuwa wakimlilia na kumwom-
bolezea. 28 Yesu akawageukia, akawaambia,
"Enyi binti za Yerusalemu, msinililie mimi bali
jililieni ninyi wenyewe na watoto wenu. 29 Kwa
maana wakati utafika mtakaposema, 'Wame-
barikiwa wanawake tasa, ambao matumbo yao
hayakuzaa, wala matiti yao hayakunyonyesha!'
30 Ndipo

" 'wataiambia milima, "Tuangukieni!"
na vilima, "Tufunikeni!" '

31 Kwa maana kama wamefanya hivi kwa mti
mbichi, kwa mti mkavu itakuwaje?"

32 Watu wengine wawili wahalifu,
walipelekwa pamoja na Yesu ili wakasulubiwe.
33 Walipofika mahali paitwapo Fuvu la Kichwa,
hapo ndipo walipomsulubisha Yesu pamoja
na hao wahalifu, mmoja upande wake wa
kuume na mwingine upande wake wa kushoto.
34 Yesu akasema, "Baba, wasamehe, kwa maana
hawajui walitendalo!" Wakagawana nguo zake
kwa kupiga kura.

35 Watu wakasimama hapo wakimwangalia,
nao viongozi wa Wayahudi wakamdhihaki
wakisema, "Aliokoa wengine! Ajiokoe
mwenyewe basi, kama yeye ndiye Kristo wa
Mungu, Mteule wake."

36 Askari nao wakaja, wakamdhihaki. Wakam-
letea siki ili anywe, 37 na wakamwambia,
"Kama wewe ni Mfalme wa Wayahudi, jiokoe
mwenyewe."

38 Kwenye msalaba juu ya kichwa chake, ku-
likuwa na maandishi haya: HUYU NDIYE MFALME
WA WAYAHUDI.

Maandishi haya yalikuwa yameandikwa kwa
lugha za Kiyunani, Kilatini na Kiebrania.

39 Mmoja wa wale wahalifu waliosulubiwa
pamoja naye akamtukana, akasema: "Wewe si
ndiye Kristo? Jiokoe mwenyewe na utuokoe na
sisi."

40 Lakini yule mhalifu mwingine akamkemea
mwenzake, akasema, "Je, wewe humwogopi
Mungu, wakati uko kwenye adhabu iyo hiyo?

41 Sisi tumehukumiwa kwa haki kwa kuwa tu-
napata tunayostahili kwa ajili ya matendo yetu.
Lakini huyu mtu hajafanya kosa lolote.”

42 Kisha akasema, “Yesu, unikumbuke
utakapokuja katika Ufalme wako.”

43 Yesu akamjibu, “Amin, nakuambia, leo hii
utakuwa pamoja nami Paradiso.”†

*Kifo Cha Yesu*

*(Mathayo 27:45-56; Marko 15:33-41; Yohana 19:28-30)*

44 Ilikuwa kama saa sita mchana, nalo giza
likafunika nchi yote hadi saa tisa, 45 kwa sababu
jua liliacha kutoa nuru. Pazia la Hekalu
likachanika vipande viwili. 46 Yesu akapaza
sauti yake akasema, “Baba, mikononi mwako
naikabidhi roho yangu.” Baada ya kusema haya,
akakata roho.

47 Yule jemadari alipoona yaliyotukia, akam-
sifu Mungu, akasema, “Hakika, mtu huyu
alikuwa mwenye haki.” 48 Watu wote waliokuwa
wamekusanyika hapo kushuhudia tukio hili
walipoyaona hayo, wakapigapiga vifua vyao
kwa huzuni na kwenda zao. 49 Lakini wale
wote waliomfahamu, pamoja na wale wanawake
waliokuwa wamemfuata kutoka Galilaya, walisi-
mama kwa mbali wakiyatazama mambo haya.

*Maziko Ya Yesu*

*(Mathayo 27:57-61; Marko 15:42-47; Yohana 19:38-42)*

---

† **23:43** Paradiso maana yake bustani nzuri, hapa ina maana mahali zinapokwenda roho za wacha Mungu, yaani watakatifu.

50 Basi kulikuwa na mtu mmoja mwema na
mwenye haki, jina lake Yosefu. Yeye alikuwa
mjumbe wa Baraza la Wayahudi,‡ 51 lakini yeye
hakuwa amekubaliana na maamuzi na vitendo
vya viongozi wenzake. Huyu alikuwa mwenyeji
wa Arimathaya huko Uyahudi, naye alikuwa
anaungojea Ufalme wa Mungu kwa matarajio
makubwa. 52 Yosefu alikwenda kwa Pilato,
akaomba apewe mwili wa Yesu. 53 Akaushusha
kutoka msalabani, akaufunga katika kitambaa
cha kitani safi, na kuuweka katika kaburi lililo-
chongwa kwenye mwamba, ambalo halikuwa
limezikiwa mtu mwingine bado. 54 Ilikuwa
Siku ya Maandalizi, nayo Sabato ilikuwa karibu
kuanza.
55 Wale wanawake waliokuwa wamekuja
pamoja na Yesu wakimfuata kutoka Galilaya
wakamfuata Yosefu, wakaliona kaburi na jinsi
mwili wa Yesu ulivyolazwa. 56 Kisha wakarudi
nyumbani, wakaandaa manukato na marhamu
ya kuupaka huo mwili. Lakini wakapumzika
siku ya Sabato kama ilivyoamriwa.

# 24

*Kufufuka Kwa Yesu*

*(Mathayo 28:1-10; Marko 16:1-8; Yohana 20:1-10)*

1 Mnamo siku ya kwanza ya juma, alfajiri
na mapema, wale wanawake walichukua

‡ **23:50** Baraza la Wayahudi hapa ina maana ya Sanhedrin ambalo lilikuwa ndilo baraza la juu kabisa la utawala wa Kiyahudi, lililoundwa na wazee 70 pamoja na kuhani mkuu.

yale manukato waliyokuwa wameyaandaa,
wakaenda kaburini. 2 Wakakuta lile jiwe
limevingirishwa kutoka kwenye kaburi, 3 lakini
walipoingia ndani, hawakuuona mwili wa
Bwana Yesu. 4 Walipokuwa wanashangaa juu
ya jambo hili, ghafula watu wawili waliokuwa
wamevaa mavazi yanayong'aa kama umeme
wakasimama karibu nao. 5 Wale wanawake,
wakiwa na hofu, wakainamisha nyuso zao
mpaka chini. Lakini wale watu wakawaambia,
"Kwa nini mnamtafuta aliye hai miongoni mwa
wafu? 6 Hayuko hapa; amefufuka! Kumbukeni
alivyowaambia alipokuwa bado yuko pamoja
nanyi huko Galilaya kwamba: 7 'Ilikuwa lazima
Mwana wa Adamu atiwe mikononi mwa watu
wenye dhambi na waovu ili asulubiwe, na siku
ya tatu afufuke.' " 8 Ndipo wakayakumbuka
maneno ya Yesu.
9 Waliporudi kutoka huko kaburini,
wakawaeleza wale wanafunzi kumi na mmoja
pamoja na wengine wote mambo haya yote.
10 Basi Maria Magdalene, Yoana, na Maria
mama yake Yakobo, pamoja na wanawake
wengine waliofuatana nao ndio waliwaelezea
mitume habari hizi. 11 Lakini hawakuwasadiki
hao wanawake, kwa sababu maneno yao
yalionekana kama upuzi. 12 Hata hivyo, Petro
akainuka na kukimbia kwenda kule kaburini.
Alipoinama kuchungulia, akaona vile vitambaa
vya kitani, ila hakuona kitu kingine. Naye
akaenda zake akijiuliza nini kilichotokea.

*Njiani Kwenda Emau*
*(Marko 16:12-13)*

13 Ikawa siku iyo hiyo, wanafunzi wawili wa
Yesu walikuwa njiani wakienda kijiji kilichoitwa
Emau, yapata maili saba* kutoka Yerusalemu.
14 Walikuwa wakizungumza wao kwa wao
kuhusu mambo yote yaliyotukia. 15 Walipokuwa
wakizungumza na kujadiliana, Yesu mwenyewe
akaja akatembea pamoja nao, 16 lakini macho
yao yakazuiliwa ili wasimtambue.

17 Akawauliza, "Ni mambo gani haya mnay-
ozungumza wakati mnatembea?"

Wakasimama, nyuso zao zikionyesha huzuni.
18 Mmoja wao, aliyeitwa Kleopa, akamuuliza, "Je,
wewe ndiye peke yako mgeni huku Yerusalemu
ambaye hufahamu mambo yaliyotukia humo
siku hizi?"

19 Akawauliza, "Mambo gani?"

Wakamjibu, "Mambo ya Yesu wa Nazareti.
Yeye alikuwa nabii, mwenye uwezo mkuu katika
maneno yake na matendo yake, mbele za Mungu
na mbele ya wanadamu wote. 20 Viongozi wa
makuhani na viongozi wetu walimtoa ahuku-
miwe kufa, nao wakamsulubisha. 21 Lakini
tulikuwa tumetegemea kwamba yeye ndiye an-
gelikomboa Israeli. Zaidi ya hayo, leo ni siku
ya tatu tangu mambo haya yatokee. 22 Isitoshe,
baadhi ya wanawake katika kundi letu wame-
tushtusha. Walikwenda kaburini leo alfajiri,
23 lakini hawakuukuta mwili wake. Walirudi
wakasema wameona maono ya malaika ambao
waliwaambia kwamba Yesu yu hai. 24 Kisha

* **24:13** Maili saba ni kama kilomita 11.2.

baadhi ya wenzetu walikwenda kaburini waka-
likuta kama vile wale wanawake walivyokuwa
wamesema, lakini yeye hawakumwona."

25 Yesu akawaambia, "Ninyi ni wajinga kiasi
gani, nanyi ni wazito mioyoni mwenu kuamini
mambo yote yaliyonenwa na manabii! 26 Je,
haikumpasa Kristo†kuteswa kwa njia hiyo na
kisha aingie katika utukufu wake?" 27 Naye
akianzia na Sheria ya Mose na Manabii wote,
akawafafanulia jinsi Maandiko yalivyosema
kumhusu yeye.

28 Nao walipokaribia kile kijiji walichokuwa
wakienda, Yesu akawa kama anaendelea mbele.
29 Lakini wao wakamsihi sana akae nao,
wakisema, "Kaa hapa nasi, kwa maana sasa ni
jioni na usiku unaingia." Basi akaingia ndani
kukaa nao.

30 Alipokuwa mezani pamoja nao, akachukua
mkate, akashukuru, akaumega, akaanza kuwa-
gawia. 31 Ndipo macho yao yakafumbuliwa,
nao wakamtambua, naye akatoweka machoni
pao. Hawakumwona tena. 32 Wakaulizana wao
kwa wao, "Je, mioyo yetu haikuwakawaka kwa
furaha ndani yetu alipokuwa anazungumza nasi
njiani na kutufafanulia Maandiko?"

33 Wakaondoka mara, wakarudi Yerusalemu.
Wakawakuta wale wanafunzi kumi na mmoja
na wale waliokuwa pamoja nao, wamekusanyika
34 wakisema, "Ni kweli! Bwana amefufuka, naye
amemtokea Simoni." 35 Kisha wale wanafunzi

† **24:26** Kristo maana yake ni Masiya, yaani Aliyetiwa mafuta.

wawili wakaeleza yaliyotukia njiani na jinsi
walivyomtambua Yesu alipoumega mkate.

*Yesu Awatokea Wanafunzi Wake*

*(Mathayo 28:16-20; Marko 16:14-18; Yohana 20:19-23; Matendo 1:6-8)*

36 Walipokuwa bado wanazungumza hayo,
Yesu mwenyewe akasimama katikati yao,
akasema, "Amani iwe nanyi!"
37 Wakashtuka na kuogopa wakidhani
kwamba wameona mzuka. 38 Lakini Yesu
akawauliza, "Kwa nini mnaogopa? Kwa nini
mna shaka mioyoni mwenu? 39 Tazameni
mikono yangu na miguu yangu, mwone kuwa ni
mimi hasa. Niguseni mwone; kwa maana mzuka
hauna nyama na mifupa, kama mnionavyo kuwa
navyo."
40 Aliposema haya, akawaonyesha mikono na
miguu yake. 41 Wakashindwa kuamini kwa
ajili ya furaha na mshangao waliokuwa nao.
Akawauliza, "Mna chakula chochote hapa?"
42 Wakampa kipande cha samaki aliyeokwa,
43 naye akakichukua na kukila mbele yao.
44 Akawaambia, "Haya ndiyo yale niliy-
owaambia nilipokuwa bado niko pamoja nanyi,
kwamba yote yaliyoandikwa kunihusu mimi
katika Sheria ya Mose, Manabii na Zaburi
hayana budi kutimizwa."
45 Ndipo akafungua fahamu zao ili waweze
kuyaelewa Maandiko. 46 Akawaambia, "Haya
ndiyo yaliyoandikwa: Kristo atateswa na siku
ya tatu atafufuka kutoka kwa wafu. 47 Toba na
msamaha wa dhambi zitatangaziwa mataifa yote

kupitia jina lake kuanzia Yerusalemu. 48 Ninyi ni
mashahidi wa mambo haya.

### *Kuahidiwa Kwa Roho Mtakatifu*

49 "Tazama nitawatumia ahadi ya Baba yangu;
lakini kaeni humu mjini hadi mtakapovikwa
uwezo utokao juu."

### *Kupaa Kwa Yesu Mbinguni*
*(Marko 16:19-20; Matendo 1:9-11)*

50 Akiisha kuwaongoza mpaka kwenye vi-
unga vya Bethania, akainua mikono yake juu
na kuwabariki. 51 Alipokuwa anawabariki,
akawaacha, akachukuliwa mbinguni. 52 Kisha
wakamwabudu na kurudi Yerusalemu wakiwa
wamejawa na furaha kuu. 53 Nao wakadumu
ndani ya Hekalu wakimtukuza Mungu. Amen.

# Yohana

*Neno Alifanyika Mwili*

1 Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno
alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa
Mungu. 2 Tangu mwanzo huyo Neno alikuwa
pamoja na Mungu.

3 Vitu vyote viliumbwa kwa yeye, wala pasipo
yeye hakuna chochote kilichoumbwa ambacho
kimeumbwa. 4 Ndani yake ndimo ulimokuwa
uzima na huo uzima ulikuwa nuru ya watu.
5 Nuru hung'aa gizani nalo giza halikuishinda.

6 Alikuja mtu mmoja aliyetumwa kutoka kwa
Mungu, jina lake Yohana. 7 Alikuja kama
shahidi apate kuishuhudia hiyo nuru, ili kwa
kupitia kwake watu wote waweze kuamini.
8 Yeye mwenyewe hakuwa ile nuru, bali alikuja
kuishuhudia hiyo nuru. 9 Kwamba nuru hal-
isi, imwangaziayo kila mtu ilikuwa inakuja
ulimwenguni.

10 Huyo Neno alikuwako ulimwenguni na
ingawa ulimwengu uliumbwa kupitia kwake,
haukumtambua. 11 Alikuja kwa walio wake,
lakini wao hawakumpokea. 12 Bali wote waliom-
pokea, aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa
Mungu, ndio wale waliaminio jina lake. 13 Hawa
ndio wasiozaliwa kwa damu, wala kwa mapenzi
ya mwili au kwa mapenzi ya mtu, bali kwa
mapenzi ya Mungu.

[14] Neno alifanyika mwili, akakaa miongoni
mwetu, nasi tukauona utukufu wake, utukufu
kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba,
amejaa neema na kweli.
[15] Yohana alishuhudia habari zake, akapaza
sauti, akisema, “Huyu ndiye yule niliyewaambia
kwamba, ‘Yeye ajaye baada yangu ni mkuu kuni-
liko mimi, kwa kuwa alikuwepo kabla yangu.’ ”
[16] Kutokana na ukamilifu wake, sisi sote tume-
pokea neema juu ya neema. [17] Kwa kuwa sheria
ilitolewa kwa mkono wa Mose, lakini neema na
kweli imekuja kupitia Yesu Kristo. [18] Hakuna
mtu yeyote aliyemwona Mungu wakati wowote,
ila ni Mungu Mwana pekee, aliye kifuani mwa
Baba ndiye ambaye amemdhihirisha.

### *Ushuhuda Wa Yohana Mbatizaji*
### *(Mathayo 3:1-12; Marko 1:1-8; Luka 3:1-18)*

[19] Huu ndio ushuhuda wa Yohana wakati
Wayahudi walipowatuma makuhani na Walawi
kutoka Yerusalemu kumuuliza, “Wewe ni nani?”
[20] Yohana alikiri waziwazi pasipo kuficha
akasema, “Mimi si Kristo.”*
[21] Wakamuuliza, “Wewe ni nani basi? Je,
wewe ni Eliya?”

Yeye akajibu, “Hapana, mimi siye.”

“Je, wewe ni yule Nabii?”

Akajibu, “Hapana.”

[22] Ndipo wakasema, “Basi tuambie wewe ni
nani ili tupate jibu la kuwapelekea wale walio-
tutuma. Wewe wasemaje juu yako mwenyewe?”

---

* **1:20** Kristo maana yake ni Masiya, yaani Aliyetiwa mafuta.

23 Akawajibu kwa maneno ya nabii Isaya,
akisema, “Mimi ni sauti ya mtu aliaye nyikani,
‘Yanyoosheni mapito ya Bwana.’ ”
24 Basi walikuwa wametumwa watu kutoka
kwa Mafarisayo 25 wakamuuliza, “Kama wewe
si Kristo, wala si Eliya na wala si yule Nabii, kwa
nini basi unabatiza?”
26 Yohana akawajibu, “Mimi ninabatiza kwa
maji,† lakini katikati yenu yupo mtu msiyemjua.
27 Yeye ajaye baada yangu, sistahili hata kufun-
gua kamba za viatu vyake.”
28 Mambo haya yote yalitukia huko Betha-
nia, ng’ambo ya Mto Yordani, mahali Yohana
alipokuwa akibatiza.

### *Yesu Mwana-Kondoo Wa Mungu*

29 Siku iliyofuata, Yohana alimwona Yesu
akimjia akasema, “Tazama, Mwana-Kondoo wa
Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu!
30 Huyu ndiye yule niliyewaambia kwamba, ‘Mtu
anakuja baada yangu ambaye ni mkuu kuni-
liko mimi, kwa kuwa alikuwepo kabla yangu.’
31 Mimi mwenyewe sikumfahamu, lakini sababu
ya kuja nikibatiza kwa maji ni ili yeye apate
kufunuliwa kwa Israeli.”
32 Kisha Yohana akatoa ushuhuda huu: “Nil-
imwona Roho akishuka kutoka mbinguni kama
hua, akakaa juu yake. 33 Mimi nisingemtam-
bua, lakini yeye aliyenituma nibatize kwa maji
alikuwa ameniambia, ‘Yule mtu utakayemwona
Roho akimshukia na kukaa juu yake, huyo ndiye
atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu.’ 34 Mimi

† **1:26** Hapa tafsiri zingine zinasema ndani ya maji.

mwenyewe nimeona jambo hili na ninashuhudia
kuwa huyu ndiye Mwana wa Mungu."

### *Wanafunzi Wa Kwanza Wa Yesu*

35 Siku iliyofuata, Yohana alikuwa huko
tena pamoja na wanafunzi wake wawili.
36 Alipomwona Yesu akipita, akasema, "Tazama,
Mwana-Kondoo wa Mungu!"

37 Wale wanafunzi wawili walipomsikia
Yohana akisema haya, wakamfuata Yesu. 38 Yesu
akageuka, akawaona wakimfuata akawauliza,
"Mnataka nini?"

Wakamwambia, "Rabi," (maana yake Mwalimu), "Unaishi wapi?"

39 Yesu akawajibu, "Njooni, nanyi mtapaona!"

Hivyo wakaenda na kupaona mahali alipokuwa anaishi, wakakaa naye siku ile, kwa kuwa ilikuwa yapata saa kumi.

40 Andrea nduguye Simoni Petro, alikuwa
mmoja wa wale wawili waliosikia yale Yohana
aliyokuwa amesema, naye ndiye alimfuata Yesu.
41 Kitu cha kwanza Andrea alichofanya ni
kumtafuta Simoni nduguye na kumwambia,
"Tumemwona Masiya" (yaani, Kristo). 42 Naye
akamleta kwa Yesu.

Yesu akamwangalia na kusema, "Wewe ni Simoni mwana wa Yohana. Utaitwa Kefa" (ambalo limetafsiriwa Petro‡).

### *Yesu Awaita Filipo Na Nathanaeli*

---

‡ **1:42** Petro kwa Kiyunani au Kefa kwa Kiaramu; maana yake ni Kipande cha mwamba.

43 Siku iliyofuata Yesu aliamua kwenda
Galilaya. Akamkuta Filipo, akamwambia,
"Nifuate."
44 Basi Filipo alikuwa mwenyeji wa Bethsaida,
mji alikotoka Andrea na Petro. 45 Filipo naye
akamkuta Nathanaeli na kumwambia, "Tumem-
wona yeye ambaye Mose aliandika habari zake
katika Sheria na ambaye pia manabii waliandika
kumhusu, yaani, Yesu wa Nazareti, mwana wa
Yosefu."
46 Nathanaeli akauliza, "Nazareti! Je, kitu cho-
chote chema chaweza kutoka Nazareti?" Filipo
akamwambia, "Njoo uone."
47 Yesu alipomwona Nathanaeli anakaribia,
akanena habari zake akasema, "Tazama huyu ni
Mwisraeli kweli kweli; hana hila ndani yake."
48 Nathanaeli akamuuliza, "Umenifahamuje?"
Yesu akamjibu, "Nilikuona ulipokuwa bado
uko chini ya mtini, kabla hata Filipo hajakuita."
49 Nathanaeli akamwambia, "Rabi, wewe ni
Mwana wa Mungu! Wewe ni Mfalme wa Israeli!"
50 Yesu akamwambia, "Unaamini kwa kuwa
nilikuambia nilikuona ulipokuwa bado uko chini
ya mtini? Basi utaona mambo makuu zaidi
kuliko hilo." 51 Ndipo akawaambia, "Amin, amin
nawaambia, ninyi mtaona mbingu ikifunguka na
malaika wa Mungu wakipanda na kushuka juu
ya Mwana wa Adamu."

# 2

*Arusi Huko Kana*

1 Siku ya tatu kulikuwa na arusi katika mji
wa Kana ya Galilaya, naye mama yake Yesu

alikuwepo pale. 2 Yesu pamoja na wanafunzi
wake walikuwa wamealikwa arusini pia. 3 Divai
ilipokwisha, mama yake Yesu akamwambia,
“Wameishiwa na divai.”
4 Yesu akamwambia, “Mwanamke, nina nini
nawe? Saa yangu haijawadia.”
5 Mama yake akawaambia wale watumishi,
“Lolote atakalowaambia, fanyeni.”
6 Basi ilikuwepo mitungi sita ya kuhifadhia
maji iliyotengenezwa kwa mawe kwa ajili ya
kujitakasa kwa desturi ya Kiyahudi; kila mtungi
ungeweza kuchukua vipipa viwili au vitatu.*
7 Yesu akawaambia wale watumishi, “Ijazeni
hiyo mitungi maji.” Nao wakaijaza ile mitungi
mpaka juu.
8 Kisha akawaambia, “Sasa choteni hayo maji
kidogo, mpelekeeni mkuu wa meza.”
Hivyo wakachota, wakampelekea. 9 Yule mkuu
wa meza akayaonja yale maji ambayo yalikuwa
yamebadilika kuwa divai. Hakujua divai hiyo
ilikotoka ingawa wale watumishi waliochota
yale maji wao walifahamu. Basi akamwita
bwana arusi kando 10 akamwambia, “Watu wote
hutoa kwanza divai nzuri, kisha huleta ile divai
hafifu wageni wakisha kunywa vya kutosha,
lakini wewe umeiweka ile nzuri kupita zote
mpaka sasa.”
11 Huu, ndio uliokuwa muujiza wa kwanza
Yesu aliofanya Kana ya Galilaya. Hivyo Yesu alid-
hihirisha utukufu wake, nao wanafunzi wake
wakamwamini.

---

* **2:6** Kipipa kimoja chenye ujazo wa lita 40; hivyo kila mtungi ulikuwa na ujazo wa lita 80 au 120.

*Yesu Atakasa Hekalu*
*(Mathayo 21:12-13; Marko 11:15-17; Luka 19:45-46)*

12 Baada ya hayo, Yesu pamoja na mama
yake, ndugu zake na wanafunzi wake, walishuka
mpaka Kapernaumu, wakakaa huko siku chache.

13 Ilipokaribia wakati wa Pasaka ya Wayahudi,
Yesu alipanda kwenda Yerusalemu. 14 Huko
Hekaluni aliwakuta watu wakiuza ng'ombe, kon-
doo na njiwa, nao wengine walikuwa wameketi
mezani wakibadili fedha. 15 Akatengeneza
mjeledi kutokana na kamba, akawafukuza wote
kutoka kwenye eneo la Hekalu, pamoja na
kondoo na ng'ombe. Akazipindua meza za
wale wabadili fedha na kuzimwaga fedha zao.
16 Akawaambia wale waliokuwa wakiuza njiwa,
"Waondoeni hapa! Mnathubutuje kuifanya
nyumba ya Baba yangu kuwa mahali pa bi-
ashara?"

17 Wanafunzi wake wakakumbuka kuwa ime-
andikwa: "Wivu wa nyumba yako utanila."

18 Ndipo Wayahudi wakamuuliza, "Unaweza
kutuonyesha ishara gani ili kuthibitisha mam-
laka uliyo nayo ya kufanya mambo haya?"

19 Yesu akawajibu, "Libomoeni hili Hekalu,
nami nitalijenga tena kwa siku tatu!"

20 Wale Wayahudi wakamjibu, "Hekalu hili
lilijengwa kwa muda wa miaka arobaini na
sita, nawe wasema utalijenga kwa siku tatu?"
21 Lakini yeye Hekalu alilozungumzia ni mwili
wake. 22 Baada ya kufufuliwa kutoka kwa wafu,
wanafunzi wake wakakumbuka yale aliyokuwa

amesema. Ndipo wakayaamini Maandiko na
yale maneno Yesu aliyokuwa amesema.
23 Ikawa Yesu alipokuwa Yerusalemu kwenye
Sikukuu ya Pasaka, watu wengi waliona ishara
na miujiza aliyokuwa akifanya, wakaamini
katika jina lake. 24 Lakini Yesu hakujiaminisha
kwao kwa sababu aliwajua wanadamu wote.
25 Hakuhitaji ushuhuda wa mtu yeyote kuhusu
mtu, kwa kuwa alijua yote yaliyokuwa moyoni
mwa mtu.

# 3

*Nikodemo Amwendea Yesu Usiku*

1 Basi palikuwa na mtu mmoja Farisayo,
jina lake Nikodemo, mmoja wa Baraza la
Wayahudi* lililotawala. 2 Huyu alimjia Yesu
usiku akamwambia, “Rabi, tunajua kuwa wewe
ni mwalimu uliyetumwa na Mungu, kwa maana
hakuna mtu awezaye kufanya miujiza hii
uifanyayo wewe, kama Mungu hayuko pamoja
naye.”
3 Yesu akamjibu, “Amin, amin nakuambia,
hakuna mtu anayeweza kuuona Ufalme wa
Mungu kama hajazaliwa mara ya pili.”
4 Nikodemo akauliza, “Awezaje mtu kuzaliwa
wakati akiwa mzee? Hakika hawezi kuingia
mara ya pili kwenye tumbo la mama yake ili
azaliwe!”
5 Yesu akamwambia, “Amin, amin nakuambia,
hakuna mtu yeyote anayeweza kuingia Ufalme

---

* **3:1** Baraza la Wayahudi hapa ina maana ya Sanhedrin ambalo lilikuwa ndilo Baraza la juu kabisa la utawala wa Kiyahudi, lililoundwa na wazee 70 pamoja na kuhani mkuu.

wa Mungu kama hajazaliwa kwa maji na kwa
Roho. 6 Mwili huzaa mwili, lakini Roho huzaa
roho. 7 Kwa hiyo usishangae ninapokuambia
huna budi 'kuzaliwa mara ya pili.' 8 Upepo hu-
vuma popote upendapo. Mvumo wake unausikia
lakini huwezi ukafahamu utokako wala uen-
dako. Ndivyo ilivyo kwa kila mtu aliyezaliwa na
Roho."

9 Nikodemo akamuuliza, "Mambo haya
yanawezekanaje?"

10 Yesu akamwambia, "Wewe ni mwalimu
mashuhuri wa Waisraeli, nawe huelewi mambo
haya? 11 Amin, amin ninakuambia, sisi tu-
nazungumza lile tunalolijua na tunashuhudia
lile tuliloliona. Lakini ninyi watu hamkubali
ushuhuda wetu. 12 Nimewaambia mambo ya
duniani, nanyi hamkuniamini, mtaniaminije
basi nitakapowaambia mambo ya mbinguni?
13 Hakuna mtu yeyote aliyekwenda mbinguni
isipokuwa yeye aliyeshuka kutoka mbinguni,
yaani, Mwana wa Adamu. 14 Kama vile Mose
alivyomwinua yule nyoka kule jangwani, vivyo
hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa
juu. 15 Ili kila mtu amwaminiye awe na uzima
wa milele.

16 "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda
ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee,
ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe
na uzima wa milele. 17 Kwa maana Mungu
hakumtuma Mwanawe kuuhukumu ulimwengu,
bali kupitia kwake ulimwengu upate kuokolewa.
18 Yeyote amwaminiye hahukumiwi, lakini
asiyeamini amekwisha kuhukumiwa, kwa

sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa
Mungu. 19 Hii ndiyo hukumu kwamba: Nuru
imekuja ulimwenguni, nao watu wakapenda
giza kuliko nuru kwa sababu matendo yao ni
maovu. 20 Kwa kuwa kila atendaye maovu
huchukia nuru, wala haji kwenye nuru ili
matendo yake maovu yasifichuliwe. 21 Lakini
yule aishiye kwa ukweli huja kwenye nuru,
ili ionekane wazi kwamba matendo yake
yametendeka katika Mungu."

### *Ushuhuda Wa Yohana Mbatizaji Kuhusu Yesu*

22 Baada ya haya, Yesu na wanafunzi wake wa-
likwenda katika nchi ya Uyahudi, nao wakakaa
huko kwa muda na kubatiza. 23 Yohana naye
alikuwa akibatiza huko Ainoni karibu na Sal-
imu kwa sababu huko kulikuwa na maji tele.
Watu wazima wakamjia huko ili kubatizwa.
24 (Hii ilikuwa kabla Yohana hajatiwa gerezani).
25 Mashindano yakazuka kati ya baadhi ya
wanafunzi wa Yohana na Myahudi mmoja
kuhusu suala la desturi ya kunawa kwa utakaso.
26 Wakamwendea Yohana wakamwambia, "Rabi,
yule mtu aliyekuwa pamoja nawe ng'ambo ya
Mto Yordani, yule uliyeshuhudia habari zake,
sasa anabatiza na kila mtu anamwendea!"
27 Yohana akawajibu, "Hakuna mtu yeyote
awezaye kupata kitu chochote isipokuwa kile tu
alichopewa kutoka mbinguni. 28 Ninyi wenyewe
ni mashahidi wangu kwamba nilisema, 'Mimi
si Kristo,† ila nimetumwa nimtangulie.' 29 Bibi
arusi ni wa bwana arusi. Lakini rafiki yake

---

† **3:28** Kristo maana yake ni Masiya, yaani Aliyetiwa mafuta.

bwana arusi anayesimama karibu naye na kusik-
iliza kutoka kwake, hufurahi sana aisikiapo sauti
ya bwana arusi. Kwa sababu hii furaha yangu
imekamilika. 30 Yeye hana budi kuwa mkuu
zaidi na mimi nizidi kuwa mdogo.”

### *Yeye Aliyetoka Mbinguni*

31 “Yeye ajaye kutoka juu yu juu ya yote, yeye
aliye wa duniani ni wa dunia, naye huzungumza
mambo ya duniani. Yeye aliyekuja kutoka
mbinguni, yu juu ya yote. 32 Yeye hushuhudia
yale aliyoyaona na kuyasikia, lakini hakuna
yeyote anayekubali ushuhuda wake. 33 Lakini
yeyote anayekubali huo ushuhuda anathibitisha
kwamba, Mungu ni kweli. 34 Yeye aliyetumwa na
Mungu husema maneno ya Mungu, kwa kuwa
Mungu humtoa Roho pasipo kipimo. 35 Baba
anampenda Mwana, naye ametia vitu vyote
mikononi mwake. 36 Yeyote anayemwamini
Mwana ana uzima wa milele, lakini yeye
asiyemwamini Mwana hatauona uzima, bali
ghadhabu ya Mungu itakuwa juu yake.”

## 4

### *Yesu Azungumza Na Mwanamke Msamaria*

1 Mafarisayo wakasikia kwamba Yesu alikuwa
anapata na kubatiza wanafunzi wengi zaidi
kuliko Yohana, 2 ingawa kwa kweli si Yesu
mwenyewe aliyekuwa akibatiza, ila ni wana-
funzi wake. 3 Bwana alipojua mambo haya,
aliondoka Uyahudi akarudi tena Galilaya.
4 Wakati huo ilimlazimu apitie Samaria.
5 Akafika kwenye mji mmoja wa Samaria uitwao

Sikari, karibu na lile shamba ambalo Yakobo
alimpa mwanawe Yosefu. [6] Huko ndiko ku-
likokuwa na kile kisima cha Yakobo. Naye
Yesu alikuwa amechoka kwa kuwa alikuwa ame-
toka safarini. Akaketi karibu na hicho kisima.
Ilikuwa yapata saa sita mchana.

[7] Mwanamke mmoja Msamaria akaja
kuteka maji, Yesu akamwambia, "Naomba
maji ninywe." [8] (Wakati huo wanafunzi
wake walikuwa wamekwenda mjini kununua
chakula.)

[9] Yule mwanamke Msamaria akamjibu, "Wewe
ni Myahudi na mimi ni Msamaria. Yawezekanaje
uniombe nikupe maji ya kunywa?" (Wayahudi
walikuwa hawashirikiani kabisa na Wasamaria.)

[10] Yesu akajibu akamwambia, "Kama ungelijua
karama ya Mungu, naye ni nani anayekuambia,
Nipe maji ninywe, wewe ungelimwomba yeye,
naye angelikupa maji yaliyo hai."

[11] Yule mwanamke akamjibu, "Bwana, wewe
huna chombo cha kutekea maji na kisima hiki
ni kirefu. Hayo maji ya uzima utayapata wapi?
[12] Kwani wewe ni mkuu kuliko baba yetu Yakobo
ambaye alitupatia kisima hiki, ambacho yeye
pamoja na watoto wake na mifugo yake walik-
itumia?"

[13] Yesu akamjibu, "Kila mtu anayekunywa
maji ya kisima hiki ataona kiu tena. [14] Lakini
yeyote anywaye maji nitakayompa hataona kiu
kamwe. Maji nitakayompa yatakuwa ndani yake
chemchemi ya maji, yakibubujika uzima wa
milele."

15 Yule mwanamke akamwambia, “Bwana, tafadhali nipe maji hayo ili nisipate kiu tena na wala nisije tena hapa kuteka maji!”

16 Yesu akamjibu, “Nenda ukamwite mumeo, uje naye hapa.”

17 Yule mwanamke akajibu, “Sina mume.”

Yesu akamwambia, “Umesema kweli kuwa
huna mume. 18 Kwa maana umeshakuwa na wanaume watano na mwanaume unayeishi naye sasa si mume wako! Umesema ukweli.”

19 Yule mwanamke akasema, “Bwana, naona
bila shaka wewe ni nabii. 20 Baba zetu waliabudu kwenye mlima huu, lakini ninyi Wayahudi mnasema ni lazima tukaabudu huko Yerusalemu.”

21 Yesu akamjibu, “Mwanamke, niamini, wakati unakuja ambapo hamtamwabudu Baba katika mlima huu, wala huko Yerusalemu.
22 Ninyi Wasamaria mnaabudu msichokijua. Sisi Wayahudi tunamwabudu Mungu tunayemjua kwa sababu wokovu unatoka kwa Wayahudi.
23 Lakini saa yaja, tena ipo, ambapo wale waabuduo halisi, watamwabudu Baba katika roho na kweli. Watu wanaoabudu namna hii,
ndio Baba anawatafuta. 24 Mungu ni Roho na wote wanaomwabudu imewapasa kumwabudu katika roho na kweli.”

25 Yule mwanamke akamwambia, “Ninafahamu kwamba Masiya (aitwaye Kristo) anakuja. Yeye akija, atatueleza mambo yote.”

26 Yesu akamwambia, “Mimi ninayezungumza nawe, ndiye.”

27 Wakati huo wanafunzi wake wakarudi, wakashangaa sana kumwona akizungumza na

mwanamke. Lakini hakuna aliyemuuliza, “Unataka nini kwake?” Au “Kwa nini unazungumza naye?”
28 Yule mwanamke akaacha mtungi wake,
akarudi mjini akawaambia watu, 29 “Njooni
mkamwone mtu aliyeniambia kila kitu nilichotenda! Je, yawezekana huyu ndiye
Kristo?”* 30 Basi wakamiminika watu kutoka
mjini wakamwendea Yesu.
31 Wakati huo wanafunzi wake walikuwa wakimsihi, “Rabi, kula angalau chochote.”
32 Lakini yeye akawajibu, “Mimi ninacho chakula ambacho ninyi hamkifahamu.”
33 Basi wanafunzi wakaanza kuulizana, “Kuna
mtu ambaye amemletea chakula?” 34 Lakini
Yesu akawajibu, “Chakula changu ni kufanya mapenzi ya Mungu ambaye amenituma na kuikamilisha kazi yake.
35 Je, ninyi hamsemi, ‘Bado miezi minne tuvune?’ Inueni macho yenu myaangalie mashamba jinsi mazao yalivyo tayari kuvunwa!
36 Mvunaji tayari anapokea mshahara wake, naye anakusanya mazao kwa ajili ya uzima wa milele. Ili yeye apandaye na yeye avunaye wafurahi pamoja.
37 Hivyo kule
kusema, ‘Mmoja hupanda na mwingine huvuna,’
ni kweli kabisa. 38 Niliwatuma mkavune mazao
ambayo hamkupanda, wengine walifanya kazi ngumu, nanyi mmevuna faida ya taabu yao.”

### *Wasamaria Wengi Waamini*

39 Wasamaria wengi katika mji ule wakamwamini Yesu kwa sababu ya ushuhuda

* **4:29** Kristo maana yake ni Masiya, yaani Aliyetiwa mafuta.

wa yule mwanamke alipowaambia kwamba,
“Ameniambia kila kitu nilichotenda.” 40 Hivyo
wale Wasamaria walipomjia, wakamsihi akae
kwao. Naye akakaa huko siku mbili. 41 Kwa
sababu ya neno lake, watu wengi wakaamini.

42 Wakamwambia yule mwanamke, “Sasa tu-
naamini, wala si kwa sababu ya maneno yako
tu, bali kwa kuwa tumemsikia sisi wenyewe.
Tumejua hakika kweli ya kwamba huyu ndiye
Kristo, Mwokozi wa ulimwengu.”

### *Yesu Amponya Mwana Wa Afisa*

43 Baada ya zile siku mbili, Yesu aliondoka
kwenda Galilaya. 44 (Basi Yesu mwenyewe
alikuwa amesema kwamba nabii hapati hes-
hima katika nchi yake mwenyewe.) 45 Alipofika
Galilaya, Wagalilaya walimkaribisha, kwani
walikuwa wameona yale aliyoyatenda huko
Yerusalemu wakati wa Sikukuu ya Pasaka. Kwa
maana wao pia walikuwa wamehudhuria hiyo
Sikukuu.

46 Hivyo Yesu akaja tena mpaka Kana ya
Galilaya, kule alikokuwa amebadili maji kuwa
divai. Huko kulikuwepo na afisa mmoja wa
mfalme, ambaye mwanawe alikuwa mgonjwa
huko Kapernaumu. 47 Huyo mtu aliposikia
kwamba Yesu alikuwa amewasili Galilaya ku-
toka Uyahudi, alimwendea na kumwomba ili
aje kumponya mwanawe, aliyekuwa mgonjwa
karibu ya kufa.

48 Yesu akamwambia, “Ninyi watu msipoona
ishara na miujiza kamwe hamtaamini.”

49 Yule afisa wa mfalme akamwambia,
"Bwana, tafadhali shuka kabla mwanangu
hajafa."
50 Yesu akamjibu, "Enenda zako, mwanao yu
hai."
Yule afisa akaamini yale maneno Yesu
aliyomwambia, akaondoka akaenda zake.
51 Alipokuwa bado yuko njiani, akakutana
na watumishi wake wakamwambia kwamba
mwanawe yu mzima. 52 Akawauliza saa ambayo
alianza kupata nafuu. Wakamwambia, "Jana
yapata saa saba, homa ilimwacha."
53 Ndipo baba wa huyo mtoto akakumbuka
kuwa huo ndio wakati ambapo Yesu alikuwa
amemwambia, "Mwanao yu hai." Kwa hiyo
yeye pamoja na wote wa nyumbani mwake
wakamwamini Yesu.
54 Hii ilikuwa ishara ya pili ambayo Yesu
alifanya aliporudi Galilaya kutoka Uyahudi.

# 5

### *Yesu Amponya Mtu Kwenye Bwawa La Bethzatha*

1 Baada ya haya, kulikuwa na Sikukuu
ya Wayahudi, naye Yesu akapanda kwenda
Yerusalemu. 2 Huko Yerusalemu, karibu na
mlango uitwao Mlango wa Kondoo, palikuwa na
bwawa moja lililoitwa kwa Kiebrania Bethza-
tha,* ambalo lilikuwa limezungukwa na kumbi

* **5:2** Bethzatha ni neno la Kiebrania ambalo maana yake ni Nyumba ya mizeituni; mahali pengine limetajwa kama Bethesda kwa Kiaramu, yaani Nyumba ya huruma, na pengine kama Bethsaida, yaani Nyumba ya uvuvi.

tano. 3 Hapa palikuwa na idadi kubwa ya wa-
siojiweza, yaani, vipofu, viwete, na waliopooza
[wakingojea maji yatibuliwe. 4 Kwa maana
malaika alikuwa akishuka wakati fulani, akay-
atibua maji. Yule aliyekuwa wa kwanza kuingia
ndani baada ya maji kutibuliwa alipona ugonjwa
wowote aliokuwa nao]. 5 Mtu mmoja alikuwako
huko ambaye alikuwa ameugua kwa miaka the-
lathini na minane. 6 Yesu alipomwona akiwa
amelala hapo, naye akijua kuwa amekuwa hapo
kwa muda mrefu, akamwambia, "Je, wataka
kuponywa?"

7 Yule mgonjwa akamjibu, "Bwana, mimi sina
mtu wa kuniingiza bwawani maji yanapotibu-
liwa. Nami ninapotaka kutumbukia bwawani,
mtu mwingine huingia kabla yangu."

8 Yesu akamwambia, "Inuka! Chukua mkeka
wako na uende." 9 Mara yule mtu akapona,
akachukua mkeka wake, akaanza kutembea.

Basi siku hiyo ilikuwa siku ya Sabato. 10 Kwa
hiyo Wayahudi wakamwambia yule mtu aliye-
ponywa, "Leo ni Sabato, si halali wewe kubeba
mkeka wako."

11 Yeye akawajibu, "Yule mtu aliyeniponya
aliniambia, 'Chukua mkeka wako na uende.' "

12 Wakamuuliza, "Ni mtu gani huyo
aliyekuambia uchukue mkeka wako uende?"

13 Basi yule mtu aliyeponywa hakufahamu ni
nani aliyemponya, kwa sababu Yesu alikuwa
amejiondoa katika ule umati wa watu uliokuwa
hapo.

14 Baadaye Yesu akamkuta yule mtu
aliyemponya ndani ya Hekalu na kumwambia,

"Tazama umeponywa, usitende dhambi tena. La
sivyo, lisije likakupata jambo baya zaidi." 15 Yule
mtu akaenda, akawaambia wale Wayahudi
kuwa ni Yesu aliyemponya.

### *Uzima Kupitia Mwana*

16 Kwa hiyo Wayahudi wakaanza kumsumbua
Yesu, kwa sababu alikuwa anafanya mambo
kama hayo siku ya Sabato. 17 Yesu akawa-
jibu, "Baba yangu anafanya kazi yake daima
hata siku hii ya leo, nami pia ninafanya kazi."
18 Maneno haya yaliwaudhi sana viongozi wa
Wayahudi. Wakajaribu kila njia wapate jinsi ya
kumuua, kwani si kwamba alivunja Sabato tu,
bali alikuwa akimwita Mungu Baba yake, hivyo
kujifanya sawa na Mungu.

### *Mamlaka Ya Mwana Wa Mungu*

19 Yesu akawaambia, "Amin, amin nawaam-
bia, Mwana hawezi kufanya jambo lolote peke
yake, yeye aweza tu kufanya lile analomwona
Baba yake akifanya, kwa maana lolote afanyalo
Baba, Mwana pia hufanya vivyo hivyo. 20 Baba
ampenda Mwana na kumwonyesha yale am-
bayo yeye Baba mwenyewe anayafanya, naye
atamwonyesha kazi kuu kuliko hizi ili mpate
kushangaa. 21 Hakika kama vile Baba awa-
fufuavyo wafu na kuwapa uzima, vivyo hivyo
Mwana huwapa uzima wale anaopenda. 22 Wala
Baba hamhukumu mtu yeyote, lakini hukumu
yote amempa Mwana, 23 ili wote wamheshimu
Mwana kama vile wanavyomheshimu Baba.
Yeyote asiyemheshimu Mwana, hamheshimu
Baba aliyemtuma.

24 “Amin, amin nawaambia, yeyote anayesikia
maneno yangu na kumwamini yeye aliyenituma,
anao uzima wa milele, naye hatahukumiwa,
bali amepita kutoka mautini, na kuingia uzi-
mani. 25 Amin, amin nawaambia, saa yaja, nayo
saa ipo, wafu watakapoisikia sauti ya Mwana
wa Mungu, nao watakaoisikia watakuwa hai.
26 Kama vile Baba alivyo na uzima ndani yake,
vivyo hivyo amempa Mwana kuwa na uzima
ndani yake. 27 Naye amempa Mwanawe mam-
laka ya kuhukumu kwa kuwa yeye ni Mwana wa
Adamu.
28 “Msishangae kusikia haya, kwa maana
saa inakuja ambapo wale walio makaburini
wataisikia sauti yake. 29 Nao watatoka nje, wale
waliotenda mema watafufuka wapate uzima na
wale waliotenda maovu, watafufuka wahuku-
miwe.

### *Shuhuda Kuhusu Yesu*

30 “Mimi siwezi kufanya jambo lolote peke
yangu. Ninavyosikia ndivyo ninavyohukumu,
nayo hukumu yangu ni ya haki kwa kuwa
sitafuti kufanya mapenzi yangu mwenyewe, bali
mapenzi yake yeye aliyenituma.
31 “Kama ningejishuhudia mimi mwenyewe,
ushuhuda wangu si kweli. 32 Lakini yuko
mwingine anishuhudiaye na ninajua kwamba
ushuhuda wake ni wa kweli.
33 “Mlituma wajumbe kwa Yohana, naye
akashuhudia juu ya kweli. 34 Si kwamba
naukubali ushuhuda wa mwanadamu, la, bali
ninalitaja hili kusudi ninyi mpate kuokolewa.
35 Yohana alikuwa taa iliyowaka na kutoa nuru,

nanyi kwa muda mlichagua kuifurahia nuru
yake.
36 “Lakini ninao ushuhuda mkuu zaidi kuliko
wa Yohana. Kazi zile nizifanyazo, zinashuhu-
dia juu yangu, zile ambazo Baba amenituma
nizikamilishe, naam, ishara hizi ninazofanya, zi-
nashuhudia kuwa Baba ndiye alinituma. 37 Naye
Baba mwenyewe ameshuhudia juu yangu. Ham-
japata kamwe kuisikia sauti yake wala kuona
umbo lake, 38 wala hamna neno lake ndani yenu,
kwa sababu hamkumwamini yeye aliyetumwa
naye. 39 Ninyi mnachunguza Maandiko mkid-
hani ya kuwa ndani yake mna uzima wa milele,
maandiko haya ndiyo yanayonishuhudia Mimi.
40 Lakini mnakataa kuja kwangu ili mpate uzima.
41 “Mimi sitafuti kutukuzwa na wanadamu.
42 Lakini ninajua kwamba hamna upendo wa
Mungu mioyoni mwenu. 43 Mimi nimekuja kwa
jina la Baba yangu, nanyi hamnipokei, lakini mtu
mwingine akija kwa jina lake mwenyewe, mtam-
pokea. 44 Ninyi mwawezaje kuamini ikiwa mna-
peana utukufu ninyi kwa ninyi, lakini hamna
bidii kupata utukufu utokao kwa Mungu?
45 “Lakini msidhani kuwa mimi nitawash-
taki mbele za Baba, mshtaki wenu ni Mose,
ambaye mmemwekea tumaini lenu. 46 Kama
mngelimwamini Mose, mngeliniamini na mimi
kwa maana aliandika habari zangu. 47 Lakini
ikiwa hamwamini aliyoandika Mose, mtaaminije
ninayoyasema?”

*Yesu Alisha Wanaume 5,000*
*(Mathayo 14:13-21; Marko 6:30-44; Luka 9:10-17)*

1 Baada ya haya, Yesu alikwenda ng'ambo ya
Bahari ya Galilaya, ambayo pia huitwa Bahari
ya Tiberia. 2 Umati mkubwa wa watu uliendelea
kumfuata, kwa sababu waliona ishara nyingi
za miujiza alizofanya kwa wagonjwa. 3 Kisha
Yesu akapanda mlimani akaketi huko pamoja na
wanafunzi wake. 4 Pasaka ya Wayahudi ilikuwa
imekaribia.
5 Yesu alipotazama na kuuona ule umati
mkubwa wa watu ukimjia, akamwambia Filipo,
"Tutanunua wapi mikate ili watu hawa wale?"
6 Aliuliza swali hili kumpima, kwa maana alisha-
jua la kufanya.
7 Filipo akamjibu, "Hata fedha kiasi cha di-
nari mia mbili,* hazitoshi kununua mikate ya
kuwapa watu hawa ili kila mtu apate kidogo."
8 Mmoja wa wanafunzi wake aitwaye Andrea,
ndugu yake Simoni Petro, akamwambia, 9 "Hapa
kuna mvulana mmoja mwenye mikate mitano ya
shayiri na samaki wawili wadogo. Lakini hivi
vitatosha nini kwa umati huu wote?"
10 Yesu akasema, "Waketisheni watu chini."
Palikuwa na majani mengi katika eneo lile, nao
watu wakaketi. Palikuwa na wanaume wapatao
5,000. 11 Ndipo Yesu akachukua ile mikate,
akamshukuru Mungu na kuwagawia wale watu
waliokuwa wameketi. Akafanya vivyo hivyo na
wale samaki. Kila mtu akapata kadiri alivyotaka.

* **6:7** Dinari 200 ni sawa na mshahara wa kibarua wa siku 200; mshahara wa kibarua ulikuwa dinari moja kwa siku.

12 Watu wote walipokwisha kula na kushiba,
akawaambia wanafunzi wake, “Kusanyeni
vipande vilivyobaki vya ile mikate, kisipotee
chochote.” 13 Hivyo wakavikusanya, wakajaza
vikapu kumi na viwili kwa vipande vya ile
mikate mitano ya shayiri na samaki wale wawili
wadogo vilivyobakishwa na waliokula.
14 Baada ya watu kuona muujiza ule Yesu
aliofanya, walianza kusema, “Hakika huyu ndiye
Nabii ajaye ulimwenguni!” 15 Yesu akijua
kwamba walitaka kuja kumfanya awe mfalme
wao, kwa nguvu, akajitenga nao akaenda mili-
mani peke yake.

### *Yesu Atembea Juu Ya Maji (Mathayo 14:22-33; Marko 6:45-52)*

16 Ilipofika jioni, wanafunzi wake waliteremka
kwenda baharini. 17 Wakaingia kwenye mashua,
wakaanza kuvuka bahari kwenda Kapernaumu.
Wakati huu kulikuwa tayari giza na Yesu
alikuwa hajajumuika nao. 18 Bahari ikacha-
fuka kwa sababu upepo mkali ulikuwa un-
avuma. 19 Wanafunzi walipokuwa wamekwenda
mwendo wa karibu maili tatu au nne,† walim-
wona Yesu akitembea juu ya maji akikaribia
mashua, nao wakaogopa sana. 20 Lakini Yesu
akawaambia, “Ni mimi. Msiogope.” 21 Ndipo
wakamkaribisha kwa furaha ndani ya mashua,
na mara wakafika ufuoni walikokuwa wakienda.

### *Watu Wanamtafuta Yesu*

† **6:19** Maili tatu au nne ni kama kilomita 5 au 6.

22 Siku iliyofuata, wale watu waliokuwa wame-
baki ng'ambo waliona kwamba palikuwepo na
mashua moja tu na kwamba Yesu hakuwa
ameondoka pamoja na wanafunzi wake, ila
walikuwa wameondoka peke yao. 23 Lakini
zikaja mashua nyingine kutoka Tiberia zikafika
karibu na mahali pale walipokula mikate baada
ya Bwana kumshukuru Mungu. 24 Mara wale
watu wakatambua kwamba Yesu hakuwepo
hapo, wala wanafunzi wake. Wakaingia
kwenye mashua hizo, wakaenda Kapernaumu ili
kumtafuta Yesu.

### *Yesu Ni Mkate Wa Uzima*

25 Walipomkuta Yesu ng'ambo ya bahari waka-
muuliza, "Rabi, umefika lini huku?"

26 Yesu akawajibu, "Amin, amin nawaambia,
ninyi hamnitafuti kwa kuwa mliona ishara na
miujiza, bali kwa sababu mlikula ile mikate
mkashiba. 27 Msishughulikie chakula kiharibika-
cho, bali chakula kidumucho hata uzima wa
milele, ambacho Mwana wa Adamu atawapa.
Yeye ndiye ambaye Mungu Baba amemtia
muhuri."

28 Ndipo wakamuuliza, "Tufanye nini ili tupate
kuitenda kazi ya Mungu?"

29 Yesu akawajibu, "Kazi ya Mungu ndiyo hii:
Mwaminini yeye aliyetumwa naye."

30 Hivyo wakamuuliza, "Utafanya ishara gani
ya muujiza, ili tuione tukuamini? Utafanya
jambo gani? 31 Baba zetu walikula mana
jangwani, kama ilivyoandikwa, 'Aliwapa mikate
kutoka mbinguni ili wale.' "

32 Yesu akawaambia, "Amin, amin nawaambia,
si Mose aliyewapa mikate kutoka mbinguni, bali
Baba yangu ndiye anawapa mkate wa kweli
kutoka mbinguni. 33 Kwa maana mkate wa
Mungu ni yule ashukaye kutoka mbinguni na
kuupa ulimwengu uzima."
34 Wakamwambia, "Bwana, kuanzia sasa tu-
patie huo mkate siku zote."
35 Yesu akawaambia, "Mimi ndimi mkate
wa uzima. Yeye ajaye kwangu, hataona
njaa kamwe na yeye aniaminiye, hataona kiu
kamwe. 36 Lakini kama nilivyowaambia, mme-
niona lakini bado hamwamini. 37 Wale wote
anipao Baba watakuja kwangu na yeyote ajaye
kwangu, sitamfukuzia nje kamwe. 38 Kwa
kuwa nimeshuka kutoka mbinguni si ili ku-
fanya mapenzi yangu, bali mapenzi yake yeye
aliyenituma. 39 Haya ndiyo mapenzi yake
yeye aliyenituma, kwamba, nisimpoteze hata
mmoja wa wale alionipa, bali niwafufue siku ya
mwisho. 40 Kwa maana mapenzi ya Baba yangu
ni kwamba kila mmoja amtazamaye, Mwana
na kumwamini awe na uzima wa milele, nami
nitawafufua siku ya mwisho."
41 Wayahudi wakaanza kunung'unika kwa
kuwa alisema, "Mimi ndimi mkate ulioshuka
kutoka mbinguni." 42 Wakasema, "Huyu si Yesu,
mwana wa Yosefu, ambaye baba yake na mama
yake tunawajua? Anawezaje basi sasa kusema,
'Nimeshuka kutoka mbinguni'?"
43 Hivyo Yesu akawaambia, "Acheni ku-
nung'unikiana ninyi kwa ninyi. 44 Hakuna
mtu awezaye kuja kwangu kama asipovutwa

na Baba aliyenituma, nami nitamfufua siku ya
mwisho. 45 Imeandikwa katika Manabii, 'Wote
watafundishwa na Mungu.' Yeyote amsikilizaye
Baba na kujifunza kutoka kwake, huyo huja
kwangu. 46 Hakuna mtu yeyote aliyemwona
Baba isipokuwa yeye atokaye kwa Mungu, yeye
ndiye peke yake aliyemwona Baba. 47 Amin,
amin nawaambia, yeye anayeamini anao uzima
wa milele. 48 Mimi ni mkate wa uzima. 49 Baba
zenu walikula mana jangwani, lakini wakafa.
50 Lakini hapa kuna mkate utokao mbinguni,
ambao mtu yeyote akiula, hatakufa. 51 Mimi ni
mkate wa uzima ule uliotoka mbinguni. Mtu
yeyote akiula mkate huu, ataishi milele. Mkate
huu ni mwili wangu, ambao nitautoa kwa ajili
ya uzima wa ulimwengu."

52 Ndipo Wayahudi wakaanza kuhojiana vikali
wao kwa wao wakisema, "Mtu huyu awezaje
kutupatia mwili wake tuule?"

53 Hivyo Yesu akawaambia, "Amin, amin
nawaambia, msipoula mwili wa Mwana wa
Adamu na kuinywa damu yake, hamna uzima
ndani yenu. 54 Mtu yeyote aulaye mwili wangu
na kunywa damu yangu, anao uzima wa milele.
Nami nitamfufua siku ya mwisho. 55 Kwa
maana mwili wangu ni chakula cha kweli na
damu yangu ni kinywaji cha kweli. 56 Yeyote
alaye mwili wangu na kunywa damu yangu,
atakaa ndani yangu nami nitakaa ndani yake.
57 Kama vile Baba aliye hai alivyonituma mimi,
na kama nami ninavyoishi kwa sababu ya Baba,
hivyo anilaye mimi ataishi kwa sababu yangu.
58 Huu ndio mkate ushukao kutoka mbinguni,

si kama ule mkate baba zenu waliokula nao
wakafa. Lakini yeye aulaye mkate huu ataishi
milele.” 59 Yesu alisema maneno haya alipokuwa
akifundisha katika sinagogi huko Kapernaumu.

### *Wafuasi Wengi Wamwacha Yesu*

60 Wengi wa wafuasi wake waliposikia jambo hili wakasema, “Mafundisho haya ni magumu. Ni nani awezaye kuyapokea?”

61 Yesu alipojua kwamba wafuasi wake wana-
nung’unika kuhusu mafundisho yake, akawaam-
bia, “Je, jambo hili limewaudhi? 62 Ingekuwaje
basi kama mngemwona Mwana wa Adamu
akipaa kwenda zake huko alipokuwa kwanza?
63 Roho ndiye atiaye uzima, mwili haufai kitu.
Maneno haya niliyowaambia ni Roho tena ni
uzima. 64 Lakini baadhi yenu hamwamini.”
Kwa maana Yesu alifahamu tangu mwanzo wale
ambao hawangemwamini miongoni mwao na
yule ambaye angemsaliti. 65 Akaendelea kusema,
“Hii ndiyo sababu niliwaambia kwamba hakuna
mtu awezaye kuja kwangu isipokuwa amejaliwa
na Baba yangu.”

66 Tangu wakati huo wafuasi wake wengi wakarejea nyuma wakaacha kumfuata.

67 Hivyo Yesu akawauliza wale wanafunzi wake kumi na wawili, “Je, ninyi pia mnataka kuondoka?”

68 Simoni Petro akamjibu, “Bwana, tuondoke
twende kwa nani? Wewe unayo maneno ya
uzima wa milele. 69 Tunaamini na kujua kuwa
wewe ndiwe Aliye Mtakatifu wa Mungu.”

70 Ndipo Yesu akajibu, “Je, sikuwachagua ninyi
kumi na wawili? Lakini mmoja wenu ni ibilisi.”
71 (Hapa alikuwa anasema juu ya Yuda, mwana
wa Simoni Iskariote. Ingawa alikuwa mmoja
wa wale kumi na wawili, ndiye ambaye baadaye
angemsaliti Yesu.)

# 7

### *Kutokuamini Kwa Ndugu Zake Yesu*

1 Baada ya mambo haya, Yesu alikwenda se-
hemu mbalimbali za Galilaya. Hakutaka kwenda
Uyahudi kwa sababu Wayahudi huko walitaka
kumuua. 2 Sikukuu ya Vibanda ya Wayahudi
ilikuwa imekaribia. 3 Hivyo ndugu zake Yesu
wakamwambia, “Ondoka hapa uende Uyahudi
ili wanafunzi Wako wapate kuona miujiza un-
ayofanya. 4 Mtu anayetaka kujulikana hafanyi
mambo yake kwa siri. Kama unafanya mambo
haya, jionyeshe kwa ulimwengu.” 5 Hata ndugu
zake mwenyewe hawakumwamini.

6 Yesu akawaambia, “Wakati wangu bado
haujawadia, lakini wakati wenu upo siku zote.
7 Ulimwengu hauwezi kuwachukia ninyi, lakini
unanichukia mimi kwa sababu ninawashuhudia
kwamba matendo yao ni maovu. 8 Ninyi nen-
deni kwenye Sikukuu, lakini mimi sitahudhuria
Sikukuu hii kwa sababu wakati wangu haujawa-
dia.” 9 Akiisha kusema hayo, akabaki Galilaya.

### *Yesu Kwenye Sikukuu Ya Vibanda*

10 Lakini ndugu zake walipokwisha kuon-
doka kwenda kwenye Sikukuu, yeye pia alik-
wenda lakini kwa siri. 11 Wayahudi wa-
likuwa wakimtafuta huko kwenye Sikukuu na
kuulizana, “Yuko wapi huyu mtu?”

12 Kulikuwa na minong’ono iliyoenea
kumhusu Yesu katika umati wa watu, wakati
wengine wakisema, “Ni mtu mwema.”

Wengine walikuwa wakisema, “La, yeye
anawadanganya watu.” 13 Lakini hakuna mtu
yeyote aliyemsema waziwazi kumhusu kwa
sababu ya kuwaogopa Wayahudi.

### *Yesu Afundisha Kwenye Sikukuu*

14 Ilipokaribia katikati ya Sikukuu, Yesu ali-
panda kwenda Hekaluni na kuanza kufundisha.
15 Wayahudi wakastaajabia mafundisho yake
wakasema, “Mtu huyu amepataje kujua mambo
haya bila kufundishwa?”

16 Ndipo Yesu akawajibu, “Mafundisho yangu
si yangu mwenyewe, bali yanatoka kwake yeye
aliyenituma. 17 Mtu yeyote akipenda kufanya
mapenzi ya Mungu, atajua kama mafundisho
yangu yanatoka kwa Mungu au ninasema kwa
ajili yangu mwenyewe. 18 Wale wanenao kwa
ajili yao wenyewe hufanya hivyo kwa kutaka
utukufu wao wenyewe. Lakini yeye atafutaye
utukufu wa yule aliyemtuma ni wa kweli, wala
hakuna uongo ndani yake. 19 Je, Mose hakuwapa
ninyi sheria? Lakini hakuna hata mmoja wenu
anayeishika hiyo sheria. Kwa nini mnataka
kuniua?”

20 Ule umati wa watu ukamjibu, “Wewe una
pepo mchafu! Ni nani anayetaka kukuua?”
21 Yesu akawajibu, “Nimefanya muujiza
mmoja na nyote mkastaajabu. 22 Lakini kwa
kuwa Mose aliwaamuru tohara (ingawa kwa
kweli haikutoka kwa Mose bali kwa baba zenu
wakuu), mnamtahiri mtoto hata siku ya Sabato.
23 Ikiwa mtoto aweza kutahiriwa siku ya Sabato
kusudi sheria ya Mose isivunjwe, kwa nini
mnanikasirikia kwa kumponya mtu mwili wake
wote siku ya Sabato? 24 Acheni kuhukumu
mambo kwa jinsi mnavyoona tu, bali hukumuni
kwa haki.”

*Je, Yesu Ndiye Kristo?*

25 Ndipo baadhi ya watu wa Yerusalemu
wakawa wanasema, “Tazameni, huyu si
yule mtu wanayetaka kumuua? 26 Mbona
yuko hapa anazungumza hadharani na wala
hawamwambii neno lolote? Je, inawezekana
viongozi wanafahamu kuwa huyu ndiye Kristo?*
27 Tunafahamu huyu mtu anakotoka, lakini
Kristo atakapokuja, hakuna yeyote atakayejua
atokako.”
28 Ndipo Yesu, akaendelea kufundisha
Hekaluni, akisema, “Ninyi mnanifahamu na
kujua nitokako. Mimi sikuja kwa ajili yangu
mwenyewe, bali yeye aliyenituma ni wa kweli
na ninyi hammjui. 29 Mimi namjua kwa kuwa
nimetoka kwake, naye ndiye alinituma.”
30 Ndipo wakatafuta kumkamata, lakini
hakuna mtu yeyote aliyethubutu kumshika

* **7:26** Kristo maana yake ni Masiya, yaani Aliyetiwa mafuta.

kwa sababu saa yake ilikuwa bado haijawadia.
31 Nao watu wengi wakamwamini, wakasema,
"Je, Kristo atakapokuja, atafanya miujiza mikuu
zaidi kuliko aliyoifanya mtu huyu?"

### *Walinzi Wanatumwa Kumkamata Yesu*

32 Mafarisayo wakasikia watu wakinong'ona mambo kama hayo kuhusu Yesu, ndipo wao pamoja na viongozi wa makuhani wakatuma walinzi wa Hekalu waende kumkamata.

33 Yesu akasema, "Mimi bado niko pamoja
nanyi kwa kitambo kidogo, kisha nitarudi kwake
yeye aliyenituma. 34 Mtanitafuta lakini hamtan-
iona, nami niliko ninyi hamwezi kuja."

35 Wayahudi wakaulizana wao kwa wao,
"Huyu mtu anataka kwenda wapi ambako
hatuwezi kumfuata? Je, anataka kwenda
kwa Wayunani ambako baadhi ya watu wetu
wametawanyikia, akawafundishe Wayunani?
36 Yeye ana maana gani anaposema, 'Mtan-
itafuta lakini hamtaniona,' na, 'nami niliko ninyi
hamwezi kuja'?"

### *Mito Ya Maji Ya Uzima*

37 Siku ile ya mwisho ya Sikukuu, siku ile kuu,
wakati Yesu akiwa amesimama huko, akapaza
sauti yake akasema, "Kama mtu yeyote anaona
kiu na aje kwangu anywe. 38 Yeyote aniaminiye
mimi, kama Maandiko yasemavyo, vijito vya
maji ya uzima vitatiririka ndani mwake." 39 Yesu
aliposema haya alimaanisha Roho Mtakatifu am-
baye wote waliomwamini wangempokea, kwani
mpaka wakati huo, Roho alikuwa hajatolewa,
kwa kuwa Yesu alikuwa bado hajatukuzwa.

### *Mgawanyiko Miongoni Mwa Watu*

40 Waliposikia maneno hayo, baadhi ya watu
miongoni mwa ule umati wakasema, "Hakika
huyu ndiye yule Nabii."

41 Wengine wakasema, "Huyu ndiye Kristo!"

Lakini wengine wakauliza, "Je, Kristo kwao
ni Galilaya? 42 Je, Maandiko hayasemi kwamba
Kristo atakuja kutoka jamaa ya Daudi na ku-
toka Bethlehemu, mji alioishi Daudi?" 43 Kwa
hiyo watu wakagawanyika kwa ajili ya Yesu.
44 Baadhi yao walitaka kumkamata, lakini
hakuna aliyethubutu kumgusa.

### *Kutokuamini Kwa Viongozi Wa Wayahudi*

45 Hatimaye wale walinzi wa Hekalu wakarudi
kwa viongozi wa makuhani na Mafarisayo
waliokuwa wamewatuma ili kumkamata Yesu,
wakaulizwa, "Mbona hamkumkamata?"

46 Wale walinzi wakajibu, "Kamwe hajanena
mtu yeyote kama yeye anenavyo."

47 Mafarisayo wakajibu, "Je, nanyi pia
mmedanganyika? 48 Je, kuna kiongozi yeyote au
mmoja wa Mafarisayo ambaye amemwamini?
49 Lakini huu umati wa watu wasiojua Sheria ya
Mose, wamelaaniwa."

50 Ndipo Nikodemo, yule aliyekuwa amemwen-
dea Yesu siku moja usiku, ambaye alikuwa
mmoja wao akauliza, 51 "Je, sheria zetu zinatu-
ruhusu kumhukumu mtu kabla ya kumsikiliza
na kufahamu alilotenda?"

52 Wakamjibu, "Je, wewe pia unatoka Galilaya?
Chunguza nawe utaona kwamba hakuna nabii

atokae Galilaya!” [ 53 Kisha wakaondoka, kila
mtu akarudi nyumbani kwake.

# 8

*Mwanamke Aliyefumaniwa Akizini*

1 Lakini Yesu akaenda katika Mlima wa
Mizeituni. 2 Alfajiri na mapema Yesu akaja tena
Hekaluni, watu wote wakakusanyika, akakaa
akaanza kuwafundisha. 3 Walimu wa sheria na
Mafarisayo wakamleta mwanamke mmoja aliye-
fumaniwa akizini. Wakamsimamisha katikati ya
umati wa watu wote. 4 Wakamwambia Yesu,
“Mwalimu, huyu mwanamke amekutwa akizini.
5 Katika sheria, Mose alituamuru kuwapiga kwa
mawe wanawake wa namna hii, mpaka wafe.
Sasa wewe wasemaje?” 6 Walimuuliza swali hili
kama mtego ili wapate sababu ya kumshtaki.

Lakini Yesu akainama akaanza kuandika ard-
hini kwa kidole chake. 7 Walipoendelea ku-
muulizauliza akainuka, akawaambia, “Kama
kuna mtu yeyote miongoni mwenu ambaye hana
dhambi na awe wa kwanza kumtupia jiwe.”
8 Akainama tena na kuandika ardhini.

9 Waliposikia haya, wakaanza kuondoka
mmoja mmoja, wakianzia wazee, hadi Yesu
akabaki peke yake na yule mwanamke akiwa
amesimama mbele yake. 10 Yesu akainuka
na kumwambia, “Wako wapi wale waliokuwa
wanakuhukumu kuwa mwenye hatia?”

11 Yule mwanamke akajibu, “Hakuna hata
mmoja Bwana.”

Yesu akamwambia, “Hata mimi sikuhukumu. Nenda zako, kuanzia sasa usitende dhambi tena.”]

*Yesu Nuru Ya Ulimwengu*

12 Kisha Yesu akasema nao tena akawaambia, “Mimi ni nuru ya ulimwengu. Mtu yeyote akinifuata hatatembea gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima.”

13 Mafarisayo wakamwambia, “Ushuhuda wako haukubaliki kwa kuwa unajishuhudia mwenyewe.”

14 Yesu akawajibu, “Hata kama najishuhudia mwenyewe, ushuhuda wangu ni kweli kwa sababu najua nilikotoka na ninakokwenda. Lakini ninyi hamjui nilikotoka wala ninakok-
wenda. 15 Ninyi mnahukumu kwa kufuata vipimo vya kibinadamu, mimi simhukumu mtu
yeyote. 16 Lakini hata kama nikihukumu, uamuzi wangu ni sahihi kwa sababu sitoi hukumu yangu peke yangu, bali niko pamoja na Baba,
aliyenituma. 17 Imeandikwa katika Sheria yenu kwamba, ushahidi wa watu wawili ni thabiti.
18 Mimi najishuhudia mwenyewe, naye Baba aliyenituma hunishuhudia.”

19 Ndipo wakamuuliza, “Huyo Baba yako yuko wapi?”

Yesu akawajibu, “Ninyi hamnifahamu mimi ni nani, wala hammfahamu Baba yangu. Kama mngenifahamu mimi, mngemfahamu na Baba
yangu.” 20 Yesu alisema maneno haya alipokuwa akifundisha katika chumba cha hazina Hekaluni. Lakini hakuna mtu aliyemkamata kwa kuwa saa yake ilikuwa haijawadia.

*Yesu Atabiri Kifo Chake Mwenyewe*

21 Yesu akawaambia tena, "Ninaenda zangu,
nanyi mtanitafuta, lakini mtakufa katika dhambi
zenu. Niendako mimi ninyi hamwezi kuja."

22 Ndipo wale Wayahudi wakasema, "Je, ata-
jiua? Je, hii ndiyo sababu amesema, 'Niendako
mimi ninyi hamwezi kuja'?"

23 Akawaambia, "Ninyi mmetoka chini, mimi
nimetoka juu. Ninyi ni wa ulimwengu huu,
mimi si wa ulimwengu huu. 24 Niliwaambia
kuwa mtakufa katika dhambi zenu, kwa maana
msipoamini ya kwamba 'Mimi Ndiye,' mtakufa
katika dhambi zenu."

25 Wakamuuliza, "Wewe ni nani?"

Naye Yesu akawajibu, "Mimi ndiye yule am-
baye nimekuwa nikiwaambia tangu mwanzo.
26 Nina mambo mengi ya kusema juu yenu na
mengi ya kuwahukumu. Lakini yeye aliyeni-
tuma ni wa kweli, nami nanena na ulimwengu
niliyoyasikia kutoka kwake."

27 Hawakuelewa kuwa alikuwa akiwaambia
juu ya Baba yake wa Mbinguni. 28 Kisha Yesu
akawaambia, "Mtakapokwisha kumwinua juu
Mwana wa Adamu, ndipo mtakapojua kuwa,
'Mimi ndiye yule niliyesema na kwamba mimi
sitendi jambo lolote peke yangu bali ninasema
yale tu ambayo Baba yangu amenifundisha.
29 Yeye aliyenituma yu pamoja nami, hajaniacha,
kwa kuwa siku zote nafanya mapenzi yake.' "
30 Wengi waliomsikia Yesu akisema maneno
haya wakamwamini.

*Wanafunzi Wa Kweli*

31 Kisha Yesu akawaambia wale Wayahudi
waliomwamini, “Kama mkidumu katika maneno
yangu, mtakuwa wanafunzi wangu kweli kweli.
32 Ndipo mtaijua kweli nayo kweli itawaweka
huru.”

33 Wao wakamjibu, “Sisi tu wazao wa Abrahamu, nasi hatujawa watumwa wa mtu yeyote. Wawezaje kusema kwamba tutawekwa huru?”

34 Yesu akajibu, “Amin, amin nawaambia,
kila atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi.
35 Mtumwa hakai nyumbani anakotumika siku
zote, lakini mwana hukaa nyumbani daima.
36 Hivyo Mwana akiwaweka huru mtakuwa huru
kweli kweli. 37 Ninajua ya kuwa ninyi ni
wazao wa Abrahamu, lakini mnatafuta wasaa
wa kuniua kwa sababu ndani yenu hamna nafasi
ya neno langu. 38 Ninasema yale niliyoyaona
mbele za Baba yangu, nanyi inawapa kufanya
yale mliyosikia kutoka kwa baba yenu.”

*Yesu Na Abrahamu*

39 Wakajibu, “Baba yetu ni Abrahamu.”

Yesu akawaambia, “Kama mngekuwa wazao
wa Abrahamu mngefanya mambo yale aliy-
ofanya Abrahamu. 40 Lakini sasa ninyi
mnatafuta kuniua, mtu ambaye nimewaambia
kweli ile niliyosikia kutoka kwa Mungu, Abra-
hamu hakufanya jambo la namna hii. 41 Ninyi
mnafanya mambo afanyayo baba yenu.”

Wakamjibu, “Sisi hatukuzaliwa kwa uzinzi. Tunaye Baba mmoja, Mungu pekee.”

42 Yesu akawaambia, “Kama Mungu angekuwa
Baba yenu, mngenipenda, kwa maana nili-
toka kwa Mungu na sasa niko hapa. Sikuja
kwa ajili yangu mwenyewe, ila yeye alini-
tuma. 43 Kwa nini hamwelewi ninayowaam-
bia? Ni kwa sababu hamwezi kusikia nisema-
cho. 44 Ninyi ni watoto wa baba yenu ibil-
isi, nanyi mnataka kutimiza matakwa ya baba
yenu. Yeye alikuwa muuaji tangu mwanzo,
wala hakushikana na kweli maana hamna kweli
ndani yake. Asemapo uongo husema yaliyo yake
mwenyewe kwa maana yeye ni mwongo na baba
wa huo uongo. 45 Lakini kwa sababu nimewaam-
bia kweli hamkuniamini! 46 Je, kuna yeyote
miongoni mwenu awezaye kunithibitisha kuwa
mwenye dhambi? Kama nawaambia yaliyo
kweli, mbona hamniamini? 47 Yeye atokaye kwa
Mungu husikia kile Mungu asemacho. Sababu
ya ninyi kutosikia ni kwa kuwa hamtokani na
Mungu.”

### *Maelezo Ya Yesu Kuhusu Yeye Mwenyewe*

48 Wayahudi wakamjibu Yesu, “Je, hatuko
sahihi tunaposema ya kwamba wewe ni
Msamaria na ya kwamba una pepo mchafu?”
49 Yesu akawajibu, “Mimi sina pepo mchafu,
bali ninamheshimu Baba yangu, nanyi mnanid-
harau. 50 Lakini mimi sitafuti utukufu wangu
mwenyewe, bali yuko anayetaka kunitukuza,
naye ndiye mwamuzi. 51 Amin, amin nawaam-
bia, mtu yeyote akilitii neno langu hataona mauti
milele.”
52 Ndipo Wayahudi wakamwambia, “Sasa
tumejua kwamba una pepo mchafu. Ikiwa

Abrahamu alikufa na vivyo hivyo manabii, nawe
unasema 'Mtu akitii neno langu hatakufa milele.'
53 Je, wewe ni mkuu kuliko baba yetu Abrahamu
ambaye alikufa na manabii ambao nao pia
walikufa? Hivi wewe unajifanya kuwa nani?"
54 Yesu akawajibu, "Kama nikijitukuza utukufu
wangu hauna maana. Baba yangu, huyo ambaye
ninyi mnadai kuwa ni Mungu wenu, ndiye
anitukuzaye mimi. 55 Ingawa hamkumjua, mimi
ninamjua. Kama ningesema simjui, ningekuwa
mwongo kama ninyi, lakini mimi ninamjua na
ninalitii neno lake. 56 Baba yenu Abrahamu al-
ishangilia kwamba angaliiona siku yangu, naye
akaiona na akafurahi."
57 Wayahudi wakamwambia, "Wewe huja-
timiza hata miaka hamsini, wewe wasema
umemwona Abrahamu?"
58 Yesu akawaambia, "Amin, amin nawaam-
bia, kabla Abrahamu hajakuwako, 'Mimi niko.' "
59 Ndipo wakaokota mawe ili kumpiga, lakini
Yesu akajificha, naye akatoka Hekaluni.

# 9

*Yesu Amponya Mtu Aliyezaliwa Kipofu*

1 Yesu alipokuwa akipita, akamwona mtu
aliyekuwa kipofu tangu kuzaliwa. 2 Wanafunzi
wake wakamuuliza, "Rabi, ni nani aliyetenda
dhambi, ni huyu mtu au wazazi wake hata
azaliwe kipofu?"
3 Yesu akawajibu, "Huyu mtu wala wazazi
wake hawakutenda dhambi. Alizaliwa kipofu
ili kazi za Mungu zidhihirishwe katika maisha

yake. 4 Yanipasa kuzifanya kazi zake yeye aliyen-
ituma wakati bado ni mchana, kwa kuwa usiku
waja ambapo hakuna mtu awezaye kufanya
kazi. 5 Wakati niko ulimwenguni, mimi ni nuru
ya ulimwengu."
6 Baada ya kusema haya, akatema mate ard-
hini, akatengeneza tope kwa mate na kumpaka
yule mtu kipofu machoni. 7 Kisha akamwambia,
"Nenda ukanawe katika bwawa la Siloamu."
(Siloamu maana yake ni aliyetumwa.) Ndipo
yule kipofu akaenda, akanawa, naye akarudi
akiwa anaona.
8 Majirani zake na wale wote waliokuwa
wamemwona hapo awali akiombaomba
wakaanza kuuliza, "Je, huyu si yule aliyekuwa
akiketi akiombaomba?" 9 Wengine wakasema,
"Ndiye."

Wengine wakasema, "Siye, bali wamefanana."

Lakini yeye akawaambia, "Mimi ndiye."

10 Wakamuuliza, "Basi macho yako yalifumbu-
liwaje?"
11 Yeye akawajibu, "Yule mtu aitwaye Yesu
alitengeneza tope, akanipaka machoni mwangu,
naye akaniambia nenda ukanawe katika Bwawa
la Siloamu, ndipo nikanawa nami nikapata
kuona!"
12 Wale wakamuuliza, "Yeye huyo mtu yuko
wapi?"

Akawajibu, "Sijui."

### *Mafarisayo Wachunguza Kuponywa Kwa Kipofu*

13 Wakamleta kwa Mafarisayo yule mtu
aliyekuwa kipofu hapo awali. 14 Basi siku hiyo

Yesu alipotengeneza tope na kuyafungua macho
ya huyo mtu ilikuwa Sabato. 15 Mafarisayo
nao wakaanza kumuuliza alivyopata kuponywa.
Naye akawaambia, “Alinipaka tope kwenye ma-
cho yangu, nikanawa na sasa ninaona.”
16 Baadhi ya Mafarisayo wakasema, “Huyu
mtu hatoki kwa Mungu, kwa sababu hashiki
Sabato.”

Lakini wengine wakasema, “Awezaje mtu
mwenye dhambi kufanya miujiza kama hii?”
Wakagawanyika.
17 Hivyo wakamwambia tena yule mtu
aliyekuwa kipofu, “Wewe ndiwe uliyefumbuliwa
macho, wasemaje kuhusu mtu huyo?” Maana
macho yako ndiyo yaliyofumbuliwa.

Yeye akawajibu, “Yeye ni nabii.”
18 Wale Wayahudi hawakuamini ya kuwa mtu
huyo alikuwa kipofu, akapata kuona, mpaka
walipowaita wazazi wake. 19 Wakawauliza, “Je,
huyu ni mtoto wenu, ambaye mnasema alizaliwa
kipofu? Imekuwaje basi sasa anaona?”
20 Wazazi wake wakajibu, “Tunajua ya kuwa
huyu ni mtoto wetu na ya kuwa alizaliwa
kipofu. 21 Lakini sisi hatujui ni kwa jinsi
gani kwamba sasa anaona, wala hatujui ni
nani aliyemfungua macho yake. Muulizeni,
yeye ni mtu mzima na anaweza kujieleza
mwenyewe.” 22 Wazazi wake walisema hivi kwa
sababu waliwaogopa Wayahudi kwani walikuwa
wamekubaliana kuwa mtu yeyote atakayemkiri
Yesu kuwa ndiye Kristo* atafukuzwa kutoka

* **9:22** Kristo maana yake ni Masiya, yaani Aliyetiwa mafuta.

sinagogi. 23 Kwa hiyo wazazi wake wakasema,
“Yeye ni mtu mzima. Muulizeni.”

24 Hivyo kwa mara ya pili wakamwita yule
aliyekuwa kipofu, nao wakamwambia, “Mpe
Mungu utukufu! Sisi tunafahamu kuwa mtu
huyu aliyekuponya ni mwenye dhambi.”

25 Akawajibu, “Mimi sijui kama yeye ni
mwenye dhambi. Lakini jambo moja ninalojua,
nilikuwa kipofu na sasa ninaona.”

26 Wakamuuliza, “Alikufanyia nini? Aliyafum-
buaje macho yako?”

27 Akawajibu, “Tayari nimekwisha kuwaam-
bia, nanyi hamtaki kunisikiliza. Mbona mnataka
kusikia tena? Je, ninyi nanyi mnataka kuwa
wanafunzi wake?”

28 Ndipo wakamtukana na kusema, “Wewe
ndiwe mwanafunzi wake, Sisi ni wanafunzi wa
Mose. 29 Tunajua kwamba Mungu alisema na
Mose, lakini kwa habari ya mtu huyu hatujui
atokako.”

30 Yule mtu akawajibu, “Hili ni jambo la
ajabu! Hamjui anakotoka, naye amenifungua
macho yangu! 31 Tunajua ya kuwa Mungu
hawasikilizi wenye dhambi, lakini huwasikiliza
wote wanaomcha na kumtii. 32 Tangu zamani
hatujasikia kwamba mtu amemponya yeyote
aliyezaliwa kipofu. 33 Kama huyu mtu hakutoka
kwa Mungu, asingeweza kufanya lolote.”

34 Wao wakamjibu, “Wewe ulizaliwa katika
dhambi kabisa, nawe unajaribu kutufundisha?”
Wakamfukuza atoke nje.

### *Upofu Wa Kiroho*

35 Yesu aliposikia kuwa wamemfukuzia nje yule mtu aliyemfumbua macho, alimkuta akamuuliza, “Je, unamwamini Mwana wa Adamu?”
36 Yule mtu akamjibu, “Yeye ni nani, Bwana? Niambie ili nipate kumwamini.”
37 Yesu akamjibu, “Umekwisha kumwona, naye anayezungumza nawe, ndiye.”
38 Yule mtu akasema, “Bwana, naamini.” Naye akamwabudu.
39 Yesu akasema, “Nimekuja ulimwenguni humu kwa ajili ya kuhukumu, ili wale walio vipofu wapate kuona, nao wale wanaoona, wawe vipofu.”
40 Baadhi ya Mafarisayo waliokuwa karibu naye wakamsikia na kumwambia, “Je, kweli sisi ni vipofu?”
41 Yesu akawajibu, “Kama mngekuwa vipofu kweli, msingekuwa na hatia ya dhambi, lakini kwa kuwa mnasema, ‘Tunaona,’ basi mna hatia.

# 10

*Mchungaji Mwema*

1 “Amin, amin nawaambia, yeye asiyeingia
katika zizi la kondoo kwa kupitia kwenye lango,
lakini akwea kuingia ndani kwa njia nyingine,
ni mwizi na mnyang’anyi. 2 Yeye anayeingia
kwa kupitia kwenye lango ndiye mchungaji wa
kondoo. 3 Mlinzi humfungulia lango na kondoo
huisikia sauti yake. Huwaita kondoo wake kwa
majina yao na kuwatoa nje ya zizi. 4 Akiisha
kuwatoa wote nje, hutangulia mbele yao na
kondoo humfuata kwa kuwa wanaijua sauti

yake. 5 Lakini kondoo hawatamfuata mgeni bali
watamkimbia, kwa sababu hawaijui sauti ya
mgeni.” 6 Yesu alitumia mfano huu, lakini wao
hawakuelewa hayo aliyokuwa akiwaambia.
7 Kwa hiyo Yesu akasema nao tena akawaam-
bia, “Amin, amin nawaambia, mimi ndimi lango
la kondoo. 8 Wote walionitangulia ni wevi na
wanyang’anyi, lakini kondoo hawakuwasikia.
9 Mimi ndimi lango, yeyote anayeingia zizini kwa
kupitia kwangu ataokoka, ataingia na kutoka,
naye atapata malisho. 10 Mwizi huja ili aibe,
kuua na kuangamiza. Mimi nimekuja ili wapate
uzima kisha wawe nao tele.
11 “Mimi ndimi mchungaji mwema. Mchungaji
mwema huutoa uhai wake kwa ajili ya kondoo.
12 Mtu wa kuajiriwa sio mchungaji mwenye
kondoo. Amwonapo mbwa mwitu akija, yeye
hukimbia na kuwaacha kondoo. Naye mbwa
mwitu hulishambulia kundi na kulitawanya.
13 Yeye hukimbia kwa sababu ameajiriwa wala
hawajali kondoo.
14 “Mimi ndimi mchungaji mwema. Ninawa-
jua kondoo wangu nao kondoo wangu wanani-
jua. 15 Kama vile Baba anavyonijua mimi, nami
ninavyomjua Baba, nami nautoa uhai wangu
kwa ajili ya kondoo. 16 Ninao kondoo wengine
ambao si wa zizi hili, inanipasa kuwaleta, nao
wataisikia sauti yangu, hivyo patakuwa na kundi
moja na mchungaji mmoja. 17 Baba yangu
ananipenda kwa kuwa ninautoa uhai wangu
ili niupate tena. 18 Hakuna mtu aniondoleaye
uhai wangu, bali ninautoa kwa hiari yangu
mwenyewe. Ninao uwezo wa kuutoa uhai

wangu na pia ninao uwezo wa kuutwaa tena. Amri hii nimepewa na Baba yangu."
19 Kwa maneno haya Wayahudi
waligawanyika. 20 Wengi wao wakasema,
"Huyu amepagawa na pepo mchafu, naye amechanganyikiwa."
21 Wengine wakasema, "Haya si maneno ya mtu aliyepagawa na pepo mchafu. Je, pepo mchafu aweza kufungua macho ya kipofu?"

### *Yesu Akataliwa Na Wayahudi*

22 Wakati huo ilikuwa Sikukuu ya Kuwekwa
wakfu kwa Hekalu* huko Yerusalemu, nao
ulikuwa wakati wa majira ya baridi. 23 Naye
Yesu alikuwa akitembea ndani ya Hekalu katika
ukumbi wa Solomoni. 24 Wayahudi wakamku-
sanyikia wakamuuliza, "Utatuweka katika hali ya mashaka mpaka lini? Kama wewe ndiye Kristo† tuambie waziwazi."
25 Yesu akawajibu, "Nimewaambia, lakini
hamwamini. Mambo ninayoyatenda kwa jina
la Baba yangu yananishuhudia. 26 Lakini
hamwamini, kwa sababu ninyi si wa kundi la
kondoo wangu. 27 Kondoo wangu huisikia sauti
yangu nami nawajua, nao hunifuata, 28 nami
ninawapa uzima wa milele, hawataangamia kamwe wala hakuna mtu atakayewapokonya
kutoka mikono yangu. 29 Baba yangu aliyenipa
hawa ni mkuu kuliko wote na hakuna awezaye

* **10:22** Sikukuu ya Kuwekwa wakfu kwa Hekalu ni Hanukkah kwa Kiebrania. † **10:24** Kristo maana yake ni Masiya, yaani Aliyetiwa mafuta.

kuwapokonya kutoka mikononi mwake. 30 Mimi
na Baba yangu tu umoja."

31 Kwa mara nyingine Wayahudi wakainua
mawe ili wampige nayo, 32 lakini Yesu akawaam-
bia, "Nimewaonyesha miujiza mingi mikubwa
kutoka kwa Baba yangu. Ni ipi katika hiyo
mnataka kunipiga mawe?"

33 Wayahudi wakamjibu, "Hatukupigi mawe
kwa sababu ya mambo mema uliyotenda, bali
ni kwa kuwa umekufuru. Wewe ingawa ni
mwanadamu unajifanya kuwa Mungu."

34 Yesu akawajibu, "Je, haikuandikwa katika
Sheria ya kwamba, 'Nimesema kuwa, ninyi ni
miungu?' 35 Kama aliwaita 'miungu,' wale am-
bao neno la Mungu liliwafikia, nayo Maandiko
hayawezi kutanguka, 36 je, mwawezaje kusema
kwamba yule ambaye Baba amemweka wakfu
na kumtuma ulimwenguni anakufuru, kwa
sababu nilisema, 'Mimi ni Mwana wa Mungu?'
37 Ikiwa sifanyi kazi za Baba yangu, basi msini-
amini, 38 lakini ikiwa nazifanya kazi za Mungu,
hata kama hamniamini mimi ziaminini hizo
kazi, ili mpate kujua na kuelewa kwamba Baba
yu ndani yangu, nami ndani yake." 39 Ndipo
wakajaribu kumkamata kwa mara nyingine,
lakini akaponyoka kutoka mikononi mwao.

40 Akaenda tena ng'ambo ya Mto Yordani
mpaka mahali pale ambapo Yohana alikuwa
akibatiza hapo awali, naye akakaa huko. 41 Watu
wengi wakamjia, nao wakawa wakisema,
"Yohana hakufanya muujiza wowote, lakini

kila jambo alilosema kumhusu huyu mtu ni
kweli.” 42 Nao wengi wakamwamini Yesu huko.

# 11

*Kifo Cha Lazaro*

1 Basi mtu mmoja jina lake Lazaro alikuwa
mgonjwa. Yeye alikuwa akiishi Bethania kijiji
cha Maria na Martha dada zake. 2 Huyu Maria,
ambaye Lazaro kaka yake alikuwa mgonjwa,
ndiye yule ambaye alimpaka Bwana mafuta
na kuifuta miguu yake kwa nywele zake.
3 Hivyo hawa dada wawili walituma ujumbe kwa
Yesu kumwambia, “Bwana, yule umpendaye ni
mgonjwa.”

4 Lakini Yesu aliposikia hayo, akasema,
“Ugonjwa huu hautaleta mauti bali umetokea ili
kudhihirisha utukufu wa Mungu, ili Mwana wa
Mungu apate kutukuzwa kutokana na ugonjwa
huu.” 5 Pamoja na hivyo, ingawa Yesu ali-
wapenda Martha, Maria na Lazaro ndugu yao,
6 baada ya kusikia kwamba Lazaro ni mgonjwa,
aliendelea kukawia huko alikokuwa kwa siku
mbili zaidi.

7 Ndipo akawaambia wanafunzi wake, “Haya,
turudi Uyahudi.”

8 Wanafunzi wake wakamwambia, “Rabi,
Wayahudi walikuwa wanataka kukupiga mawe,
nawe unataka kurudi huko?”

9 Yesu akawajibu, “Si kuna saa kumi na mbili
za mchana katika siku moja? Wala watem-
beao mchana hawawezi kujikwaa kwa maana
wanaona nuru ya ulimwengu huu. 10 Lakini

wale watembeao usiku hujikwaa kwa sababu
hakuna nuru ndani yao."
11 Baada ya kusema haya, Yesu akawaam-
bia, "Rafiki yetu Lazaro amelala, lakini naenda
kumwamsha."
12 Wanafunzi wakamwambia, "Bwana, kama
amelala usingizi ataamka." 13 Hata hivyo, Yesu
alikuwa anazungumzia kuwa Lazaro amekufa,
lakini wanafunzi wake hawakuelewa, walidhani
kwamba anasema Lazaro amelala usingizi tu.
14 Kwa hiyo Yesu akawaambia waziwazi,
"Lazaro amekufa. 15 Hata hivyo nafurahi kwa
kuwa sikuwepo huko kabla ya Lazaro kufa, ili
mpate kuamini. Lakini sasa twendeni kwake."
16 Tomaso aliyeitwa Pacha akawaambia wana-
funzi wenzake, "Sisi nasi twendeni tukafe
pamoja naye."

### *Yesu Ndiye Ufufuo Na Uzima*

17 Yesu alipowasili huko alikuta Lazaro
amekuwa kaburini siku nne. 18 Basi Bethania
ulikuwa karibu na Yerusalemu umbali wa karibu
maili mbili,* 19 na Wayahudi wengi walikuwa
wamekuja kuwafariji Martha na Maria kwa ajili
ya kufiwa na ndugu yao. 20 Martha aliposikia
kwamba Yesu anakuja, alitoka kwenda kumlaki,
ila Maria alibaki nyumbani.
21 Martha akamwambia Yesu, "Bwana, kama
ungalikuwa hapa, ndugu yangu hangalikufa.
22 Lakini sasa ninajua kuwa chochote utaka-
chomwomba Mungu, atakupa."
23 Yesu akamwambia, "Ndugu yako atafufuka."

---

* **11:18** Maili mbili ni kama kilomita tatu.

24 Martha akamjibu, “Ninajua ya kuwa ata-
fufuka wakati wa ufufuo wa wafu siku ya
mwisho.”
25 Yesu akamwambia, “Mimi ndiye huo ufufuo
na uzima. Yeye aniaminiye mimi, hata akifa
atakuwa anaishi 26 na yeyote aishiye na kuni-
amini hatakufa kabisa hata milele. Je, unasadiki
haya?”
27 Martha akamwambia, “Ndiyo Bwana, ni-
naamini ya kuwa wewe ndiwe Kristo,† Mwana
wa Mungu, yeye ajaye ulimwenguni.”

### *Yesu Alia*

28 Baada ya kusema haya Martha alik-
wenda, akamwita Maria dada yake faraghani na
kumwambia, “Mwalimu yuko hapa anakuita.”
29 Maria aliposikia hivyo, akaondoka upesi
akaenda mpaka alipokuwa Yesu. 30 Yesu alikuwa
hajaingia kijijini, bali alikuwa bado yuko mahali
pale alipokutana na Martha. 31 Wale Wayahudi
waliokuwa pamoja na Maria nyumbani wakim-
fariji walipoona ameondoka haraka na kutoka
nje, walimfuata wakidhani ya kwamba alikuwa
anakwenda kule kaburini kulilia huko.
32 Maria alipofika mahali pale Yesu alipokuwa,
alipiga magoti miguuni Pake na kusema,
“Bwana, kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu
hangalikufa.”
33 Yesu alipomwona Maria akilia na wale
Wayahudi waliokuja pamoja naye pia wakilia,
Yesu alisikia uchungu moyoni, akafadhaika sana.
34 Akauliza, “Mmemweka wapi?”

† **11:27** Kristo maana yake ni Masiya, yaani Aliyetiwa mafuta.

Wakamwambia, “Bwana, njoo upaone.”
35 Yesu akalia machozi.
36 Ndipo Wayahudi wakasema, “Tazama jinsi alivyompenda Lazaro!”
37 Lakini wengine wakasema, “Je, yule aliyefungua macho ya kipofu, hakuweza kumfanya na huyu asife?”

### *Yesu Amfufua Lazaro*

38 Yesu kwa mara nyingine akiwa amefadhaika sana, akafika penye kaburi. Hilo kaburi lilikuwa pango ambalo jiwe lilikuwa limewekwa kwenye
ingilio lake. 39 Yesu akasema, “Liondoeni hilo jiwe.”

Martha ndugu yake yule aliyekuwa amekufa akasema, “Lakini Bwana, wakati huu atakuwa ananuka kwani amekwisha kuwa kaburini siku nne.”
40 Yesu akamwambia, “Sikukuambia kwamba kama ukiamini utauona utukufu wa Mungu?”
41 Kwa hiyo wakaliondoa lile jiwe kutoka kaburini. Yesu akainua macho yake juu akasema, “Baba, ninakushukuru kwa kuwa
wanisikia. 42 Ninajua ya kuwa wewe hunisikia siku zote, lakini nimesema haya kwa ajili ya umati huu uliosimama hapa, ili wapate kuamini ya kuwa wewe umenituma.”
43 Baada ya kusema haya, Yesu akapaza sauti
yake akaita, “Lazaro, njoo huku!” 44 Yule
aliyekuwa amekufa akatoka nje, mikono yake na miguu yake ikiwa imeviringishiwa vitambaa vya kitani na leso usoni pake.

Yesu akawaambia, “Mfungueni, mwacheni aende zake.”

## *Shauri La Kumuua Yesu*
## *(Mathayo 26:1-5; Marko 14:1-2; Luka 22:1-2)*

45 Hivyo Wayahudi wengi waliokuwa
wamekuja kumfariji Maria, walipoona yale Yesu
aliyoyatenda wakamwamini. 46 Lakini baadhi
yao wakaenda kwa Mafarisayo na kuwaambia
mambo Yesu aliyoyafanya. 47 Kwa hiyo viongozi
wa makuhani na Mafarisayo wakaita mkutano
wa baraza.

Wakaulizana, "Tufanyeje? Huyu mtu
anafanya ishara nyingi. 48 Kama tukimwacha
aendelee hivi, kila mtu atamwamini, nao
Warumi watakuja na kupaharibu mahali petu
patakatifu na taifa letu."

49 Mmoja wao aliyeitwa Kayafa, ambaye
alikuwa kuhani mkuu mwaka huo, akasema,
"Ninyi hamjui kitu chochote! 50 Hamjui kwamba
ni afadhali mtu mmoja afe kwa ajili ya watu,
kuliko taifa lote liangamie?"

51 Hakusema haya kutokana na mawazo yake
mwenyewe bali kama kuhani mkuu mwaka
huo, alitabiri kuwa Yesu angelikufa kwa ajili
ya taifa la Wayahudi, 52 wala si kwa ajili ya
taifa hilo pekee, bali pia kwa ajili ya watoto wa
Mungu waliotawanyika, ili kuwaleta pamoja na
kuwafanya wawe wamoja. 53 Hivyo tangu siku
hiyo wakawa wanafanya mipango ili wamuue
Yesu.

54 Kwa hiyo Yesu akawa hatembei hadharani miongoni mwa Wayahudi, bali alijitenga akaenda sehemu iliyo karibu na jangwa kwenye kijiji kiitwacho Efraimu. Akakaa huko na wanafunzi wake.

55 Basi Pasaka ya Wayahudi ilipokuwa
imekaribia, watu wengi walitoka vijijini
wakaenda Yerusalemu kabla ya Pasaka ili
wakajitakase. 56 Watu wakawa wanamtafuta
Yesu, nao waliposimama kwenye eneo la Hekalu
waliulizana, Je, mtu huyu hatakuja kamwe
kwenye Sikukuu? 57 Viongozi wa makuhani
na Mafarisayo walikuwa wametoa amri kuwa
yeyote atakayejua mahali Yesu aliko, lazima atoe
taarifa ili wapate kumkamata.

# 12

### *Maria Ampaka Yesu Mafuta Huko Bethania (Mathayo 26:6-13; Marko 14:3-9)*

1 Siku sita kabla ya Pasaka, Yesu alikwenda
Bethania mahali ambako Lazaro aliyekuwa ame-
fufuliwa na Yesu alikuwa anaishi. 2 Wakaandaa
karamu kwa heshima ya Yesu. Martha
akawahudumia wakati Lazaro alikuwa mion-
goni mwa waliokaa mezani pamoja na Yesu.
3 Kisha Maria akachukua chupa ya painti moja*
yenye manukato ya nardo† safi ya thamani
kubwa, akayamimina miguuni mwa Yesu na
kuifuta kwa nywele zake. Nyumba nzima ikajaa
harufu nzuri ya manukato.

4 Ndipo Yuda Iskariote mwana wa Simoni,
mmoja wa wale wanafunzi ambaye ndiye
angemsaliti Yesu, akasema, 5 “Kwa nini

---

* **12:3** Painti moja ni kama nusu lita. † **12:3** Nardo ni aina ya mafuta yaliyokuwa yanatengenezwa kutokana na mimea yenye mizizi inayotoa harufu nzuri.

manukato haya hayakuuzwa kwa dinari 300‡
na fedha hizo wakapewa maskini?” 6 Yuda
alisema hivi si kwa kuwa aliwajali maskini, bali
kwa kuwa alikuwa mwizi, kwani ndiye alikuwa
akitunza mfuko wa fedha akawa anaiba kile
kilichowekwa humo.
7 Yesu akasema, “Mwacheni. Aliyanunua
manukato hayo ili ayaweke kwa ajili ya siku ya
maziko yangu. 8 Maskini mtakuwa nao siku zote,
lakini mimi hamtakuwa nami siku zote.”

### *Shauri La Kumuua Lazaro*

9 Umati mkubwa wa Wayahudi walipojua
kwamba Yesu alikuwa huko Bethania, walikuja
si tu kwa ajili ya Yesu, lakini pia kumwona
Lazaro ambaye Yesu alikuwa amemfufua. 10 Kwa
hiyo viongozi wa makuhani wakafanya mpango
wa kumuua Lazaro pia, 11 kwa kuwa kutokana
na habari za kufufuliwa kwake Wayahudi wengi
walikuwa wanamwendea Yesu na kumwamini.

### *Kuingia Kwa Yesu Yerusalemu Kwa Ushindi (Mathayo 21:1-11; Marko 1:1-11; Luka 19:28-40)*

12 Siku iliyofuata umati mkubwa uliokuwa
umekuja kwenye Sikukuu walisikia kwamba
Yesu angekuja Yerusalemu. 13 Basi wakachukua
matawi ya mitende, wakatoka kwenda kumlaki,
huku wakipaza sauti wakisema,
“Hosana!”§

“Amebarikiwa yeye ajaye kwa Jina la Bwana!”

‡ **12:5** Dinari 300 ni sawa na mshahara wa kibarua wa siku 300.
§ **12:13** Kiebrania kusema Okoa, basi likawa neno la shangwe.

“Amebarikiwa Mfalme wa Israeli!”
14 Yesu akamkuta mwana-punda akampanda,
kama ilivyoandikwa,
15 “Usiogope, Ewe binti Sayuni;
tazama, Mfalme wako anakuja,
amepanda mwana-punda!”
16 Wanafunzi wake Yesu mwanzoni
hawakuelewa mambo haya, lakini Yesu
alipotukuzwa, ndipo walipokumbuka kuwa
mambo haya yalikuwa yameandikwa kwa ajili
yake na alitendewa yeye.
17 Wale waliokuwepo wakati Yesu alipomwita
Lazaro kutoka kaburini na kumfufua kutoka
kwa wafu, waliendelea kushuhudia. 18 Ni
kwa sababu pia walikuwa wamesikia kwamba
alikuwa ametenda muujiza huu ndiyo maana
umati wa watu ukaenda kumlaki. 19 Hivyo
Mafarisayo walipoona hayo wakaambiana,
“Mnaona, hamwezi kufanya lolote. Angalieni,
ulimwengu wote unamfuata yeye!”

### *Yesu Anatabiri Kifo Chake*

20 Basi palikuwa Wayunani fulani miongoni
mwa wale waliokuwa wamekwenda kuabudu
wakati wa Sikukuu. 21 Hawa wakamjia Filipo,
ambaye alikuwa mwenyeji wa Bethsaida huko
Galilaya, wakiwa na ombi. Wakamwambia,
“Tungependa kumwona Yesu.” 22 Filipo
akaenda akamweleza Andrea, nao wote wawili
wakamwambia Yesu.
23 Yesu akawajibu, “Saa imewadia ya Mwana
wa Adamu kutukuzwa. 24 Amin, amin nawaam-
bia, mbegu ya ngano isipoanguka ardhini na
kufa, hubakia kama mbegu peke yake. Lakini

ikifa huzaa mbegu nyingi. 25 Mtu yeyote
anayependa maisha yake atayapoteza, naye ay-
achukiaye maisha yake katika ulimwengu huu
atayaokoa hata kwa uzima wa milele. 26 Mtu
yeyote akinitumikia lazima anifuate, nami ma-
hali nilipo ndipo mtumishi wangu atakapokuwa.
Mtu akinitumikia, Baba yangu atamheshimu.

27 “Sasa roho yangu imefadhaika sana. Niseme
nini? ‘Baba, niokoe katika saa hii.’ Lakini ni
kwa kusudi hili nimeufikia wakati huu. 28 Baba,
litukuze jina lako.”

Ndipo ikaja sauti kutoka mbinguni, “Nimeli-
tukuza, nami nitalitukuza tena.” 29 Ule umati
wa watu uliokuwa mahali pale uliisikia nao
ukasema, “Hiyo ni sauti ya radi,” wengine
wakasema, “Malaika ameongea naye.”

30 Yesu akawaambia, “Sauti hii imesikika kwa
faida yenu, wala si kwa faida yangu. 31 Sasa
ni saa ya hukumu kwa ajili ya ulimwengu
huu, sasa mkuu wa ulimwengu huu atatupwa
nje. 32 Lakini mimi, nikiinuliwa kutoka nchi,
nitawavuta watu wote waje kwangu.” 33 Yesu
aliyasema haya akionyesha ni kifo gani ataka-
chokufa.

34 Ule umati wa watu ukapiga kelele ukasema,
“Tumesikia kutoka Sheria kwamba ‘Kristo* ad-
umu milele,’ wewe wawezaje kusema, ‘Mwana
wa Adamu hana budi kuinuliwa juu’? Huyu
‘Mwana wa Adamu’ ni nani?”

35 Ndipo Yesu akawaambia, “Bado kitambo
kidogo nuru ingalipo pamoja nanyi. Enendeni

---

* **12:34** Kristo maana yake ni Masiya, yaani Aliyetiwa mafuta.

maadamu mna nuru, msije mkakumbwa na giza.
Mtu anayetembea gizani hajui anakokwenda.
36 Wekeni tumaini lenu katika nuru hiyo ili
mpate kuwa wana wa nuru." Baada ya kusema
haya, Yesu aliondoka, akajificha wasimwone.

### *Wayahudi Waendelea Kutokuamini*

37 Hata baada ya Yesu kufanya miujiza hii
yote mbele yao, bado hawakumwamini. 38 Hili
lilikuwa ili kutimiza lile neno la nabii Isaya
lililosema:

"Bwana, ni nani aliyeamini ujumbe wetu,
na mkono wa Bwana umefunuliwa kwa nani?"

39 Kwa hivyo hawakuamini, kwa sababu Isaya
anasema mahali pengine:

40 "Amewafanya vipofu,
na kuifanya mioyo yao kuwa migumu,
ili wasiweze kuona kwa macho yao,
wala kuelewa kwa mioyo yao,
wasije wakageuka nami nikawaponya."

41 Isaya alisema haya alipoona utukufu wa Yesu
na kunena habari zake.

42 Lakini wengi miongoni mwa viongozi wa
Wayahudi walimwamini, lakini kwa sababu ya
Mafarisayo hawakukiri waziwazi kwa maana
waliogopa kufukuzwa katika masinagogi. 43 Wao
walipenda sifa za wanadamu kuliko sifa zitokazo
kwa Mungu.

### *Amwaminiye Yesu Hatabaki Gizani*

44 Yesu akapaza sauti akasema, "Yeyote ani-
aminiye, haniamini mimi peke yangu, bali yeye

aliyenituma. [45] Yeyote anionaye mimi, amem-
wona yeye aliyenituma. [46] Mimi nimekuja
kama nuru ulimwenguni, ili kwamba kila mtu
aniaminiye asibaki gizani.
[47] "Mimi simhukumu mtu yeyote anayesikia
maneno yangu na asiyatii, kwa maana sikuja
kuuhukumu ulimwengu, bali kuuokoa. [48] Yuko
amhukumuye yeye anikataaye mimi na ku-
tokuyapokea maneno yangu, yaani, yale ma-
neno niliyosema yenyewe yatamhukumu siku ya
mwisho. [49] Kwa maana sisemi kwa ajili yangu
mwenyewe, bali Baba aliyenituma aliniamuru ni
nini cha kusema na jinsi ya kukisema. [50] Nami
ninajua amri zake huongoza hadi kwenye uzima
wa milele. Hivyo lolote nisemalo, ndilo lile Baba
aliloniambia niseme."

# 13

## *Yesu Awanawisha Wanafunzi Wake Miguu*

[1] Ilikuwa mara tu kabla ya Sikukuu ya Pasaka.
Yesu alijua ya kuwa wakati wake wa kuondoka
ulimwenguni ili kurudi kwa Baba umewadia.
Alikuwa amewapenda watu wake waliokuwa
ulimwenguni, naam, aliwapenda hadi kipimo
cha mwisho.
[2] Wakati alipokuwa akila chakula cha jioni
na wanafunzi wake, ibilisi alikuwa amekwisha
kutia ndani ya moyo wa Yuda Iskariote, mwana
wa Simoni, wazo la kumsaliti Yesu. [3] Yesu akijua
ya kwamba Baba ameweka vitu vyote chini ya
mamlaka yake na kwamba yeye alitoka kwa
Mungu na alikuwa anarudi kwa Mungu, [4] hivyo
aliondoka chakulani, akavua vazi lake la nje,

akajifunga kitambaa kiunoni. 5 Kisha akamim-
ina maji kwenye sinia na kuanza kuwanawisha
wanafunzi wake miguu na kuikausha kwa kile
kitambaa alichokuwa amejifunga kiunoni.

6 Alipomfikia Simoni Petro, Petro
akamwambia, "Bwana, je, wewe utaninawisha
mimi miguu?"

7 Yesu akamjibu, "Hivi sasa hutambui lile
ninalofanya, lakini baadaye utaelewa."

8 Petro akamwambia, "La, wewe hutaninaw-
isha miguu kamwe."

Yesu akamjibu, "Kama nisipokunawisha,
wewe huna sehemu nami."

9 Ndipo Simoni Petro akajibu, "Usininawishe
miguu peke yake, Bwana, bali pamoja na mikono
na kichwa pia!"

10 Yesu akamjibu, "Mtu aliyekwisha kuoga
anahitaji kunawa miguu tu, kwani mwili wake
wote ni safi. Ninyi ni safi, ingawa si kila
mmoja wenu." 11 Kwa kuwa yeye alijua ni nani
ambaye angemsaliti, ndiyo sababu akasema si
kila mmoja aliyekuwa safi.

12 Alipomaliza kuwanawisha miguu yao, alivaa
tena mavazi yake, akarudi alikokuwa ameketi,
akawauliza, "Je, mmeelewa nililowafanyia?
13 Ninyi mnaniita mimi 'Mwalimu' na 'Bwana,'
hii ni sawa, maana ndivyo nilivyo. 14 Kwa
hiyo, ikiwa mimi niliye Bwana wenu na Mwal-
imu wenu nimewanawisha ninyi miguu, pia
hamna budi kunawishana miguu ninyi kwa
ninyi. 15 Mimi nimewawekea kielelezo kwamba
imewapasa kutenda kama vile nilivyowatendea
ninyi. 16 Amin, amin nawaambia, mtumishi si

mkuu kuliko bwana wake, wala aliyetumwa si
mkuu kuliko yule aliyemtuma. 17 Sasa kwa kuwa
mmejua mambo haya, heri yenu ninyi kama
mkiyatenda.
18 “Sisemi hivi kuhusu ninyi nyote. Ninawa-
jua wale niliowachagua. Lakini ni ili Andiko
lipate kutimia, kwamba, ‘Yeye aliyekula chakula
changu, ameinua kisigino chake dhidi yangu.’
19 “Ninawaambia mambo haya kabla haya-
jatukia, ili yatakapotukia mpate kuamini ya
kuwa Mimi ndiye. 20 Amin, amin nawaambia,
yeyote anayempokea yule niliyemtuma anipokea
mimi, naye anipokeaye mimi ampokea yeye
aliyenituma mimi.”

*Yesu Anatabiri Kusalitiwa Kwake*
*(Mathayo 26:20-25; Marko 14:17-21; Luka 22:21-23)*

21 Baada ya kusema haya, Yesu alifadhaika
sana moyoni, akasema, “Amin, amin nawaam-
bia, mmoja wenu atanisaliti.”
22 Wanafunzi wake wakatazamana bila kujua
kuwa alikuwa anamsema nani. 23 Mmoja wa
wanafunzi wake ambaye Yesu alimpenda sana,
alikuwa ameegama kifuani mwa Yesu. 24 Simoni
Petro akampungia mkono yule mwanafunzi,
akamwambia, “Muulize anamaanisha nani.”
25 Yule mwanafunzi akamwegemea Yesu, aka-
muuliza, “Bwana, tuambie, ni nani?”
26 Yesu akajibu, “Ni yule nitakayempa hiki
kipande cha mkate baada ya kukichovya kwenye
bakuli.” Hivyo baada ya kukichovya kile
kipande cha mkate, akampa Yuda Iskariote,

mwana wa Simoni. [27] Mara tu baada ya
kukipokea kile kipande cha mkate, Shetani
akamwingia.

Yesu akamwambia Yuda, "Lile unalotaka kuli-
tenda litende haraka." [28] Hakuna hata mmoja
wa wale waliokuwa wameketi naye mezani aliy-
eelewa kwa nini Yesu alimwambia hivyo. [29] Kwa
kuwa Yuda alikuwa mtunza fedha, wengine
walifikiri Yesu alikuwa amemwambia akanunue
vitu vilivyohitajika kwa ajili ya Sikukuu, au
kuwapa maskini chochote. [30] Mara tu baada ya
kupokea ule mkate, Yuda akatoka nje. Wakati
huo ulikuwa ni usiku.

### *Yesu Atabiri Petro Kumkana*

*(Mathayo 26:31-35; Marko 14:27-31; Luka 22:31-34)*

[31] Baada ya Yuda kutoka nje, Yesu akasema,
"Sasa Mwana wa Adamu ametukuzwa, naye
Mungu ametukuzwa ndani yake. [32] Ikiwa Mungu
ametukuzwa ndani ya Mwana, Mungu atam-
tukuza Mwana ndani yake mwenyewe naye
atamtukuza mara.

[33] "Watoto wangu, mimi bado niko pamoja
nanyi kwa kitambo kidogo. Mtanitafuta, na
kama vile nilivyowaambia Wayahudi, vivyo
hivyo sasa nawaambia na ninyi. Niendako, ninyi
hamwezi kuja.

[34] "Amri mpya nawapa: Mpendane kama
mimi nilivyowapenda ninyi, vivyo hivyo nanyi
mpendane. [35] Kama mkipendana ninyi kwa
ninyi, kwa njia hii, watu wote watajua kuwa
ninyi ni wanafunzi wangu."

36 Simoni Petro akamuuliza, “Bwana, un-
akwenda wapi?”

Yesu akamjibu, “Ninakokwenda huwezi kuni-
fuata sasa, lakini utanifuata baadaye.”

37 Petro akamuuliza tena, “Bwana, kwa nini
siwezi kukufuata sasa? Mimi niko tayari kuutoa
uhai wangu kwa ajili yako.”

38 Yesu akamjibu, “Je, ni kweli uko tayari
kuutoa uhai wako kwa ajili yangu? Amin, amin
nakuambia, kabla jogoo hajawika, utanikana
mara tatu.”

# 14

*Yesu Awatia Moyo Wanafunzi Wake*

1 Yesu akawaambia, “Msifadhaike mioyoni
mwenu, mnamwamini Mungu, niaminini na
mimi pia.
2 Nyumbani kwa Baba yangu kuna
makao mengi. Kama sivyo, ningeliwaam-
bia. Naenda kuwaandalia makao.
3 Nami
nikienda na kuwaandalia makao, nitarudi tena
na kuwachukua mkae pamoja nami, ili mahali
nilipo, nanyi mpate kuwepo.
4 Ninyi mnajua njia
ya kufika ninakokwenda.”

*Yesu Ndiye Njia Ya Kwenda Kwa Baba*

5 Tomaso akamwambia, “Bwana, sisi hatujui
unakokwenda, tutaijuaje njia?”

6 Yesu akawaambia, “Mimi ndimi njia na kweli
na uzima. Mtu hawezi kuja kwa Baba isipokuwa
kwa kupitia kwangu.
7 Kama mngenijua mimi,
mngemjua na Baba pia. Tangu sasa, mnamjua
Baba yangu, tena mmemwona.”

8 Filipo akamwambia, “Bwana, tuonyeshe
Baba yako yatosha.”
9 Yesu akamjibu, “Filipo, nimekaa nanyi muda
huu wote hata usinijue? Mtu yeyote aliyeniona
mimi, amemwona Baba. Sasa wawezaje kusema,
‘Tuonyeshe Baba’? 10 Je, huamini ya kuwa mimi
niko ndani ya Baba, naye Baba yuko ndani
yangu? Maneno ninayowaambia siyasemi kwa
ajili yangu mwenyewe, bali Baba akaaye ndani
yangu ndiye atendaye hizi kazi. 11 Nisadiki
mimi kwamba niko ndani ya Baba na Baba yuko
ndani yangu, la sivyo, niaminini kwa sababu ya
zile kazi nizitendazo. 12 Amin, amin nawaam-
bia, yeyote aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo
yeye atazifanya, naam na kubwa kuliko hizi
atazifanya, kwa sababu mimi ninakwenda kwa
Baba. 13 Nanyi mkiomba lolote kwa Jina langu,
hilo nitalifanya, ili Baba apate kutukuzwa katika
Mwana. 14 Kama mkiniomba lolote kwa Jina
langu nitalifanya.

*Yesu Aahidi Roho Mtakatifu*

15 “Kama mnanipenda, mtazishika amri zangu.
16 Nami nitamwomba Baba, naye atawapa
Msaidizi mwingine akae nanyi milele. 17 Huyo
ndiye Roho wa kweli ambaye ulimwengu
hauwezi kumpokea, kwa sababu haumwoni
wala haumjui. Ninyi mnamjua kwa kuwa
yuko pamoja nanyi naye anakaa ndani yenu.
18 Sitawaacha ninyi yatima, naja kwenu. 19 Bado
kitambo kidogo ulimwengu hautaniona tena, ila
ninyi mtaniona, kwa kuwa mimi ni hai, ninyi
nanyi mtakuwa hai. 20 Wakati huo mtajua

ya kuwa mimi niko ndani ya Baba na ninyi
mko ndani yangu na mimi niko ndani yenu.
21 Yeyote mwenye amri zangu na kuzishika ndiye
anipendaye, naye anipendaye atapendwa na
Baba yangu, nami nitampenda na kujidhihirisha
kwake."

22 Ndipo Yuda, siyo Iskariote, akamwambia,
"Bwana, itakuwaje kwamba utajidhihirisha
kwetu na si kwa ulimwengu?"

23 Yesu akamjibu, "Mtu yeyote akinipenda
atalishika neno langu na Baba yangu atampenda,
nasi tutakuja kwake na kufanya makao yetu
kwake. 24 Mtu yeyote asiyenipenda hayashiki
maneno yangu na maneno niliyowapa si yangu
bali ni ya Baba aliyenituma.

25 "Nimewaambia mambo haya yote wakati
bado niko pamoja nanyi. 26 Lakini huyo
Msaidizi, yaani, huyo Roho Mtakatifu, ambaye
Baba atamtuma kwenu kwa Jina langu, atawa-
fundisha mambo yote na kuwakumbusha yote
niliyowaambia. 27 Amani nawaachia, amani
yangu nawapa, amani hii niwapayo si kama
ile ulimwengu utoayo. Msifadhaike mioyoni
mwenu, wala msiogope.

28 "Mlinisikia nikisema, 'Ninakwenda
zangu, lakini nitarudi tena.' Kama kweli
mngelinipenda mngelifurahi kwa kuwa naenda
kwa Baba, kwani Baba ni mkuu kuniliko
mimi. 29 Nimewaambia mambo haya kabla
hayajatukia, ili yatakapotukia mpate kuamini.
30 Sitasema nanyi zaidi, kwa sababu yule mkuu
wa ulimwengu huu anakuja, naye hana kitu
kwangu, 31 lakini ulimwengu upate kujua kuwa

ninampenda Baba, nami hufanya vile Baba alivyoniamuru.
"Haya inukeni; twendeni zetu.

# 15

*Yesu Mzabibu Wa Kweli*

1 "Mimi ndimi mzabibu wa kweli na Baba
yangu ndiye mkulima. 2 Kila tawi ndani yangu
lisilozaa matunda, Baba yangu hulikata, nalo kila
tawi lizaalo, hulisafisha ili lipate kuzaa matunda
zaidi. 3 Ninyi mmekwisha kuwa safi kwa sababu
ya lile neno nililonena nanyi. 4 Kaeni ndani
yangu, nami nikae ndani yenu. Kama vile
tawi lisivyoweza kuzaa matunda lisipokaa ndani
ya mzabibu, vivyo hivyo ninyi msipokaa ndani
yangu hamwezi kuzaa matunda.

5 "Mimi ni mzabibu, ninyi ni matawi. Akaaye
ndani yangu, nami ndani yake, huyo huzaa sana,
maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya
jambo lolote. 6 Mtu yeyote asipokaa ndani yangu,
hutupwa nje kama tawi na kunyauka. Matawi
kama hayo hukusanywa na kutupwa motoni,
yakateketea. 7 Ninyi mkikaa ndani yangu na ma-
neno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni lolote
mtakalo, nanyi mtatendewa. 8 Kwa hiyo Baba
yangu hutukuzwa, kwa vile mzaavyo matunda
mengi, nanyi mtakuwa wanafunzi wangu.

9 "Kama vile Baba alivyonipenda mimi, hivyo
ndivyo mimi nilivyowapenda ninyi. Basi kaeni
katika pendo langu. 10 Mkizishika amri zangu
mtakaa katika pendo langu, kama mimi nilivy-
ozishika amri za Baba yangu na kukaa katika

pendo lake. 11 Nimewaambia mambo haya ili
furaha yangu iwe ndani yenu na furaha yenu
iwe kamili. 12 Amri yangu ndiyo hii: Mpendane
kama mimi nilivyowapenda ninyi. 13 Hakuna
mtu mwenye upendo mkuu kuliko huu, mtu
kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake.
14 Ninyi ni rafiki zangu mkifanya ninayowaa-
muru. 15 Siwaiti ninyi watumishi tena, kwa
sababu watumishi hawajui bwana wao analo-
fanya, bali nimewaita ninyi rafiki, kwa maana
nimewajulisha mambo yote niliyoyasikia kutoka
kwa Baba yangu. 16 Si ninyi mlionichagua, bali
mimi ndiye niliyewachagua ninyi na kuwaweka
mwende mkazae matunda, na matunda yenu
yapate kudumu. Ili nalo lolote mtakalomwomba
Baba katika Jina langu, awape ninyi. 17 Amri
yangu ndiyo hii: Mpendane.

### *Ulimwengu Wawachukia Wanafunzi*

18 "Kama ulimwengu ukiwachukia ninyi, kum-
bukeni kwamba ulinichukia mimi kabla yenu.
19 Kama mngekuwa wa ulimwengu, ulimwengu
ungeliwapenda kama vile unavyowapenda walio
wake. Kwa sababu ninyi si wa ulimwengu,
lakini mimi nimewachagua kutoka ulimwengu,
hii ndiyo sababu ulimwengu unawachukia.
20 Kumbukeni lile neno nililowaambia, 'Hakuna
mtumishi aliye mkuu kuliko bwana wake.'
Kama wamenitesa mimi, nanyi pia watawatesa.
Kama wamelishika neno langu, watalishika na
neno lenu pia. 21 Watawatendea ninyi haya yote
kwa ajili ya Jina langu, kwa sababu hawamjui
yeye aliyenituma. 22 Kama sikuja na kusema

nao wasingalikuwa na hatia ya dhambi. Lakini
sasa hawana udhuru kwa ajili ya dhambi zao.
23 Yeyote anayenichukia mimi, anamchukia pia
na Baba yangu. 24 Kama sikuwa nimefanya
miujiza ambayo haijapata kufanywa na mtu
mwingine yeyote, wasingalikuwa na hatia ya
dhambi. Lakini sasa wameiona miujiza hii
na bado wakatuchukia mimi na Baba yangu.
25 Lakini hii ni kutimiza lile neno lililoandikwa
kwenye Sheria kwamba, 'Walinichukia pasipo
sababu.'

26 "Lakini atakapokuja huyo Msaidizi ni-
takayemtuma kwenu kutoka kwa Baba, yaani,
huyo Roho wa kweli atokaye kwa Baba, yeye
atanishuhudia mimi. 27 Ninyi nanyi itawa-
pasa kushuhudia kwa sababu mmekuwa pamoja
nami tangu mwanzo.

# 16

1 "Nimewaambia mambo haya yote ili msije
mkaiacha imani. 2 Watawatenga na masi-
nagogi. Naam, saa yaja ambayo mtu yey-
ote atakayewaua atadhani kwa kufanya hivyo
anamtumikia Mungu. 3 Nao watawatenda haya
kwa sababu hawamjui Baba wala mimi. 4 Lakini
nimewaambia ninyi mambo haya, ili saa hiyo
ikiwadia mpate kukumbuka ya kuwa nilikuwa
nimewaambia. Sikuwaambia mambo haya
tangu mwanzo kwa sababu nilikuwa pamoja
nanyi.

### *Kazi Ya Roho Mtakatifu*

5 “Sasa mimi ninakwenda kwake yeye aliyen-
ituma, lakini hakuna hata aniulizaye, ‘Un-
akwenda wapi?’ 6 Kwa sababu nimewaambia
mambo haya, mioyo yenu imejawa na huzuni.
7 Lakini nawaambia kweli, yafaa mimi nion-
doke, kwa kuwa nisipoondoka, huyo Msaidizi
hatakuja kwenu, lakini nikienda nitamtuma
kwenu. 8 Naye atakapokuja, atauthibitishia
ulimwengu kuhusu dhambi, haki na hukumu.
9 Kwa habari ya dhambi, kwa sababu hawani-
amini mimi, 10 kwa habari ya haki, kwa sababu
ninakwenda kwa Baba, nanyi hamtaniona tena,
11 kwa habari ya hukumu, kwa sababu yule
mkuu wa ulimwengu huu amekwisha kuhuku-
miwa.

12 “Bado ninayo mambo mengi ya
kuwaambia, lakini hamwezi kuyastahimili
sasa. 13 Atakapokuja huyo Roho wa kweli
atawaongoza awatie katika kweli yote. Yeye
hatanena kwa ajili yake mwenyewe, bali atanena
yale yote atakayosikia, naye atawaonyesha
mambo yajayo. 14 Atanitukuza mimi, kwa maana
atayachukua yaliyo yangu na kuwajulisha ninyi.
15 Vyote alivyo navyo Baba ni vyangu. Ndiyo
maana nimesema Roho atachukua yaliyo yangu
na kuwajulisha ninyi.

16 “Bado kitambo kidogo nanyi hamtaniona na
tena bado kitambo kidogo nanyi mtaniona.”

### *Huzuni Itageuka Kuwa Furaha*

17 Baadhi ya wanafunzi wakaulizana, “Ana
maana gani asemapo, ‘Bado kitambo kidogo

nanyi hamtaniona na tena bado kitambo ki-
dogo nanyi mtaniona'? Naye ana maana gani
asemapo, 'Kwa sababu ninakwenda kwa Baba'?"
18 Wakaendelea kuulizana, "Ana maana gani
asemapo, 'Kitambo kidogo'? Hatuelewi hilo
analosema."
19 Yesu akatambua kuwa walitaka kumuuliza
juu ya hilo, hivyo akawaambia, "Je, mnaulizana
nina maana gani niliposema, 'Bado kitambo
kidogo nanyi hamtaniona na tena bado ki-
tambo kidogo nanyi mtaniona'? 20 Amin,
amin nawaambia, ninyi mtalia na kuomboleza,
lakini ulimwengu utafurahi. Ninyi mtahuzu-
nika, lakini huzuni yenu itageuka kuwa fu-
raha. 21 Mwanamke anapokuwa na utungu
wa kuzaa huwa na maumivu kwa sababu saa
yake imewadia. Lakini mtoto akiisha kuzaliwa,
yule mwanamke husahau maumivu hayo kwa
sababu ya furaha ya kuzaliwa mtoto ulimwen-
guni. 22 Hivyo ninyi mna maumivu sasa, lakini
nitawaona tena, nayo mioyo yenu itafurahi na
furaha yenu hakuna awaondoleaye. 23 Katika
siku hiyo hamtaniuliza neno lolote. Amin, amin
nawaambia, kama mkimwomba Baba jambo
lolote kwa jina langu, yeye atawapa. 24 Mpaka
sasa hamjaomba jambo lolote kwa Jina langu.
Ombeni nanyi mtapewa, ili furaha yenu ipate
kuwa kamili.

### *Amani Kwa Wanafunzi*

25 "Nimewaambia mambo haya kwa mafumbo.
Saa yaja ambapo sitazungumza nanyi tena kwa
mafumbo bali nitawaeleza waziwazi kuhusu
Baba. 26 Siku hiyo mtaomba kwa Jina langu.

Wala sitawaambia kwamba nitamwomba Baba
kwa ajili yenu, 27 kwa maana Baba mwenyewe
anawapenda, kwa sababu mmenipenda mimi
na mmeamini kwamba nimetoka kwa Mungu.
28 Nilitoka kwa Baba na kuja ulimwenguni, sasa
naondoka ulimwenguni na kurudi kwa Baba."

29 Ndipo wanafunzi wake wakasema, "Sasa
unazungumza waziwazi, wala si kwa mafumbo.
30 Sasa tumejua kwamba wewe unajua mambo
yote, wala hakuna haja ya mtu kukuuliza
maswali. Kwa jambo hili tunaamini kwamba
ulitoka kwa Mungu."

31 Yesu akawajibu, "Je, sasa mnaamini?
32 Saa inakuja, naam, imekwisha kuwadia,
mtakapotawanyika kila mmoja kwenda nyum-
bani kwake na kuniacha peke yangu. Lakini
mimi siko peke yangu kwa sababu Baba yu
pamoja nami. 33 Nimewaambia mambo haya,
ili mpate kuwa na amani mkiwa ndani yangu.
Ulimwenguni mtapata dhiki. Lakini jipeni moyo,
kwa maana mimi nimeushinda ulimwengu."

# 17

*Yesu Ajiombea Mwenyewe*

1 Baada ya Yesu kusema haya, alitazama
kuelekea mbinguni akawaombea na kusema:

"Baba, saa imewadia. Umtukuze Mwanao,
ili Mwanao apate kukutukuza wewe. 2 Kwa
kuwa umempa mamlaka juu ya wote wenye
mwili ili awape uzima wa milele wale uliompa.
3 Nao uzima wa milele ndio huu, wakujue
wewe uliye Mungu wa pekee, wa kweli na

Yesu Kristo uliyemtuma. 4 Nimekutukuza
wewe duniani kwa kuitimiza ile kazi uliyonipa
niifanye. 5 Hivyo sasa, Baba, unitukuze mbele
zako kwa ule utukufu niliokuwa nao pamoja
na wewe kabla ulimwengu haujakuwepo.

*Yesu Awaombea Wanafunzi Wake*

6 "Nimelidhihirisha jina lako kwa wale ulion-
ipa kutoka ulimwengu. Walikuwa wako,
nawe ukanipa mimi, nao wamelitii neno
lako. 7 Sasa wamejua ya kuwa vyote
ulivyonipa vimetoka kwako, 8 kwa kuwa
maneno yale ulionipa nimewapa wao, nao
wameyapokea na kujua kwamba kweli nime-
toka kwako, nao wameamini kuwa wewe ulin-
ituma. 9 Ninawaombea wao. Mimi siuombei
ulimwengu, bali nawaombea wale ulionipa
kwa sababu wao ni wako. 10 Wote walio
wangu ni wako na walio wako ni wangu,
nami nimetukuzwa ndani yao. 11 Mimi sasa
simo tena ulimwenguni, lakini wao bado
wamo ulimwenguni, nami naja kwako. Baba
Mtakatifu, uwalinde kwa uweza wa jina
lako ulilonipa, ili wawe na umoja kama sisi
tulivyo wamoja. 12 Nilipokuwa pamoja nao,
niliwalinda, wakawa salama kwa lile jina
ulilonipa. Hakuna hata mmoja aliyepotea,
isipokuwa yule aliyekusudiwa upotevu, ili
Maandiko yapate kutimia.

13 "Lakini sasa naja kwako, nami ninasema
mambo haya wakati bado nikiwa ulimwen-
guni, ili wawe na furaha yangu kamili
ndani yao. 14 Nimewapa neno lako, nao

ulimwengu umewachukia kwa kuwa wao
si wa ulimwengu kama mimi nisivyo wa
ulimwengu huu. 15 Siombi kwamba uwaon-
doe ulimwenguni, bali uwalinde dhidi ya
yule mwovu. 16 Wao si wa ulimwengu
huu, kama vile mimi nisivyo wa ulimwengu.
17 Uwatakase kwa ile kweli, neno lako ndilo
kweli. 18 Kama vile ulivyonituma mimi
ulimwenguni, nami nawatuma vivyo hivyo.
19 Kwa ajili yao najiweka wakfu ili wao nao
wapate kutakaswa katika ile kweli.

*Yesu Awaombea Wote Wamwaminio*

20 "Siwaombei hawa peke yao, bali
nawaombea na wale wote watakaoniamini
kupitia neno lao 21 ili wawe na umoja kama
vile wewe Baba ulivyo ndani yangu na mimi
nilivyo ndani yako, wao nao wawe ndani
yetu, ili ulimwengu upate kuamini ya kuwa
wewe ndiye uliyenituma mimi. 22 Utukufu ule
ulionipa nimewapa wao, ili wawe na umoja
kama sisi tulivyo wamoja. 23 Mimi ndani yako
na wewe ndani yangu, ili wawe wamekamilika
katika umoja na ulimwengu upate kujua ya
kuwa umenituma, nami nimewapenda wao
kama unavyonipenda mimi.

24 "Baba, shauku yangu ni kwamba, wale
ulionipa wawe pamoja nami pale nilipo,
ili waweze kuuona utukufu wangu, yaani,
utukufu ule ulionipa kwa kuwa ulinipenda
hata kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.
25 "Baba Mwenye Haki, ingawa ulimwengu
haukujui, mimi ninakujua, nao wanajua ya

kuwa umenituma. [26] Nimefanya jina lako
lijulikane kwao nami nitaendelea kufanya li-
julikane, ili kwamba upendo ule unaonipenda
mimi uwe ndani yao na mimi mwenyewe
nipate kuwa ndani yao."

# 18

*Yesu Akamatwa*
*(Mathayo 26:47-56; Marko 14:43-50; Luka 22:47-53)*

[1] Yesu alipomaliza kuomba, akaondoka na wanafunzi wake wakavuka Bonde la Kidroni. Upande wa pili palikuwa na bustani, yeye na wanafunzi wake wakaingia humo.

[2] Basi Yuda, yule aliyemsaliti alipafahamu ma-
hali hapo kwani Yesu alikuwa akikutana humo
na wanafunzi wake mara kwa mara. [3] Hivyo
Yuda akaja bustanini. Aliongoza kikosi cha askari wa Kirumi, na baadhi ya maafisa kutoka kwa viongozi wa makuhani na Mafarisayo. Nao walikuwa wamechukua taa, mienge na silaha.

[4] Yesu akijua yale yote yatakayompata, akajitokeza mbele yao akawauliza, "Mnamtafuta nani?"

[5] Wao wakamjibu, "Yesu wa Nazareti."

Yesu akawajibu, "Mimi ndiye." Yuda, yule
aliyemsaliti alikuwa amesimama pamoja nao.
[6] Yesu alipowaambia, "Mimi ndiye," walirudi
nyuma na kuanguka chini!

[7] Akawauliza tena, "Mnamtafuta nani?"

Nao wakamjibu, "Yesu wa Nazareti."

[8] Yesu akawaambia, "Nimekwisha kuwaambia kuwa, mimi ndiye; kwa hiyo kama mnanitafuta

mimi, waacheni hawa watu waende zao.”
9 Hii ilikuwa ili litimie lile neno alilosema, “Sikumpoteza hata mmoja miongoni mwa wale ulionipa.”

10 Simoni Petro, aliyekuwa na upanga, akaufuta na kumkata sikio la kuume mtumishi wa kuhani mkuu. Jina la mtumishi huyo aliitwa Malko.

11 Yesu akamwambia Petro, “Rudisha upanga wako kwenye ala yake. Je, hainipasi kukinywea kikombe alichonipa Baba?”

*Yesu Mbele Ya Kuhani Mkuu*

12 Hivyo wale askari, wakiwa pamoja na majemadari wao na maafisa wa Wayahudi, wakamkamata Yesu na kumfunga.
13 Kwanza wakampeleka kwa Anasi, mkwewe Kayafa, aliyekuwa kuhani mkuu mwaka ule.
14 Kayafa ndiye alikuwa amewashauri Wayahudi kwamba imempasa mtu mmoja kufa kwa ajili ya watu.

*Petro Anamkana Yesu*

*(Mathayo 26:69-70; Marko 14:55-64; Luka 22:66-71)*

15 Simoni Petro pamoja na mwanafunzi mwingine walikuwa wakimfuata Yesu. Huyu mwanafunzi mwingine alikuwa anafahamika kwa kuhani mkuu, hivyo aliingia ndani ya ukumbi pamoja na Yesu.
16 Lakini Petro alisimama nje karibu na lango, ndipo yule mwanafunzi mwingine, aliyejulikana na kuhani mkuu, akazungumza na msichana aliyekuwa analinda lango, akamruhusu Petro aingie ndani.

17 Yule msichana akamuuliza Petro, “Je, wewe
pia si mmoja wa wanafunzi wa mtu huyu?”

Petro akajibu, “Sio mimi.”

18 Wale watumishi na askari walikuwa wamesimama wakiota moto wa makaa kwa sababu palikuwa na baridi, Petro naye alikuwa amesimama pamoja nao akiota moto.

*Kuhani Mkuu Amhoji Yesu*

19 Wakati huo kuhani mkuu akawa anamuuliza Yesu kuhusu wanafunzi wake na mafundisho yake.

20 Yesu akamjibu, “Nimekuwa nikizungumza
waziwazi mbele ya watu wote. Siku zote nime-
fundisha katika masinagogi na Hekaluni, mahali
ambapo Wayahudi wote hukusanyika. Sikusema
jambo lolote kwa siri. 21 Mbona unaniuliza
mimi maswali? Waulize wale walionisikia yale
niliyowaambia. Wao wanajua niliyosema.”

22 Alipomaliza kusema hayo, mmoja wa askari aliyekuwa amesimama karibu naye, akampiga Yesu kofi usoni, kisha akasema, “Je, hivyo ndivyo unavyomjibu kuhani mkuu?”

23 Yesu akamjibu akasema, “Kama nimesema
jambo baya, shuhudia huo ubaya niliousema.
Lakini kama nimesema yaliyo kweli, mbona
umenipiga?” 24 Ndipo Anasi akampeleka Yesu
kwa kuhani mkuu Kayafa, akiwa bado amefungwa.

*Petro Amkana Yesu Tena*

*(Mathayo 26:71-75; Marko 14:69-72; Luka 22:58-62)*

25 Wakati huo Simoni Petro alikuwa amesimama akiota moto. Baadhi ya wale

waliokuwepo wakamuuliza, “Je, wewe si mmoja
wa wanafunzi wake?”
Petro akakana, akasema, “Sio mimi.”
26 Mmoja wa watumishi wa kuhani mkuu,
ndugu yake yule mtu ambaye Petro alikuwa
amemkata sikio, akamuuliza, “Je, mimi
sikukuona kule bustanini ukiwa na Yesu?”
27 Kwa mara nyingine tena Petro akakana, naye
jogoo akawika wakati huo huo.

### *Yesu Apelekwa Kwa Pilato*
*(Mathayo 27:1-2, 11-14; Marko 15:1-5; Luka 23:1-5)*

28 Ndipo Wayahudi wakamchukua Yesu ku-
toka kwa Kayafa na kumpeleka kwenye jumba
la kifalme la mtawala wa Kirumi.* Wakati
huo ilikuwa ni alfajiri, ili kuepuka kuwa najisi
kwa taratibu za ibada, Wayahudi hawakuin-
gia ndani kwa sababu ya sheria za Kiyahudi.
Wangehesabiwa kuwa najisi kama wangein-
gia nyumbani mwa mtu asiye Myahudi na
wasingeruhusiwa kushiriki katika Sikukuu ya
Pasaka. 29 Hivyo Pilato akatoka nje walikokuwa
akawauliza, “Mmeleta mashtaka gani kumhusu
mtu huyu?”
30 Wao wakamjibu, “Kama huyu mtu hakuwa
mhalifu tusingemleta kwako.”
31 Pilato akawaambia, “Basi mchukueni ninyi
mkamhukumu kwa kufuata sheria zenu.”
Wayahudi wakamjibu, “Sisi haturuhusiwi
kutoa hukumu ya kifo kwa mtu yeyote.”

---

* **18:28** Jumba la mfalme la mtawala wa Kirumi lilikuwa linaitwa Praitorio.

32 Walisema hivyo ili yale maneno aliyosema
Yesu kuhusu kifo atakachokufa yapate kutimia.
33 Kwa hiyo Pilato akaingia ndani ya jumba
la kifalme, akamwita Yesu, akamuuliza, “Wewe
ndiye mfalme wa Wayahudi?”
34 Yesu akamjibu, “Je, unauliza swali hili
kutokana na mawazo yako mwenyewe, au
uliambiwa na watu kunihusu mimi?”
35 Pilato akamjibu, “Mimi si Myahudi, ama
sivyo? Taifa lako mwenyewe na viongozi wa
makuhani wamekukabidhi kwangu. Umefanya
kosa gani?”
36 Yesu akajibu, “Ufalme wangu si wa
ulimwengu huu. Ufalme wangu ungekuwa wa
ulimwengu huu, wafuasi wangu wangenipigania
ili nisitiwe mikononi mwa Wayahudi. Lakini
kama ilivyo, ufalme wangu hautoki hapa
ulimwenguni.”
37 Pilato akamuuliza, “Kwa hiyo wewe ni
mfalme?” Yesu akajibu, “Wewe wasema
kwamba mimi ni mfalme. Kwa kusudi hili niliza-
liwa, na kwa ajili ya hili nilikuja ulimwenguni,
ili niishuhudie kweli. Mtu yeyote aliye wa kweli
husikia sauti yangu.”
38 Pilato akamuuliza Yesu, “Kweli ni nini?”
Baada ya kusema haya Pilato akaenda nje
tena akawaambia wale viongozi wa Wayahudi
waliomshtaki Yesu, “Sioni kosa lolote alilotenda
mtu huyu. 39 Lakini ninyi mna desturi yenu
kwamba wakati wa Pasaka nimwachie huru
mfungwa mmoja mnayemtaka. Je, mnataka
niwafungulie huyu ‘Mfalme wa Wayahudi’?”

40 Wao wakapiga kelele wakisema, “Si huyu
mtu, bali tufungulie Baraba!” Yule Baraba
alikuwa mnyang’anyi.

# 19

*Yesu Ahukumiwa Kusulubiwa*
*(Mathayo 27:15-31; Marko 15:6-20; Luka 23:13-25)*

1 Ndipo Pilato akamtoa Yesu akaamuru apigwe
mijeledi. 2 Askari wakasokota taji ya miiba,
wakamvika Yesu kichwani. Wakamvalisha joho
la zambarau. 3 Wakawa wanapanda pale alipo
tena na tena, wakisema, “Salamu! Mfalme wa
Wayahudi!” Huku wakimpiga makofi usoni.
4 Pilato akatoka tena nje akawaambia wale
waliokusanyika, “Tazameni, namkabidhi Yesu
kwenu kuwajulisha kwamba mimi sikumwona
ana hatia.” 5 Kwa hiyo Yesu akatoka nje akiwa
amevaa ile taji ya miiba na lile vazi la zambarau.
Pilato akawaambia, “Tazameni, huyu hapa huyo
mtu!”
6 Wale viongozi wa makuhani na maafisa
walipomwona, wakapiga kelele wakisema,
“Msulubishe! Msulubishe!”

Pilato akawaambia, “Mchukueni ninyi mkamsulubishe, mimi sioni hatia juu yake.”

7 Wayahudi wakamjibu, “Sisi tunayo sheria na
kutokana na sheria hiyo, hana budi kufa kwa
sababu yeye alijiita Mwana wa Mungu.”
8 Pilato aliposikia haya, akaogopa zaidi.
9 Akaingia tena ndani ya jumba la kifalme, aka-
muuliza Yesu, “Wewe umetoka wapi?” Lakini
Yesu hakumjibu. 10 Pilato akamwambia, “Wewe

unakataa kuongea na mimi? Hujui ya kuwa
nina mamlaka ya kukuachia huru au kukusulu-
bisha?”
11 Ndipo Yesu akamwambia, “Wewe
hungekuwa na mamlaka yoyote juu yangu
kama hungepewa kutoka juu. Kwa hiyo yeye
aliyenitia mikononi mwako ana hatia ya dhambi
iliyo kubwa zaidi.”
12 Tangu wakati huo, Pilato akajitahidi
kutafuta njia ya kumfungua Yesu, lakini
Wayahudi wakazidi kupiga kelele wakisema,
“Ukimwachia huyu mtu, wewe si rafiki wa
Kaisari. Mtu yeyote anayedai kuwa mfalme
anampinga Kaisari.”
13 Pilato aliposikia maneno haya akamtoa Yesu
nje tena akaketi katika kiti chake cha hukumu,
mahali palipoitwa Sakafu ya Jiwe, kwa Kiebrania
paliitwa Gabatha* 14 Basi ilikuwa siku ya Maan-
dalio ya Pasaka, yapata kama saa sita hivi.

Pilato akawaambia Wayahudi, “Huyu hapa mfalme wenu!”
15 Wao wakapiga kelele, “Mwondoe! Mwon-
doe! Msulubishe!”

Pilato akawauliza, “Je, nimsulubishe mfalme wenu?”

Wale viongozi wa makuhani wakamjibu, “Sisi hatuna mfalme mwingine ila Kaisari.”
16 Ndipo Pilato akamkabidhi Yesu kwao ili
wamsulubishe.

---

* **19:13** Gabatha ni neno la Kiebrania ambalo maana yake ni Sakafu ya jiwe; ni mahali pa wazi palipoinuliwa ambako palitumika kama mahakama.

*Kusulubiwa Kwa Yesu*
*(Mathayo 27:32-44; Marko 15:21-32; Luka 23:26-43)*

Kwa hiyo askari wakamchukua Yesu. 17 Yesu,
akiwa ameubeba msalaba wake, akatoka
kuelekea mahali palipoitwa Fuvu la Kichwa
(kwa Kiebrania ni Golgotha). 18 Hapo ndipo
walipomsulubisha. Pamoja naye walisulubisha watu wengine wawili, mmoja kila upande wake, naye Yesu katikati.

19 Pilato akaamuru tangazo liandikwe na liwekwe juu kwenye msalaba wa Yesu, likasema: “YESU WA NAZARETI, MFALME WA WAYAHUDI.”
20 Kwa kuwa mahali hapo Yesu aliposulubiwa palikuwa karibu na mjini, Wayahudi wengi walisoma maandishi haya yaliyokuwa yameandikwa kwa lugha za Kiebrania, Kiyunani
na Kilatini. 21 Viongozi wa makuhani wa
Wayahudi wakapinga, wakamwambia Pilato, “Usiandike ‘Mfalme wa Wayahudi,’ bali andika kwamba mtu huyu alisema yeye ni mfalme wa Wayahudi.”

22 Pilato akawajibu, “Nilichokwisha kuandika, nimeandika!”

*Mavazi Ya Yesu Yagawanywa*

23 Askari walipokwisha kumsulubisha Yesu, walichukua nguo zake wakazigawa mafungu manne, kila askari fungu lake. Ila walikubaliana wasilichane lile vazi lake kwa maana lilikuwa halina mshono bali limefumwa tangu juu hadi
chini. 24 Wakaambiana, “Tusilichane ila tulipigie
kura ili kuamua ni nani atalichukua.”

Hili lilitukia ili Maandiko yapate kutimizwa
yale yaliyosema,
“Wanagawana nguo zangu,
na vazi langu wanalipigia kura.”
Hayo ndiyo waliyoyafanya wale askari.
25 Wakati huo huo karibu na msalaba wa
Yesu walikuwa wamesimama mama yake, na
dada wa mamaye, na Maria mke wa Klopa,
na Maria Magdalene. 26 Yesu alipomwona
mama yake mahali pale pamoja na yule
mwanafunzi aliyempenda wamesimama karibu,
akamwambia mama yake, “Mwanamke, huyo
hapo ndiye mwanao,” 27 kisha akamwambia yule
mwanafunzi, “Nawe huyo hapo ndiye mama
yako.” Tangu wakati huo yule mwanafunzi
akamchukua mama yake Yesu nyumbani kwake.

*Kifo Cha Yesu*

*(Mathayo 27:45-56; Marko 15:33-41; Luka 23:44-49)*

28 Baada ya haya, Yesu hali akijua kuwa
mambo yote yamemalizika, alisema ili kutimiza
Maandiko, “Naona kiu.” 29 Hapo palikuwa
na bakuli lililojaa siki. Kwa hiyo waka-
chovya sifongo kwenye hiyo siki, wakaiweka
kwenye ufito wa mti wa hisopo, wakampelekea
mdomoni. 30 Baada ya kuionja hiyo siki, Yesu
akasema, “Imekwisha.” Akainamisha kichwa
chake, akaitoa roho yake.

*Yesu Achomwa Mkuki Ubavuni*

31 Kwa kuwa ilikuwa siku ya Maandalio ya
Pasaka, Wayahudi hawakutaka miili ibaki msal-
abani siku ya Sabato, hasa kwa kuwa hiyo

Sabato ingekuwa Sikukuu. Wakamwomba Pilato
aamuru miguu ya wale waliosulubiwa ivunjwe
ili wafe haraka miili iondolewe kwenye misal-
aba. 32 Kwa hiyo askari wakaenda wakavunja
miguu ya mtu wa kwanza aliyesulubiwa pamoja
na Yesu na yule mwingine pia. 33 Lakini
walipomkaribia Yesu, wakaona ya kuwa amek-
wisha kufa, hivyo hawakuvunja miguu yake.
34 Badala yake mmoja wa wale askari akam-
choma mkuki ubavuni na mara pakatoka damu
na maji. 35 Mtu aliyeona mambo hayo ndiye
alitoa ushuhuda, nao ushuhuda wake ni kweli.
Anajua kuwa anasema kweli, naye anashuhudia
ili pia nanyi mpate kuamini. 36 Kwa maana
mambo haya yalitukia ili Maandiko yapate ku-
timia, yale yasemayo, “Hakuna hata mfupa wake
mmoja utakaovunjwa.” 37 Tena Andiko lingine
lasema, “Watamtazama yeye waliyemchoma.”

### *Maziko Ya Yesu*
### *(Mathayo 27:57-61; Marko 15:42-47; Luka 23:50-56)*

38 Baada ya mambo haya, Yosefu wa
Arimathaya, aliyekuwa mfuasi wa Yesu, ingawa
kwa siri kwa sababu ya kuwaogopa Wayahudi,
alimwomba Pilato ruhusa ili kuuchukua
mwili wa Yesu. Pilato alimruhusu, hivyo
akaja, akauchukua. 39 Naye Nikodemo, yule
ambaye kwanza alimwendea Yesu usiku,
akaja, akaleta mchanganyiko wa manemane
na manukato, yenye uzito wa zaidi ya kilo

thelathini† 40 Wakauchukua mwili wa Yesu,
wakaufunga katika sanda ya kitani safi pamoja
na yale manukato, kama ilivyokuwa desturi ya
Wayahudi. 41 Basi palikuwa na bustani karibu
na mahali pale aliposulubiwa, na pale ndani
ya ile bustani palikuwa na kaburi jipya, ambalo
halikuwa limezikiwa mtu bado. 42 Kwa hiyo, kwa
kuwa ilikuwa siku ya Wayahudi ya Maandalio,
nalo kaburi hilo lilikuwa karibu, wakamzika
Yesu humo.

# 20

*Kufufuka Kwa Yesu*

*(Mathayo 28:1-8; Marko 16:1-8; Luka 24:1-12)*

1 Alfajiri na mapema siku ya kwanza ya juma,
kulipokuwa kungali giza bado, Maria Magdalene
alikwenda kaburini na kukuta lile jiwe limeon-
dolewa penye ingilio. 2 Hivyo akaja akikimbia
kwa Simoni Petro pamoja na yule mwanafunzi
mwingine ambaye Yesu alimpenda, na kusema,
“Wamemwondoa Bwana kaburini, na hatujui
walikomweka!”

3 Petro na yule mwanafunzi mwingine
wakaondoka mara kuelekea kaburini. 4 Wote
wawili walikuwa wanakimbia, lakini yule
mwanafunzi mwingine akakimbia mbio zaidi
kuliko Petro, akatangulia kufika kaburini.
5 Alipofika, akainama na kuchungulia mle
kaburini, akaona vile vitambaa vya kitani mle
ndani, lakini hakuingia. 6 Ndipo Simoni Petro

---

† **19:39** Zaidi ya kilo 30; tafsiri nyingine zinasema ratili 100, na nyingine ratili 75, ambazo ni kama kilo 34.

akaja, akimfuata nyuma akaenda moja kwa
moja hadi ndani ya kaburi. Naye akaona vile
vitambaa vya ile sanda vikiwa pale chini 7 na
kile kitambaa kilichokuwa kichwani mwa Yesu.
Kitambaa hicho kilikuwa kimekunjwa mahali pa
peke yake, mbali na vile vitambaa vya kitani vya
ile sanda. 8 Kisha yule mwanafunzi aliyetangulia
kufika kaburini naye akaingia ndani, akaona,
akaamini, 9 (kwa kuwa mpaka wakati huo
walikuwa bado hawajaelewa kutoka Maandiko
kwamba ilikuwa lazima Yesu afufuke kutoka
kwa wafu).
10 Kisha hao wanafunzi wakaondoka wakarudi
nyumbani kwao.

### *Yesu Anamtokea Maria Magdalene (Mathayo 28:9-10; Marko 16:9-11)*

11 Lakini Maria Magdalene akasimama nje ya
kaburi akilia. Alipokuwa akilia, akainama,
kuchungulia mle kaburini, 12 naye akaona
malaika wawili wamevaa mavazi meupe,
wameketi pale mwili wa Yesu ulipokuwa
umelazwa, mmoja upande wa kichwani na
mwingine upande wa miguuni.
13 Wakamuuliza Maria, "Mwanamke, mbona
unalia?"
Akawaambia, "Nalia kwa kuwa wamem-
chukua Bwana wangu na sijui walikomweka."
14 Baada ya kusema hayo, akageuka, akamwona
Yesu amesimama, lakini hakumtambua.
15 Yesu akamwambia, "Mwanamke, mbona
unalia? Unamtafuta nani?"
Maria akidhani ya kuwa aliyekuwa anaongea
naye ni mtunza bustani, kwa hiyo akamwambia,

"Bwana, kama ni wewe umemchukua, tafadhali nionyeshe ulikomweka, nami nitamchukua."

16 Yesu akamwita, "Maria!"

Ndipo Maria akamgeukia Yesu na kusema naye kwa Kiebrania, "Rabboni!" (maana yake Mwalimu).

17 Yesu akamwambia, "Usinishike, kwa maana sijapaa kwenda kwa Baba. Lakini nenda kwa ndugu zangu ukawaambie, 'Ninapaa kwenda kwa Baba yangu ambaye ni Baba yenu, kwa Mungu wangu ambaye ni Mungu wenu.' "

18 Kwa hiyo Maria Magdalene akaenda kuwatangazia wanafunzi wa Yesu, akisema, "Nimemwona Bwana!" Naye akawaambia kwamba Yesu alikuwa amemweleza mambo hayo yote.

### *Yesu Awatokea Wanafunzi Wake*

*(Mathayo 28:16-20; Marko 16:14-18; Luka 24:36-49)*

19 Ikawa jioni ya ile siku ya kwanza ya juma,
wanafunzi wake walikuwa pamoja, milango
ikiwa imefungwa kwa kuwaogopa Wayahudi.
Naye Yesu aliwatokea, akasimama katikati yao,
akasema, "Amani iwe nanyi!" 20 Baada ya
kusema haya, akawaonyesha mikono yake na
ubavu wake. Wanafunzi wake wakafurahi sana
walipomwona Bwana.

21 Yesu akawaambia tena, "Amani iwe nanyi!
Kama vile Baba alivyonituma mimi, mimi nami
nawatuma ninyi." 22 Naye alipokwisha kusema
haya, akawavuvia, akawaambia, "Pokeeni Roho
Mtakatifu. 23 Mkimwondolea mtu yeyote dhambi

zake, zitaondolewa, na yeyote msiyemwondolea
dhambi zake, hazitaondolewa.”

### *Yesu Anamtokea Tomaso*

24 Lakini Tomaso, aliyeitwa Didimasi, yaani
Pacha, mmoja wa wale kumi na wawili, hakuwa
pamoja nao Yesu alipokuja. 25 Hivyo wale wana-
funzi wengine wakamwambia, “Tumemwona
Bwana.”

Lakini yeye akawaambia, “Nisipoona zile
alama za misumari mikononi mwake, na
kuweka kidole changu kwenye hizo alama za
misumari na mkono wangu ubavuni mwake,
sitaamini.”

26 Baada ya siku nane, wanafunzi wake wa-
likuwa tena pamoja ndani ya nyumba, naye
Tomaso alikuwa pamoja nao. Ndipo Yesu akaja
milango ikiwa imefungwa na kusimama katikati
yao akasema, “Amani iwe nanyi.” 27 Kisha
akamwambia Tomaso, “Weka kidole chako hapa
na uone mikono yangu, nyoosha mkono wako
uguse ubavuni mwangu. Usiwe na shaka, bali
uamini tu.”

28 Tomaso akamwambia, “Bwana wangu na
Mungu wangu!”

29 Yesu akamwambia, “Umeamini kwa kuwa
umeniona? Wamebarikiwa wale ambao hawa-
jaona lakini wameamini.”

### *Kusudi La Kitabu Hiki*

30 Yesu alifanya miujiza mingine mingi mbele
za wanafunzi wake, ambayo haikuandikwa
katika kitabu hiki. 31 Lakini haya yameandikwa

ili mweze kuamini ya kuwa Yesu ndiye Kristo,*
Mwana wa Mungu, na kwa kumwamini mpate
uzima katika jina lake.

# 21

*Yesu Awatokea Wanafunzi Saba*

1 Baada ya haya Yesu akawatokea tena
wanafunzi wake kando ya Bahari ya Tiberia.*
Yeye alijionyesha kwao hivi: 2 Simoni Petro,
Tomaso aitwaye Didimasi, yaani Pacha,
Nathanaeli wa Kana ya Galilaya, wana wa
Zebedayo na wanafunzi wengine wawili
walikuwa pamoja. 3 Simoni Petro akawaambia
wenzake, “Mimi naenda kuvua samaki.” Nao
wakamwambia, “Tutakwenda pamoja nawe.”
Wakatoka, wakaingia ndani ya mashua, lakini
usiku ule hawakupata chochote.

4 Mara baada ya kupambazuka, Yesu akasi-
mama ufuoni, lakini wanafunzi hawakumtam-
bua kwamba alikuwa Yesu.

5 Yesu akawaambia, “Wanangu, je, mna
samaki wowote?”

Wakamjibu, “La.”

6 Akawaambia, “Shusheni nyavu upande wa
kuume wa mashua yenu nanyi mtapata samaki.”
Wakashusha nyavu na tazama wakapata samaki
wengi mno hata wakashindwa kuvutia zile
nyavu zilizojaa samaki ndani ya mashua.

---

* **20:31** Kristo maana yake ni Masiya, yaani Aliyetiwa mafuta.

* **21:1** Yaani Bahari ya Galilaya.

7 Yule mwanafunzi aliyependwa na Yesu
akamwambia Petro, “Huyu ni Bwana!” Si-
moni Petro aliposikia haya, akajifunga nguo
yake kwa kuwa alikuwa uchi, naye akajitosa
baharini. 8 Wale wanafunzi wengine wakaja kwa
ile mashua huku wakikokota ule wavu uliyojaa
samaki, maana hawakuwa mbali na nchi kavu,
ilikuwa yapata dhiraa 200† 9 Walipofika ufuoni,
wakaona moto wa makaa na samaki wakiokwa
juu yake na mikate.

10 Yesu akawaambia, “Leteni baadhi ya hao
samaki mliovua sasa hivi.”

11 Simoni Petro akapanda kwenye mashua na
kuukokota ule wavu pwani. Ulikuwa umejaa
samaki wakubwa 153. Ingawa samaki walikuwa
wengi kiasi hicho, ule wavu haukuchanika.
12 Yesu akawaambia, “Njooni mpate kifungua
kinywa.” Hakuna hata mmoja wa wanafunzi
aliyethubutu kumuuliza, “Wewe ni nani?” Kwa
sababu walijua ya kuwa ni Bwana. 13 Yesu akaja,
akachukua ule mkate, akawapa na vivyo hivyo
akawagawia pia wale samaki. 14 Hii ilikuwa
mara ya tatu Yesu kuwatokea wanafunzi wake
baada yake kufufuliwa kutoka kwa wafu.

### *Yesu Amuuliza Petro Kama Anampenda*

15 Walipokwisha kula, Yesu akamuuliza Simoni
Petro, “Je, Simoni mwana wa Yohana, una-
nipenda kweli kuliko hawa?”

Yeye akamjibu, “Ndiyo Bwana, wewe unajua
ya kuwa ninakupenda.”

---

† **21:8** Dhiraa 200 ni kama mita 90.

Yesu akamwambia, “Lisha wana-kondoo wangu.”
16 Yesu akamwambia tena, “Simoni, mwana wa Yohana, wanipenda?”

Petro akamjibu, “Ndiyo Bwana, wewe unajua ya kuwa ninakupenda.”

Yesu akamwambia, “Chunga kondoo zangu.”

17 Kwa mara ya tatu Yesu akamuuliza Petro, “Simoni mwana wa Yohana, unanipenda?”

Petro akahuzunika sana kwa kuwa Yesu alimuuliza mara ya tatu, “Unanipenda?” Akamjibu, “Bwana, wewe unajua yote, unajua ya kuwa ninakupenda.”

Yesu akamwambia, “Lisha kondoo wangu.
18 Amin, amin nakuambia, ulipokuwa kijana ulivaa na kwenda unakotaka, lakini utakapokuwa mzee utanyoosha mikono yako na mtu mwingine atakuvika na kukupeleka usipotaka kwenda.”
19 Yesu alisema haya ili kuashiria ni kifo cha aina gani Petro atakachomtukuza nacho Mungu. Kisha Yesu akamwambia Petro, “Nifuate!”

20 Petro akageuka, akamwona yule mwanafunzi aliyependwa na Yesu akiwafuata. (Huyu ndiye yule mwanafunzi aliyeegama kifuani mwa Yesu walipokula naye chakula cha mwisho na kuuliza, “Bwana, ni nani atakayekusaliti?”)
21 Petro alipomwona huyo mwanafunzi, akamuuliza Yesu, “Bwana na huyu je?”

22 Yesu akamjibu, “Ikiwa nataka aishi mpaka nitakaporudi, inakuhusu nini? Wewe inakupasa unifuate!”
23 Kwa sababu ya maneno haya ya Yesu, uvumi ukaenea miongoni mwa ndugu kwamba huyu mwanafunzi hangekufa. Lakini

Yesu hakusema kuwa hangekufa. Yeye alisema tu kwamba, “Ikiwa nataka aishi mpaka nitakaporudi, inakuhusu nini?”

24 Huyu ndiye yule mwanafunzi anayeshuhudia mambo haya na ndiye ambaye ameandika habari hizi. Nasi tunajua ya kuwa ushuhuda wake ni kweli.

25 Lakini kuna mambo mengine mengi ambayo Yesu alifanya. Kama yote yangeliandikwa, nadhani hata ulimwengu wote usingekuwa na nafasi ya kutosha kuweka vitabu vyote ambavyo vingeandikwa. Amen.